

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA ISHIRINI

Kikao cha Kumi – Tarehe 22 Mei, 2015

(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Naibu Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, kwa mwaka wa Fedha 2015/2016.

MHE. CAPT. JOHN Z. CHILIGATI (K.n.y. MHE. ANNA M. ABDALLAH - MWENYEKITI WA KAMATI YA ULINZI NA USALAMA):

Taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016.

MHE. JOSEPH R. SELASINI (K.n.y. MHE. GODBLESS J. LEMA - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI JUU YA WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI):

Taarifa ya Msemaji wa Mkuu wa Kambi ya Upinzani Makadirio ya Matumizi ya Fedha kwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016.

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:

Hotuba ya Bajeti ya Wazira ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka wa fedha 2015/2016.

MHE. CAPT. JOHN Z. CHILIGATI (K.n.y. MHE. ANNA M. ABDALLAH - MWENYEKITI WA KAMATI YA ULINZI NA USALAMA):

Taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016.

MHE. MASOUD ABDALLA SALIM - MSEMaji MKUU WA KAMBI YA UPINZANI JUU YA WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Fedha kwa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016.

MASWALI NA MAJIBU

NAIBU SPIKA: Kama ilivyo ada, tunaanza na Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, swali la kwanza linaulizwa na Mheshimiwa Magolyo Ezekiel Maige, kwa niaba yake, endelea Mheshimiwa!

Na. 69

Utekelezaji wa Mpango wa MMAM – Msalala

MHE. DUNSTAN L. KITANDULA (K.n.y. MHE. EZEKIEL M. MAIGE) aliuliza:

Wananchi wa Msalala wameitikia wito wa kujenga zahanati katika kila kijiji na kituo cha afya kwa kila kata na mpaka sasa kuna miradi 48 ya zahanati na minne ya vituo vya aya.

(a) Je, Serikali ina utaratibu gani wa kutekeleza mpango huo wa MMAM?

(b) Je, Serikali ipo tayari kutoa fedha za miradi hiyo ili nguvu za wananchi zisipotee bure?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ezekiel Magolyo Maige, Mbunge wa Msalala, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango wa Maendeleo wa Afya ya Msingi (MMAM) ni sehemu ya utekelezaji wa Sera ya Afya ya mwaka 2007 ambayo inaelekeza ujenzi wa zahanati kila kijiji na kituo cha afya kila kata. Ujenzi wa zahanati na vituo vya afya nchini unafanyika kwa ubia kati ya wananchi na Halmashauri kupitia Mpango wa Fursa na Vikwazo kwa Maendeleo (O&OD). Sehemu kubwa ya miradi hii huibuliwa na kutekelezwa na wananchi wenyewe na Halmashauri huchangia nguvu kidogo ili kukamilisha miradi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2014/2015, Halmashauri ya Wilaya ya Msalala ilitengewa fedha za MMAM jumla ya shilingi milioni 180 ili kusaidia nguvu za wananchi kwa lengo la kujenga nyumba za watumishi katika Zahanati za Mwalugulu, Mhandu, Bukwangu, Ntobo B na Buluma. Fedha zilizopokelewa na Halmashauri hadi sasa ni shilingi milioni 45 ambazo zimetumika kujenga nyumba ya watumishi, nyumba mbili kwa pamoja (*two in one*).

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuhakikisha nguvu za wananchi hazipoteti bure, Serikali katika bajeti ya mwaka 2014/2015, ilitenga na kutumia shilingi milioni 135 ili kukamilisha majengo ya zahanati katika vijiji tisa ambavyo ni Itinde, Ngaya, Mwakazuka, Mwakata, Ndala, Nyamigege, Mega, Ikinda na Bushing'we. Fedha hizo zimetumika kupaua Zahanati hizo zilizojengwa kwa nguvu za wananchi.

Vilevile katika bajeti ya mwaka 2015/2016, Serikali imetenga shilingi milioni 315 kutokana na mapato ya ndani kwa ajili ya kukamilisha majengo haya ili yaanze kutumika. Serikali iitaendelea kutenga fedha kwa ajili ya miradi ya kuboresha huduma za afya kadiri uwezo wa makusanyo ya fedha utakavyokuwa unaimarika.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kitandula, ameridhika, Mheshimiwa Maige mwenyewe!

MHE. EZEKIEL M. MAIGE: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza, kwa kuwa wananchi wa Halmashauri ya Wilaya ya Msalala na Jimbo la Msalala kwa ujumla wamefanya kazi kubwa sana kama

ambavyo swali la msingi limeeleza na kiasi cha fedha kinachotolewa na Serikali ni kidogo kwa maana shilingi milioni 100 alizosisema hazitoshi kukamilisha hata maboma ya zahanati kwenye vijiji vitano. Nataka kujua, Serikali ina mpango gani maalum wa kuongeza mgao wa fedha ili maboma haya ambayo kwa sasa yanafikia zaidi ya 38 yaweze kukamilika katika mwaka wa fedha ambao tunauanza?

Swali la pili, kwa kuwa kazi hii kubwa iliyofanywa na wananchi wa Msalala kwa kiasi kikubwa sana imechangiwa na msukumo wa Mbunge wa eneo husika ambaye katika hizi zahanati zote mchango wake binafsi na kupitia Mfuko wa Jimbo ni zaidi ya 30%. Je, Serikali inasema nini kwa Wabunge wa aina hii hasa kwenye nyakati tulizonazo?

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru.

NAIBU SPIKA: Majibu ya swali hilo, Naibu Waziri, TAMISEMI, Mheshimiwa Majaliwa Kassim Majaliwa!

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU): Mheshimiwa Naibu Spika, naanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Maige kwa kazi kubwa anayoifanya juu ya usimamizi wa shughuli za miradi kwenye Jimbo lake na hasa kitendo cha ufuatiliaji wa mara kwa mara kwa sababu jana tulikuwa wote pia akitaka ufafanuzi wa kina juu ya jambo hili.

Nataka nimhakikishie kama nilivyosema kwenye jibu la msingi kwamba nguvu za wananchi zilizotumika kwenye Jimbo la Msalala kupitia mapato ya ndani tumetenga jumla ya shilingi milioni 315. Hata hivyo, hatukuishia hapo tu, bado kwenye bajeti yetu ndani ya Serikali tumetenga fedha jumla ya shilingi milioni 215 kuzipeleka Msalala ili kukamilisha shughuli mbalimbali zinazoendelea pale na hasa kuunga mkono jitihada za wananchi wale. Kwa hiyo, hizo ndiyo jitihada ambazo sasa hivi tunazifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia natambua kazi kubwa inayofanywa na wadau wa Kampuni ya *Accacia*, wametenga fedha ambazo jumla ya shilingi bilioni tatu ambazo zitasaidia kupandisha hadhi ya vituo vya afya kuwa hospitali ambazo zitaweza kutoa tiba ya kiwango cha juu ili kupanua wigo wa matibabu yanayotolewa kwenye Jimbo lake.

Kwa hiyo, kwa misaada hii ambayo tunaipata na wadau ambao tunashughulika nao inatusaidia zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi tunatambua kwamba tuna majengo 26 yako katika hatua mbalimbali za ukamilishaji wa zahanati, lakini tuna majengo mawili ya vituo vya afya, kuna Hospitali ya Wilaya nayo ina majengo ambayo pia yapo katika hatua mbalimbali. Haya nayo tumeendelea

kuwasiliana na Halmashauri kuona namna ambavyo tunaweza kuongeza zaidi bajeti ili pia tuweze kufanya kazi pamoja na wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, Mheshimiwa Maige ni mmoja kati ya Wabunge hodari na sisi tunajua kazi yako nzuri, umetoa mchango mkubwa sana Serikalini. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge apate matumaini kwamba wananchi wanatambua jitihada zake na bado anafanya nafasi kwenye eneo lake na tunaomba Mungu amwezeshe ili apande juu zaidi. Ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Swali linalofuata ni la Mheshimiwa Selemani Said Bungara, Mbunge wa Kilwa Kusini, kwa niaba yake tafadhali, naangalia nyuma kule, Mheshimiwa Rajab Mbarouk!

Na. 70

Ujenzi wa Barabara Kutoka Singino – Kwa Mkocho – Kivinje

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED (K.n.y. MHE. SELEMANI S. BUNGARA)
aliuliza:-

Kipande cha barabara toka Singino - Kwa Mkocho hadi Kivinje chenye urefu wa kilomita 2.5 kimekuwa kero kubwa kwa watumiaji wake kutokana na mashimo na makorongo makubwa yaliyopo; na tarehe 18 Oktoba, 2010 Mheshimiwa Rais aliahidi kutengeneza kwa kiwango cha lami kipande hicho ndani ya Awamu ya Pili ya uongozi wake:-

(a) Je, Serikali inasemaje kuhusu ahadi hii ya Rais?

(b) Je, ni lini ujenzi wa kipande hicho utaanza?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Majaliwa, jibu kwa Mheshimiwa Selemani Said Bungara (Mheshimiwa Bwege)!

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Selemani Said Bungara, Mbunge wa Kilwa Kusini lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Mheshimiwa Rais mwezi Oktoba, 2010 alitoa ahadi ya kujengwa kwa kiwango cha lami, kipande cha kilomita 2.5 katika barabara ya Singino - Kwa Mkocho hadi Kivinje. Kazi ya kwanza iliyofanywa na Halmashauri katika kutekeleza ahadi ya Mheshimiwa Rais ni

kuifanyia usanifu barabara hiyo ambapo imejulikana kuwa zinahitajika shilingi bilioni 1.487 kwa ajili ya kujenga kilomita 4.5 ni zaidi ya ahadi ya Mheshimiwa Rais.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2013/2014, Halmashauri ilipelekewa shilingi milioni 350 ili kuanza ujenzi huo. Vile vile katika mwaka wa fedha 2014/2015, zilishatolewa shilingi milioni 500 ili kuendeleza pia ujenzi wa barabara hiyo ambapo kazi inayoendelea ni uwekaji wa changarawe. Katika mwaka wa fedha 2015/2016 tumetenga fedha jumla ya shilingi milioni 650 ili kukamilisha ujenzi huo tena kwa kiwango cha lami.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Rajab nilikuona!

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri labda nimuulize maswali madogo.

Mheshimiwa Waziri haoni kwamba kutokukamilisha ahadi ya Rais kwa kipindi cha miaka mitano kwa barabara ya kilomita 2.5 ambayo imeanzia Singino - Kwa Mkocho hadi Kivinje ni kuwahakikishia ama kuwathibitisha wananchi wa Kilwa kwamba Chama cha Mapinduzi na Serikali yake kupitia ahadi za Rais kimewadanganya na kimewaongopea na itakuwa ni njia sahihi ya kuwanyima kura CCM mwaka huu wa 2015?

Swali la pili, Mheshimiwa Waziri unaweza kuwahakikishiaje wananchi hawa kwamba shilingi milioni 650 ambazo zimebaki ambazo zimeshindwa kutolewa katika kipindi cha miaka mtano na hadi tunaingia kwa awamu ya Rais mwingine kweli zinaweza kupatikana fedha hizi ili zikafanyie kazi hiyo?

NAIBU SPIKA: Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Majaliwa!

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU): Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa umakini iliyonayo ahadi kama hii ya kilomita 2.5 tunaikamilisha tena kwa kilomita 4.5 siyo 2.5 za Mheshimiwa Rais, tumeongeza huduma zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo ni kuwahakikishia kwamba Serikali hii ni makini na Chama cha Mapinduzi kinatambua umuhimu wa miundombinu hasa ya barabara na tunatambua pia tatizo lililopo pale kati ya Singino na Kilwa Kivinje na kwa bahati nzuri nimepita nimeona kazi ile inaendelea vizuri.

Kwa hiyo, wananchi wa pale waamini kwamba ahadi ya Mheshimiwa Rais anapohidi inaweza kukamilishwa ndani ya kipindi chake na Mheshimiwa Rais anamaliza wakati wake, mwezi Oktoba na nimeeleza kwenye mpango wetu wa fedha za mwaka huu wa mwaka 2015/2016 ambao ndiyo unaanza Julai, tumetenga shilingi milioni 600. Mheshimiwa Mbunge, tupitishie bajeti hii ili tukakamilishe kazi hiyo na itakamilishwa kabla ya kipindi kile kwa sababu sasa tumeshafikia zaidi ya 75% kwa kuweka kiwango cha lami kilomita 4.5 zaidi ya ahadi ya Mheshimiwa Rais. Ndiyo uone kwamba Chama cha Mapinduzi kinafanya kweli katika kufanya kazi yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuwahakikishia wananchi wale kupeleka fedha hili halina shida, Bunge tulilonalo sasa ni la bajeti na tunatarajia Wabunge watatupitishia bajeti hii ili tufanye kazi za maendeleo katika maeneo yote bila kujali eneo hilo ni la mwana-CCM au mwana chama kingine cha siasa. Tunafanya kazi kwa Watanzania wote na kwa hiyo basi tutahakikisha tunapeleka hizo fedha na tutakamilisha hiyo kazi kwa kiwango cha lami ili wananchi waweze kusafiri kwa urahisi kutoka Kilwa Kivinje na kuja maeneo ya nje ya Kilwa Kivinje. Nashukuru sana.

NAIBU SPIKA: Nilikuona Mheshimiwa Mbunge wa Nkenge, swali la nyongeza!

MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi. Nina swali moja tu la nyongeza. Mheshimiwa Rais alipotembelea Jimbo la Nkenge wakati anakuja kuangalia utekelezaji wa Ilani si mbali sana mwaka jana, Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi alituhidi kwamba atatutengenezea barabara zetu ya kutoka Bunazi kwenda Minziro, kutoka Mishenye kwenda Luzinga na kutoka Kagera kwenda Kashenye na mbaya zaidi wananchi walikuwa wameelewa anaongelea lami, lakini kwa kuwa leo yupo ningetamani sana atuambie, je, hizi barabara zitatengenezwa kabla ya mwezi wa nane?

NAIBU SPIKA: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mheshimiwa John Magufuli!

WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa kwamba Mheshimiwa Rais alipotembelea maeneo anayoyataja Mheshimiwa Mbunge na hasa kutokana na ombi maalum lililotolewa na Mheshimiwa Mbunge kwa ajili ya kuwahudumia wananchi katika barabara zinazohusika Serikali iliahidi kuwa itazishughulikia barabara hizi zitengenezwe ili ziweze kupitika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu kesho ndiyo bajeti yangu nimwombe Mheshimiwa Mbunge asubiri tu kidogo, nataka kumhakikishia kwamba barabara hizo kama ambavyo ziliahidiwa na Mwenyekiti wa Chama

cha Mapinduzi na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, tutazitengeneza kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara. Kwa bahati nzuri katika bajeti ya mwaka huu fedha za Mfuko wa Barabara zimeongezwa na zitafika shilingi bilioni 866. (Makofi)

NAIBU SPIKA: Nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi. Tunaelekea Wizara ya Katiba na Sheria, swali ni la Mheshimiwa Sabreena Sungura na Mheshimiwa Machali kwa niaba yake.

Na. 71

Chuo cha Uongozi wa Mahakama

MHE. MOSES J. MACHALI (K.n.y. MHE. SABREENA H. SUNGURA) aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kukipa nguvu ya kisheria Chuo cha Uongozi wa Mahakama kuwa Chuo Maalum kwa ajili ya kuzalisha Mahakimu tu kama ilivyo Shule ya Sheria?

NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria, ningependa kujibu swali la Mheshimiwa Sabreena Hamza Sungura, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Uendeshaji wa Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto, Sura ya 405 inakipa chuo hicho mamlaka ya kutoa mafunzo endelevu kwa watumishi wote wa Mahakama ili kuwaongezea ujuzi katika utoaji wa huduma za Mahakama.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nimfahamishe Mheshimiwa Mbunge kwamba hakuna chuo hata kimoja kinachozalisha Mahakimu, bali vyuo vyote vinazalisha wahitimu wa Shahada za Sheria (LLB) ambapo mhitimu ataamua aidha kuajiriwa kama Hakimu au Wakili baada ya kukidhi masharti ya ajira husika.

NAIBU SPIKA: Jibu la kisayansi hilo. Mheshimiwa Machali una swali la nyongeza kwenye jibu hilo! Endelea.

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipa fursa niulize maswali mawili madogo ya nyongeza.

Swali la kwanza, kumekuwa na mchakato hapa nchini wa ku-phase out Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo ambao wana kiwango cha elimu cha cheti pamoja na diploma na hatimaye kuanza kuajiri wale wenye shahada ya kwanza na kuendelea. Ningependa kupata kauli ya Serikali, je, Chuo hiki cha

Mahakama bado kinaendelea ku-*train* Mahakimu wa ngazi ya cheti pamoja na diploma?

Swali la pili, kama bado chuo hiki kinaendelea ku-*train* Mahakimu hawa ambao pengine kumekuwa na *process* ya ku-*phase out*. Hamuoni kwamba pengine mna *misuse resource* za chuo hicho kwa kuendelea ku-*train* watu hawa ambao upande mmoja inaonekana hawatakiwi kulingana na wakati tulio nao. Nini mkakati wa Serikali kuhusiana na mambo haya?

NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Naibu Spika, niseme kwamba Chuo cha Uongozi wa Mahakama (IJA) Lushoto, kinatoa mafunzo ya aina mbili; mafunzo ya kwanza ni ya Cheti cha Sheria na Stashahada ya Sheria (diploma).

Mheshimiwa Naibu Spika, tunayo kampasi Lushoto na sasa hivi imefunguliwa kampasi Mwanza. Kwa hiyo, mafunzo yale bado yanaendelea na kama jana Mheshimiwa Mbunge alisikiliza vizuri bajeti yetu, mwaka huu tunatarajia kudahili wanafunzi zaidi ya 1,000. Chuo hicho sasa kinatumika kwa ajili ya kutoa mafunzo elekezi na mahsusi kwa Majaji, Mahakimu na watu wengine ambao wanataka labda kupata sasa ile *practical training* katika masuala mahsusi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe mfano katika mwaka huu ambapo Mheshimiwa Rais aliteua Majaji 20 wale wote licha ya kwamba tayari ni Majaji, lakini walikwenda pale wakakaa wiki tatu wakipikwa.

Kwa hiyo, hiyo ndiyo tofauti kwamba, chuo bado kinaendelea na taaluma hizi za cheti na diploma bado zinahitajika, watu hawa sasa wanaajiriwa kama Makarani wa Mahakama, lakini pia katika taasisi na idara mbalimbali za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo kauli ambayo naweza kuitoa ya Serikali ni kwamba, bado tunahitaji wataalam wa sheria katika ngazi ya cheti na diploma. Lakini Mahakimu kwa sasa hivi tunachukua watu wenye Shahada ya Sheria na sharti ni lazima upitie Shule ya Sheria ili kuweza kuajiriwa kuwa Hakimu.

NAIBU SPIKA: Tunaendelea Waheshimiwa Wabunge na Wizara ya Maji na swali linaulizwa na Mheshimiwa Daudi Mciwa Malole, Mbunge wa hapa hapa, kwa niaba yake Mheshimiwa Chibulunje.

Na. 72

Chanzo Kikuu cha Maji Dodoma Mjini – Mzakwe

MHE. HEZEKIAH N. CHIBULUNJE (K.n.y. MHE. DKT. DAVID M. MALLOLE)
aliuliza:-

Wananchi wa vijiji vya Gawaye, Mchemwa, Nzasa na Chihanga wanalinda chanzo kikuu cha maji (Mzakwe) lakini vijiji hivi havina maji:-

(a) Je, kwa nini wananchi hawa wanaojitolea kukilinda chanzo hiki cha maji nao wasipatiwe maji ya uhakika ili kuwapa moyo kwa kazi nzuri wanayoifanya?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha baadhi ya miundombinu ya maji kwenye baadhi ya vijiji vya Dodoma kama vile Mapinduzi, Nzuguni, Chololo, Mbabala, Ipala, Matumbulu na Nkulabi katika Kata ya Mpunguzi?

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. David Mciwa Mallole, Mbunge wa Dodoma Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli vijiji hivi vipo karibu na chanzo cha maji cha Mzakwe kwa kuwa Serikali inatekeleza programu ndogo ya maji na usafi wa mazingira vijijini, Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma ipo katika utekelezaji wa miradi ya maji katika vijiji 11 vikiwemo vya Gawaye, Mchemwa na Chihanga. Nia ya Serikali ni kuhakikisha wananchi wote mijini na vijijini wanapata huduma ya maji kutoka vyanzo mbalimbali vya maji kwa gharama nafuu.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, hatua za kuboresha miundombinu ya maji katika vijiji vya Kata ya Mpunguzi ni kama ifuatavyo:-

(i) Kupitia Halmashauri alipatikana mfadhili ambaye ni Shirika la Maendeleo la Uswisi lililofanya ukarabati kwenye vijiji vya Mapinduzi na Chololo ambapo kwa upande wa kijiji cha Mapinduzi bomba lilikarabatiwa na pampu zilinunuliwa na kufungwa na huduma ya maji inapatikana vizuri.

(ii) Kwa upande wa kijiji cha Ipala, Halmashauri ilifanya matengenezo ya kawaida ili kuhakikisha huduma ya maji inaendelea kupatikana.

(iii) Katika kijiji cha Nkulabi upembuzi yakinifu kwa ajili ya kufanya ukarabati unaendelea. Vijiji vya Nzasa, Mbalala na Matumbulu vimepewa

vipaumbele katika awamu ya pili ya utekelezaji wa Programu ya maendeleo ya sekta ya maji.

(iv) Kijiji cha Nzuguni kitapatiwa huduma ya maji kutoka Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mjini Dodoma (DUWASA) na kazi ya ulazaji wa bomba kuu imekwishafanyika.

MHE. HEZEKIAH N. CHIBULUNJE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili ya nyongeza. Kwanza, nataka nishukuru sana kwa majibu ya Serikali kuhusu mipango ya maji katika vijiji hivi vilivyotajwa. Kwa vile vijiji hivi vinavyozunguka mradi wa chanzo cha maji cha Mzakwe kwa muda mrefu vimekuwa havina maji na Waziri amesema kwamba, tayari mipango ipo ya kuwapatia maji vijiji hivi vya Nzasa, Chihanga na vinginevyo, nataka nijue ni lini hasa mpango wa kuvipatia maji hivi vijiji vinavyozunguka mradi wa maji wa Mzakwe utatekelezwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, katika Jimbo langu la Chilonwa pale katika Kijiji cha Wilunze uko mradi wa maji ambao ni wa muda mrefu sana kupitia ahadi ya vile Vijiji Kumi mpaka sasa haujatekelezwa, ni lini maji yatakwenda pale Wilunze?

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza kama nilivyosema katika jibu langu la msingi ni kwamba, vijiji hivi viko kwenye chanzo, lakini pia viko katika mpango wa vijiji 11 ambako unatekelezwa na vijiji hivi viko katika hatua mbalimbali za utekelezaji na kadiri fedha itakavyopatikana tutaendelea kuvikamilisha na vile ambavyo havipo, basi tutatekeleza katika awamu ya pili ya programu ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kijiji alichokitaja katika Jimbo lake huko Chilonwa, nimwahidi Mheshimiwa Mbunge tu kwamba, kadiri fedha zitakapopatikana tutaendelea kutekeleza na kama itashindikana basi katika programu inayofuata tutatekeleza.

NAIBU SPIKA: Nakushukuru sana. Tunaendelea na Swali la Mheshimiwa Rebecca Michael Mngodo. Mheshimiwa Selasini kwa niaba yake.

Na. 73

Tatizo la Maji Kuwa na Fluoride Nyingi – Meru

MHE. JOSEPH R. SELASINI (K.n.y. MHE. REBECCA M. MNGODO) aliuliza:-

Baadhi ya wananchi waishio katika Wilaya ya Meru, Kata ya Maji ya Chai na maeneo ya Ngurdoto wanapata athari mbaya ya afya ya kuwa na meno

yenye rangi ya *brown* na miguu ya matege kutokana na maji kuwa na *fluoride* iliyoziidi; na ni wajibu wa Serikali kuhakikisha kuwa wananchi wake wanapata maji safi na salama kutokana na kodi wanazolipa:-

Je, Serikali imefanya nini kukabiliana na tatizo hilo la ongezeko la *fluoride* kwenye maji katika eneo hilo?

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Rebecca Michael Mngodo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, vyanzo vya maji vyenye madini mengi ya *fluoride* vinapatikana katika mikoa kadhaa ya nchi yetu. Mikoa iliyoathirika zaidi na madini hayo ni pamoja na Kilimanjaro, Manyara, Singida, Mwanza na Arusha. Katika jitihada za kukabiliana na hali ya viwango vikubwa vya madini ya *fluoride* kwenye maji ya kunywa, Wizara inaendesha zoezi la kuhakiki ubora wa maji katika vyanzo vya maji ili kubaini vyanzo vilivyoathirika pamoja na kufanya utafiti wa jinsi ya kupunguza madini ya *fluoride* katika maji ya kunywa kwa kutumia teknolojia rahisi na ya gharama nafuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Wilaya ya Meru jumla ya vyanzo 121 vimebainishwa na kuhakikiwa ubora wake na matokeo yameonesha kuwa asilimia 55 ya vyanzo vya maji vilivyokaguliwa vina viwango vya *fluoride* chini ya miligramu nne kwa lita moja ya maji inayokubalika Kitaifa. Hii ni pamoja na vyanzo vya maji vya miradi ya Vijiji Kumi vya Halmashauri ya Meru. Wizara ikishirikiana na Halmashauri husika itaendelea kuhamasisha utumiaji wa vyanzo vyenye madini ya *fluoride* yanayokidhi viwango na inapobidi teknolojia iliyoifanywa utafiti *Bonechar* itumike katika maeneo ambayo maji yake yana madini mengi ya *fluoride*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ikishirikiana na Kampuni ya Utafiti wa Uboora wa Maji ya Kimarekani, imefanya majaribio ya kuondoa kemikali za sumu na vimelea vya magonjwa katika maji. Utafiti huo umefanywa kutumia mitambo ya kisasa inayotumia nishati ya jua inayoweza kutumika katika ngazi ya jamii kwa maeneo ya mijini na vijijini.

Mitambo hiyo imefanywa majaribio katika Kituo cha Utafiti Ngurdoto na imeweza kuondoa madini ya *fluoride* katika maji kutoka kiasi cha miligramu 20 kwa lita hadi kufikia miligramu 0.06 katika lita moja ya maji. Shirika la Afya Duniani limeweka kiwango salama cha *fluoride* kwenye maji kuwa miligramu 1.5 kwa lita ya maji. Serikali inafanya utaratibu wa upatikanaji wa mitambo hiyo ili iweze kutumika katika miradi ya maji itakayotekelezwa katika maeneo yenye matatizo ya madini ya *fluoride*.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Selasini nilikuona swali la nyongeza!

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa kushirikiana na Mbunge wa Rombo imefanya jitihada kubwa sana za kutatua tatizo la maji katika Wilaya ya Rombo, hususan Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wametembelea mara kadhaa katika Jimbo langu kwa ajili ya kuhakikisha tumetatua tatizo la maji na kufanikisha kuchimba visima katika Kijiji cha Kahe, Leto, Ulauri, Mahorosha, Msalanga, Kiraeni, Shimbi Mashariki, Ngareni, Ngoyoni na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya visima hivi ambavyo tayari maji yamepatikana bado miundombinu haijajengwa. Ningependa kujua ni lini sasa Serikali itapeleka fedha ili miundombinu iweze kutengenezwa ili wananchi wapate faida inayotokana na miradi hii?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, Mheshimiwa Rais alipotembelea Wilaya ya Rombo kwa ajili ya ufunguzi wa Barabara ya Tarakea – Mkuu, wananchi wa Rombo walimwomba kabla ya kumaliza kipindi chake aweze kuwezesha kupatikana kwa marambo katika ukanda wa chini wa Jimbo la Rombo ili kuweza kuinga maji ya mvua ambayo yanatiririka kutoka milimani kwenda nchi jirani ya Kenya wapate kuyatumia kwa ajili ya shughuli za wanyama na binadamu. Ningependa kujua ni lini sasa Serikali itatekeleza ahadi hii ya Rais?

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge kila mara Mheshimiwa Selasini aliposema habari ya Rombo naona mnatabasamu, kuna nini Rombo? Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu ya swali hilo. *(Kicheko)*

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimshukuru kwa kutambua na kushukuru jitihada ambazo Serikali imefanya na tumeshirikiana nae na amekuwa mfuatiliaji mzuri sana na hatimaye tumeweza kufikia hatua ya kuchimba hivyo visima.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimwahidi tu Mheshimiwa Mbunge na hata Bunge lililopita nilikuwa nimemwahidi kwamba, tutaweza kufika kule lakini tutakapopata fedha tu ni lazima tujenge miundombinu katika visima hivyo ambavyo tumeshavichimba.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, ni kuhusu ahadi ya Mheshimiwa Rais. Nataka niseme tu kwamba, kila ahadi ya Mheshimiwa Rais imeratibiwa na imewekwa na ni lazima itekelezwe. Nataka nimwahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba, kupitia Bunge hili bajeti itakayokuja tutalitambua hilo kama bado fedha hazijapatikana, tutaendelea kuifuatilia na kuendelea kuifuatilia na

kuhakikisha kwamba tunatekeleza. Hizo ni ahadi za chama sasa Mheshimiwa Mbunge asiwe na wasiwasi.

NAIBU SPIKA: Rafiki yangu Mheshimiwa Kombo, kwanza pole sana, swali la nyongeza! (Kicheko)

MHE. MUSA HAJI KOMBO: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana hasa kwa muda mrefu kwa kutomuona rafiki yako Kombo. (Kicheko)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa maamuzi ya 2020 Millennium nchi iliweka ahadi kwamba, itakapofika mwaka 2020 nchi hii watu watakuwa wanapata maji safi na salama, lakini kutokana na matatizo haya makubwa sana yaliyopo katika nchi yetu, hebu Mheshimiwa Waziri atueleze hali halisi ikoje ya msimamo huu na maamuzi haya ya nchi.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, nikubaliane naye kwamba mipango hiyo ilikuwepo na inaendelea kutekelezwa na kila muda inafanyiwa tathmini.

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo maeneo ambayo iwe katika afya, miundombinu au maji, tumeendelea kutekeleza, lakini sisi Wizara ya Maji katika kufikia malengo hayo ndiyo maana Wizara yetu ilikuwa miongoni mwa vipaumbele kwa kutambua umuhimu wa huduma ya maji na tumetekeleza kwa kadri inavyowezekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, malengo hayo hata kama hayajafikiwa basi ni ukosefu wa fedha, lakini nia ya Serikali ni kuendelea kutekeleza malengo hayo kwa kuhakikisha kwamba, tunawafikia wananchi na wanapata huduma ya maji na hata bajeti yetu tutakayowasilisha imelenga katika kutimiza malengo hayo.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tuendeleee na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, swali la Mheshimiwa Abdalla Haji Ali, Mbunge wa Kiwani.

Na. 74

Mkakati wa Kuondoa Ajali Barabarani

MHE. ABDALLAH HAJI ALI aliuliza:-

Pamoja na juhudi kubwa za Jeshi la Polisi (Usalama Barabarani) kupambana na ajali nchini, bado ajali zimekuwa zikiongezeka kila siku:-

(a) Je, Serikali ina mkakati gani mahususi wa kuondoa tatizo hili?

(b) Je, ni nini sababu ya ajali zinazotokea mara kwa mara?

(c) Je, ni Watanzania wangapi waliopoteza maisha kutokana na ajali za barabarani kuanzia Januari, 2014 hadi Novemba, 2014?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu Swali la Mheshimiwa Abdalla Haji Ali, Mbunge wa Kiwani, lenye sehemu (a), (b) na (c), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na athari kubwa za ajali za barabarani kwa Taifa, Serikali ina mikakati madhubuti ya kupambana na tatizo hili. Mikakati hiyo ni pamoja na kuongeza wigo wa elimu ya usalama barabarani kwa watumiaji wa vyombo vya moto kwa njia za redio, luninga, machapisho na vipeperushi.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, mikakati mingine ni kuboresha mifumo ya utendaji kazi katika maeneo ya ukaguzi wa mabasi na malori, mfumo wa ufuatiliaji wa magari barabarani (*car tracking system*) na mfumo wa utoaji nukta katika leseni za Madereva utakaodhibiti tabia za madereva wazembe. (*Makofi*)

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, tafiti za kisayansi zinaonesha kuwa, ziko sababu kuu tatu zinazosababisha ajali; ya kwanza ni makosa ya kibinadamu yanayochangia asilimia 74 ya ajali zinazotokea. Pili, ubovu wa vyombo vya usafiri, unachangia asilimia 12 na hali ya miundombinu ya barabarani ambayo inaweza kuchangia asilimia 14.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kipindi cha Januari hadi Novemba, 2014 jumla ya Watanzania 3,528 walipoteza maisha kutokana na ajali na 14,137 kujeruhiwa katika ajali 2,887 zilizotokea.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Abdalla Haji Ali, swali la nyongeza!

MHE. ABDALLAH ALI HAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, nina maswali mawili madogo ya nyongeza. Mheshimiwa Waziri katika jibu lake la msingi amesema 74% ya ajali barabarani zinasababishwa na makosa ya kibinadamu, lakini hakuyataja ni makosa gani hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, inasemekana kuwa baadhi ya madereva wanaokwenda mikoani wanapokuwa nje ya Dar es Salaam huwaachia Makondakta wao usukani kusaidiwa kazi jambo ambalo linaweza kusababisha ajali.

Je, Serikali inawashughulikiaje madereva wenye tabia hii? Ahsante.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza, nimesema kwamba makosa 74% yanatokana na chanzo cha binadamu, binadamu ambaye anaendesha gari, baadhi yao huamua kunywa pombe, dereva anapokunywa pombe ni sehemu ya 74% ya ajali zinazotokea, lakini pili, ni maamuzi anayoyafanya katika kuendesha kwake. Anapoamua ku-over take gari sehemu ya mlima, haoni mbele au kuna gari, haoni kinachokuja kwenye cross na kadhalika, haya ni jumla ya makosa ya binadamu.

Kwa hiyo, tukiyadhibiti haya na hapa ni lazima niseme kwamba kuna baadhi ya watu wanapuuza tunaposema kwamba tukiwashughulikia madereva, tukiwaweka sawa ajali zitapungua. Tukielewana na madereva na wakafuata Sheria ambazo zinatakiwa, kwa kweli ajali 74% tunaweza kupunguza kwa ajili hiyo tu. Kwa hiyo, tushirikiane ili hili liweze kutimia.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili lilikuwa linahusu kubadilishana madereva kwa kupewa makondakta, Jeshi la Polisi la Usalama barabarani huwa mabasi yanapoondoka yanahakikisha kwamba madereva wale ambao wanapewa magari wana sifa. Linalotokea katikakati ya barabara ni taabu kulijua lakini pia kuna utaratibu ambao tumeupanga wa kuhakikisha kwamba sifa za dereva, picha zake na kadhalika zinatangazwa kwenye magari, kwa hiyo, abiria wanaweza kutusaidia sana kusema kwamba abiria ametoka na ameingia nani, tumeshatangaza namba ambazo wanaweza kutumia kwa ajili hii na tuko tayari kusaidiana kuondoa kadhia hii ya kupoteza wenzetu.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim, lakini kama utaanza na taarifa tutashukuru, endelea na swali.

MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana na nina swali moja dogo la nyongeza. Maelezo ya Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kwamba, abiria wanaweza kutusaidia kwa kutoa taarifa kuhusu tabia za madereva wetu. Huu ni ulimwengu wa sayansi na teknolojia, mara nyingi hapa Bungeni Serikali imekuwa ikisema kwamba unaandaa mpango wa kuweka *CCTV camera* ili kutambua madereva wenye tabia hizi mbaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili limekuwa likiachiwa na mara nyingi mmesema kwamba hakuna fedha za kutosha, lakini vifo vimekuwa vinaongezeka siku hadi siku. Inaonekana bado Serikali haijafilia maanani suala hili la kupunguza ajali barabarani, Mheshimiwa Naibu Waziri atuambie mkakati hasa wa ziada ule mliotuhidi kwamba mtaweka *CCTV camera*. Je, ni lini zitapatikana na kuwekwa katika maeneo yote Tanzania?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Masoud hujatupatoa taarifa lakini, Mheshimiwa Niabu Waziri majibu!

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri nisisitize kwamba abiria wana mcnango mkubwa kuliko *camera* na hili tulijue kwamba Abiria ambaye anaona kinachotokea atatupa taarifa na zitakuwa za uhakika na wazi na zimesikia kuliko kutegemea *camera*. Sitaki nipuuze *camera*, *camera* tuna mpango wa kuziweka, lakini *CCTV camera* za kwenye magari kwa maana hasa ni *car track system* tunaweka mtambo ambao utakuwa unaangalia ni nini kinatokea speed ya *driver* wakati watu wako ofisini na kwenye gari kutakuwa na *gadget* ambayo itasaidia ili kurusha ile taarifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi, katika mikakati yetu ya karibuni ya kutekeleza ni hiyo kuweka *car tracking system* ambayo itatupa taarifa ya kila kinachotokea kwa dereva na kwenye basi la abiria.

NAIBU SPIKA: Tunaendelea na swali linalofuata kwenye Wizara hii hii, nalo linauliozwa na Mheshimiwa Profesa Peter Mahamudu Msolla, Mbunge wa Kilolo.

Na. 75

Ongezeko la Ajali za Magari

MHE. PROF. PETER M. MSOLLA aliuliza:-

Katika siku za hivi karibuni kumekuwepo na ongezeko kubwa la ajali za magari barabarani na kusababisha vifo, majeraha na upotevu wa mali:-

Je, Serikali inatoa kauli gani kuhusiana na matukio haya?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Peter Mahamudu Msolla, Mbunge wa Kilolo, kama ifuatavyo:-

Nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa kumekuwepo na mfululizo wa ajali mbaya kati ya mwezi wa Machi na Aprili mwaka huu ambazo zimesababisha vifo na majeruhi wengi. Hata hivyo, takwimu za jumla zinaonesha kupungua kwa ajali za barabarani ambapo kwa kipindi cha Januari hadi Aprili, 2015 yalikuwa ni matukio 2,718 ya ajali zote ukilinganisha na ajali 6,050 zilizotokea katika kipindi kama hicho mwaka 2014.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, utafiti unaonesha kuwa vyanzo vya ajali hapa nchini ni pamoja na makosa ya binadamu, uchakavu wa vyombo na ubovu wa miundombinu ambayo inachangia asilimia 7.3. Serikali kupitia Jeshi la Polisi, Kikosi cha Usalama Barabarani kinachukua hatua mbalimbali kukabiliana na ajali ili vifo na majeruhi yasiyo ya lazima yasitokee. Miongoni mwao:-

(i) Kutoa elimu ya umma kwa kushirikisha wadau mbalimbali wakiwemo abiria au wasafiri kuhusu usalama wa barabarani, elimu hiyo hutolewa kwa kupitia vyombo mbalimbali vya mawasiliano na kwenye mikusanyiko ya watu kama vile sherehe za maadhimisho ya Wiki ya Nenda kwa Usalama Barabarani.

(ii) Kupanga askari wa doria katika maeneo tete kwa ajali na kuongeza vitendea kazi vya kisasa vya kubaini makosa ya usalama barabarani na kuwadhibiti madereva wanaovunja Sheria.

(iii) Kuboresha Sheria na Kanuni mbalimbali za usalama barabarani zikiwemo Kanuni zinazowataka wamiliki wa magari ya mizigo kuweka viakisi mwanga na pia Kanuni zinazomtaka dereva kupata elimu ya udereva inayolingana na aina ya gari analopaswa kuendesha ili kuleta ufanisi katika taaluma hiyo.

(iv) Kuendelea kudhibiti makosa au mwenendo hatarishi wa madereva kama vile mwendo kasi, ulevi na kutokufuata ratiba ya mabasi ya abiria vitendo ambavyo huchangia ajali kwa kiwango kikubwa, kazi hii hufanywa kwa njia ya doria ya pamoja kati ya kikosi cha usalama barabarani na Mamlaka ya Udhubiti wa Usafiri wa baharini na nchi kavu yaani *SUMATRA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatoa wito kwa kila mtumiaji wa barabara kuhakikisha anawajibika kikamilifu kwa nafasi yake kwa kuzingatia utii wa Sheria bila ya shuruti, kukemea uvunjifu wa sheria na kutoa taarifa dhidi ya vitendo dhidi ya uvunjaji wa Sheria ili kuhakikisha barabara zetu zinakuwa salama na kuepusha madhara ya ajali.

MHE. PROF. PETER M. MSOLLA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu ya Naibu Waziri, lakini kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amekiri kwamba vyanzo vikuu vya ajali ya magari barabarani ni pamoja na mwendo mkali na ulevi wa madereva na hapo nyuma Serikali ilikuwa imeanza utaratibu wa kufunga *speed governor* ili kupunguza mwendo. Je, Serikali imefikia wapi katika zoezi hili ili kupunguza idadi ya ajali?

Pili, kuhusu ulevi, Mheshimiwa Naibu Waziri hakuzungumza namna wanavyokabiliana na tatizo hili. Katika nchi zingine kuna namna ya kuwachunguza madereva kama wamezidisha kunywa pombe kwa kutumia

breathalyzer, je, Serikali yetu inatumiaje utaratibu huu ambao kwenye nchi zingine umeonesha kuwa umekuwa na mafanikio makubwa sana?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba kulikuwa na mpango wa kupunguza *speed* za madereva kwa kutumia *speed governor*. Mpango huu ulifaa pale mwanzoni, lakini utaalim ambao ulikuja kwa madereva na wamilikiwa wa magari ukafanya mpango wote huu kutokuwa na maana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo ambayo tunayafanya sasa hivi kuhakikisha kwamba tunai-govern *speed* kama nilivyosema ni mpango huo wa *car tracking system* ambao tutauweka, lakini pia tunatumia *camera* kwa ajili ya kupima mwendo kasi wa madereva na pia kuna *patrols* ambazo zinafanyika katika maeneo mbalimbali ambayo yana *check* kwamba madereva wanafuata taratibu za mwendo ambazo zimeoneshwa kwenye barabara wanazotumia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ulevi ni kweli kwamba ulevi unasababisha mambo mengi na haikukosewa kuitwa ni baba wa maafa. Sasa hili ni tatizo kubwa kwa sasa tunachofanya ni kwamba kabla dereva hajakalia usukani kutoka katika kituo chake tunatumia vipima ulevi ambavyo tukiona ana dalili ya kuwa ameongeza chochote anakuwa haruhusiwi kuendesha basi na wamiliki wanalazimika kumtafuta mwingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni kwamba, kama tunamkuta katikati ya Barabara amelewa, adhabu ambayo tunampa ni kuhakikisha kwamba tunamnyang'aya leseni asiwe dereva wa gari la abiria pengine anaweza kuendesha familia yake tu.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na swali la Wizara ya Ujenzi linaulizwa na Mheshimiwa Said Amour Arfi.

MHE. SAID A. ARFI: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi baada ya siku 900 tangu nimewasilisha swali hili katika Ofisi yako, sasa leo Serikali itoe majibu.

Na. 76

Ujenzi wa Barabara ya Mpanda – Uvinza

MHE. SAID A. ARFI aliuliza:-

Je, ni lini barabara ya kutoka Mpanda hadi Uvinza itajengwa kwa kiwango cha lami ili kuunganisha Mikoa ya Rukwa, Katavi na Kigoma?

NAIBU SPIKA: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Mhandisi Lwenge.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Said Amour Arfi, Mbunge wa Jimbo la Mpanda Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Mpanda Uvinza yenye urefu wa kilomita 194 ni sehemu ya barabara kuu ya Tunduma-Sumbawanga-Mpanda-Uvinza-Kasulu-Nyakanazi. Katika Bajeti ya mwaka wa fedha 2014/2015, Serikali imetenga sh. 4,539,210,000 kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Mpanda - Uvinza ambapo awamu ya kwanza itahusisha sehemu ya barabara kutoka Mpanda – Usimbili yenye urefu wa kilomita 30. Zabuni kwa ajili ya kumpata Mkandarasi wa Ujenzi wa barabara hiyo imetangazwa na uchambuzi wa zabuni unaendelea kwa ajili ya kuanza barabara husika kwa kiwango cha lami.

NAIBU SPIKA: Swali la nyongeza, Mheshimiwa Arfi!

MHE. SAID A. ARFI: Mheshimiwa Naibu Spika, ukijua ulikotoka unakuwa na sababu za kusema, sina budi kwanza kuipongeza Wizara hii ya ujenzi, nakumbuka mwaka 2005, nilipoingia kwa mara ya kwanza katika Bunge hili, Mikoa ya Kanda ya Magharibi kwa maana ya Tabora, Kigoma, Katavi na Rukwa ilikuwa haikifikiki kwa barabara za lami leo angalau tumeona dalili za kuwepo hizo barabara za lami, ni lazima tuwashukuru kwa yule ambaye anaweza kushukuru na muungwana, basi nasema ahsante sana angalau mmeweza kutufanyia hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nina maswali mawili ya nyongeza. La kwanza, wakati Wizara ikijibu swali hili ambalo liliulizwa na Mheshimiwa Kakoso, Mbunge wa Mpanda Vijijini, alisema kwamba barabara hii itajengwa kuanzia Mpanda mpaka Vikonge, umbali wa kilomita 35. Katika majibu ya Mheshimiwa Waziri hapa anasema itajengwa kutoka Mpanda mpaka Usimbili kwa umbali wa kilomita 30.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nashindwa kujua hiyo tofauti ya kilomita 35 na 30, lakini pia Usimbili ni eneo ambalo halifahamiki ni *Chiefdom*, ni Utawala wa Kichifu wa Mtemi Nsipata Mtemi, ambaye ni marehemu, Utawala ule ulikuwa unaitwa ni Utawala wa Usimbili. Sasa hii Usimbili naomba Mheshimiwa Waziri aniambie ni eneo gani mahususi katika barabara hiyo?

Swali la pili, pamoja na jitihada hizo nzuri ambazo zimefanywa na Wizara hii, bado kuna malalamiko ya fidia katika eneo la kutoka Mpanda Mjini mpaka

Stalike, je, sasa unaweza kutusaidia kwa mpango maalum kabisa kuwaondoa katika kero hii wananchi na hususan wapiga kura katika eneo la Mpanda Mjini?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nizipokee pongezi ambazo ametoa kwa Serikali ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa suala la barabara ya Mpanda – Usimbili, kilomita 30 au 35, tunachokifanya ni kwamba, barabara yote tunakuwa tumeweka katika vitu vinitwa *Lots* au *packages*, kwa hiyo, kilomita hizi zisikupe shida Mheshimiwa Mbunge, ni kwamba hiyo sehemu itakayoendelea ni lazima itaanzia pale ambapo waliishia katika *lot* ya kwanza. Hili suala la jina unalolisema hili tutakwenda ku-check tuone hali halisi hapo kwenye kilomita 30 panaitwa vipi, lakini tulifikiri tukitaja jina hili Mheshimiwa Mbunge utaweza kuelewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika suala la pili kuhusu malalamiko ya fidia, kama tulivyokwishatangaza kwamba malipo ni lazima yazingatie Sheria ya Barabara ambayo tumeiweka namba 13 ya mwaka 2007, kwamba watu ambao barabara imewafuata, ni lazima walipwe fidia kwa mujibu wa Sheria na wale ambao wako ndani ya Hifadhi ya barabara hawawezi kulipwa kwa mujibu wa Sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, masuala ya fidia siku zote yamekuwa, watu wakishapata fedha mara nyingi ndiyo wanaanza kulalamika kuwa fedha hazitoshi, lakini fedha zile tunalipa kulingana na Sheria iliyopo kwa sasa. Kwa hiyo, kama kuna mambo mengine ya ziada ambayo yanahusiana si kwa viwango, haya tutakwenda kuyaangalia.

MHE. ABDALLAH A. NJWAYO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili niulize swali la nyongeza kwenye swali hili namba 76 la Mheshimiwa Said Arfi, lakini kabla sijafanya hivyo naomba kwanza kuushukuru uongozi wa Bunge na wadau wote waliowezesha kunipeleka hospitali ya Apollo, India kupata matibabu ya goti, nimerudi salama, afya yangu inaendelea kuimarika. Pia nawashukuru wananchi wa Tandahimba ambao mara nyingi wamekuwa wakifuatilia afya yangu na kuniombea nipone, tuko pamoja na kazi ya kutekeleza llani ya CCM, tutaendelea kuifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo naomba sasa kuuliza swali dogo. Kwa kuwa tatizo la kuunganisha barabara Mpanda hadi Uvinza linafanana sana na tatizo lililopo kati ya Mtwara, Tandahimba, Newala hadi Masasi na kwa sababu ahadi ya Rais ilikuwa kabla hajatoka madarakani barabara hiyo itajengwa kwa kiwango cha lami na katika kikao cha RCC cha mwisho cha Mkoa wa Mtwara tulitangaziwa kwamba barabara sasa itaanza kujengwa kilomita 50, ningepena kujua jambo hili limefikia wapi sasa? Ahsante.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli barabara anayoisema kutoka Mtwara – Tandahimba – Masasi ni ahadi ya Rais na tumeahidi katika bajeti hii kwamba tungeweza kuanza kujenga kilomita 50. Taratibu za kuanza mchakato wa kuanisha usanifu ili tuweze kutangaza tenda ile, ziko katika hatua za mwisho. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba barabara hii itanza kujengwa kama tulivyoahidi.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kakoso, nilikuona!

MHE. MOSHI S. KAKOSO: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa barabara ya Mpanda kwenda Uvinza kwa kiwango cha lami inajenga kilomita 35, eneo hili limekuwa ni chakavu sana kwa kupisha ujenzi wa kiwango cha lami. Je, Serikali ina mpango gani wa kufanya matengenezo ya dharura kutoka Mpanda mpaka maeneo ya Vikonge, ili iweze kupitisha magari kwa urahisi kwa sababu hii ni mbaya sana? Naomba kujua.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hiyo anayoisema tutaitengeneza kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara. Kwa hiyo, katika mwaka huu wa fedha tumetenga fedha kwa ajili ya kufanya hayo matengenezo maalum ili kusudi barabara hiyo iweze kupitika. Namwagiza Meneja wa TANROAD wa Mkoa wa Katavi aanze hiyo kazi mapema iwezekanavyo.

NAIBU SPIKA: Swali la mwisho kwa siku ya leo. Swali la Mheshimiwa Al-Shaymaa Kwegyir, kwa niaba yake Mheshimiwa Omari Rashid Nundu!

Na. 77

Ujenzi wa Barabara ya Bagamoyo- Msata

MHE. OMARI R. NUNDU (K.n.y. MHE AL-SHAYMAA J. KWEGYIR): Barabara inayoendelea kujengwa kutoka Bagamoyo hadi Msata imechukua muda mrefu sana kukamilika hasa kipande kinachounganisha Mto Ruvu:-

(a) Je, ni kitu gani kinakwamisha kukamilika kwa barabara hiyo na ni lini sasa itakamilishwa?

(b) Je, Serikali inawajibika vipi na hasara inayotokana na ucheleweshaji wa kukamilika kwa barabara hiyo?

(c) Je, ni fedha kiasi gani zimetumika mpaka sasa katika jumla ya gharama ya ujenzi wote wa hiyo barabara?

NAIBU SPIKA: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Ujenzi, Engineer Lwenge!

NAIBU WAZIRI WA UJENZI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Al-Shaymaa Kwegyir, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c), kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Bagamoyo - Msata. Yenye urefu wa kilomita 64 unatekelezwa katika awamu mbili ambapo awamu ya kwanza ilihusisha ujenzi wa kilomita sitini ambao kwa sasa umekamilika kwa asilimia 98.2. Kazi pekee iliyobaki ni ujenzi wa mizani ya kupimia magari eneo la Makofia.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha awamu ya pili ya mradi huu ni ujenzi wa Daraja kubwa la Ruvu Chini, Daraja la Kariakoo na Madaraja mengine katika Bonde la Mto Ruvu lenye urefu wa kilomita nne. Kutokana na Bonde la Ruvu kuwa na udongo wa mfinyazi, Mkandarasi anafanya kazi kwa umakini ili kupata ubora unaotakiwa kimkataba. Kazi katika Bonde hili inatarajiwa kukamilika Machi, 2016. Hivyo, hakuna ucheleweshaji wowote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile hakuna ucheleweshaji wowote mpaka sasa, hakuna hasara kwani kilomita 60 za awamu ya kwanza zimekamilika na zinatumiwa kwa magari yanayotoka na yanayokwenda Msata na awamu ya pili inayohusisha ujenzi katika Bonde la Ruvu chini inaendelea vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa mradi huu utakapokamilika kwa awamu zote mbili utagharimu jumla ya shilingi bilioni 125.68.

MHE. OMARI R. NUNDU: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kutoa jibu ambalo ni zuri na ni la uhakika. Pia niungane na Mheshimiwa Arfi kuipongeza Serikali kwa jumla kwa maendeleo ya barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika barabara hii kuna faida mbili ambazo zinaonekana wazi, naitumia barabara hiyo kwa sasa hivi. Kwanza inatupunguzia urefu; pili utaona maendeleo ambayo yanatokea kwa kasi kubwa sana na tatu ni barabara ambayo inakufanya ufike Dar-es-Salaam kwa wakati mfupi. Hata hivyo, kuna tatizo moja ambalo ningependa nijue kama Serikali wanalijua na pengine sio barabara hiyo tu, lakini barabara nyingine zote kuliko ambako hakukuwa na barabara kabla ya sasa.

Kuna taarifa kuwa unaposafiri kwenye barabara ile alfajiri sana au jioni sana, kunakuwa na majambazi. Nataka kujua kama Serikali wanalijua hilo na kama wanalifanya kazi. Hilo ni swali langu la kwanza.

Swali la pili, barabara pacha ya barabara hiyo ni barabara kutoka Bagamoyo mpaka Tanga. Sasa tumeambiwa barabara hii inamalizika Machi mwaka kesho. Tungependa kujua pia barabara ile ya kutoka Tanga mpaka Bagamoyo hasa kwa kipande kile cha kutoka Tanga mpaka Pangani ambacho ni kilomita hamsini tu, kitaanza lini na kitamalizika lini? Ahsante sana.

WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la kwanza la majambazi barabarani, kazi ya Wizara ya Ujenzi ni kutengeneza barabara. Kwa hiyo, nafikiri Wizara inayohusika na majambazi watamjibu vizuri. (Kicheko)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la barabara la kilomita 178 kutoka Tanga kuja Bagamoyo, ile barabara ipo ndani ya ufadhili wa Afrika Mashariki na zimetengwa dola milioni mia mbili, ambazo zitahusisha kujenga barabara hiyo kutoka Bagamoyo kwenda Tanga, hadi Malindi upande ule wa Kenya. Kazi za *feasibility study* na *detailed design* zimemalizika. Kwa hiyo, hatua za mwisho za kuhakikisha kwamba Kandarasi anapatikana kwa ajili ya kujenga barabara ile ambayo nayo ni *shortcut* na ina faida kubwa na inafadhiliwa na *African Development Bank* ziweze kufanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kumalizika kwa barabara hii nataka kumhakikisha Mheshimiwa rafiki yangu, babu yangu, kwamba barabara hii ilikuwa imejengwa kwa awamu mbili. Awamu ya kwanza ni ile ya kilomita 64 ambazo zipo katika hatua ya mwisho kama alivyojibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

Awamu ya pili, ni ile ambayo inahusisha kwenye lile daraja, ambapo kama umepitia hivi karibuni, hata lile daraja la Kariakoo ambalo lina mita zaidi ya 85, lipo kwenye hatua ya *deck*, pamoja na madaraja mengine yale matano yameshaanza kujengwa na Mkandarasi anafanya kazi vizuri sana. Nataka kuwahakikishia Waheshimiwa wote kwamba barabara hii itakamilika kama ambavyo imepangwa.

NAIBU SPIKA: Nilikuona Mheshimiwa Diana Chilolo, swali la nyongeza!

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa kuwa Serikali imekuwa ikifanya kazi nzuri sana ya kutengeneza barabara kwa kiwango cha lami karibu nchi nzima, lakini imekuwa haina utaratibu wa haraka wa kufanya *maintenance* pale barabara inapopata mashimo, mfano, barabara ya Singida kwenda Shelui. Je, Serikali itakuwa na utaratibu sasa wa kupeleka hela katika Mameneja wa *TANROADS* kwa ajili ya *maintenance* kila wakati?

NAIBU SPIKA: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri Ujenzi!

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze kwa namna ambavyo anafagilia utengenezaji wa barabara. Ndiyo maana Serikali ilianzisha Mfuko wa Barabara ili tuhakikishe kwamba barabara zetu tunazozitengeneza kwa kiwango cha lami ziweze kupata matengenezo stahiki na kwa muda unaotakiwa. Kwa hiyo, nimhakikishe Mheshimiwa Diana Chilolo kwamba, maeneo yale ambayo barabara imeanza kuharibika, Serikali itapeleka fedha kwa Mameneja wa Mikoa ili waweze kufanya matengenezo ambayo yanatakiwa kutengenezwa na barabara ile iweze kupitika muda wote.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Betty Machangu, nilikuona!

MHE. BETTY E. MACHANGU: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Napenda kuulizia kwamba barabara zinajengwa na hususan Dar-es-Salaam kwa mfano na mitaro ile inayojengwa na hizi barabara haifunikwi, mwisho wa siku takataka nyingi zinaingia kwenye hii mitaro na wakati wa mafuriko tulishuhudia sisi wenyewe Dar-es-Salaam. Sasa nataka niulize, kwa nini wanajenga bila ya kufunika hii mitaro? Ni *substandard* au ndiyo makubaliano au ni Makandarasi wa nje wanatujengea vibaya?

NAIBU SPIKA: Majibu ya swali hilo la *multiple choice*. Mheshimiwa Naibu Waziri ujenzi!

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli zipo barabara ambazo *design* yake ama usanifu wake ni kwamba ile mitaro ni *open* yaani ipo wazi haifunikwi, lakini pia inawezekana kukawa na *option* nyingine ya kufunika. Sasa unakuwa na *choice* kulingana na bajeti zenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri tuhimize wananchi wetu, maeneo yale ambayo mitaro ipo *open* wasiwe wanatupa takataka. Ie mitaro kazi yake ni kuchukua maji kutoka barabarani siyo kuhifadhi takataka. Kwa hiyo, hili jambo la kuweka takataka ni jambo ambalo tunaweza tukasaidiana na wananchi ili barabara zetu ziweze kudumu.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge nawashukuru sana kwa awamu hii ya maswali. Nashukuru tumeweza kuyamaliza kwa wakati. Tuna wageni wengi kidogo, kwa hiyo, naomba tuvumiliane niweze kuwatambulisha wote na wageni wetu ni kama ifuatavyo:-

Nitaanza na wageni ambao wapo katika jukwaa la Mheshimiwa Spika ambao ni wageni wa Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa Mheshimiwa Dkt. Hussein Mwinyi ambao ni pamoja na wafuatao: Ndugu Job Masima, Katibu Mkuu wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Ahsante

Nakala ya Mtandao (Online Document)

karibu sana. Ndugu Mwitango, Naibu Katibu Mkuu; Luteni Jenerali Samuel Ndomba, Mnadhibu Mkuu wa Jeshi; *Major General* Raphael Muhuga, Mkuu wa JKT; *Major General* Charles Mzanila, Mkuu wa Shirika la Mizinga. *Major General* Salum Mustafa Kijuu, Mkuu wa *Land Force Command*; *Major General* Joseph Furaha Kapwani, Mkuu wa Kamandi ya Anga; Brigedia Jenerali Gaston Shaban Laswai, Mkuu wa Kamandi ya Wanamaji; Brigedia Jenerali Bahati, Mkuu wa Shirika la Nyumbu na Ndugu Egelbert Ndauka, Kamishna wa Sera na Mipango. Karibuni sana. *(Makofi)*

Pili, tuna wageni wa Mheshimiwa Mathias Chikae, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, ambao ni wafuatao:- Ndugu Mbaraka Abdulwakil, Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Ndani; Bi. Muamini Malemi, Naibu Katibu Mkuu; *IGP* Ernest Mangu, Mkuu wa Jeshi la Polisi; *CGI* Sylvester Ambokile, Kamishna Jenerali wa Uhamiaji; *CGP* John Minja, Mkuu wa Jeshi la Magereza; Ndugu Pius Nyambacha, Mkuu wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji; Ndugu Dickson Maimu, Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (*NIDA*). Karibuni sana. *(Makofi)*

Bado tupo Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Tuna Johari Juma Suluhu, Kamishna wa Uhamiaji Zanzibar; Hamda Makame, Kamishna wa Polisi Zanzibar; Athumani Diwani Msuya, Mkurugenzi wa Upelelezi na Makosa ya Jinai ya Jeshi la Polisi; ahsante sana na tunakupongeza kwa uteuzi huo wa hivi karibuni. Makamishna wote wa Jeshi la Polisi, Magereza, Uhamiaji, Zimamoto na Maafisa wote kutoka Wizarani karibuni sana. *(Makofi)*

Kwa maana hiyo, niwaombe wageni wetu wote kutoka Jeshi la Polisi na Askari wengine ambao sikuwataja wasimame. Kutoka Jeshi la Polisi, Jeshi la Magereza. Ahsanteni sana na karibuni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Lema alikuwa ananiuliza hapa mbona Polisi wengi sana leo. Nikamwambia hapana, wapo kikazi zaidi hawana shida! *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Waziri, Ame Pereira Silima, ana mgeni wake Bi. Mwanamina Haji, mke wake. Karibu sana umuunge mkono Mzee hapa, lakini pia anao wageni wengine 21 kutoka Zanzibar wakiongozwa na Ndugu Said Said. Wageni wa Mheshimiwa Ame Silima kutoka Zanzibar msimame! Karibu sana popote pale mlipo. *(Makofi)*

Tuna wageni watano wa Mheshimiwa Mathias Chikawe, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi ambao ni viongozi wa CCM kutoka Mkoa wa Lindi, wakiongozwa na Ndugu Ibrahim Mpwawa Katibu Mwenezi wa CCM Mkoa wa Lindi. Wale mliotoka Lindi msimame pale mlipo! Karibuni sana. *(Makofi)*

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Pia Mheshimiwa Chikawe ana wageni wengine saba, ambao ni Mabalazi wa Usalama barabarani (*Road Safety Ambassadors*), wanaotumia mitambo ya kijamii kushirikiana na Jeshi la Polisi, Kikosi cha Usalama barabarani katika kukabiliana na ajali za barabarani nchini kwa kuripoti matukio yote ya uvunjifu wa sheria za barabara. Wakiongozwa na Ndugu Gibson Urassa. Karibuni sana! Hatukujua kama kuna watu wa namna hii. (*Makofi*)

Wageni wengine kumi na tano wa Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu ambao ni viongozi wa UWT kutoka Ilala Dar-es-Salaam. Wageni wa Mheshimiwa Zungu! Wapo pale juu. Karibuni sana, karibuni sana na niwahakikishieni Mheshimiwa Zungu anafanya kazi nzuri sana hapa Bungeni, hakuna kama Zungu huko Ilala.

Wageni 22 wa Mheshimiwa Felister Bura ambao ni washiriki wa *Miss UDOM* kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma. Karibuni sana wapo kwenye kona pale juu kabisa.

Kama nilivyosema Waheshimiwa Wabunge mnivumilie nina wageni wengi kidogo. Wageni wa Mheshimiwa Godless Lema, ambao ni Ndugu Neema Lema, mke wake; Ndugu Elifuraha Mtowe, Mkurugenzi wa *Arusha Development Foundation* na Ndugu Rosemary Mtowe, mke wa Elifuraha Mtowe.

Kuna mgeni wa Ndugu Riziki Lulida, Ndugu Salum Ng'ondo kutoka Nangalu, Lindi. Karibu sana.

Wageni wa Mheshimiwa Iddi Azzan, ni viongozi watatu wa kundi la *Modern Taarab* kutoka Magomeni Dar-es-Salaam. Karibuni sana wapo kwenye kona kule.

Wageni waliopo kwa ajili ya mafunzo ni wafuatao:-

Wageni wawili kutoka *House of Prayers Centre* ya Tabata Segerea, Dar-es-Salaam. Chini ya Apostol Patrick Kayimbi Emanuel ambao ni Bi. Prakseda David na Munira Tiria. Karibuni sana popote pale mlipo.

Tuna wanafunzi sitini na Walimu kumi kutoka shule ya Msingi Msalato Dodoma. Karibuni sana na hasa wanafunzi mpate kujifunza jinsi Bunge linavyofanya kazi.

Wageni 41 ambao ni wakulima kutoka Mtandao wa Vikundi vya Wakulima Tanzania MVIWATA, pamoja na viongozi kutoka *Agricultural Non State Actors Forum (ANSAF)*. Wageni wa MVIWATA karibuni sana! Natumaini mmefuatana na Mkurugenzi wenu Bwana Ruvuga, karibuni sana!

Matangazo ya kazi mengine ni haya yafuatayo:-

Mheshimiwa Gregory Teu kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii, anawaomba Wajumbe wa Kamati ya Huduma za Jamii waende kwenye kikao mchana saa nane, kule ukumbi wa Msekwa B saa nane mchana.

Mheshimiwa Mary Manjelwa, anaomba Wajumbe wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira wakutane ukumbi namba 229, saa nane mchana, jengo la Utawala.

Mheshimiwa Peter Serukamba, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Miundombinu anaomba Wajumbe wa Kamati ya Miundombinu, saa nane mchana, mkutane ukumbi namba 136 Hazina.

Katibu!

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha wa 2015/2016 - Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Sasa naomba nimwite Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Chikawe aanze kusoma, kama mtoa hoja na una dakika 45!

HOTUBA YA WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI, MHESHIMIWA MATHIAS MEINRAD CHIKAWA (MB), KUHUSU MAKADIRIO YA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2014/2015 KAMA ILIVYOSOMWA BUNGENI

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia taarifa iliyowasilishwa mbele ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge la Ulinzi na Usalama, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu, likubali sasa kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, kwa mwaka wa fedha 2015/2016. Aidha, naomba hotuba yangu hii yote iingie kwenye *Hansard* kama ilivyo katika kitabu cha hotuba kwa kuwa, hii nitakayoisoma hapa itakuwa ni muhtasari tu wa hotuba hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naomba kuchukua nafasi hii kutoa salamu za rambirambi kwa familia na wananchi wa mikoa mbalimbali ya Tanzania kutokana na mvua kubwa iliyonyesha katika vipindi tofauti mwaka huu na kusababisha mafuriko na hivyo kuleta adha kubwa kwa wananchi ikiwemo

vifo, uharibifu wa mali na Miundombinu. Aidha, nawapa pole nyingi Ndugu na Jamaa wa marehemu waliopoteza maisha yao kutokana na matukio hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia kutumia fursa hii kutoa masikitiko yangu kwa familia na wananchi kwa ujumla kutokana na vifo, ulemavu, upotevu na uharibifu wa mali na miundombinu vilivyosababishwa na ajali za barabarani, majini na nchi kavu katika kipindi chote toka mwezi Julai, 2014. Aidha, nawapa pole Ndugu na Jamaa wa marehemu waliopoteza maisha katika matukio hayo. Namwomba Mwenyezi Mungu aziweke roho za marehemu wote mahali pema peponi. Amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa umuhimu mkubwa naomba niwashukuru, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete na Makamu wa Rais, Mheshimiwa Dkt. Mohamed Gharib Bilal kwa maelekezo yao mbalimbali na Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Pinda kwa kuhimiza utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee naomba kutumia fursa hii kumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuendelea kuniamini katika nafasi hii ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, aidha, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri aliyoitoa mapema katika Mkutano huu wa Bunge ambayo imetoa mwelekeo wa kazi za Serikali kwa ujumla katika mwaka wa fedha 2015/2016.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuishukuru kwa dhati kabisa, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ulinzi na Usalama chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Anna Margareth Abdallah, Mbunge wa Viti Maalum kwa kuyachambua Makadirio ya Mapato ya Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka 2015/2016. Naishukuru pia Kamati hiyo kwa maelekezo na ushauri wao wenye lengo la kuboresha utendaji kazi wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, majukumu ya Msingi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ni kulinda usalama wa raia na mali zao, kuhifadhi na kurekebisha wafungwa, kutekeleza programu ya huduma kwa jamii, kuwezesha na kudhibiti uingiaji na utokaji nchini wa raia na wageni, kutoa huduma za Zimamoto na Uokoaji, kuwahudumia Wakimbizi waliopo nchini na kuandaa na kutoa vitambulisho vya Taifa.

Majukumu haya yanatekelezwa kupitia Jeshi la Polisi, Jeshi la Magereza, Idara ya Huduma kwa Jamii, Idara ya Uhamiaji, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, Idara ya Wakimbizi na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa ya utekelezaji wa malengo ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010 katika kipindi cha 2014/2015. Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ina malengo saba ya kutekeleza yanayotokana na Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2010. Taarifa ya utekelezaji wa malengo hayo kwa mwaka 2014/2015 ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kujenga vituo na kupeleka Askari Polisi katika ngazi ya Tarafa au Jimbo; tangu kuanza kwa dhana ya Polisi Jamii na pili ili kuendana na falasafa ya ugatuaji wa madaraka, Jeshi la Polisi limepeleka katika Tarafa na Kata, Shehia, Askari 7,789 nchi nzima kwa lengo la kupeleka huduma za Polisi hadi ngazi ya chini kabisa ya Utawala.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuimarisha na kuboresha mfumo wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai; katika mwaka 2014/2015, ushirikiano wa kiutendaji kati ya Jeshi la Polisi na Taasisi zinazounda Jukwaa la Hakijinau uliendelea kuimarika. Jeshi la Polisi liliendelea kuongeza ufanisi katika upelelezi wa makosa ya jinai na hivyo kufanikisha kuongeza kiwango cha mafanikio ya kesi Mahakamani kwa asilimia 15.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kufanikisha lengo, Jeshi la Polisi, limetoa mafunzo kwa Askari Wapelelezi 590 wa vyeo mbalimbali ili kuwajengea uwezo katika kukusanya, kujenga ushahidi wa kupeleleza, ikiwemo mbinu za kisasa za upelelezi na kufanya ufaulu wa kesi kufikia asilimia 11.8 toka asilimia 3.9 kwa kipindi kama hicho mwaka uliopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2015/2016, Jeshi la Polisi litaongeza kasi na ufanisi zaidi katika upelelezi wa kesi za jinai ili kufikia kiwango cha juu zaidi cha mafanikio.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuwapatia wananchi mafunzo ya Ulinzi Shirikishi; Wizara imeendesha kampeni mahsusi ya kuhamasisha Wizara, Idara, na Taasisi mbalimbali za Serikali kujenga miundombinu ya amani katika ngazi za Mikoa, Wilaya, Tarafa, Kata, Shehia kwa kutumia sheria na taratibu zilizopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Jeshi la Polisi liliendesha programu 23 zilizolenga kujenga uwezo kwa wananchi katika kupunguza uhalifu katika maeneo yao. Kanda Nane zimepatiwa uwezo wa kuzuia uhalifu kupitia mpango wa mifugo na mazizi salama, vilevile warsha 54 za uhamasishaji zimefanyika kwa wananchi juu ya ulinzi shirikishi. Kata 1,335 na Shehia 165 zimepatiwa mbinu za kuzuia uhalifu na pia kuingizwa katika Baraza la Maendeleo la Kata.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kuimarisha Mafunzo ya Askari na Vyombo vya Ulinzi na Usalama; katika mwaka wa fedha 2014/2015, Jeshi la Polisi limetoa

mafunzo ya mbinu za kisasa za upelelezi kwa Wakuu wa Upelelezi wa Mikoa, Wilaya, Wakaguzi na Askari wa ngazi za chini wapatao 250 pamoja na wadau wa Haki Jinai. Mafunzo haya yalifanyika katika Mikoa ya Dodoma, Kagera, Kinondoni, Manyara, Mtwara, Mwanza, Singida na Tanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupunguza msongamano wa Wafungwa na Mahabusu Magerezani; hatua mbalimbali zinaendelea kuchukuliwa katika kukabiliana na msongamano wa mahabusu na Wafungwa. Idadi ya Wafungwa na Mahabusu waliokuwa Magerezani imepungua kutoka 33,831 Mwezi Machi, 2014 hadi kufikia 33, 027 Machi, 2015. Uwezo wa sasa wa Magereza kisheria ni kuhifadhi wafungwa 29,559 ikilinganishwa uwezo uliopo awali wa kuhifadhi Wafungwa 27,653.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2014/2015, Wizara imechukua hatua mbalimbali za kukabiliana na tatizo la msongamano magerezani kwa utaratibu wa *parole*, kifungo cha nje na msamaha wa Rais kama ilivyoainishwa katika aya ya 14 ya hotuba yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuimarisha uzalishaji wa mbegu bora za kilimo katika maeneo ya Magereza; katika mwaka 2014/2015, Jeshi la Magereza limeendelea kulima mbegu bora za kilimo katika mashamba ya Magereza ya Nachwingwea, Lindi; Wami Kuu, Morogoro na Karanga, Mkoa wa Kilimanjaro. Matarajio ni kuvuna tani 50 za mbegu za alizeti na tani 20 za mbegu za ufuta. Katika mwaka 2015/2016 Jeshi la Magereza linatarajia kulima na kuhudumia hekta 1,300 za mazao mbalimbali kwa matarajio ya kuvuna tani 1,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (*NIDA*); katika mwaka 2014/2015, Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa imeendelea kutekeleza Ilani ya uchaguzi kama ipasavyo. Mpaka kufikia mwezi Machi, 2015 *NIDA* imesajili na kuwatambua watu 6,256,768 kwa Zanzibar na katika Mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Lindi, Mtwara, Morogoro na Tanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, imetengeneza vitambulisho 2,567,980 na kuvigawa kwa wananchi katika Mikoa ya Dar es Salaam na Zanzibar na matumizi ya vitambulisho hivyo yameanza. Vitambulisho vya Taifa kwa wananchi wa Mikoa ya Pwani, Lindi, Mtwara, Morogoro na Tanga vinaendelea kutengenezwa na vitagawiwa kwa kadri taratibu za usajili zitakavyokamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika jitihada za kuongeza kasi ya utoaji wa vitambulisho vya Taifa, Serikali imeongeza vifaa vya usajili kutoka 280 hadi kufikia 1,506. Vile vile imeingia mkataba na Serikali ya Watu wa Korea kwa ajili ya kupata fedha za kujenga Kituo Kikuu cha Uchakataji na Uzalishaji wa Vitambulisho wa Taifa, Kituo cha Uokozi wakati wa majanga pamoja na ofisi 13 za utambuzi na usajili za Wilaya ambapo matayarisho ya ujenzi yamekwishaanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya Usalama Nchini; hali ya Uhalifu; wajibu wa kwanza wa Serikali ni kulinda usalama wa raia na mali zao na kuhakikisha uwepo wa amani na utulivu. Nchi yetu imeendelea kuienzi amani na utulivu uliopo kama msingi mkuu wa Taifa, ambao umejengwa na kuendelea kuimarishwa tangu tupate uhuru mwaka 1961 katika kipindi cha miaka 51 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar. Uwepo wa amani na utulivu nchini umechangia katika ustawi wa nchi yetu kiuchumi, kijamii na kisiasa, ambapo kumezingatiwa na kutambuliwa kuwa miongoni mwa vipaumbele katika ukuaji wa uchumi wa Taifa letu na maendeleo binafsi ya wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wake Jeshi la Polisi limeendelea kutekeleza kikamilifu jukumu lake la Kikatiba na Kisheria la kulinda na kudumisha amani na utulivu nchini kwa kubaini, kuzuia, na kutanzua vitendo vya uhalifu, makosa ya usalama barabarani, migogoro, vurugu na fujo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha kuanzia Julai, 2014 hadi Machi 2015, jumla ya makosa makubwa makubwa ya jinai 47,942 yaliripotiwa katika vituo vya Polisi kote nchini ikilinganishwa na makosa 62,756 yaliyoripotiwa katika kipindi kama hicho mwaka 2014. Hii ni pungufu ya makosa ya jinai 14,814 sawa na asilimia 31.

Mheshimiwa Naibu Spika, upungufu huu unatokana na upatikanaji wa taarifa za uhalifu mapema na utekelezaji wa mkakati wa Polisi Jamii unaohusisha ushirikishwaji wa wananchi katika vita dhidi ya uhalifu nchini. Sababu nyingine kuu ni kuongezeka kwa wigo wa doria, misako na operesheni maalum za Jeshi la Polisi Mijini na Vijijini. Mchanganuo wa makosa haya umeainishwa katika aya ya 20 ya hotuba yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika miaka ya hivi karibuni ajali za barabarani zimekuwa tishio kwa maisha ya watu na mali zao. Takwimu zinaonesha kuwa, katika kipindi cha Julai, 2014 hadi Machi, 2015 ajali za barabarani 8,072 zilitokea ambapo watu 2,883 walipoteza maisha na wengine 9,370 walijeruhiwa. Katika mwaka 2014 kulitokea ajali 45,275 ambazo zilisababisha vifo vya watu 3,799 na wengine 16,635 walijeruhiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na takwimu za 2014/2015 kuonesha kuwa ajali hizo zimepungua, bado ajali hizo zimeendelea kuleta madhara makubwa kwa wananchi. Kwa kuzingatia hali hiyo, Serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali ikiwemo marekebisha ya sheria, kanuni na kuimarisha doria na ukaguzi wa vyombo na madereva.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na wadau wengine wa masuala ya usalama barabarani limeendelea kusimamia

utekelezaji wa sheria za usalama barabarani ambapo jumla ya makosa madogo madogo 601,550 yaliripotiwa na wakosaji kutozwa faini na wengine kufikishwa Mahakamani. Takwimu zinaonesha kuwa vyanzo vikuu vya ajali ni mwendo kasi, uzembe wa madereva, ubovu wa vyombo vya usafiri na wakati mwingine ubovu wa miundombinu.

Mheshimiwa Spika, kutokana na makosa ya usalama barabarani, Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na *SUMATRA*, Shirika la Viwango Tanzania (*TBS*), *TANROADS* na shule za udereva zilizosajiliwa zimeendelea kuchukua hatua za kuzuia na kudhibiti vyanzo vya ongezeko la ajali za barabarani.

Hatua hizo ni pamoja na kutoa elimu ya kuzingatia sheria za usalama barabarani kwa watumiaji wa barabara wakiwemo madereva wa bodaboda, kuendeleza doria za masafa mafupi na marefu katika barabara kuu, ukaguzi wa magari kwa kutumia tochi za kutambua madereva wanaozidisha mwendo kasi, kuendelea kusimamia zoezi la utoaji wa leseni mpya za udereva, kuhamasisha abiria kutoa taarifa mapema za madereva wanaokiuka sheria za usalama barabarani, kuwaelekeza wamiliki wa mabasi kubandika kwenye mabasi yao namba za simu za Viongozi wa Polisi na kuwachukulia hatua za kinidhamu askari wanaojihusisha na vitendo vya kuomba na kupokea rushwa kutoka kwa madereva.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika siku za karibuni kumejitokeza matukio ya kuvamiwa kwa vituo vya Polisi ambapo Askari Polisi wameuawa pamoja na kuporwa silaha na risasi. Mnamo tarehe 21 Januari, 2015 usiku katika kituo cha Polisi Ikwiriri, Rufiji, majambazi wakiwa na bunduki, walivamia kituo cha Polisi na kuwaua Askari Wawili na kisha kupora bunduki aina ya *SMG* mbili, *SR 2*, *Anti riot Gun* moja, *Shortgun* moja na risasi 60.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, tukio lingine la kuvamiwa kwa Kituo cha Polisi lilitokea tarehe 30 Machi, 2015 barabara ya Kilwa kwenye kizuizi cha Polisi eneo la shule ya Sekondari *St. Mathew Kongowe*, Kata ya Vikindu, Wilayani Mkuranga. Majambazi wasiofahamika wakiwa na mapanga na silaha zingine za jadi walimuua Askari mmoja na kisha kupora bunduki moja aina ya *SMG* ikiwa na risasi 30.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla idadi ya matukio ya uvamizi ya vituo vya Polisi imeongezeka kutoka sita kwa mwaka 2014 hadi nane kwa mwaka huu. Katika matukio haya Askari saba waliuawa na bunduki 22 ziliporwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, inakemea tabia hii ya kuvamiwa kwa Vituo vya Polisi ambayo inaambatana na dalili za vimelea vya ugaidi na kuomba jamii isaidie kuwafichua wahalifu wanaotenda vitendo hivyo kwa manufaa ya usalama

wetu. Ushirikiano baina ya Jeshi la Polisi na wananchi umewezesha kukamatwa kwa bunduki 20 na watuhumiwa 23 miongoni mwao tisa wamefikishwa Mahakamani na wengine wapo chini ya uangalizi maalum.

Mheshimiwa Spika, Mapitio ya Utekelezaji wa Bajeti ya mwaka 2014/2015 na Malengo ya mwaka 2015/2016. Mapato na Matumizi; katika mwaka 2014/2015, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ilipangiwa kukusanya mapato ya Sh. 156,667,945,79, hadi kufikia tarehe 31 Machi, mwaka huu, Wizara ilikuwa imekusanya Sh. 125,907,779,521 sawa na asilimia 80.4 ya lengo la mwaka. Katika mwaka 2015/2016, Wizara imelenga kukusanya mapato ya Sh. 178,969,264,691.

Mheshimiwa Naibu Spika, mifumo na nguvu zaidi zitaelekezwa katika kuziba mianya ya uvujaji wa mapato hususan katika kuimarisha na kuboresha matumizi ya benki kwa ajili ya kufanya malipo ya huduma zinazotolewa na taasisi za Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2014/2015, Wizara iliidhinishiwa jumla ya Sh. 936,386,935,197 kwa ajili bajeti ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo. Hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2015, jumla ya sh. 575,119,649,579 zilikuwa zimetumika, sawa na asilimia 61 ya bajeti ya mwaka mzima ambapo Sh. 292,331,740,187 zimetumika kulipia mishahara, matumizi mengineyo Sh. 237,959,341,245 na fedha za maendeleo ni Sh. 44,828,568,147. Katika mwaka wa fedha wa 2015/2016 Wizara inategemea kutumia Sh. 872,703,062,000 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Polisi: Maboresho ya Jeshi la Polisi; Jeshi la Polisi limeendelea na utekelezaji wa awamu ya kwanza ya programu ya maboresho ya mwaka 2010/2011 hadi 2014/2015 ambapo limemteua Mshauri Mwelekezi kwa ajili ya kufanya tathmini ya awamu ya kwanza na kupendekeza hatua madhubuti za kuendelea nayo katika awamu ya pili. Mitaala ya Vyuo vyote vya Polisi imebadilishwa na kufuata mfumo wa *NACTE* unaolenga katika utendaji kazi, *Competence Based Education Training* kuliko ile ya kitaaluma yaani *Knowledge Based Education Training* zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Polisi Jamii; katika mwaka 2014/2015 programu za usalama wetu kwanza, utii wa sheria bila shuruti, familia yetu haina mhalifu na ulinzi shirikishi zimeendelea kupata mwikio chanya kutoka kwa wananchi ambapo vikundi vya ulinzi shirikishi 9,538 vimeanzishwa nchi nzima. Aidha, idadi ya Askari wanaofanya kazi kama Maafisa wa Polisi Jamii katika ngazi za Tarafa, Kata na Shehia imeongezwa kutoka watatu hadi watano. Katika mwaka 2015/2016, Jeshi la Polisi litaendelea kuongeza idadi ya Askari katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mauaji ya Wanawake, Wazee na watu wenye U-*albino*; Jeshi la Polisi linahakikisha kuwa mauaji ya Wazee hasa wanawake yanadhibitiwa katika Mikoa ya Mwanza, Shinyanga, Simiyu, Singida, Geita na Tabora. Aidha, kutokana na tatizo la mauaji ya watu wenye U-*albino* katika jamii ya Kitanzania, Wizara imeunda Kikosi Kazi Maalum kinachojumuisha vyombo vya ulinzi na usalama na taasisi zingine za haki jinai.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na hatua hiyo, watuhumiwa 286 wamekamatwa na kufikishwa Mahakamani ambapo watuhumiwa 30 wamehukumiwa na Mahakama, watuhumiwa 28 waliachiwa huru kutokana na ushahidi hafifu. Sambamba na hilo majalada 35 ya kesi yapo kwa Mwendesha Mashtaka yakiandaliwa hati za Mashtaka na watuhumiwa 193 upelelezi unaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi hiki tunasikitika kuwa, yametokea mauaji ya watu watatu wenye ulemavu wa ngozi, yaani watu wenye u-*albino*, katika Mikoa ya Simiyu, Singida na Geita. Katika matukio hayo watuhumiwa 17 wamekatwa ambapo saba walifikishwa Mahakamani, wengine saba wameachiwa huru kutokana na ushahidi hafifu na watuhumiwa watatu upelelezi dhidi yao unaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, watu watatu wenye u-*albino* wamejeruhiwa katika Mikoa ya Tabora wawili, Rukwa mmoja, kwa kukatwa sehemu mbalimbali za miili yao. Katika matukio hayo watuhumiwa nane walikamatwa, kati yao hao sita wamefikishwa Mahakamani na wawili upelelezi dhidi yao bado unaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, matukio haya yanaifedhehesha sana nchi na hivyo naendelea kutoa wito kwa jamii kuona kuwa tatizo hili ni la kwetu sote na hatuna budi kushirikiana ili kulikomesha. Katika mwaka 2015/2016, Serikali itahakikisha kuwa, mauaji ya wanawake, wazee na watu wenye u-*albino* yanadhibitiwa kwa kufanya mikakati mbalimbali, kama ilivyoainishwa katika Aya ya 31 ya Hotuba yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuzuia biashara ya dawa za kulevyo; katika mwaka 2014/2015, mapambano dhidi ya biashara haramu ya dawa za kulevyo yaliendelezwa kwa kuzifanyia kazi taarifa za wananchi na kufanya misako, doria na *operation*. Hadi kufikia Disemba 14 kilo 282 za dawa za kulevyo aina ya *heroin*, *cocaine*, *cannabis*, *morphine* na *mandrax* zilikamatwa sambamba na watuhumiwa 395 na kufikishwa Mahakamani. Vile vile kilo 14,036.59 za bangi na kilo 3,866.2 za mirungi zilikamatwa na watuhumiwa 7,226 nao kufikishwa Mahakamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kushughulikia Uhalifu katika Shughuli za Kisiasa na Kijamii; katika mwaka 2014/2015, Jeshi la Polisi liliendelea kufanya kazi za ulinzi na usalama katika maeneo mbalimbali kwa lengo la kudumisha amani na utulivu nchini. Hatua hii imewezesha kuwepo kwa hali ya utulivu wakati wa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa mwaka 2014, hali ya utulivu na usalama katika michakato ya kisiasa, kama mikutano ya Vyama vya Siasa na shughuli za kila siku za kijamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kwa kuzingatia majukumu muhimu yaliyopo mbele yetu ya Kura za Maoni kwa Katiba inayopendekezwa pamoja na Uchaguzi Mkuu mwaka huu wa 2015, Wizara inatoa wito kwa wananchi na jamii kwa ujumla, kuzingatia umuhimu wa kuwepo amani na usalama katika hatua zote. Vile vile tunawasahi Viongozi na wananchi wote kujiepusha na vitendo vya aina yoyote ya uvunjifu wa amani na pia, kushirikiana na Jeshi la Polisi kwa kutoa taarifa stahiki pale dalili au vitendo viovu vinapojitokeza. Katika mwaka 2015/2016, Jeshi la Polisi litaendelea kutekeleza wajibu wake wa ulinzi na usalama na amani kwa ukamilifu kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ajira, Mafunzo na Upandishwaji Vyeo Askari Polisi; katika mwaka 2014/2015, jumla ya Askari Polisi wapatao 3,193 walijajiriwa. Aidha, Askari 3,357 wa vyeo mbalimbali walipandishwa vyeo, kama ilivyoainishwa katika Aya ya 37 ya Hotuba yangu ya Bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2015/2016, Jeshi la Polisi litaajiri Askari wapya 3,500 na kuwapandisha vyeo Askari 6,274.

Mheshimiwa Naibu Spika, Vitendea Kazi na Makazi kwa Askari Polisi. Idadi ya watu na mahitaji ya huduma ya usalama wa raia na mali zao yanazidi kuongezeka kila mwaka. Ili kukabiliana na changamoto ya uchache wa miundombinu ya makazi kwa Askari Polisi, Serikali kupitia Shirika la Uzalishaji Mali la Jeshi la Polisi, imeanza kujenga nyumba 330 za Askari katika eneo la Kunduchi, nyumba 20 za Maafisa katika eneo la Oyster Bay, Mikocheni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Programu ya Urekebishaji wa Wafungwa; Jeshi la Magereza limeendelea kutekeleza Programu za Urekebishaji wa Wafungwa kwa kuwapa stadi katika kilimo na viwanda vidogo vidogo. Aidha, zoezi la matengenezo ya matrekta liliendelea katika Vituo vya Babati, Manyara, Ushora, Singida, Kwa Mgumi – Tanga, Karanga – Kilimanjaro, Ngwara – Mbeya, Nachingwea – Lindi, Kyabakari – Mara, Kongwa – Dodoma, Wami Kuu – Morogoro, Karialankulu – Katavi, Matongo – Simiyu, Ilagara na Kibondo – Kigoma.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2015/2016, Jeshi la Magereza limelenga kuendelea kuyafanyia matengenezo matrekta yaliyopo pamoja na zana zake katika magereza mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2014/2015, Jeshi la Magereza liliendelea na jukumu la urekebishaji wa wafungwa kupitia ufugaji wa ng'ombe wa nyama 8,626, ng'ombe wa maziwa 2,587, pamoja na mifugo mingine ambayo ni mbuzi, kondoo, sungura, kuku wa mayai na bata weupe. Huduma mbalimbali za mifugo ziliboreshwa, kama vile chanjo, dawa za tiba na huduma za kuogecha mifugo kwenye Magereza yote yaliyo na mifugo.

Aidha, huduma za uhamilishaji wa mifugo ziliendelea kuboreshwa kwenye Magereza ya Ubena – Pwani, Kingolwira na Mbigili – Morogoro, King'ang'a – Dodoma, Mugumu – Mara, Kitengule – Kagera, Kilimo – Urambo, Tabora na Gereza za Arusha.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2015/2016, Jeshi la Magereza linatajia kuhudumia ng'ombe wa nyama 9,300 na ng'ombe wa maziwa 3,000, mbuzi 3,240, kondoo 510, pamoja na wanyama wengine wadogo wadogo kwa kununua chanjo na dawa za kutosha ili kuboresha mashamba ya malisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafunzo kwa Askari na Watumishi wa Jeshi; katika mwaka wa fedha 2014/2015, Jeshi la Magereza limeendelea kutoa mafunzo mbalimbali ndani na nje ya Jeshi kwa ajili ya Maafisa na Askari. Mafunzo hayo ni yale yanayohusu uendeshaji wa Magereza na Taaluma nyingine mbalimbali. Jumla ya Askari wapya 1,444 wanaendelea na mafunzo ya awali Chuo cha Magereza – Kiwira, Mbeya. Mafunzo mengine yanayoendeshwa kwa sasa yameainishwa katika aya ya 45 ya Hotuba yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2015/2016, Jeshi la Magereza linatarajia kuajiri Askari wapya 1,500 na Watumishi Raia 15 na kutoa mafunzo ya uendeshaji wa Magereza kwa Maafisa wa Askari 3,200.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kuboresha Usafiri na Usafirishaji; katika Mwaka wa Fedha 2014/2015, Jeshi la Magereza limeweza kununua magari saba kwa ajili ya kuboresha shughuli za utawala. Katika mwaka 2015/2016, Jeshi la Magereza linatarajia kununua magari matano kwa ajili ya shughuli za utawala.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kuimarisha Kilimo cha Umwagiliaji; katika kuepuka kilimo cha kutegemea mvua, mwaka 2014/2015, Jeshi la Magereza liliendelea na ujenzi wa miundombinu ya kilimo cha umwagiliaji katika Gereza la Idete kule Morogoro. Kazi ya uhamishaji wa njia ya maji imefanyika kwa 100%, ujenzi wa banio la mfereji limejengwa kwa 95% na kazi za ujenzi wa tuta na

kingo za mfereji huu zimekamilika kwa 70%. Katika Mwaka 2015/2016, Jeshi linakusudia kuendelea na ukamilishaji wa mradi huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Uzalishaji la Magereza; Shirika hili limeendelea na uzalishaji wa bidhaa zitokanazo na kilimo, mifugo na viwanda vidogo vidogo. Kwa upande wa kilimo, jumla ya eneo la ekari 4,500 limelimwa kwa matarajio ya kuvuna tani 5,265 za mazao mbalimbali. Aidha, Shirika hili kupitia Kikosi cha Ujenzi cha Jeshi la Magereza, limeendelea kufanya kazi mbalimbali za ujenzi kwa majengo ya taasisi za Serikali na watu binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, matarajio ya mwaka 2015/2016, ni kuongeza shughuli za uzalishaji kwa kuingia ubia na wawekezaji wa ndani na nje ya nchi ili kupata mtaji wa kutosha kukidhi soko la bidhaa zitokanazo na kilimo, mifugo, samani za ofisi, samani za nyumbani, bidhaa za ngozi na shughuli za ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Matumizi ya Nishati Mbadala Magerezani; katika kukabiliana na changamoto zinazotokana na matumizi makubwa ya kuni Magerezani na hivyo kuwepo tishio la uharibifu wa mazingira, Jeshi la Magereza limeendelea kuchukua za kuanza matumizi ya *biogas* na makaa ya mawe kama nishati mbadala kwa ajili ya kupikia chakula cha wafungwa Magerezani; matumizi ya *biogas* yanaendelea katika Gereza la Ukonga. Aidha, matumizi ya makaa ya mawe yanaendelea katika Magereza ya Songwe, Tukuyu na Ruanda yaliyoko Mkoani Mbeya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa Jeshi lipo katika mchakato wa kutumia majiko yanayotumia kuni kidogo ambayo yameanza kutumika katika Gereza la Karanga, Mwanga – Kilimanjaro, Kibondo, Bangwe – Kigoma na Sumbawanga – Rukwa. Matarajio ni kueneza matumizi ya nishati hii katika Magereza mengine yenye matumizi makubwa ya kuni kadiri uwezo wa fedha utakavyoturuhusu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Utunzaji wa Hifadhi ya Mazingira; utunzaji wa mazingira ni miongoni mwa shughuli za kila siku za Jeshi la Magereza. Shughuli za kuandaa vitalu vya miche na upandaji miti zinaendelea sambamba na maandalizi ya msimu wa kilimo kwa kila kituo; katika kuadhimisha Siku ya Upandaji Miti Kitaifa, tarehe 1 April, 2014 ilipandwa jumla ya miti 2,021,850 katika Magereza yote nchini.

Aidha, Mradi wa Hifadhi ya Mazingira na Upandaji Miti ambao unatekelezwa na Jeshi la Magereza kwa ushirikiano na *Tanzania Forest Fund* katika Magereza ya Mgagao, Isupilo – Iringa, Kambi Ihangha – Njombe na Mkwaya – Ruvuma, umewezesha kupandwa jumla ya miti laki nane.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2015/2016, Jeshi litaingiza Magereza mengine katika mpango huo, ambayo ni Magereza ya Msalato – Dodoma, Bariadi – Simiyu na Ngudu – Mwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Idara ya Uhamiaji; Idara hii ina jukumu la kudhibiti uingiaji, utokaji na ukaaji wa wageni na pia kuwawezesha raia wa Tanzania kupata hati za kusafirira. Aidha, Idara hii ndiyo inayoratibu mchakato wa Maombi ya Uraia kwa wageni wanaoomba uraia wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hali ya Ulinzi na Usalama Mpakani; katika kipindi cha Julai hadi Machi, 2015, Idara iliendelea kutoa huduma za kiuhamiaji katika mipaka na vituo vya kuingia na kutoka nchini ambako wageni 1,005,652 waliingia na wengine 892,614 walitoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Misako na Doria; katika kipindi hiki cha Julai, 2014 hadi Machi, 2015, Idara ya Uhamiaji iliendelea kufanya doria na misako sehemu mbalimbali ambapo watuhumiwa wa uhamiaji haramu 3,944 walikamatwa na kuchukuliwa hatua mbalimbali za kisheria, ikilinganishwa na wahamiaji haramu 5,576 waliokamatwa katika kipindi kama hiki mwaka jana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupungua kwa watuhumiwa wa uhamiaji waliokamatwa, kunatokana na kuongezeka kwa udhibiti na hivyo kuogopa kuingia au kuishi nchini kinyume cha sheria. Katika mwaka wa fedha 2015/2016, Idara ya Uhamiaji inatarajia kununua magari 24, lori moja, pikipiki 57 na maboti saba kwa ajili ya kuimarisha shughuli za misako na doria dhidi ya wahamiaji haramu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Vibali Mbalimbali Vinavyotolewa kwa Wageni; Wizara, kupitia Idara ya Uhamiaji, imetoa vibali vya ukaazi kwa wageni wawekezaji, wageni wanaopata ajira katika makampuni mbalimbali na wageni wengine walioingia nchini kwa malengo mbalimbali ambapo wageni 13,603 walipewa Hati za Ukaazi kama ilivyoainishwa katika Ibara ya 54 ya Hotuba yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hati za Safari; katika kipindi cha Julai, 2014 hadi Machi, 2015, Idara ya Uhamiaji imetoa Hati za Safari 48,553 kwa Watanzania ambapo kati ya Hati hizo 46,779 ni za kawaida, 1,346 ni za Afrika Mashariki, 303 za Kibalozi, 125 za Kiutumishi. Aidha, ili kukabiliana na changamoto zitokanazo na mabadiliko ya teknolojia ya udhibiti wa *Passport*, Idara inaendelea na mchakato wa kuhakikisha huduma za kiuhamiaji zinatolewa kwa njia ya kielektroniki, ambapo huduma za uhamiaji kama vile utoaji wa Hati za Safari, Vibali vya Ukaazi na Visa, zitatolewa kwa njia ya kielektroniki na kuongezewa alama za usalama za siri.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Naibu Spika, Wageni Waliopatiwa Uraia wa Tanzania; katika kipindi cha Julai, 2014 hadi Machi, wageni 192 wa Mataifa mbalimbali walipatiwa uraia. Mchanganuo wa wageni hao na Mataifa wanayotoka umeainishwa katika Aya ya 56 ya Hotuba yangu ya Bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania Waliopatiwa Uraia wa Mataifa Mengine na Walirudishwa Nchini; katika kipindi cha Julai, 2014 hadi Machi, 2015, Watanzania 38 waliukana uraia wa Tanzania kwa kupata uraia wa Mataifa mengine, hivyo kupoteza sifa ya kuwa raia wa Tanzania kwa mujibu wa Sheria ya Uraia Namba 6 ya mwaka 1995. Aidha, katika kipindi hicho Watanzania watoro (*Stowaways*) 39 walirudishwa nchini kutoka nchi mbalimbali, hususan nchi za Kusini mwa Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ajira na Mafunzo; katika kipindi cha Julai, 2014 hadi Machi, 2015, Idara ya Uhamiaji imewapeleka Askari wake 298 kwenye mafunzo ya awali ya uhamiaji katika Chuo cha Polisi Moshi; Watumishi 71 waliopo kazini wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu ndani ya nchi. Matarajio kwa mwaka 2015/2016 ni kuajiri watumishi wapya 1,066 na kutoa mafunzo kwa watumishi 600 waliopo kazini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Majengo ya Ofisi; Idara ya Uhamiaji imekamilisha ujenzi wa Ofisi ya Uhamiaji Mkoa wa Singida, ujenzi wa Ofisi za Uhamiaji katika Mikoa ya Manyara, Pwani, Geita, Mtwara na Lindi unaendelea. Aidha, Mshauri Mwelekezi amepatikana kwa ajili ya kukamilisha michoro ya ujenzi wa Ofisi katika Wilaya ya Ileje, Mbeya na Kituo cha Kirongwe, Wilayani Rorya, Mkoani Mara ambapo ujenzi utanza mwaka wa fedha 2015/2016. Pia, katika mwaka wa fedha 2015/2016, Idara inatarajia kufanya ukarabati wa awamu ya pili wa Majengo ya Chuo cha Uhamiaji Moshi na Jengo nla Makao Makuu Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, Makazi ya Askari; katika mwaka wa fedha 2014/2015, Idara ya Uhamiaji imekamilisha ujenzi wa nyumba tano za Viongozi Mtoni Kijichi, Dar-es-Salaam pamoja na nyumba za Afisa Uhamiaji Mkoa wa Ruvuma. Idara inaendelea pia na ujenzi wa nyumba ya Makazi ya Maafisa Uhamiaji wa Mikoa ya Kigoma na Mwanza.

Aidha, Mshauri Mwelekezi amepatikana kwa ajili ya kukamilisha michoro ya nyumba za Makazi ya Askari Kisongo, Mkoani Arusha na ujenzi utanza katika mwaka wa fedha 2015/2016. Vile vile Idara itafanya ukarabati wa nyumba 17 za Makazi Mkoani Tabora.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji; jukumu la msingi la Jeshi la Zimamoto na Uokoaji ni kuinga na kupunguza vifo, majeruhi,

uharibifu wa mali unaotokana na moto, mafuriko, ajali za barabarani, kimbunga na dharura zote zisizo za jinai.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hali ya Vituo vya Zimamoto na Uokoaji Nchini; Jeshi la Zimamoto na Uokoaji lina jumla ya Vituo 52 nchi nzima, tofauti na mahitaji halisi ambayo ni Vituo 152 vinavyotakiwa kuwepo. Hali hii inasababisha kuwepo na mahitaji makubwa ya huduma hii muhimu, hususan Wilayani. Katika Mwaka wa Fedha 2015/2016, Jeshi linatarajia kujenga Vituo vitatu vya Zimamoto katika Jiji la Dar-es-Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, mahitaji makubwa ya magari ya kuzima moto ni makubwa kwa kuwa, katika magari 83 yaliyopo nchi nzima, magari 35 tu ndio mazima. Ili kuweza kutoa huduma kwa ufanisi yanahitajika magari 280. Katika Mwaka wa Fedha 2015/2016, Jeshi linatarajia kununua gari moja la kuzimia moto pamoja na magari matano kwa ajili ya shughuli za ukaguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ukaguzi wa Tahadhari na Kinga Dhidi ya Moto na Majanga; moja ya jukumu la msingi la Jeshi la Zimamoto na Uokoaji ni kufanya ukaguzi wa tahadhari na kinga dhidi ya moto. Hadi kufikia Machi, 2015, Jeshi limekagua maeneo 38,441. Matarajio katika mwaka wa fedha 2015/2016, ni kukagua maeneo 63,500 nchi nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, Matukio ya Moto na Majanga Mengine; Jeshi la Zimamoto na Uokoaji limeendelea kutekeleza majukumu yake ya msingi, hususan kupambana na majanga ya moto pamoja na kufanya maokozi mbalimbali. Mpaka kufikia mwezi Machi, 2015, Jeshi limeshiriki kuzima moto katika matukio 2,018 na kufanya maokozi 607 katika maeneo mbalimbali nchini, yakiwemo mafuriko yaliyotokea Kahama, Shinyanga, Mwanza na Dar-es-Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mafunzo kwa Askari na Watumishi; Jeshi la Zimamoto na Uokoaji limeendelea na juhudi mbalimbali ili kuwapatia Askari na Maafisa wake mafunzo kwa lengo la kuboresha utendaji katika majukumu yao. Katika mwaka wa fedha 2014/2015, watumishi, askari na raia 821 wamepatiwa mafunzo katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Elimu kwa Umma; katika mwaka 2014/2015, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji limeendelea kutoa elimu kwa umma juu ya namna ya kukabiliana na majanga mbalimbali ya moto kupitia vyombo vya habari, ikiwemo *television*, redio, magazeti na matangazo kupitia magari ya zimamoto na uokoaji. Katika mwaka wa fedha ujao Jeshi la Zimamoto litaongeza kasi ya utoaji elimu kwa umma kwa lengo la kupunguza majanga ya moto na mengineyo.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (*NIDA*); Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa katika mwaka wa fedha 2014/2015 imesajili wananchi 505,408 katika Mkoa ya Pwani; wananchi 353,442 katika Mkoa ya Lindi; 512,827 Mtwara; wananchi 862,392 wa Morogoro na wananchi 847,900 katika Mkoa wa Tanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, imetengeneza vitambulisho 1,299,829 vya wananchi wa Unguja na Pemba pamoja na Mkoa wa Dar-es-Salaam na ugawaji wa vitambulisho hivyo kwa wananchi hao unaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2015/2016, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kupitia Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa imepanga kufungua Ofisi za Usajili Wilayani na kuendelea kusajili wananchi katika maeneo hayo. Mamlaka itanunua vifaa vya usajili 500, vifaa vya kugawia vitambulisho 700, mashine za kusomea vitambulisho 1,300.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu kupitia Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa kwa mwaka wa fedha 2015/2016, inalenga kuzishirikisha Taasisi nyingine za Serikali katika usajili wa makundi maalum ya watu, ili kupunguza gharama za usajili. Kwa kuanzia itashirikiana na Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu katika kuwasajili wanafunzi wote katika Vyuo vya Elimu ya Juu, ili Vitambulisho visaidie katika utoaji na urejeshwaji wa mikopo kwa wanafunzi hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Huduma kwa Jamii; Idara ya *Probation* na Huduma kwa Jamii ambayo, imesimamia utekelezaji wa adhabu mbadala kwa kifungo gerezani chini ya Sheria ya *Probation* na Sheria ya Huduma kwa Jamii, hivi sasa inatekeleza programu hii kwenye Wilaya 63 za Mikoa 21 Tanzania Bara. Hadi kufikia Machi, 2015, Taarifa za uchunguzi wa kijamii 1,575 ziliandaliwa na kuwezesha wafungwa 1,217 kunufaika na programu hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, huduma kwa wakimbizi. Katika mwaka wa 2014/2015, Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya Marekani imeanza kutekeleza mpango maalum wa kuwahamishia nchini Marekani wakimbizi wenye asili ya DRC na Burundi wapatao 32,000. Sambamba na mpango huo maalum, utaratibu wa kawaida wa kuwahamishia wakimbizi katika nchi ya tatu umeendelea kutekelezwa ambapo kipindi cha kuanzia Julai 2014 hadi Aprili, 2015 wakimbizi 877 walipelekwa huko Ulaya na Marekani.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuongeza udhibiti wa wakimbizi wanaotoroka kwenye makambi/makazi yao na kwenda maeneo yasiyo stahili, Wizara imekamilisha uhakiki wa wakimbizi, kuwapiga picha na kuchukua alama za vidole ambazo zinawekwa kwenye kanzidata (*database*).

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, kutokana na kuzuka kwa vurugu kuelekea Uchaguzi Mkuu wa Burundi, katika kipindi cha mwezi Aprili na Mei, 2015, Tanzania imepokea wakimbizi wapya takribani 20,000 walioingia nchini kupitia Mkoa wa Kigoma. Kwa upande mwingine hali ya amani na utulivu nchini DRC bado haijatengemaa. Hivyo zoezi la uhamasishaji wa urejeshwaji wa hiyari halifanyiki kwa sasa. Kabla ya kuanza kupokea wimbi jipya la wakimbizi toka Burundi, nchi yetu ilikuwa na wakimbizi 89,069 kutoka mataifa ya DRC, Burundi na wachache kutoka nchi za Somalia, Rwanda, Uganda na Sudani ya Kusini. Aidha, Serikali imehitimisha suala la waliokuwa wakimbizi toka Burundi wa mwaka 1972 wapatao 162,156 kwa kuwapa uraia na kuwaruhusu kuishi nchini kihalali.

Mheshimiwa Spika, vita dhidi ya biashara haramu ya usafirishaji wa binadamu. Katika mwaka wa fedha wa 2014/2015, Sekretarieti ya Kupambana na Biashara Haramu ya Usafirishaji wa Binadamu imeratibu vikao vinne vya Kamati ya Kitaifa ya Kupambana na Biashara Haramu ya Usafirishaji wa Binadamu. Aidha, imekamilisha kuandaa kanuni na sheria husika na kusambaza vitabu cha anwani na majina ya watoa huduma kwa waathirika wa biashara haramu ya usafirishaji binadamu.

Mheshimiwa Spika, usajili wa vyama vya kijamii na vya kidini. Katika mwaka 2014/2015, Wizara imeendelea na jukumu la usajili na ukaguzi wa vyama vya kijamii na kidini ili kuvisimamia na kuhakikisha uwepo wa amani na utulivu katika jamii. Hadi kufikia mwezi Machi, 2015, maombi ya vyama 571 yalipokelewa ambapo 457 vimesajiliwa, 32 wamekataliwa, tafadhali angalia aya 76 ya hotuba yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, shukrani, natoa shukrani zangu za dhati kwa Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ulinzi na Usalama chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Anna Margareth Abdallah, Mbunge Viti Maalum kwa kuyapitia na kuyachambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka wa fedha 2015/2016. Maelekezo na ushauri wa Kamati hiyo utaisaidia Wizara katika kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, nachukua pia fursa hii kuwashukuru nchi washirika wa maendeleo ikiwemo China, Marekani, Ujerumani, Japan, Uturuki, Korea Kusini, Umoja wa Falme za Kiarabu, Misri na taasisi za *INTERPOL*, *IOM*, *EU*, *UNHCR*, *DFID*, *USAID*, *UNICEF*, *WFP* na *Pharm Access* pamoja na wadau wengine wote kwa misaada yao ambayo imeongeza uwezo wa kiutendaji katika Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

Mheshimiwa Spika, maombi ya fedha. Baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu lipitishie makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka 2015/2016 ya shilingi 872,703,062,000 kwa ajili ya bajeti ya matumizi ya kawaida na miradi ya

Nakala ya Mtandao (Online Document)

maendeleo. Kati ya makadirio hayo, shilingi 778,305,656,000 ni za matumizi ya kawaida ambapo shilingi 348,834,203,000 ni matumizi mengineyo na mishahara shilingi 429,471,453,000. Makadirio ya shilingi 94,397,406,000 ni kwa ajili ya mipango ya maendeleo. Mchanganuo ni kama ifuatavyo:-

(a) Fungu 14 – Jeshi la Zimamoto na Uokoaji

(i) Matumizi Mengineyo	Sh.19,861,172,000/=
(ii) Mishahara	Sh.14,521,186,000/=
(iii) Matumizi ya maendeleo	Sh.1,500,000,000/=
Jumla	Sh. 35,882,358,000/=

(b) Fungu 28 – Jeshi la Polisi

(i) Matumizi Mengineyo.....	Sh.196,801,709,000/=
(ii) Mishahara.....	Sh. 284,314,668,000/=
(iii) Matumizi ya maendeleo.....	Sh. 8,510,968,000/=
Jumla	Sh. 489,627,345,000/=

(c) Fungu 29 – Jeshi la Magereza

(i) Matumizi Mengineyo	Sh. 67,665,836,000/=
(ii) Mishahara	Sh.97,750,249,000/=
(iii) Matumizi ya maendeleo	Sh.1,621,716,000/=
Jumla	Sh.167,037,801,000/=

(d) Fungu 51 – Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na NIDA

(i) Matumizi Mengineyo	Sh. 21,776,072,000/=
(ii) Mishahara	Sh. 4,069,558,000/=
(iii) Matumizi ya maendeleo	Sh. 76,964,722,000/=
Jumla	Sh.102,810,352,000/=

(e) Fungu 93 – Idara ya Uhamiaji

(i) Matumizi Mengineyo	Sh. 42,729,414,000/=
(ii) Mishahara.....	Sh. 28,815,792,000/=
(iii) Matumizi ya maendeleo	Sh. 5,800,000,000/=
Jumla	Sh. 77,345,206,000/=
Jumla Kuu	Sh. 872,703,062,000/=

Mheshimiwa Spika, nakushukuru wewe, Waheshimiwa Wabunge wote pamoja na wananchi wote kwa kunisikiliza. Aidha, Hotuba hii pia inapatikana katika tovuti ya Wizara yenye jina www.moha.go.tz.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

**HOTUBA YA WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI MHESHIMIWA MATHIAS
MEINRAD CHIKAWA (MB.), AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA
MATUMIZI YA WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI
KWA MWAKA 2015/2016 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

I. UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia taarifa iliyowasilishwa mbele ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ulinzi na Usalama, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka wa fedha wa 2015/2016.

2. **Mheshimiwa Spika**, awali ya yote naomba kuchukua nafasi hii kutoa salamu za rambirambi kwa familia na wananchi wa mikoa mbalimbali ya Tanzania kutokana na mvua kubwa iliyonyesha katika vipindi tofauti mwaka huu na kusababisha mafuriko na hivyo kuleta adha kubwa kwa wananchi ikiwemo vifo na uharibifu wa mali na miundombinu. Aidha, nawapa pole nyingi ndugu na jamaa wa marehemu waliopoteza maisha yao kutokana na matukio hayo.

3. **Mheshimiwa Spika**, naomba pia kutumia fursa hii kutoa masikitiko yangu kwa familia na wananchi kwa ujumla kutokana na vifo, ulemavu, upotevu na uharibifu wa mali na miundombinu vilivyosababishwa na ajali za barabarani, majini na nchi kavu katika kipindi chote toka mwezi Julai 2014. Aidha, nawapa pole sana ndugu na jamaa wa marehemu waliopoteza maisha katika matukio hayo. Namuomba Mwenyezi Mungu aziweke roho za marehemu wote mahali pema peponi, Amina.

4. **Mheshimiwa Spika**, kwa umuhimu mkubwa sana naomba ninawashukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete na Makamu wa Rais, Mheshimiwa Dkt. Mohamed Gharib Bilal kwa maelekezo yao mbalimbali na Waziri Mkuu Mheshimiwa Mizengo Peter Pinda (Mb), kwa kuhimiza utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

5. **Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya kipekee naomba kumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuonyesha imani kwangu ya kuniamini kuendelea katika nafasi hii ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi. Aidha, napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri aliyoitoa mapema katika mkutano huu wa Bunge ambayo imetoa mwelekeo wa kazi za Serikali kwa ujumla katika mwaka wa fedha 2015/2016.

6. **Mheshimiwa Spika**, napenda kuishukuru kwa dhiti kabisa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ulinzi na Usalama chini ya Mwenyekiti wake, Mheshimiwa Anna Margareth Abdallah, Mbunge wa Viti Maalum, kwa kuyachambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka 2015/2016. Naishukuru pia Kamati hiyo kwa maelekezo na ushauri wao wenye lengo la kuboresha utendaji kazi wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

7. **Mheshimiwa Spika**, majukumu ya msingi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ni kulinda usalama wa raia na mali zao, kuhifadhi na kuwarekebisha wafungwa, kutekeleza Programu ya Huduma kwa Jamii, kuwezesha na kudhibiti uingiaji na utokaji nchini wa raia na wageni, kutoa huduma za zimamoto na uokoaji, kuwahudumia wakimbizi waliopo nchini na kuandaa na kutoa vitambulisho vya Taifa. Majukumu haya yanatekelezwa kupitia Jeshi la Polisi, Jeshi la Magereza, Idara ya Huduma kwa Jamii, Idara ya Uhamiaji, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, Idara ya Wakimbizi na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa.

II. TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MALENGO YA ILANI YA UCHAGUZI YA CCM YA MWAKA 2010 KATIKA KIPINDI CHA 2014/2015

8. **Mheshimiwa Spika**, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ina malengo 7 ya kutekeleza yanayotokana na Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010. Taarifa ya utekelezaji wa malengo hayo kwa mwaka 2014/2015 ni kama ifuatavyo:-

Kujenga vituo na Kupeleka Askari Polisi katika ngazi ya Tarafa/Jimbo

9. **Mheshimiwa Spika**, tangu kuanza kwa dhana ya Polisi Jamii na pia ili kuendana na falsafa ya ugatuaji wa madaraka, Jeshi la Polisi limepeleka katika Tarafa/Jimbo na Kata/Shehia jumla ya askari 7,789 nchi nzima kwa lengo la kupeleka huduma ya kipolisi hadi ngazi ya chini kabisa.

Kuimarisha na Kuboresha Mfumo wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai

10. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2014/2015, ushirikiano wa kiutendaji kati ya Jeshi la Polisi na taasisi zinazounda Jukwaa la Haki Jinai uliendelea kuimarika. Taasisi zinazounda Jukwaa la Haki Jinai ni Jeshi la Polisi, Ofisi ya

Mkurugenzi wa Mashtaka, Jeshi la Magereza na Mahakama. Kwa upande wake Jeshi la Polisi liliendelea kuongeza ufanisi katika upelelezi wa makosa ya jinai na hivyo kufanikiwa kuongeza kiwango cha mafanikio ya kesi mahakamani kwa asilimia 15. Ili kufanikisha lengo hilo Jeshi la Polisi limetoa mafunzo kwa askari wapelelezi 590 wa vyeo mbalimbali ili kuwajengea uwezo katika kukusanya/kujenga ushahidi wa kupeleleza ikiwemo mbinu za kisasa za upelelezi na kufanya ufaulu wa kesi kufikia asilimia 11.8 toka asilimia 3.9 kwa kipindi kama hicho. Aidha, mifumo ya utendaji kazi ndani ya Jeshi la Polisi imeimarishwa. Katika mwaka 2015/2016, Jeshi la Polisi litaongeza kasi na ufanisi zaidi katika upelelezi wa kesi za jinai ili kufikia kiwango cha juu zaidi cha mafanikio.

Kuwapatia Wananchi Mafunzo ya Ulinzi Shirikishi

11. **Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendesha kampeni mahsusni ya kuhamasisha Wizara, Idara na Taasisi mbalimbali za Serikali kujenga miundombinu ya amani katika ngazi za Mikoa, Wilaya, Tarafa/Jimbo na Kata/shehia kwa kutumia sheria na taratibu zilizopo. Aidha, Jeshi la Polisi liliendesha programu 23 zilizolenga kujenga uwezo kwa wananchi katika kupunguza uhalifu katika maeneo yao. Kanda 8 zimepatiwa uwezo wa kuzuia uhalifu kupitia mpango wa mifugo na mazizi salama. Vilevile, warsha 54 za Uhamasishaji zimefanyika kwa wananchi juu ya ulinzi Shirikishi. Jumla ya Kata 1,335 na Shehia 165 zimepatiwa mbinu za kuzuia uhalifu na pia kuingizwa katika Baraza la Maendeleo la Kata (WDC)

Kuimarisha Mafunzo ya Askari wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama

12. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2014/15 Jeshi la polisi limetoa mafunzo ya mbinu za kisasa za upelelezi kwa wakuu wa upelelezi wa Mikoa, Wilaya, Wakaguzi na Askari wa Ngazi za Chini (*Rank and File*) wapatao 250 pamoja na wadau wa haki jinai. Mafunzo hayo yalifanyika katika Mikoa ya Dodoma, Kagera, Kinondoni, Manyara, Mtwara, Mwanza, Singida na Tanga.

Kupunguza msongamano wa Wafungwa na Mahabusu Magerezani

13. **Mheshimiwa Spika**, tatizo la msongamano wa wafungwa na mahabusu katika magereza bado lipo licha ya hatua mbalimbali zinazoendelea kuchukuliwa katika kukabiliana nalo. Hata hivyo idadi ya wafungwa na mahabusu waliokuwa magerezani imepungua kutoka 33,831 Machi, 2014 hadi kufikia 33,027 Machi, 2015. Kati ya hao wafungwa ni 15,504 na mahabusu ni 17,523. Uwezo wa sasa wa Magereza kisheria ni kuhifadhi wafungwa na mahabusu 29,552 ikilinganishwa na uwezo uliokuwepo awali wa kuhifadhi wafungwa 27,653.

14. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2014/2015 Wizara imechukua hatua mbalimbali za kukabiliana na tatizo la msongamano Magerezani kwa njia zifuatazo:-

(i) Kutumia utaratibu wa Parole; ambao unatumika kuwaachia wafungwa wa vifungo virefu wenye tabia njema magerezani ili watumikie sehemu ya vifungo vyao iliyobaki nje ya Magereza chini ya masharti maalum. Hadi kufikia mwezi Machi, 2015 jumla ya wafungwa 258 walifaidika na utaratibu huu. Aidha, juhudi zinaendelea za kuifanyia marekebisho Sheria ya Bodi za Parole Na.25 ya mwaka 1994 ili kuwawezesha wafungwa wengi kunufaika na mpango huu.

(ii) Kutumia kifungo cha nje kwa mujibu wa Sheria ya Magereza Namba 34 ya mwaka 1967. Hadi mwezi Machi, 2015 jumla ya wafungwa 525 walikuwa wanatumikia kifungo cha nje.

(iii) Msamaha wa Mheshimiwa Rais anaoutoa kwa wafungwa kulingana na mamlaka aliyonayo. Jumla ya wafungwa 4,082 walifaidika na msamaha wa Rais uliotolewa tarehe 9 Desemba, 2014 wakati wa sherehe za kuadhimisha miaka 53 ya Uhuru wa Tanzania Bara. Wafungwa wengine 4,129 waliachiliwa kwa msamaha wa Rais uliotolewa tarehe 26 Aprili, 2015 katika kilele cha sherehe za miaka 51 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar.

Kuimarisha uzalishaji wa Mbegu Bora za Kilimo katika maeneo ya Magereza

15. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2014/2015, Jeshi la Magereza limeendelea kulima mbegu bora za kilimo katika mashamba ya Magereza ya Nachingwea – Lindi, Wami Kuu – Morogoro na Karanga – Kilimanjaro. Mbegu zilizolimwa na kutarajiwa kuvunwa ni alizeti tani 50 na ufuta tani 20 ambazo zitauzwa kwa Wakala wa Mbegu za Kilimo nchini (*Agricultural Seed Agency - ASA*). Katika mwaka 2015/2016, Jeshi la Magereza linatarajia kulima na kuhudumia hekta 1,300 za mazao mbalimbali ya mahindi, maharage, mpunga na mazao mengine na kutarajia kuvuna tani 1,000.

Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA)

16. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2014/2015 Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa imeendelea kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya ipasavyo. Mpaka kufikia mwezi machi 2015 imesajili na kuwatambua watu 6,256,768 kwa Zanzibar na katika mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Lindi, Mtwara, Morogoro na Tanga. Aidha, imetengeneza vitambulisho 2,567,980 na kuvigawa kwa wananchi katika mkoa wa Dar es Salaam (2,056,560) na Zanzibar (511,420) ambapo matumizi ya vitambulisho hivyo yameanza. Vitambulisho vya Taifa kwa wananchi wa mikoa

ya Pwani, Lindi, Mtwara, Morogoro, na Tanga vinaendelea kutengenezwa na vitagawiwa kwa kadri taratibu za usajili zinavyokamilika.

17. **Mheshimiwa Spika**, katika jitihada za kuongeza kasi ya utoaji wa Vitambulisho vya taifa, Serikali imeongeza vifaa vya usajili kutoka 280 hadi kufikia 1,506. Vilevile imeingia mkataba na Serikali ya Watu wa Korea kwa ajili ya kupata fedha za kujenga kituo kikuu cha uchakataji na uzalishaji wa vitambulisho vya Taifa, kituo cha uokozi wakati wa majanga pamoja na ofisi 13 za utambuzi na usajili za wilaya ambapo matayarisho ya ujenzi yameanza.

III. HALI YA USALAMA NCHINI **Hali ya Uhalifu**

18. **Mheshimiwa Spika**, wajibu wa kwanza wa Serikali ni kulinda usalama wa raia na mali zao na kuhakikisha uwepo wa amani na utulivu. Nchi yetu imeendelea kuenzi amani na utulivu uliopo kama msingi mkuu wa Taifa ambao umejengwa na kuendelea kuimarishwa tangu tupate uhuru mwaka 1961 na katika kipindi cha miaka 51 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar. Kuwepo kwa amani na utulivu huo kumechangia katika ustawi wa Nchi yetu kiuchumi, kijamii na kisiasa ambapo kumezingatiwa na kutambuliwa kuwa miongoni mwa vipaumbele katika ukuaji wa uchumi wa Taifa letu na maendeleo binafsi ya wananchi wetu. Kwa upande wake, Jeshi la Polisi limeendelea kutekeleza kikamilifu jukumu lake la kikatiba na kisheria la kulinda na kudumisha amani na utulivu nchini kwa kubaini, kuzuia na kutanzua vitendo vya uhalifu, makosa ya usalama barabarani, migogoro, vurugu na fujo.

19. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Julai 2014 hadi Machi, 2015 jumla ya makosa makubwa ya jinai 47,942 yaliripotiwa katika vituo vya Polisi kote nchini ikilinganishwa na makosa 62,756 yaliyoripotiwa katika kipindi kama hiki mwaka 2014. Hii ni pungufu ya makosa 14,814 sawa na asilimia 31. Upungufu huu unatokana na upatikanaji wa taarifa za uhalifu mapema na utekelezaji wa mkakati wa Polisi Jamii unaohusisha ushirikishwaji wa wananchi katika vita dhidi ya uhalifu nchini. Sababu nyingine kuu ni kuongezeka kwa wigo wa doria, misako na operesheni maalum za Jeshi la Polisi mijini na vijijini.

20. **Mheshimiwa Spika**, makosa hayo ya jinai yanayoripotiwa katika vituo vya polisi yamegawanyika katika makundi makuu matatu. Makundi hayo ni makosa dhidi ya binadamu, makosa ya kuwania mali na makosa dhidi ya maadili ya jamii. Makosa ya kuwania mali yamepungua kutoka 37,526 mwaka 2014 hadi 28,520 mwaka 2015. Huu ni upungufu wa makosa 9,006 sawa na asilimia 23.9. Makosa dhidi ya binadamu yamepungua kutoka 11,070 mwaka 2014 hadi 8,715 mwaka 2015. Huu ni upungufu wa makosa 2,355 sawa na asilimia 21.3. Makosa dhidi ya maadili yamepungua kutoka 14,160 mwaka 2014 hadi 10,707 mwaka 2015. Huu ni upungufu wa makosa 3,453 sawa na asilimia

24.4. Upungufu huu umetokana na kuimarika kwa doria, misako na operesheni maalum za Jeshi la Polisi na ushirikiano wa kiutendaji uliopo kati ya Jeshi la Polisi na vyombo vingine vya dola.

21. **Mheshimiwa Spika**, katika miaka ya hivi karibuni ajali za barabarani zimekuwa tishio kwa maisha ya watu na mali. Takwimu zinaonyesha kuwa katika kipindi cha Julai hadi Machi, 2015 ajali za barabarani 8,072 zilitokea katika maeneo mbalimbali ambapo watu 2,883 walipoteza maisha na wengine 9,370 walijeruhiwa. Katika mwaka 2014 ajali zilizotokea ni 45,275 ambazo zilisababisha vifo vya watu 3,799 na wengine 16,635 kujeruhiwa. Pamoja na takwimu za mwaka 2015 kuonyesha kuwa ajali hizo zimepungua, bado ajali hizi zimeendelea kuleta madhara makubwa kwa wananchi. Kwa kuzingatia hali hiyo Serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali zikiwemo marekebisho ya sheria, kanuni na kuimarisha doria na ukaguzi wa vyombo na madereva. Aidha, Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na wadau wengine wa masuala ya usalama barabarani limeendelea kusimamia utekelezaji wa Sheria za Usalama Barabarani ambapo jumla ya makosa madogo madogo 601,550 yaliripotiwa na wakosaji kutozwa faini na wengine kufikishwa mahakamani. Vilevile, takwimu zinaonyesha kuwa vyanzo vikuu vya ajali ni mwendokasi, uzembe wa madereva, ubovu wa vyombo vya usafiri na wakati mwingine ubovu wa miundombinu.

22. **Mheshimiwa Spika**, kutokana na makosa ya usalama barabarani, Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na wadau wengine ambao ni SUMATRA, Shirika la Viwango Tanzania (TBS), TANROADS na Shule za Udereva zilizosajiliwa limeendelea kuchukua hatua za kuzuia na kudhibiti vyanzo vya ongezeko la ajali za barabarani. Hatua hizo ni pamoja na kutoa elimu ya kuzingatia Sheria za Usalama Barabarani kwa watumiaji wa barabara wakiwemo madereva wa bodaboda, kuendeleza doria za masafa mafupi na marefu katika barabara kuu, ukaguzi wa magari, kutumia kamera (tochi) za kutambua madereva wanaoendesha mwendo kasi, kuendelea kusimamia zoezi la utoaji wa leseni mpya za udereva, kuwahamasisha abiria kutoa taarifa mapema za madereva wanaokiuka Sheria za Usalama Barabarani, kuwaelekeza wamiliki wa mabasi kubandika kwenye mabasi yao namba za simu za viongozi wa Polisi na kuwachukulia hatua za kinidhamu askari wanaojihusisha na vitendo vya kuomba na kupokea rushwa toka kwa madereva.

23. **Mheshimiwa Spika**, katika siku za karibuni kumejitokeza matukio ya kuvamiwa kwa vituo vya polisi ambapo askari polisi wameuawa pamoja na kuporwa silaha na risasi. Mnamo tarehe 21 Januari, 2015 usiku huko kituo cha Polisi Ikwiriri - Rufiji majambazi wakiwa na bunduki walivamia kituo cha Polisi na kuwaua askari wawili (2) kisha kupora bunduki aina ya SMG 2, SAR 2, Anti Riot gun 1, Shotgun 1 na risasi 60. Aidha, tukio lingine la kuvamiwa kwa kituo cha polisi lilitokea tarehe 30 Machi, 2015 huko barabara ya Kilwa kwenye kizuizi cha

Polisi eneo la Shule ya Sekondari St. Mathew Kongowe kata ya Vikindu Wilayani Mkuranga. Majambazi wasiofahamika wakiwa na mapanga na silaha zingine za jadi walimuua askari mmoja kisha kupora bunduki 1 aina ya SMG ikiwa na risasi 30.

24. **Mheshimiwa Spika**, kwa ujumla, idadi ya matukio ya uvamizi wa vituo vya polisi imeongezeka kutoka 6 kwa mwaka 2014 hadi 8 kwa mwaka 2015. Katika matukio hayo jumla ya askari 7 waliuawa kwa mchanganuo ufuatao;- Chamazi 2, Mkuranga 2 na Ushirombo 3. Aidha, bunduki 22 ziliporwa ambapo Chamazi 2, Mkuranga 1, Ushirombo 17 na Tanga 2. Serikali kupitia Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi inakemea tabia hii ya kuvamiwa kwa vituo vya polisi ambayo inaambatana na dalili za vimelea vya ugaidi na kuomba jamii iwafichue waovu wanaotenda vitendo hivi ili kuendelea kuwahudumia wananchi vizuri.

25. **Mheshimiwa Spika**, Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na raia wema limeweza kukamata bunduki 20 zilizoporwa au kuibiwa katika vituo vya polisi kama ifuatavyo:- Ushirombo 17, Kisaki 1 na Tanga 2. Kupatikana kwa bunduki katika Mkoa wa Tanga kulisababisha kugundulika kwa kundi la wahalifu katika mapango ya Mleni yaliyopo Amboni, ambapo Jeshi la Polisi lilifanya operesheni katika eneo hilo. Aidha, jumla ya watuhumiwa 23 walikamatwa katika operesheni hiyo ambapo watuhumiwa 9 walifikishwa mahakamani na wengine wamewekwa chini ya uangalizi maalumu.

MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MWAKA 2014/2015 NA MALENGO YA MWAKA 2015/2016

MAPATO NA MATUMIZI

26. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2014/2015, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ilipangiwa kukusanya mapato ya shilingi 156,667,945,791, hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2015, Wizara ilikuwa imekusanya shilingi 125,907,779,521 sawa na asilimia 80.4 ya lengo la mwaka. Katika mwaka 2015/2016, Wizara imelenga kukusanya mapato ya shilingi 178,969,264,691. Mifumo na nguvu zaidi zitaelekezwa katika kuziba mianya ya uvujaji wa mapato hususan katika kuimarisha na kuboresha matumizi ya benki kwa ajili ya kufanya malipo ya huduma zitolewazo na taasisi za Wizara.

27. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2014/2015, Wizara iliidhinishiwa jumla ya shilingi 936,386,935,197 kwa ajili ya bajeti ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo. Hadi kufikia tarehe 31 Machi 2015 jumla ya shilingi 575,119,649,579 zilikuwa zimetumika sawa na asilimia 61 ya bajeti ya mwaka mzima, ambapo shilingi 292,331,740,187 zimetumika kulipia mishahara, matumizi mengineyo shilingi 237,959,341,245 na fedha za maendeleo ni shilingi

44,828,568,147. Katika mwaka 2015/2016, Wizara inategemea kutumia shilingi 872,703,062,000 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo.

JESHI LA POLISI

Maboresho ya Jeshi la Polisi

28. **Mheshimiwa Spika**, napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba Jeshi la Polisi limeendelea na utekelezaji wa awamu ya kwanza ya Programu ya Maboresho ya Jeshi la Polisi ya mwaka 2010/11 hadi 2014/15. Programu hii pamoja na mambo mengine, ililenga kulifanya Jeshi la Polisi kuwa la kisasa, lenye watendaji wenye weledi na linaloshirikiana na jamii katika kubaini, kuzuia, kudhibiti na kukabili uhalifu na vitendo vyote vinavyosababisha uvunjifu wa amani. Jeshi la Polisi litaendeleza kasi ya mabadiliko ya kiutendaji yaliyoanza katika awamu iliyopita ya uongozi. Aidha, ili kupima utekelezaji kwa awamu ya kwanza ulivyofanyika, limemteua mshauri mwelekezi kwa ajili ya kufanya tathmini ya maboresho hayo na kisha kupendekeza hatua madhubuti za kuendelea nayo kwa awamu ya pili. Sambamba na maboresho hayo, **Mitaala ya vyo vyote vya Polisi imebadilishwa na kufuata mfumo wa NACTE unaolenga katika utendaji zaidi (Competency Based Education Training) kuliko ile ya kitaaluma (Knowledge Based Education Training) zaidi.**

Polisi Jamii

29. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2014/15 Jeshi la Polisi liliendelea kuwahamasisha wananchi kutekeleza kwa vitendo dhana ya Polisi Jamii na kuifanya kuwa ni mkakati mkuu wa kuzuia uhalifu katika maeneo wanayoishi. Programu za Usalama Wetu Kwanza, Utii wa Sheria Bila Shuruti, Familia Yetu haina Mhalifu na Ulinzi Shirikishi zimeendelea kupata mwitikio chanya kutoka kwa wananchi. Programu hizi zimewezesha kuanzishwa kwa vikundi vya Ulinzi Shirikishi 9,538 nchi nzima. Hatua hizo ziliwezesha Jeshi kuongeza idadi ya askari wanaofanya kazi kama Maofisa wa Polisi Jamii katika ngazi ya Tarafa/Jimbo na Kata/Shehia kutoka watatu hadi watano kwa kila kata 3,335 na Shehia 338 nchini. Katika mwaka 2015/16 Jeshi la Polisi litaendelea kuongeza idadi ya askari wanaofanya kazi katika ngazi ya Tarafa/Jimbo na Kata/Shehia.

Mauaji ya Wanawake, Wazee na Watu wenye ulemavu wa Ngozi (Albino)

30. **Mheshimiwa Spika**, katika kuhakikisha kuwa mauaji ya wazee hasa wanawake yanadhibitiwa katika mikoa ya Mwanza, Shinyanga, Simiyu, Singida, Geita na Tabora, na pia tatizo la mauaji ya watu wenye ulemavu wa ngozi katika jamii ya kitanzania, Wizara imeunda kikosi kazi maalum kinachojumuisha vyombo vya ulinzi na usalama na taasisi nyingine za haki jinai. Kutokana na hatua hiyo jumla ya watuhumiwa 286 wamekamatwa na kufikishwa

mahakamani ambapo watuhumiwa 30 wamehukumiwa na mahakama, watuhumiwa 28 waliachiwa huru kutokana na ushahidi hafifu, majalada 35 yapo kwa mwendesha mashtaka yakiandaliwa hati za mashtaka na watuhumiwa 193 upelelezi unaendelea.

31. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi hiki tunasikitika kuwa yametokea mauaji ya watu watatu (3) wenye ulemavu wa ngozi katika Mikoa ya Simiyu (1), Singida (1) na Geita (1). Katika matukio hayo watuhumiwa 17 walikamatwa kuhusiana na matukio hayo ambapo 7 walifikishwa mahakamani, watuhumiwa 7 waliachiwa huru kutokana na ushahidi hafifu na watuhumiwa 3 upelelezi unaendelea. Aidha, watu watatu wenye ulemavu huo wamejeruhiwa katika Mikoa ya Tabora (2) na Rukwa (1) kwa kukatwa sehemu mbalimbali za miili yao. Katika matukio haya watuhumiwa 8 walikamatwa, kati ya hao 6 walifikishwa mahakamani na 2 upelelezi unaendelea. Kimsingi matukio haya yanaifedhehesha nchi na hivyo tunaiomba jamii yote ione kuwa tatizo hili ni la kwetu sote na pia tunawaomba tushirikiane ili kuondokana na tabia hii. Katika upande mwingine, jumla ya waganga wa jadi wanaotuhumiwa kupiga ramli chochezi 194 walikamatwa, watuhumiwa 123 wamefikishwa mahakamani, kati ya hao 4 walipatikana na hatia na kupewa adhabu na mahakama. Aidha, watuhumiwa 2 walitakiwa kutojishughulisha na uganga na pia kuwa chini ya uangalizi wa Polisi (*Police Supervisee*) ambapo kesi 71 zipo chini ya upelelezi. Katika mwaka 2015/16 Serikali itahakikisha kuwa mauaji ya wanawake, wazee na watu wenye ulemavu wa ngozi yanadhibitiwa kwa kufanya yafuatayo:-

(i) Kuendelea kushirikiana na raia wema, Mamlaka za Serikali za Mitaa na taasisi zinazoratibu shughuli za waganga wa jadi, kuwabaini, kuwakamata na kuwafikisha mahakamani waganga wanaohibitika kupiga ramli chochezi na kusababisha mauaji ya wazee, wanawake na watu wenye ulemavu wa ngozi.

(ii) Kuendelea kushirikiana na raia wema na Mamlaka za Serikali za Mitaa kuwabaini, kuwakamata na kuwafikisha mahakamani wahalifu wanaokodishwa kufanya mauaji ya wazee, wanawake na watu wenye ulemavu wa ngozi.

(iii) Kuendelea kutumia taarifa za kiintelijensia kuwabaini, kuwakamata na kuwafikisha mahakamani wanaotuhumiwa kutoa fedha kwa waganga wa jadi kwa lengo la kuambiwa waliowaua ndugu zao au kupewa mbinu na masharti ya kupata utajiri wa haraka;

(iv) Kuendelea kuiimarisha Kamisheni mpya ya Intelijensia ya Jinai kwa kuongeza rasilimali watu na vitendea kazi kuanzia ngazi ya Makao Makuu hadi ngazi ya Kata/Shehia ili kujenga uwezo wa kupata taarifa mapema za uhalifu.

(v) Kuendelea kufanya misako ya waganga wanaojihusisha na upigaji rami chochezi na kuwafikisha mahakamani kujibu tuhuma zinazo wakabili.

Kuzuia Biashara ya Madawa ya Kulevya

32. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2014/15 mapambano dhidi ya biashara haramu ya dawa za kulevya yaliendelezwa. Jeshi la Polisi liliendelea kuzifanyia kazi taarifa za wananchi zilizolenga kuwadhibiti wafanyabiashara wa dawa za kulevya. Aidha misako, doria na operesheni maalum zilifanyika nchi nzima ikiwemo katika bahari ya Hindi na fukwe zake, mipakani na viwanja vya ndege ili kudhibiti uingizaji wa dawa za kulevya nchini. Hadi kufikia Desemba 2014 jumla ya kilo 282 za dawa za kulevya za viwandani ambazo ni Heroine, Cocaine, Cannabis resin, morphine na mandrax zilikamatwa, na pia watuhumiwa 395 walikamatwa na kufikishwa mahakamani. Vilevile, kilo 14,036.59 za bhanghi na kilo 3,866.19 za mirungi zilikamatwa ambapo watuhumiwa 7,226 walikamatwa na kufikishwa mahakamani.

Ubadilishanaji wa Taarifa za Wahalifu na Uhalifu

33. **Mheshimiwa Spika**, Jeshi la Polisi limeendelea kushirikiana na vyombo vingine vya Ulinzi na Usalama ndani na nje ya nchi kwa lengo la kuzuia uhalifu unaovuka mipaka usitokee ndani ya ardhi ya Tanzania. Ili kufikia azma hiyo na kwa ushirikiano wa vyombo hivyo, kumeanzishwa mkakati wa kupambana na uhalifu katika maeneo ya mipakani ya Tunduma, Kasumulu na Namanga. Matokeo ya ushirikiano huo yamewezesha kukamatwa kwa watuhumiwa 129 akiwemo kiongozi mkuu aliyekuwa akiendesha mashambulizi dhidi ya polisi mjini Songea. Aidha, mkakati huo utaendelezwa katika maeneo yote nchini. Ili kudhibiti usalama mipakani mbwa 350 na farasi 30 wameongezwa kwenye vituo mbalimbali nchini ikiwemo vya mipakani vilivyopo Himo, Rusumo, Kabanga, Mtukula, Tunduma na Namanga. Katika mwaka 2015/16 Jeshi la Polisi litaendelea kushirikiana na vyombo vya Ulinzi na Usalama ndani na nje ya nchi kwa lengo la kuzuia uhalifu unaovuka mipaka usitokee ndani ya ardhi ya Tanzania.

Kudhibiti Uvunjifu wa Amani unaotokana na Migogoro ya Ardhi

34. **Mheshimiwa Spika**, Jeshi la Polisi limeendelea kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa na Serikali Kuu ili kuzuia mauaji, majeruhi na uharibifu wa mali unaosababishwa na migogoro ya ardhi. Kwa kushirikiana na mamlaka husika kumefanyika utafiti katika mikoa minne juu ya kuimarisha usalama katika matumizi sahihi ya ardhi na jinsi ya kuigawa kwa wakulima na wafugaji katika mikoa ya Morogoro, Dodoma, Singida na Manyara. Aidha, kwa kupitia Jeshi la Polisi kumeanzishwa programu ya Kilimo na Ufugaji Salama. Programu hii itasaidia kuuelimisha umma namna ya matumizi

na ugawaji bora wa ardhi katika himaya zao kwa kuzingatia usalama. Aidha, kumeanzishwa programu ya makazi na wazee salama ili kuzuia mauaji na majeruhi kwa wazee. Katika mwaka 2015/16 Jeshi la Polisi litaendelea kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa na Serikali Kuu ili kuzuia mauaji, majeruhi na uharibifu wa mali unaosababishwa na migogoro ya ardhi.

Kushughulikia Uhalifu katika Shughuli za Kisiasa na Kijamii

35. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2014/15 Jeshi la Polisi liliendelea kufanya kazi za ulinzi wa usalama katika maeneo mbalimbali kwa lengo la kudumisha amani na utulivu nchini. Hatua hii imewezesha kuwepo kwa hali ya utulivu wakati wa Uchaguzi wa Serikali za mitaa mwaka 2014, hali ya Utulivu na Usalama katika michakato ya kisiasa kama mikutano ya vyama vya siasa na shughuli za kila siku za kijamii. Aidha, kwa kuzingatia majukumu muhimu yaliyopo mbele yetu ya kura za maoni kwa katiba inayopendekezwa pamoja na Uchaguzi Mkuu 2015, Jeshi la Polisi linatoa wito kwa wananchi na jamii yote ya Tanzania kwa ujumla kuzingatia umuhimu wa kuwepo amani na usalama katika hatua zote. Vilevile, linawasihi viongozi na wananchi wote kujiepusha na vitendo vya aina yoyote ya uvunjifu wa amani na pia kushirikiana na Jeshi kwa kutoa taarifa stahiki pale dalili au vitendo viovu vinapojitokeza. Katika mwaka 2015/16 Jeshi la Polisi litaendelea kutekeleza wajibu wake wa ulinzi wa usalama na amani kwa ukamilifu kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu.

Ulinzi wa Amani Nje ya Nchi

36. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2014/15 Jeshi la Polisi liliendelea kutoa mchango wake katika Operesheni za Ulinzi wa Amani (*Peace Keeping Missions*) nje ya nchi ambapo jumla ya askari 74 wa vyeo mbalimbali kati yao wanaume 57 na wanawake 17 waliruhusiwa kwenda nchini Sudan. Aidha, ushiriki endelevu wa askari polisi wetu katika kazi za ulinzi wa amani nje ya nchi ni ishara na ushahidi kwamba askari polisi wetu wanao weledi na nidhamu inayokidhi viwango vya kitaifa na kimataifa. Katika mwaka 2015/16, Wizara yangu kupitia Jeshi la Polisi itaendelea kuwaruhusu maafisa, wakaguzi na askari kufanya mitihani maalum itakayowawezesha kushiriki katika Operesheni za Ulinzi wa Amani ndani na nje ya nchi.

Ajira, Mafunzo na Upandishwaji Vyeo Askari Polisi

37. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2014/2015 jumla ya askari polisi wapya 3,193 walijajiriwa. Aidha, askari 3,357 wa vyeo mbalimbali walipandishwa vyeo, kati yao Koplo (CPL) 438, Sajenti (SGT) 734, Sajenti Meja (SSGT) 485, Wakaguzi Wasaidizi (A/INSP) 709, wakaguzi 461, Warakibu Wasaidizi wa Polisi (ASP) 290, Warakibu wa Polisi (SP) 118, Warakibu Waaandamizi wa Polisi (SSP) 75, Kamishna Wasaidizi wa Polisi (ACP) 29, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi

(SACP)1, Naibu Kamishna (DCP) 14 na Kamishna (CP) 3. Kuhusu mafunzo, jumla ya askari na maafisa 792 wamepatiwa mafunzo katika vyuo vya ndani na nje ya nchi. Katika mwaka 2015/2016, Jeshi la Polisi litaajiri askari wapya 3,500 na kuwapandisha vyeo askari 6,274.

Vitendea Kazi na Makazi Kwa Askari Polisi

38. **Mheshimiwa Spika**, idadi ya watu na mahitaji ya huduma ya usalama wa raia na mali zao yanazidi kuongezeka kila mwaka. Ili kukabiliana na changamoto ya uchache wa miundombinu ya makazi kwa askari Polisi, Serikali kupitia Shirika la Uzalishajimali la Jeshi la Polisi (*Tanzania Police Force Corporation Sole*) imeanza kujenga nyumba 330 za askari katika eneo la Kunduchi, nyumba 20 za maafisa wa Polisi eneo la Mikocheni, Kituo cha Polisi daraja A pamoja na ofisi ya Kamanda wa Mkoa (RPC) Mkoa wa kipolisi Kinondoni. Ujenzi huo unafanyika kwa ushirikiano kati ya Shirika na mwekezaji kwa kulifanyia maboresho eneo la Osterbay ambapo ujenzi umefikia asilimia 45.

Usimamizi wa Nidhamu za Askari

39. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2014/2015 hatua za kinidhamu ziliendelea kuchukuliwa kwa maafisa, wakaguzi na askari polisi waliobainika kujihusisha na vitendo vya ukiukwaji wa maadili mema ya Jeshi la Polisi. Jumla ya askari 300 walishtakiwa kijeshi, 118 walipewa adhabu ya kufukuzwa kazi na 19 walifikishwa mahakamani. Aidha, maafisa 13, wakaguzi 2 na askari 54 wa vyeo mbalimbali waliandikiwa barua za onyo. Katika mwaka 2015/2016, Jeshi la Polisi litaongeza upekuzi kwa askari wake na kwa vijana wanaoomba kujiunga na Jeshi ili kuwa na askari wenye nidhamu ya hali ya juu na moyo wa dhati wa kulitumikia Jeshi na Taifa kwa ujumla.

Sifa na Zawadi kwa Askari

40. **Mheshimiwa Spika**, Jeshi la Polisi liliendelea kutoa sifa na zawadi kwa askari waliotekeleza majukumu yao kwa umahiri mkubwa. Katika mwaka 2014/15 jumla ya askari 91 walitunukiwa sifa na zawadi mbalimbali kwa maafisa, wakaguzi, askari na watumishi raia wanaotekeleza majukumu yao kwa ufanisi mkubwa na kuwatunukia sifa na zawadi stahiki. Jeshi la Polisi limetoa sifa/zawadi kwa watendaji 223 walionyesha ubunifu, ujasiri, uadilifu, uaminifu na utendaji mzuri kwa maafisa 7, wakaguzi 11, askari 167, watumishi raia 11 na wadau 27. Aidha, jumla ya shilingi 19,240,000 zimetumika kuwazawadia askari na watumishi hao waliofanya kazi vizuri zaidi kwa kipindi cha Julai hadi Machi, 2015. Katika mwaka 2015/2016, Jeshi la Polisi litaendelea kuwatambua maafisa, wakaguzi, askari na watumishi raia wanaotekeleza majukumu yao kwa ufanisi mkubwa na kuwatunuku sifa na zawadi stahiki.

JESHI LA MAGEREZA

Usafirishaji wa Mahabusu kwenda Mahakamani na Kurudi Magerezani.

41. **Mheshimiwa Spika**, jukumu la kuwasindikiza mahabusu kwenda mahakamani na kurudi Gereza linaendelea kutekelezwa katika Mikoa ya Dar es Salaam na Pwani na Wilaya za Arusha mjini na Dodoma mjini. Utaratibu huu umesaidia mahabusu kusikilizwa kesi zao na kupata haki za kisheria kwa wakati. Katika mwaka 2015/2016, lengo limepangwa kuendelea kuimarisha huduma hii katika Wilaya nyingine za Mkoa wa Dodoma.

Programu za Urekebishaji wa Wafungwa

42. **Mheshimiwa Spika**, Jeshi la Magereza limeendelea kutekeleza programu za urekebishaji wa wafungwa kwa kuwapa stadi katika kilimo na viwanda vidogo vidogo. Aidha, zoezi la matengenezo ya matrekta liliendelea katika vituo vya Babati – Manyara, Ushora – Singida, Kwamgumi – Tanga, Karanga – Kilimanjaro, Ngwala – Mbeya, Nachingwea – Lindi, Kiabakari – Mara, Kongwa - Dodoma, Wami Kuu – Morogoro, Kalilankulu – Katavi, Matongo – Simiyu, Ilagala na Kibondo – Kigoma. Katika mwaka 2015/2016 Jeshi limelenga kuendelea kuyafanyia matengenezo matrekta yaliyopo pamoja na zana zake katika magereza mbalimbali nchini.

43. **Mheshimiwa Spika**, katika kuimarisha shughuli za viwanda vidogo vidogo magerezani, Jeshi limefanya ukarabati wa Kiwanda cha Mianzi kilichopo Gereza Njombe. Aidha, kazi ya kufunga mashine nane (8) za kutengeneza mabakuli na vikombe katika Kiwanda cha Uhunzi Ukonga - Dar es Salaam imekamilika. Kiwanda hiki kitatengeneza mabakuli na vikombe kwa matumizi ya wafungwa magerezani pamoja na kutengeneza vifaa mbalimbali na kuvuza. Katika mwaka wa fedha 2015/2016 Jeshi la Magereza litaendelea kuimarisha viwanda vidogo vidogo vilivyopo katika magereza mbalimbali nchini kwa kuvipatia nyenzo na malighafi ili viendeele kutekeleza jukumu la msingi la kuwarekebisha wafungwa.

44. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2014/2015 Jeshi la Magereza liliendelea na jukumu la urekebishaji wa wafungwa kupitia ufugaji wa ng'ombe wa nyama 8,626 na ng'ombe wa maziwa 2,587 pamoja na mifugo mingine ambayo ni mbuzi, kondoo, nguruwe, sungura, kuku wa mayai na bata weupe. Huduma mbalimbali za mifugo ziliboreshwa kama vile chanjo, dawa za tiba na huduma za kuogeshea mifugo kwenye magereza yote yaliyo na mifugo. Aidha, huduma za uhamilishaji wa mifugo ziliendelea kuboreshwa kwenye Magereza ya Ubena – Pwani, Kingolwira na Mbigiri – Morogoro, King'ang'a – Dodoma, Mugumu – Mara, Kitengule - Kagera, Kilimo Urambo – Tabora na Gereza Arusha. Mwaka 2015/2016, Jeshi la Magereza linatarajia

kuhudumia jumla ya ng'ombe wa nyama 9,300 na ng'ombe wa maziwa 3,000, mbuzi 3,240, kondoo 510 pamoja na wanyama wengine wadogo wadogo kwa kununua chanjo na dawa za kutosha na kuboresha mashamba ya malisho.

Mafunzo kwa Askari na Watumishi wa Jeshi

45. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2014/2015 Jeshi la Magereza limeendelea kutoa mafunzo mbalimbali ndani na nje ya Jeshi kwa ajili ya maafisa na askari. Mafunzo hayo ni yale yanayohusu uendeshaji wa Magereza na taaluma nyingine mbalimbali. Jumla ya askari wapya 1,444 wanaendelea na mafunzo ya awali Chuo cha Magereza Kiwira – Mbeya. Mafunzo mengine yanayoendeshwa kwa sasa ni ya Uongozi wa ngazi ya juu (*Gazetted Officer's course*) wanafunzi 96 na Uongozi Daraja la Pili (*Advanced Leadership course*) wanafunzi 206. Aidha, askari 48 wanaendelea na mafunzo ya Cheti cha Sheria katika Chuo cha Ukonga - Dar es Salaam na askari 75 wanaendelea na mafunzo ya Afisa Mteule (RSM) Chuo cha Kingolwira - Morogoro. Sambamba na hayo, jumla ya askari na watumishi 457 wanajiendeleza katika mafunzo ya taaluma mbalimbali nje ya vyuo vya Jeshi la Magereza. Mafunzo haya yatasaidia sana kuongeza weledi na kuwajengea uwezo wa kiutendaji watumishi hao katika utoaji wa huduma kwa wananchi. Katika mwaka 2015/2016, Jeshi la Magereza linatarajia kuajiri askari wapya 1,500 na watumishi raia 15 na kutoa mafunzo ya uendeshaji wa magereza kwa maafisa na askari 3,200.

Kuboresha Usafiri na Usafirishaji

46. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2014/2015 Jeshi la Magereza limeweza kununua gari saba (7) kwa ajili ya kuboresha shughuli za utawala ambayo ni *station wagon* nne (4), basi kubwa moja (1), basi dogo moja (1) na gari moja (1) la kubebea wagonjwa. Katika kuendelea na juhudi za kuboresha huduma ya usafiri na usafirishaji magerezani, katika mwaka 2015/2016 Jeshi la Magereza linatarajia kununua gari tano (5) aina ya *Station Wagon* kwa ajili ya shughuli za utawala.

Kuimarisha Kilimo cha Umwagiliaji

47. **Mheshimiwa Spika**, katika kuepuka kilimo cha kutegemea mvua, katika mwaka 2014/2015 Jeshi la Magereza liliendelea na ujenzi wa miundombinu ya kilimo cha umwagiliaji katika Gereza Idete – Morogoro. Kazi ya uhamishaji wa njia ya maji imefanyika kwa asilimia 100, ujenzi wa banio la mfereji limejengwa kwa asilimia 95 pamoja na kazi za ujenzi wa tuta na kingo za mfereji mkuu zimekamilika kwa asilimia 70. Katika mwaka 2015/2016 Jeshi linakusudia kuendelea na ukamilishaji wa mradi huo.

Shirika la Uzalishajimali la Magereza

48. **Mheshimiwa Spika**, Shirika la Uzalishajimali la Magereza limeendelea na uzalishaji wa bidhaa zitokanazo na kilimo, mifugo na viwanda vidogo vidogo. Kwa upande wa kilimo, jumla ya eneo la ekari 4,500 limelimwa kwa matarajio ya kuvuna tani 5,265 za mazao mbalimbali. Aidha, Shirika kupitia Kikosi cha Ujenzi cha Jeshi la Magereza limeendelea kufanya kazi mbalimbali za ujenzi wa majengo ya Taasisi za Serikali na watu binafsi zikiwemo za ujenzi wa uzio wa Tume ya Sayansi na Teknolojia Kijitonyama - Dar es Salaam, ujenzi wa maghala ya kuhifadhi chakula ya Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula Chang'ombe – Dar es Salaam pamoja na maandalizi ya ujenzi wa jengo la Ofisi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi - Dodoma. Matarajio ya mwaka 2015/2016 ni kuongeza shughuli za uzalishaji kwa kuingia ubia na wawekezaji wa ndani na nje ya nchi ili kupata mtaji wa kutosha kuweza kukidhi soko la bidhaa zitokanazo na kilimo, mifugo, samani za ofisi, samani za nyumbani, bidhaa za ngozi na shughuli za ujenzi.

Matumizi ya Nishati Mbadala Magerezani

49. **Mheshimiwa Spika**, katika kukabiliana na changamoto zinazotokana na matumizi makubwa ya kuni magerezani na hivyo kuwepo fishio la uharibifu wa mazingira, Jeshi la Magereza limeendelea kuchukua hatua za kuanza matumizi ya gesi itokanayo na tungamotaka (*Biogas*) na makaa ya mawe kama nishati mbadala kwa ajili ya kupikia chakula cha wafungwa magerezani. Matumizi ya gesi itokanayo na tungamotaka yanaendelea katika Gereza Ukonga. Aidha, matumizi ya makaa ya mawe yanaendelea katika Magereza ya Songwe, Tukuyu na Ruanda yaliyopo mkoani Mbeya. Kwa sasa, Jeshi lipo katika mchakato wa kutumia majiko yanayotumia kuni kidogo ambayo yameanza kutumika katika Gereza Karanga, Mwanga – Kilimanjaro, Kibondo, Bangwe – Kigoma na Sumbawanga – Rukwa. Matarajio ni kueneza matumizi ya nishati hii katika magereza mengine yenye matumizi makubwa ya kuni kadri uwezo wa fedha utakavyoruhusu.

Utunzaji na Hifadhi ya Mazingira

50. **Mheshimiwa Spika**, utunzaji wa mazingira ni miongoni mwa shughuli za kila siku za Jeshi la Magereza. Shughuli za kuandaa vitalu vya miche na upandaji miti zinaenda sambamba na maandalizi ya msimu wa kilimo kwa kila kituo. Katika kuadhimisha siku ya upandaji miti kitaifa tarehe 1 Aprili, 2014 ilipandwa jumla ya miti 221,850 katika magereza yote nchini. Aidha, Mradi wa Hifadhi ya Mazingira na Upandaji miti ambao unatekelezwa na Jeshi la Magereza kwa ushirikiano na *Tanzania Forest Fund* katika Magereza ya Mgagao, Isupilo – Iringa, Kambi Ihangana – Njombe na Mkwaya – Ruvuma umewezesha kupandwa jumla ya miti 800,000. Katika mwaka 2015/16 Jeshi

litayaingiza magereza mengine katika mpango huo ambayo ni Magereza Msalato - Dodoma, Bariadi - Simiyu na Ngudu – Mwanza.

IDARA YA UHAMIAJI

51. **Mheshimiwa Spika**, Idara ya Uhamiaji ina jukumu la kudhibiti uingiaji, utokaji na ukaaji wa wageni, na pia kuwawezesha raia wa Tanzania kupata hati za kusafiria. Aidha, Idara hii ndio inayoratibu mchakato wa maombi ya uraia kwa wageni wanaoomba uraia wa Tanzania.

Hali ya Ulinzi na Usalama Mipakani.

52. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Julai hadi Machi, 2015 Idara iliendelea kutoa huduma kwa kufuata sheria na kanuni za kiuhamiaji kwenye mipaka kwa wageni wanaoingia na kutoka nchini. Katika kipindi hicho, jumla ya wageni 1,005,652 waliingia na wengine 892,614 walitoka.

Misako na Doria

53. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi hiki cha Julai 2014 hadi Machi, 2015 Idara ya Uhamiaji iliendelea kufanya doria na misako sehemu mbalimbali za migodini, mahoteli na kwengineko yenye lengo la kudhibiti wahamiaji haramu nchini. Jumla ya watuhumiwa wa uhamiaji haramu 3,944 walikamatwa na kuchukuliwa hatua mbalimbali za kisheria ikilinganishwa na wahamiaji haramu 5,576 waliokamatwa katika kipindi hiki mwaka jana. Kupungua kwa watuhumiwa wa uhamiaji waliokamatwa kunatokana na kuongezeka kwa udhibiti na hivyo kuogopa kuingia au kuishi nchini kinyume cha sheria. Katika mwaka wa fedha 2015/2016 Idara ya Uhamiaji inatarajia kununua gari 24, lori 1, pikipiki 57 na boti 7 kwa ajili ya kuimarisha shughuli za misako na doria dhidi ya wahamiaji haramu katika sehemu mbalimbali nchini zikiwemo zile za mipakani.

Vibali Mbalimbali Vilivyotolewa kwa Wageni

54. **Mheshimiwa Spika**, Wizara kupitia Idara ya Uhamiaji imetoa vibali vya ukaazi kwa wageni wawekezaji, wageni waliopata ajira katika makampuni mbalimbali na wageni wengine walioingia nchini kwa malengo mbalimbali kwa kufuata sheria na taratibu za kiuhamiaji kulingana na aina ya kibali kinachoombwa na mgeni. Jumla ya wageni 13,603 walipewa hati za ukaazi kwa mchanganuo ufuatao; daraja "A" 1,088, daraja "B" 9,016 daraja "C" 3,499, hati za ufuasi 357 na hati za msamaha 2,159.

Hati za Safari.

55. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Julai 2014 hadi Machi 2015, Idara ya Uhamiaji imetoa jumla ya hati za safari 48,553 kwa Watanzania waliotaka kusafiri nje ya nchi kwa madhumuni mbalimbali. Kati ya hati hizo 46,779 ni za kawaida, 1,346 ni za Afrika Mashariki, 303 za Kibalozi, na 125 za Kiutumishi. Aidha, kukua kwa hali ya utandawazi kumesababisha kubadilika kwa teknolojia ya udhibiti wa pasipoti na hati nyingine za safari. Ili kukabiliana na hali hiyo, Idara inaendelea na mchakato wa kuhakikisha huduma za kiuhamiaji zinatolewa kwa njia ya ki-elektroniki (Uhamiaji mtandao), ambapo huduma za uhamiaji kama vile utoaji wa hati za safari, vibali vya ukaazi na visa zitatolewa kwa njia ya ki-elektroniki na kuongezewa alama za siri.

Wageni Waliopatiwa Uraia wa Tanzania

56. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Julai 2014 hadi Machi, 2015 wageni 192 walipatiwa uraia. Wageni waliopata uraia ni wa kutoka India (86), Pakistani (18), Kenya (14), Somalia (5), Uingereza (4), Italia (1), Rwanda (6), Yemeni (33), Burundi (2), Lebanon (2), China (4), Lesotho (1), Bangladesh (1), Zimbabwe (1), Wasiokuwa na Utaifa (1), Ureno (1), Ghana (2), Sudan (1), Sirilanka (4), Eritrea (1), Ukraine (1), Urusi (1), na Guinea Bissau (2).

Watanzania waliopatiwa Uraia wa Mataifa Mengine na Waliorudishwa Nchini

57. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Julai 2014 hadi Machi, 2015, Watanzania 38 waliukana uraia wa Tanzania kwa sababu mbalimbali na kupata uraia wa mataifa mengine kama ifuatavyo; Ujerumani (11), Namibia (2), Norway (11), Botswana (2), Uganda (2), Belgium (1), Lesotho (1), Sweden (1), Urusi (1), Kenya (1) na Uingereza (5) hivyo kupoteza haki ya kuwa raia wa Tanzania kwa mujibu wa Sheria ya Uraia Na.6 ya mwaka 1995. Aidha, katika kipindi hiki Watanzania watoro (stowaways) 39 walirudishwa nchini toka nchi mbalimbali (hususan nchi za kusini mwa Afrika).

Ajira na Mafunzo

58. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Julai 2014 hadi Machi 2015, Idara ya Uhamiaji imewapeleka askari wapya 298 kwenye mafunzo ya awali ya uhamiaji katika Chuo cha Polisi Moshi (MPA). Watumishi 71 waliopo kazini wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi na mrefu ndani ya nchi, kati yao watumishi 25 walihudhuria mafunzo ya muda mfupi na 46 walihudhuria mafunzo ya muda mrefu. Katika mwaka 2015/2016, Idara ya Uhamiaji inatarajia kuajiri watumishi wapya 1,066 na kutoa mafunzo kwa watumishi 600 waliopo kazini.

Majengo ya Ofisi

59. **Mheshimiwa Spika**, Idara ya Uhamiaji imekamilisha ujenzi wa Ofisi ya Uhamiaji Mkoa wa Singida. Aidha, ujenzi wa Ofisi za Uhamiaji katika Mikoa ya Manyara, Pwani, Geita, Mtwara na Lindi unaendelea. Aidha, Mshauri elekezi amepatikana kwa ajili ya kukamilisha michoro ya ujenzi wa ofisi katika Wilaya ya Ileje - Mbeya na Kituo cha Kirongwé Wilayani Rorya mkoani Mara ambapo ujenzi utanza mwaka wa fedha 2015/2016. Pia katika mwaka wa fedha 2015/2016 Idara inatarajia kufanya ukarabati wa awamu ya pili wa majengo ya Chuo cha Uhamiaji – Moshi na jengo la Makao Makuu – Dar es Salaam.

Makazi ya Askari

60. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2014/2015, Idara ya Uhamiaji imekamilisha ujenzi wa nyumba tano za viongozi Mtoni Kijichi – Dar es Salaam pamoja na nyumba za Afisa Uhamiaji Mkoa wa Ruvuma. Idara inaendelea pia na ujenzi wa nyumba ya makazi ya Maafisa Uhamiaji wa Mikoa ya Kigoma na Mwanza. Aidha, mshauri mwelekezi amepatikana kwa ajili ya kukamilisha michoro ya nyumba za makazi ya askari huko Kisongo mkoani Arusha na ambapo ujenzi utanza mwaka wa fedha 2015/2016. Vilevile, Idara itafanya ukarabati wa nyumba za makazi kumi na saba (17) mkoani Tabora katika mwaka wa fedha 2015/2016.

JESHI LA ZIMAMOTO NA UOKOAJI

61. **Mheshimiwa Spika**, jukumu la msingi la Jeshi la Zimamoto na Uokoaji ni kuinga na kupunguza vifo, majeruhi, uharibifu wa mali unaotokana na moto, mafuriko, ajali za barabarani, kimbunga na dharura zote zisizo za jinai.

Hali ya vituo vya Zimamoto na Uokoaji Nchini

62. **Mheshimiwa Spika**, Jeshi la Zimamoto na uokoaji lina jumla ya vituo 52 nchi nzima tofauti na mahitaji halisi ambayo ni vituo 152 vinavyotakiwa kuwepo. Hali hii inasababisha kuwepo na mahitaji makubwa ya huduma hii muhimu hususan katika maeneo ya wilayani. Katika mwaka 2015/16 Jeshi linatarajia kujenga vituo vitatu (3) vya zimamoto katika jiji la Dar es Salaam. Aidha, Jeshi lina mahitaji makubwa ya gari za kuzima moto kwani katika gari 83 zilizopo nchi nzima gari 35 ndio nzima ambapo mahitaji ni gari zisizopungua 280 ili kutoa huduma kwa ufanisi. Katika mwaka 2015/16 Jeshi linatarajia kununua gari moja (1) la kuzimia moto pamoja na gari tano (5) kwa ajili ya shughuli za ukaguzi

Ukaguzi wa tahadhari na kinga dhidi ya moto na majanga

63. **Mheshimiwa Spika**, moja ya jukumu la msingi la Jeshi la Zimamoto na Uokoaji ni kufanya ukaguzi wa tahadhari na kinga dhidi ya moto nchi nzima. Katika mwaka 2014/15 kufikia mwezi Machi, 2015 Jeshi limekagua jumla ya maeneo 38,441. Katika mwaka wa fedha 2015/16 Jeshi linatarajia kukagua maeneo 63,500 nchi nzima.

Matukio ya moto na majanga mengine

64. **Mheshimiwa Spika**, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji limeendelea kutekeleza majukumu yake ya msingi hususan kupambana na majanga ya moto pamoja na kufanya maokozi mbalimbali. Mpaka kufikia mwezi Machi, 2015, Jeshi limeshiriki kuzima moto katika matukio 2,018 nchi nzima. Aidha, Jeshi limefanya maokozi 607 katika maeneo mbalimbali nchini yakiwemo mafuriko wilayani Kahama mkoani Shinyanga, mkoani Mwanza na katika jiji la Dar es Salaam.

Mafunzo kwa Askari na Watumishi

65. **Mheshimiwa Spika**, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji limeendelea na juhudi mbalimbali ili kuwapatia askari na maafisa wake mafunzo kwa lengo la kuboresha utendaji katika majukumu yake. Katika mwaka 2014/15 watumishi askari na raia wamepatiwa mafunzo katika maeneo mbalimbali ikiwemo mafunzo ya ndani na nje ya nchi. Katika mafunzo ya ndani ya nchi, watumishi 16 wamepatiwa mafunzo kama ifuatavyo; shahada (6), shahada (5) na shahada ya Uzamili (5) na katika mafunzo ya nje ya nchi, maafisa watano (5) walipatiwa mafunzo ya ulinzi na usalama nchini China. Aidha, Askari na Maafisa 800 walipatiwa mafunzo ya uaskari na namna ya kukabiliana na majanga ya moto. Katika mwaka 2015/16 Jeshi litaendelea kutoa mafunzo kwa askari na watumishi mbalimbali ili kuboresha utendaji kazi.

Elimu kwa Umma

66. **Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka 2014/2015 Jeshi la Zimamoto na Uokoaji limeendelea kutoa elimu kwa umma juu ya namna ya kukabiliana na majanga mbalimbali ya moto kupitia vyombo vya habari ikiwemo televisheni, radio, magazeti na matangazo kupitia gari za Zimamoto na Uokoaji. Katika mwaka wa fedha, 2015/2016 Jeshi la Zimamoto na Uokoaji litaongeza kasi ya utoaji elimu kwa umma kwa lengo la kupunguza majanga ya moto na mengineyo nchini.

MAMLAKA YA VITAMBULISHO VYA TAIFA (NIDA)

67. **Mheshimiwa Spika**, Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa katika mwaka wa fedha 2014/15 imesajili wananchi wa mkoa wa Pwani (505,408), Lindi (353,442), Mtwara (512,827), Morogoro (862,392) na Tanga (847,900). Aidha, imetengeneza vitambulisho 1,269,829 vya wanachi wa Unguja na Pemba pamoja na mkoa wa Dar-es-Salaam na ugawaji wa vitambulisho hivyo kwa wananchi hao unaendelea. Aidha, Mamlaka imenunua vifaa vya usajili (MEU) 1,000, vifaa vya kugawia vitambulisho (PCID) 200, mashine za kusomea vitambulisho (Card Readers) 600 na mashine za kuchapishia vitambulisho (Printer) 2. Vilevile, imeanza ujenzi wa kituo cha kutunzia kumbukumbu na kituo cha uokozi wakati wa majanga (Data recovery centre) na ofisi 13 za usajili za wilaya Tanzania Bara na Zanzibar. Mamlaka imefanya ukarabati katika ofisi za wilaya zinazotumika katika zoezi la utambuzi na usajili katika mikoa ya Pwani, Morogoro, Lindi, Mtwara na Tanga. Vilevile, imeajiri watumishi wapya 216.

68. **Mheshimiwa spika**, katika mwaka wa fedha 2015/2016 Wizara yangu kupitia Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa imepanga kufungua ofisi za usajili katika Wilaya hapa nchini na kuendelea kusajili wananchi katika Wilaya hizo. Mamlaka itanunua vifaa vya usajili 500, vifaa vya kugawia vitambulisho 700, mashine za kusomea vitambulisho 1,300. Aidha, itaendelea na zoezi la uwekaji wa mitandao ya mawasiliano kati ya ofisi za Wilaya na Makao Makuu pamoja na shughuli ya upanuzi wa jengo la Makao Makuu ya Mamlaka. Vilevile, itaajiri watumishi wapya 800.

69. **Mheshimiwa Spika**, Wizara yangu kupitia Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa katika mwaka wa fedha 2015/16 inalenga kuzishirikisha taasisi nyingine za Serikali katika usajili wa makundi maalumu ya watu ili kupunguza gharama za usajili. Kwa kuanzia itashirikiana na Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu katika kuwasajili wanafunzi wote katika vyuo vya elimu ya juu ili vitambulisho visaidie katika utoaji na urejeshwaji wa mikopo kwa wanafunzi hao, itashirikiana na Mamlaka nyingine husika katika usajili wa madereva kwa ajili ya kuwatambua. Aidha, itashirikiana na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) katika kuongeza wigo wa kuwasajili wanachama wapya wa mfuko ambao watumia kitambulisho cha taifa katika kupata huduma za mfuko huo.

HUDUMA KWA JAMII

70. **Mheshimiwa Spika**, Idara ya Probesheni na Huduma kwa Jamii ambayo inasimamia utekelezaji wa Adhabu Mbadala wa Kifungo gerezani, chini ya Sheria ya Probesheni na Sheria ya Huduma kwa Jamii hivi sasa inatekeleza Programu hiyo kwenye Wilaya 63 za Mikoa 21 ya Tanzania Bara, ambayo ni Arusha, Dar es Salaam, Dodoma, Iringa, Kilimanjaro, Mara, Mbeya, Tanga, Singida, Mtwara, Mwanza, Ruvuma, Shinyanga, Kagera, Pwani,

Morogoro, Njombe, Geita, Tabora, Simiyu na Manyara. Hadi kufikia Machi, 2015 jumla ya Taarifa za Uchunguzi wa Kijamii 1,575 ziliandaliwa na kuwezesha wafungwa 1,217 kunufaika na programu hiyo ambapo wanaume ni 940 na wanawake ni 277. Miongoni mwa wafungwa hao, 132 wametumikia adhabu ya Probesheni na wafungwa 1,085 wametumikia adhabu ya Huduma kwa Jamii kwa kufanya kazi za kijamii, hivyo kupunguza gharama za uendeshaji katika magereza na vilevile taasisi wanazozifanyia kazi. Katika mwaka wa fedha 2015/2016 Wizara inatarajia kuongeza mikoa mingine miwili ya Kigoma na Rukwa, hivyo kufanya wigo wa matumizi ya Adhabu Mbadala kufikia mikoa 23 ya Tanzania Bara. Aidha, wahalifu wa vifungo vya muda mfupi usiozidi miaka mitatu wataendelea kusimamiwa kutekeleza Adhabu Mbadala nje ya kifungo gerezani.

HUDUMA KWA WAKIMBIZI

71. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2014/2015, Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya Marekani imeanza kutekeleza Mpango Maalum wa kuwahamishia nchini Marekani wakimbizi wenye asili ya DRC na Burundi wapatao 32,000. Maandalizi yanaendelea ya kuanza kukarabati uwanja wa ndege wa Kasulu ili uweze kutumika kuwasafirisha wakimbizi hao pamoja na kujenga miundombinu itakayotumika katika zoezi hilo (*resettlement processing facility*). Wakati huo huo, utaratibu wa kuwahamishia Wakimbizi katika nchi ya tatu umeendelea kutekelezwa. Katika kipindi cha kuanzia Julai 2014 hadi Aprili, 2015 wakimbizi 877 walipelekwa huko Ulaya na Marekani.

72. **Mheshimiwa Spika**, katika kuongeza udhibiti wa wakimbizi wanaotoroka kwenye makambi/makazi yao na kwenda maeneo yasiyo stahili, Wizara imekamilisha uhakiki wa wakimbizi, kuwapiga picha na kuchukua alama za vidole ambazo zinawekwa kwenye kanzidata (*database*). Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, uhakiki huo ulikamilika mwezi Agosti, 2014 ambapo jumla ya wakimbizi 57,127 walihakikiwa na kuchukuliwa alama za vidole pamoja na kupigwa picha.

73. **Mheshimiwa Spika**, kutokana na kuzuka kwa vurugu kuelekea Uchaguzi Mkuu wa Burundi, katika kipindi cha mwezi Aprili na Mei, 2015 Tanzania imepokea wakimbizi wapya takribani 20,000 walioingia nchini kupitia mkoa wa Kigoma. Kwa upande mwingine hali ya amani na utulivu nchini DRC bado haijatengemaa, hivyo zoezi la uhamasishaji wa urejeaji wa hiyari halifanyiki kwa sasa. Kabla ya kuanza kupokea wimbi jipya la wakimbizi toka Burundi, nchi yetu ilikuwa na wakimbizi 89,069 kutoka mataifa ya DRC, Burundi na wachache kutoka nchi za Somalia, Rwanda, Uganda na Sudani ya Kusini. Aidha, Serikali imehitimisha suala la waliokuwa wakimbizi toka Burundi wa mwaka 1972 wapatao 162,156 kwa kuwapa uraia na kuwaruhusu kuishi nchini kihalali.

URATIBU WA KUSHUGHULIKIA MALALAMIKO

74. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2014/2015 Wizara kupitia Idara ya Kushughulikia Malalamiko imeendelea kutekeleza majukumu mbalimbali ya kuwahudumia wananchi wenye malalamiko kuhusu vyombo vya usalama chini ya Wizara. Hadi kufikia Machi, 2015 jumla ya malalamiko 132 yalipokelewa kwa njia ya barua, simu, barua pepe, nukushi na ana kwa ana yalishughulikiwa. Kati yake malalamiko 93 yalipatiwa ufumbuzi na wahusika kujulishwa na mengine 39 yanaendelea kushughulikiwa. Katika mwaka 2015/16 Wizara itaendelea kupokea na kushughulikia malalamiko ya wananchi na watumishi wa Wizara na kufanya uchunguzi wa kina ndani na nje ya ofisi.

VITA DHIDI YA BIASHARA HARAMU YA USAFIRISHAJI WA BINADAMU

75. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha wa 2014/2015 Sekretarieti ya Kupambana na Biashara Haramu ya Usafirishaji wa Binadamu imeratibu vikao vinne vya Kamati ya Kitaifa ya Kupambana na Biashara Haramu ya Usafirishaji wa Binadamu. Aidha, imekamilisha kuandaa Kanuni 2 za Sheria ya Kupambana na Biashara Haramu ya Usafirishaji wa Binadamu nchini na vilevile kusambaza Kitabu cha anwani na majina ya Watoa Huduma kwa waathirika wa Biashara Haramu ya Usafirishaji Binadamu (*Directory of Service Provider*). Katika mwaka 2015/16 Kamati itaendelea kutoa elimu zaidi kwa umma juu ya kupambana na Biashara Haramu ya Usafirishaji wa Binadamu, kuimarisha Sekretarieti yake na kuendelea kutengeneza na kutoa elimu kwa wadau juu ya kanuni za Sheria ya Kupambana na Biashara Haramu ya Usafirishaji Binadamu ya Mwaka 2008.

USAJILI WA VYAMA VYA KIJAMII NA VYA KIDINI

76. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2014/2015 Wizara imeendelea na jukumu la usajili na ukaguzi wa Vyama vya Kijamii na Kidini kwa lengo la kuvisimamia ili kuhakikisha kunakuwepo na amani na utulivu katika jamii. Hadi kufikia mwezi Machi, 2015 maombi ya vyama 571 yalipokelewa ambapo 501 ni ya vyama vya kijamii na 70 ni ya kidini. Kati ya maombi hayo, vyama 457 vilisajiliwa ambapo 415 ni vya kijamii na 42 ni vya kidini. Maombi ya vyama 32 yalikataliwa ambapo 23 ni ya kidini na 9 ni ya kijamii. Maombi ya vyama 82 yanaendelea kushughulikiwa. Aidha, ukaguzi wa vyama umefanyika katika Mkoa wa Kigoma. Uhakiki wa vyama umeendelea kufanyika ikiwa ni pamoja na kuboresha kanzidata ili kuwa na kumbukumbu sahihi kwa vyama vyote vilivyosajiliwa ambavyo vipo hai. Vilevile, hatua za kuvifutia usajili vyama visivyotekeleza wajibu wao kulingana na Sheria zimeanza kuchukuliwa, ambapo jumla ya vyama 24 vimepewa taarifa ya kusudio la kuvifuta. Hatua hizi zinaendelea kuchukuliwa kwa vyama vingine zaidi. Katika mwaka wa 2015/2016

Wizara itaendelea kusajili vyama, kufanya uhakiki wa vyama vilivyo hai na kufanya ukaguzi katika Mikoa 9 ya Tanzania Bara.

KUIMARISHA MATUMIZI YA TEHAMA WIZARANI

77. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2014/2015 Wizara imeendelea na mkakati wa kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika maeneo mbalimbali ili kuboresha huduma zitolewazo. Aidha, imefunga miundombinu ya kimtandao katika Makao Makuu ya Wizara Dar es Salaam na kwenye Ofisi za Wizara Dodoma. Kupitia mradi wa *Government Network* imefunga miundombinu ya mtandao na pia kutoa mafunzo kwa wataalamu kuhusu matumizi ya miundombinu hiyo. Katika mwaka 2015/16 Wizara itaendelea na mkakati wa kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika huduma inazotoa sambamba na kufanya mapitio ya Mpango Mkakati wa TEHAMA wa Wizara wa mwaka 2011/12 - 2013/14.

KUBOresha SERA, SHERIA, KANUNI NA MIKAKATI

78. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2014/2015 Wizara imeendelea na hatua za kuboresha sera, sheria, kanuni na mikakati mbalimbali ili kuimarisha utendaji kazi na huduma inazozitoa katika jamii. Jumla ya rasimu 3 za sera zimeandaliwa, sera 1 ipo katika mapitio, sheria mbili zimepitishwa na Bunge na rasimu za sheria 3 zipo katika hatua mbalimbali za maandalizi. Aidha, kanuni mbalimbali za sheria zimeandaliwa na kuidhinishwa. Katika mwaka 2015/16 Wizara itaendelea na ukamilishaji wa undaji wa sera, sheria, kanuni na mikakati mbalimbali ili kuidhinishwa na kuanza kutumika.

MAPAMBANO DHIDI YA VVU/UKIMWI

79. **Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kuchukua juhudi mbalimbali za kukabiliana na maambukizi mapya ya virusi vya UKIMWI na UKIMWI kwa Askari na Watumishi wote wa Wizara. Juhudi hizi ni pamoja na utekelezaji wa kazi mbalimbali za mapambano hayo katika Vyombo vya Ulinzi na Usalama na Idara ndani ya Wizara.

80. **Mheshimiwa Spika**, Jeshi la Magereza limeendeleza juhudi mbalimbali za kuimarisha mapambano hayo kwa kutoa mafunzo ya elimu rika kuhusu UKIMWI kwa askari, familia za askari na wafungwa pamoja na kuendelea kuwahamasisha watumishi wa Jeshi la Magereza na wafungwa kupima kwa hiari ili kujua hali ya afya zao kuhusu maambukizi ya Virusi vya UKIMWI. Juhudi hizo ni pamoja na kuimarisha huduma za tiba na matunzo kwa watu waishio na VVU katika Zahanati na Vituo vya Afya vya Magereza ya Ubena, Ruanda, Butimba, Arusha, Mtego wa Simba, Segerea, Ukonga, Mahabusu Iringa, Bangwe na Chuo cha Maafisa Ukonga. Aidha, kwa kupitia ufadhili wa Shirika la

Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Udhhibiti wa Uhalifu na Dawa za Kulevya (UNODC), mafunzo yametolewa kwa watumishi 40 ambao watakuwa waelimishaji wa masuala ya UKIMWI katika Magereza ya Idete – Morogoro, Njombe, Kongwa - Dodoma, Mkuza - Pwani, Mahabusu Sumbawanga-Rukwa, Malya-Shinyanga, Biharamulo - Kagera, Tarime - Mara, Mbozi - Mbeya na Kibondo - Kigoma. Katika mwaka wa fedha 2015/2016, mkazo zaidi utakuwa katika kutoa elimu ya kujikinga kuepukana na UKIMWI kwa wafungwa na mahabusu magerezani na pia kwa askari na familia zao pamoja na kuhimiza uanzishwaji wa vikundi vya watumishi na wafungwa waishio na VVU (*Post test Clubs*) katika vituo mbalimbali vya Magereza nchini.

81. **Mheshimiwa Spika**, Idara ya Uhamiaji imeendelea kutoa elimu pamoja na kuwahudumia watumishi wanaoishi na VVU na UKIMWI kwa lengo la kupunguza maambukizo mapya ya UKIMWI mahala pa kazi kwa familia za askari. Aidha Idara ya Uhamiaji imesambaza vipeperushi katika vituo vya kuingilia nchini vinavyolenga kutoa elimu juu ya maambukizo ya VVU na UKIMWI pamoja na athari zake. Pia siku ya watumishi na familia (*family day*) kwa watumishi wa Idara ya Uhamiaji katika mikoa yote ya Tanzania iliadhimishwa ambapo watumishi na familia zao walihudhuria na kupata ushauri nasaha kuhusu VVU na UKIMWI pamoja na kupima afya zao.

82. **Mheshimiwa Spika**, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji limetekeleza afua (*interventions*) mbalimbali kama vile mafunzo ya elimu rika kuhusu UKIMWI kwa Askari na Maafisa, pamoja na watumishi raia. Aidha katika mwaka 2015/16 Jeshi litaendelea kuwahamasisha Askari na watumishi kupima afya kwa hiari ili kujua hali zao kuhusu maambukizi ya Virusi vya UKIMWI.

USHIRIKISHAJI WA WAFANYAKAZI NA USHIRIKI KATIKA MICHEZO

83. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2014/15 Wizara imeendelea kuwashirikisha wafanyakazi katika maamuzi mbalimbali yanayohusu utendaji kazi wa Wizara kupitia Mabaraza ya Wafanyakazi yaliyopo. Jumla ya vikao viwili vya kisheria vya Baraza la Wafanyakazi vilifanyika na uamuzi mbalimbali kufikiwa. Aidha, watumishi wameweza pia kushiriki na kushinda kwa kishindo michezo mbalimbali ikiwemo ile ya SHIMIWI, Mei Mosi na BONANZA kwa lengo la kujenga afya zao na kukuza ushirikiano baina yao. Katika mwaka 2015/2016 Wizara itaendelea kuwashirikisha wafanyakazi katika maamuzi yanayofikiwa kwa mujibu wa sheria na pia kutoa nafasi ya kushiriki katika michezo.

MAFUNZO, AJIRA MPYA NA KUPANDISHWA VYEO WATUMISHI

84. **Mheshimiwa Spika**, katika jitihada za kuwaendeleza kitaaluma watumishi ndani ya Wizara, watumishi 20 waliweza kuhudhuria mafunzo ya muda mrefu katika kozi mbalimbali zikiwemo za shahada, stahada na cheti.

Aidha, mafunzo ya awali kwa waajiriwa wapya 15 yalitolewa na watumishi wapya 9 walijiriwa pamoja na kuidhinisha ajira 52 za wataalamu wa kigeni hususan katika makambi ya wakimbizi. Vilevile, watumishi 132 walipandishwa vyeo na watumishi 19 walithibitishwa kazini. Katika mwaka 2015/16 Wizara inatarajia kuwapeleka masomoni watumishi 42 katika mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu na kuwapandisha vyeo watumishi kadri watakavyopata sifa kulingana na miundo yao ya kiutumishi.

IV. TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA AHADI ZA SERIKALI BUNGENI 2014/15

85. **Mheshimiwa Spika**, utekelezaji wa ahadi zilizotolewa na Serikali Bungeni katika mwaka 2014/2015, umezingatiwa katika Taarifa ya utekelezaji wa malengo ya Ilani ya Uchaguzi eneo la II na katika hotuba hii eneo la IV la Mapitio ya utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka 2014/2015. Ahadi hizo zipo katika maeneo ya vitendea kazi, ajira na mafunzo, misako na doria, ujenzi na ukarabati wa ofisi, vituo, nyumba na magereza, zoezi la utambuzi na usajili wa watu na kuwarejesha wakimbizi kwao. Kwa ujumla wake, taarifa ya utekelezaji wa ahadi za Serikali zilizotolewa Bungeni katika mwaka 2014/2015, ni kama inavyoonyesha katika **Kiambatisho Na. 1** cha Hotuba hii.

V. SHUKRANI

86. **Mheshimiwa Spika**, natoa shukrani zangu za dhati kwa wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ulinzi na Usalama chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Anna Margareth Abdallah Mbunge Viti Maalum kwa kuyapitia na kuyachambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka wa fedha 2015/2016. Maelekezo na ushauri wa Kamati hiyo utaisaidia Wizara katika kutekeleza majukumu yake.

87. **Mheshimiwa Spika**, shukrani za pekee nazitoa kwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Pereira Ame Silima, Mbunge wa Chumbuni, Katibu Mkuu Bwana Mbarak Abdulwakil, Naibu Katibu Mkuu Bibi Mwamini Malemi, Inspekta Jenerali wa Polisi Bwana Ernest Mangu, Kamishna Jenerali wa Magereza Bwana John Minja, Kamishna Jenerali wa Zimamoto na Uokoaji Bwana Pius Nyambacha, Kamishna Mkuu wa Uhamiaji Bwana Sylvester Ambokile, Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa Bwana Dickson Maimu, Makamishna, Wakurugenzi na Wakuu wote wa Idara na Vitengo, Makamanda, Askari pamoja na Wafanyakazi wote wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ambao wamefanikisha maandalizi ya hotuba hii na pia kwa kusaidia kufanikisha majukumu ya Wizara.

88. **Mheshimiwa Spika**, nachukua pia fursa hii kuwashukuru nchi washirika wa maendeleo ikiwemo China, Marekani, Ujerumani, Japan, Uturuki, Korea

Kusini, Umoja wa Falme za Kiarabu, Misri na taasisi za INTERPOL, IOM, EU, UNHCR, DFID, USAID, UNICEF, WFP na Pharm Access pamoja na wadau wengine wote kwa misaada yao ambayo imeongeza uwezo wa kiutendaji katika Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

VI. MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA 2015/2016

89. **Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu lipitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka 2015/2016 ya shilingi 872,703,062,000 kwa ajili ya bajeti ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo. Kati ya makadirio hayo, shilingi 778,305,656,000 ni za matumizi ya kawaida ambapo shilingi 348,834,203,000 ni matumizi mengineyo na mishahara shilingi 429,471,453,000. Makadirio ya shilingi 94,397,406,000 ni kwa ajili ya mipango ya maendeleo. Mchanganuo ni kama ifuatavyo:-

(a) Fungu 14 – Jeshi la Zimamoto na Uokoaji

(i)	Matumizi Mengineyo	Sh.19,861,172,000/=
(ii)	Mishahara	Sh.14,521,186,000/=
(iii)	Matumizi ya maendeleo	Sh.1,500,000,000/=
	Jumla	Sh.35,882,358,000/=

(b) Fungu 28 – Jeshi la Polisi

(i)	Matumizi Mengineyo	Sh.196,801,709,000/=
(ii)	Mishahara	Sh.284,314,668,000/=
(iii)	Matumizi ya maendeleo	Sh.8,510,968,000/=
	Jumla	Sh.489,627,345,000/=

(c) Fungu 29 – Jeshi la Magereza

(i)	Matumizi Mengineyo	Sh.67,665,836,000/=
(ii)	Mishahara shilingi	Sh.97,750,249,000/=
(iii)	Matumizi ya maendeleo	Sh.1,621,716,000/=
	Jumla	Sh.167,037,801,000/=

(d) Fungu 51 – Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na NIDA

(i)	Matumizi Mengineyo	Sh. 21,776,072,000/=
(ii)	Mishahara	Sh.4,069,558,000/=
(iii)	Matumizi ya maendeleo	Sh.76,964,722,000/=
	Jumla	Sh.102,810,352,000/=

(e) Fungu 93 – Idara ya Uhamiaji

(i)	Matumizi Mengineyo	Sh.42,729,414,000/=
(ii)	Mishahara	Sh.28,815,792,000/=

(iii) Matumizi ya maendeleoSh.5,800,000,000/=
Jumla Sh.77,345,206,000/=
Jumla Kuu Sh.872,703,062,000/=

90. **Mheshimiwa Spika**, nakushukuru wewe, Waheshimiwa Wabunge wote pamoja na Wananchi Wengine wote kwa kunisikiliza. Aidha, Hotuba hii inapatikana pia katika tovuti ya Wizara yenye jina www.moha.go.tz.

91. **Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Hoja imetolewa na imeungwa mkono. Tunakushukuru sana Mheshimiwa Chikawe, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi kwa hotuba nzuri ambayo umeitoa hapa.

Kabla hatujaendelea, kwa sababu *gallery* zetu zilijaa baadhi ya wageni walikuwa nje, niwatambulisha wageni 21 ambao wanatoka Jimboni kule Chumbuni Zanzibar, ni wageni wa Mheshimiwa Pereira Silima, Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi. Pale mlipo wale wageni kutoka Zanzibar msimame. Karibuni sana wageni wetu. (*Makofi*)

Pia mke wa Mheshimiwa Godbless Lema alikuwa hakupata nafasi, Mama Neema pale alipo kama amepata nafasi asimame. Ahsante sana na karibu sana. (*Makofi*)

Pia kuna wageni 12 wa Mheshimiwa Amos Makalla kutoka Kamati ya Wakulima wanaolima Bonde la Mgongola, Mvomero. Naomba msimame wale watu wa Mgongola, karibuni sana. (*Makofi*)

Baada ya matangazo hayo, sasa naomba nimuite Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ili aweze kusoma hotuba yake, Mheshimiwa Dkt. Hussein Mwinyi, karibu sana, una dakika 45 pia.

HOTUBA YA WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA MHESHIMIWA DKT. HUSSEIN ALI MWINYI (MB) AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2015/16 KAMA ILIVYOSOMWA BUNGENI

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA: Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ulinzi na Usalama, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali kupokea, kujadili na kupitisha Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka wa fedha 2015/2016.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, naomba hotuba yangu iliyo kwenye kitabu iingie kwenye *Hansard* yote kama ilivyo kwani nitakayoisoma hapa itakuwa ni muhtasari tu wa hotuba hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema, aliyenijalia kuwa na uzima na afya njema na kuniwezesha kuwasilisha hotuba yangu ya bajeti kwa mwaka 2015/2016. Aidha, namshukuru kwa dhati Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi ya Usalama ya Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuendelea kuniamini kuiongoza Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Napenda kurejea ahadi yangu kwa Mheshimiwa Rais na Watanzania wenzangu kuwa nitaendelea kutumia uwezo, nguvu zangu zote kutekeleza majukumu yangu kwa haki, weledi, uaminifu, uadilifu na unyenyekevu wa hali ya juu ili kufanikisha malengo ya Wizara kwa hakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile napenda kutumia fursa hii kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Wasaidizi wake Wakuu, Makamu wa Rais, Mheshimiwa Dkt. Mohamed Gharib Bilal na Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda kwa kuiongoza nchi yetu vema na kwa usimamizi na utekelezaji mzuri wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2010-2015. Aidha, napenda kumpongeza Spika wa Bunge hili Mheshimiwa Anne Semamba Makinda, Naibu Spika, Mheshimiwa Job Ndugai pamoja na Wenyeviti wa Bunge kwa kuendesha vizuri shughuli za Bunge. Kwa namna ya pekee, naungana na wenzangu kukupongeza Mheshimiwa Spika kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Jukwaa la Bunge la Nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC). Namwomba Mwenyezi Mungu azidi kuwapa baraka, hekima, busara na nguvu za kuendelea kuiongoza Bunge hili katika kutekeleza majukumu yake mazito na nyeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutumia nafasi hii kwa mara nyingine kumshukuru Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ulinzi na Usalama, Mheshimiwa Anna Abdallah na Wajumbe wote wa Kamati hii Tukufu kwa kuendelea kunipa ushirikiano wa kutosha katika kuiongoza Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Kwa uhakika, Kamati hii kwa kipindi chote imekuwa mhimili imara kwetu kwa kusimamia, kuiongoza, kushauri, kufuatilia na kutembelea miradi mbalimbali inayotekelezwa na Wizara kwa lengo la kujionea wenyewe maendeleo na kufahamu changamoto tunazokabiliana nazo. Kwa uzito wa kipekee kabisa, na kwa niaba ya wapiganaji shupavu wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania, tunawapongeza na kuwashukuru kwa ziara yao ya kihistoria waliyoifanya tarehe 12-19 Aprili, 2015 kutembelea Wapiganaji wetu walioko nchini DRC. Ziara hiyo imeongeza ari na morali ya kazi kwa Wapiganaji wetu wote. Ushauri na maelekezo ya Kamati umechangia kwa kiasi kikubwa katika maendeleo ya sekta ya ulinzi na usalama hapa nchini. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, naungana na wenzangu wote waliotangulia kuwapa pole wale waliopatwa na majanga pamoja na kufiwa na ndugu, jamaa na wapendwa wao katika matukio mbalimbali yaliyotokea nchini yakiwemo mafuriko yaliyotokea katika maeneo mbalimbali na ajali mbalimbali za vyombo vya usafiri yakiwemo mabasi ya abiria. Aidha, nachukua fursa hii kutoa salamu za pole kwa Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wote kwa kuondokewa na mpendwa wetu, Mheshimiwa Kapteni Mstaafu John Damian Komba, Mbunge wa Jimbo la Mbinga Magharibi. Naomba Mwenyezi Mungu azilaze roho za Marehemu mahali pema peponi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2015 ni mwaka ambao Watanzania watahusika na masuala mengi muhimu yakiwemo kujiandikisha katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura na kushiriki katika Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani. Hivyo, nikiwa kama Mtanzania na kwa kuzingatia kuwa Wizara yangu ni mdau mkubwa katika kufanikisha mustakabali wa Taifa letu, naungana na Watanzania wengi wenye mapenzi mema na nchi yetu kuwaasa wananchi kushiriki kwa ukamilifu na kwa utulivu mkubwa katika kufanikisha masuala hayo muhimu kwa mustakabali wa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo ya utangulizi, napenda sasa kuchukua fursa hii kuwasilisha kwa muhtasari hotuba yangu ambayo kiujumla imejikita katika maeneo makuu yafuatayo: Malengo na majukumu ya Wizara; Utekelezaji wa Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ulinzi na Usalama, Hali ya Usalama na mipaka katika mwaka 2014/2015; Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya mwaka 2014/15 na Mpango na Makadirio ya Bajeti kwa mwaka 2015/2016.

Mheshimiwa Naibu Spika, malengo na majukumu ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Kama ilivyo katika Dira yetu, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa inaendelea kuwa Taasisi iliyotukuka ya kulinda na kudumisha amani na usalama wa Taifa. Vivyo hivyo, tumeendelea kulinda Jamhuri ya Muungano wa Tanzania dhidi ya adui wa aina yoyote kutoka ndani au nje ya nchi na kuhakikisha kuwa mamlaka ya nchi na maslahi ya Taifa letu yako salama sanjari na dhima yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kufanikisha dira na dhima hii, malengo ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa yameendelea kuwa kama ifuatavyo:-

(i) Kuwa na Jeshi dogo la Ulinzi wa Nchi lenye wataalam waliobobea, zana bora, vifaa vya kisasa na mawasiliano salama;

(ii) Kuendeleza mazingira bora ya kufanyia kazi na makazi kwa kuimarisha yaliyopo na kujenga mapya;

Nakala ya Mtandao (Online Document)

(iii) Kuimarisha tafiti za kijeshi katika Mashirika ya Mzinga na Nyumbu na kuhawilisha teknolojia mpya;

(iv) Kuendelea kuwajengea vijana wa Kitanzania moyo wa uzalendo, ukakamavu, maadili mema na utaifa;

(v) Kuimarisha utayari wa Jeshi la akiba;

(vi) Kuhifadhi na kumiliki maeneo yake ya ardhi kwa ajili ya matumizi ya Jeshi; na

(vii) Kuendelea kudumisha amani na usalama kwa kushirikiana na nchi nyingine duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kufikia malengo yaliyoainishwa, Wizara itaendelea kusimamia utekelezaji wa majukumu yafuatayo:-

(i) Uandikishwaji wa Wanajeshi wenye sifa zinazohitajika kwa Jeshi kwa ajili ya Ulinzi wa Taifa na kuwapatia mafunzo na mazoezi ya kinadharia na kivitendo;

(ii) Kuwapatia Wanajeshi makazi, zana, vifaa na vitendea kazi vipya, bora na vya kisasa;

(iii) Kusimamia matunzo na matumizi mazuri ya zana, vifaa na vitendea kazi kwa ujumla;

(iv) Kuimarisha mafunzo na mazoezi ya kijeshi ikiwa ni pamoja na shughuli za uendeshaji mafunzo ya ulinzi wa mgambo;

(v) Kuboresha mitaala ya mafunzo ya JKT kwa vijana waliojiunga na mafunzo hayo kwa mujibu wa sheria au kwa utaratibu wa kujitolea ili iwaandae vijana hao kuwa wakakamavu, wenye nidhamu na kuwajengea moyo wa uzalendo na mshikamano wa kitaifa katika kutekeleza shughuli za kujitegemea;

(vi) Kuendeleza utafiti na uhawilishaji wa teknolojia za kijeshi na kuzalisha mali kupitia mashirika ya Mzinga na Nyumbu;

(vii) Kuwezesha uzalishaji wa Shirika la Uzalishaji Mali la Jeshi la Kujenga Taifa (SUMAJKT) kuwa wa tija na faida itakayochangia katika uendeshaji wa shughuli za Jeshi la Kujenga Taifa;

(viii) Kushirikiana na mamlaka za kiraia pale inapobidi katika kukabiliana na majanga na dharura za kitaifa;

(ix) Kuimarisha mazingira bora ya kuishi na kufanyia kazi; na

(x) Kuimarisha ushirikiano na nchi nyingine duniani katika masuala ya kijeshi.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa maoni na ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Ulinzi na Usalama ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Wakati Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ulinzi na Usalama ilipokaa na kujadili Makadirio ya Mapato, Mpango na Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka 2014/2015 ilitoa maoni, ushauri na maelekezo kadhaa kwa Wizara hii yaliyolenga kuboresha utendaji na utekelezaji wa majukumu yake. Napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa maoni, ushauri na maelekezo yaliyotolewa yamefanywa kazi.

Aidha, hoja mbalimbali zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge wakati wa majadala huo pia zimezingatiwa katika Mpango na Bajeti ya mwaka 2015/2016 ninayowasilisha leo hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya ulinzi na usalama katika nchi za Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati. Hali ya Ulinzi na Usalama katika nchi za ukanda wa Afrika Mashariki na Kati ni shwari. Hata hivyo, ukanda huu umekuwa ukikabiliwa na matishio mbalimbali ya kiusalama yakiwemo mashambulizi ya mara kwa mara ya kigaidi kutoka kundi la Al Shabab la nchini Somalia. Ingawa kundi hili limekuwa likidai kulenga nchi zenye Majeshi katika operesheni za Umoja wa Afrika nchini Somalia "*The African Union Mission in Somalia (AMISOM)*," mwenendo wao umekuwa ukiashiria tofauti. Kwa msingi huo, Vyombo vyetu vya Ulinzi na Usalama kwa kushirikiana na raia wema vimekuwa macho na nyendo za wafuasi wa kundi hili. Pamoja na hali hiyo, usalama wa nchi yetu umeendelea kuwa shwari

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hali hiyo kumekuwepo na matukio machache yasiyokuwa ya kawaida na yenye dalili za uhalifu uliopitiliza (*extended crime*). Matukio haya yamepelekea mauaji ya Askari wa JWTZ na wa Polisi na uporaji wa silaha. Naomba nichukue fursa hii kulifahamisha Bunge lako Tukufu kwamba juhudi kubwa zimefanyika na zinaendelea kufanywa na vyombo vyetu vyote vya ulinzi na usalama katika kukabiliana na wahalifu hao na mtandao wao. Tunawashukuru wananchi kwa ushirikiano wao katika kukabiliana na njama za uhalifu huu au kuwezesha wahalifu kukamatwa. Aidha, tunawaasa wananchi wote kuwa macho na maadui hao na kuwaomba waendeleo kushirikiana na vyombo vya ulinzi na usalama kukabiliana nao.

Mheshimiwa Naibu Spika, vikundi vya uasi vyenye silaha vya "*The Democratic Forces for the Liberation of Rwanda (FDLR)*", "*The Allied Democratic Forces*" (*ADF*) na "*The Lord's Resistance Army*" (*LRA*),

Nakala ya Mtandao (Online Document)

vimesababisha hali ya usalama kuwa tete Mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo. Ingawa Kikundi cha *FDLR* kilitakiwa kujisalimisha mapema tarehe 2 Januari, 2015 kwa Majeshi ya Umoja wa Mataifa (*United Nations Organization Stabilization Mission in the DR Congo – MONUSCO*) hakikutekeleza kama kilivyotakiwa kwani hadi kufikia tarehe ya mwisho, ni asilimia 30 tu ya waasi hao walikuwa wamejisalimisha. Kutokana na hali hii, taratibu za kukikabili Kikundi hicho zimeshakamilika chini ya Umoja wa Mataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa nchi ya Somalia na Sudan Kusini kumekuwa na hali tete ya usalama hususan nchini Somalia kutokana na mapambano yanayoendelea baina ya majeshi ya *AMISOM* na kundi la Kigaidi la Al-Shabaab. Aidha, hali ya uhusiano bado ni tete kati ya Serikali ya Sudan Kusini inayoongozwa na Rais Salva Kiir na kikundi kinachomuunga mkono Dkt. Riek Machar aliyekuwa Makamu wa Rais. Hata hivyo, mazungumzo ya amani yanayoendelea yameanza kuonyesha mwelekeo wa kupatikana ufumbuzi wa uhasama uliopo kati ya pande hizo mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa uharamia wa baharini, hakuna matukio yaliyojitokeza katika mwaka 2014/2015. Hata hivyo, vyombo vyetu vinaendelea kufanya ulinzi mkali kwenye eneo letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya usalama wa mipaka. Kufuatana na juhudi kubwa zinazofanywa na vyombo vyetu vya ulinzi na usalama kwa kushirikiana na wananchi, majaribio ya ugaidi na matendo maovu ya biashara za madawa ya kulevyu, uhamiaji haramu na ujambazi kwa ujumla yamepungua na kupelekea hali ya mipaka kuwa shwari. Kwa ujumla hali ya mipaka yetu imekuwa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka wa Mashariki. Mpaka huu unahusisha eneo la nchi yetu katika Bahari ya Hindi ambalo lina urefu wa kilometa 1,424. Katika mpaka huu, Tanzania inapakana na nchi ya Kenya, Visiwa vya Ushelisheli, Komoro na Msumbiji. Hali ya usalama katika mpaka huu imeendelea kuwa shwari na bila matukio ya uharamia.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka wa Kaskazini. Mpaka huu una urefu wa kilometa 1,221 ambapo Tanzania imepakana na nchi za Kenya na Uganda. Hali ya usalama katika mpaka huu kwa ujumla ilikuwa shwari. Hata hivyo, matukio ya uharibifu wa alama za mipaka (*beacons*) na ujenzi holela unaofanywa na baadhi ya watu waishio maeneo ya mipakani kwa lengo la kujipatia ardhi kwa ajili ya kilimo, malisho ya mifugo, biashara na ujenzi wa makazi yameendelea kujitokeza na kuwa changamoto kubwa kwa usalama wa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka wa Magharibi. Mpaka huu una urefu wa kilometa 1,220. Katika mpaka huu, Tanzania imepakana na nchi za Burundi,

Rwanda na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC). Ingawa hali ya usalama wa mpaka huu kwa ujumla imekuwa shwari, matukio ya ujambazi wa kutumia silaha maeneo ya nchi kavu na katika Ziwa Tanganyika ambayo kwa sehemu kubwa yanafanywa na watu wenye silaha na vikundi vinavyohasimiana nchini DRC na masalia ya waasi nchini Burundi yameendelea kujitokeza. Katika ujambazi huo, makundi hayo yamekuwa yakiwashambulia wavuvi na kuwanyang'anya vifaa vya uvuvi na hata kuwajeruhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka wa Kusini. Mpaka huu una urefu wa kilomita 1,536 ambapo Tanzania inapakana na nchi za Msumbiji, Malawi na Zambia. Hali ya usalama katika mpaka huu imeendelea kuwa shwari. Pamoja na kwamba hatua ya mwisho ya kufikia usuluhishi wa mpaka bado haujafikiwa, hali ya kiusalama imeendelea kuwa shwari na wananchi wa pande zote wanaendelea na shughuli zao bila bugudha yoyote ya kiulinzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya ugaidi na uharamia. Vitendo vya kigaidi na uharamia vimeendelea kuwa tishio kubwa duniani. Mwelekeo wa matukio ya ugaidi hivi sasa ni matumizi ya mbinu na zana za kisasa ikiwemo teknolojia ya habari na mawasiliano katika kufanikisha malengo yao bila kugundulika kiurahisi. Baadhi ya makundi ya ugaidi yanayoendesha harakati zake maeneo mbalimbali duniani ni pamoja na kundi la *ISIS*, *Boko Haram*, *Al Qaeda* na *Al Shabaab*. Makundi hayo yanaendesha kampeni za kurubuni na kuandikisha makundi ya vijana kutoka mataifa mbalimbali ili kujiunga nayo, hali ambayo inalifanya tishio la ugaidi kusambaa maeneo mengi duniani na kutokuwa na mipaka. Kutokana na ukubwa wa maeneo ya mipaka ya nchi yetu na kuwepo kwa mipenyo katika mipaka hiyo, upo uwezekano wa makundi ya kihalifu kutoka nje kuingia nchini na kufanya uhalifu ikiwemo kueneza itikadi zenye msimamo mkali pamoja na ugaidi. Tunaendelea kuwatahadharisha wananchi kuwa macho na kuyatolea taarifa matukio yanayotishia usalama wa nchi pindi yanapojitokeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi letu pamoja na kushirikiana vema na vyombo vingine vya ulinzi na usalama hapa nchini, pia limeshirikiana na Majeshi mbalimbali katika kukabiliana na vitendo vya kigaidi kwa kuimarisha doria na kuhakikisha eneo hilo la bahari linakuwa salama pamoja na vyombo vya usafirishaji baharini vinaendelea na shughuli zake bila tishio lolote. Ushirikiano na Majeshi mbalimbali umekuwa katika nyanja za mazoezi na operesheni za pamoja ambapo katika kipindi hiki, JWTZ lilifanya operesheni za pamoja katika Bahari ya Hindi na Majeshi rafiki ya nchi za Kenya, Msumbiji na Afrika Kusini.

Mheshimiwa Spika, mapitio ya utekelezaji wa mpango na bajeti ya mwaka 2014/2015. Katika mwaka 2014/2015, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ilikadiria kukusanya mapato ya jumla ya shilingi 60,506,000.00 kutoka katika Mafungu yake matatu ya 38-NGOME, 39-JKT na 57-Wizara. Hadi kufikia mwezi

Machi, 2015, Mafungu hayo yalifanikiwa kukusanya mapato ya jumla ya shilingi 47,268,778 sawa na asilimia 78.1 ya makadirio. Makusanyo hayo ni madogo kwa vile chanzo chake kikuu ni mauzo ya hati za zabuni ambapo sasa utangazaji huo unafanywa pia GPSA na hivyo kufanya mapato yake kupungua.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika bajeti ya mwaka wa fedha 2014/2015, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa liliidhinishiwa jumla ya shilingi 1,269,076,056,000 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Maendeleo katika Mafungu yake matatu. Kati ya fedha hizo, shilingi 1,020,076,056,000 zilitengwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi 249,000,000,000.00 ni kwa ajili ya Matumizi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, kufuatia maelekezo ya Hazina ya kurekebisha vitabu vya bajeti vya mwaka 2014/2015, bajeti ya Mafungu ilibadilika na kuwa shilingi 1,312,502,196,000/= kukiwa na ongezeko la shilingi 43,426,140,000/= sawa na asilimia 3.42. Kati ya fedha hizo, shilingi 1,063,659,696,000/= zilitengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 248,842,500,000/= ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Mchanganuo wa bajeti hiyo kwa kuzingatia Mafungu ya Wizara ni kama ifuatavyo:-

Matumizi ya Kawaida kwa NGOME yalikuwa Sh.839,635,388,000/=, kwa JKT, ilikuwa ni Sh. 204,556,662,000/= na kwa Wizara ilikuwa Sh.19,457,646,000/= . Kwa upande wa Matumizi ya Maendeleo, NGOME walitengewa Sh.12,000,000,000, JKT Sh.7,000,000,000 na Wizara Sh.229,842,500,000/= . Jumla Kuu kwa Mafungu yote ni Sh.1,312,502,196,000/=

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia mwezi Machi 2015, Wizara ilikuwa imepokea jumla ya Sh.919,748,922,788/= sawa na asilimia 70.07 ya bajeti. Kati ya fedha hizo Sh.846,248,922,788/= sawa na asilimia 92 zilitumika kwa shughuli za kawaida ikiwemo kulipa mishahara na posho mbalimbali muhimu. Kwa upande wa Matumizi ya Maendeleo, fedha zilizopokelewa ni Sh.73,500,000,000/= sawa na asilimia 29.53 ya fedha zote zilizoidhinishwa kwa ajili ya shughuli za maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tathmini ya fedha zilizopokelewa inaonyesha kwamba mwenendo wa upatikanaji wa fedha kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida hususan fedha za mishahara na chakula kwa wanajeshi katika kipindi hicho kiujumla ulikuwa ni wa kuridhisha. Fedha kwa ajili ya mishahara na marupurupu zilipokelewa kulingana na makisio ya bajeti. Hata hivyo, fedha za Matumizi Mengineyo hazikutolewa kulingana na bajeti, fedha zilizotolewa hadi Machi, 2015 zilikuwa asilimia 61.03 ya bajeti ya matumizi mengineyo. Kwa upande wa shughuli za maendeleo, hadi kufikia mwezi Machi, 2015, fedha zilizotolewa zilikuwa asilimia 29.53 ya bajeti yake. Kiasi hicho ni kidogo sana ukilinganisha na mahitaji halisi yakiwemo kulipia madeni ya kimkataba ya ndani na nje. Hali hii

pia imeathiri kasi ya upatikanaji wa vifaa na utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, mafanikio ya utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya mwaka 2014/2015. Matumizi ya shughuli za Kawaida. Katika mwaka 2014/2015, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, lilifanikiwa kutekeleza shughuli mbalimbali katika kufikia malengo yake. Shughuli hizo ni pamoja na kuwapatia stahili mbalimbali wanajeshi, watumishi wa umma na vijana walioko katika mafunzo ya JKT na kutoa huduma muhimu za chakula, tiba, sare, umeme, maji, simu na mafuta ya uendeshaji kwa majukumu ya ulinzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, majukumu ya kiulinzi yaliyotekelezwa katika kipindi hicho ni pamoja na kufanyika mafunzo na mazoezi ya kijeshi, mafunzo ya ulinzi wa mgambo, upatikanaji wa huduma za afya na tiba kwa maafisa, askari na wananchi, ushirikiano wa kiulinzi na kijeshi na nchi nyingine, ushirikiano na Jumuiya za Kikanda na Kimataifa, ushirikiano wa Jeshi na mamlaka za kiraia, mafunzo ya JKT ya kujitolea na ya mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2014/2015, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, pamoja na ufinyu wa bajeti imefanikiwa kutekeleza shughuli za kawaida zifuatazo:-

(i) Kulipia gharama za matumizi ya mahitaji muhimu ya umeme, maji, simu na huduma za uendeshaji wa majukumu za kimsingi;

(ii) Kulipia stahili mbalimbali za wanajeshi, vijana wa Jeshi la Kujenga Taifa na watumishi wa umma;

(iii) Kuimarisha ushirikiano na nchi nyingine duniani katika nyanja za kijeshi na ulinzi; na

(iv) Kuendesha majukumu ya ulinzi yakiwemo ya mafunzo ya kijeshi, mafunzo ya ulinzi wa Mgambo na matengendo ya vifaa na zana za kijeshi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafunzo na mazoezi ya kijeshi. Katika mwaka 2014/2015, Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania limeendelea kutoa mafunzo na mazoezi kwa Wanajeshi wake ili kulifanya kuwa imara na tayari muda wote kutekeleza majukumu yake ya kiulinzi. Aidha, Jeshi letu liliendelea kushiriki katika mafunzo na mazoezi ya pamoja na nchi marafiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafunzo ya ulinzi wa Mgambo. Mafunzo ya ulinzi wa Mgambo kwa wananchi yameendelea kutolewa na Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania. Katika kipindi cha mwaka 2014/2015, JWTZ kwa

kushirikiana na vyombo vya Usalama limeendesha mafunzo katika ngazi mbalimbali ambapo jumla ya wananchi 14,107 walifuzu.

Mheshimiwa Naibu Spika, huduma za afya na tiba. Katika kipindi hiki, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa imeendelea kutoa huduma za tiba kwa maafisa, askari, watumishi wa umma, familia za Wanajeshi na wananchi kwa ujumla. Huduma hizo zimekuwa zikitolewa katika hospitali na vituo vya tiba vya Jeshi hapa nchini. Aidha, huduma hizo zimeboreshwa baada ya kukamilika kwa mradi wa ujenzi na ukarabati wa Chuo cha Sayansi za Tiba katika Kambi ya Lugalo. Chuo hicho kinatarajiwa kuwa Chuo Kikuu Kishiriki cha Sayansi za Tiba cha Muhimbili. Chuo hicho sasa kina uwezo wa kutoa elimu ngazi ya Shahada na Stashahada ya Juu kwa fani za Udaktari, Uuguzi, Maabara na Afya ya Jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushirikiano wa kiulinzi na kijeshi na nchi nyingine. Ushirikiano kati ya nchi yetu na nchi nyingine katika nyanja ya kijeshi ni suala muhimu katika mustakabali wa ulinzi na usalama duniani. Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania limeendelea kuwa na ushirikiano mzuri na majeshi ya nchi nyingine hususan katika eneo linalohusu nafasi za mafunzo. Jeshi letu limeendelea kupeleka maafisa wa ngazi mbalimbali kusoma katika vyuo vya kijeshi vya nchi nyingine zikiwemo China, Kenya, Uganda, Zambia, Rwanda, Afrika Kusini, Marekani, Ujerumani, Uingereza, Urusi na Falme za Kiarabu. Pia, maafisa kutoka katika baadhi ya nchi hizi wapo hapa nchini katika vyuo vyetu vya kijeshi kwa mafunzo. Vyuo hivyo ni Chuo cha Maafisa - Monduli, Chuo cha Ukamanda na Unadhimu - Arusha na Chuo cha Ulinzi wa Taifa - Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, kushirikiana na Jumuiya za Kikanda na Kimataifa. Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania, limeendelea kushiriki katika operesheni za ulinzi wa amani chini ya Umoja wa Nchi za Afrika (*African Union*) na Umoja wa Mataifa. Hadi sasa nchi yetu imeendelea kuwa na vikosi vyake Darfur nchini Sudan na nchini DRC. Pia, Kombaria mbili za Polisi Jeshi zipo nchini Lebanoni kwa majukumu kama hayo. Vikosi na maafisa wa JWTZ waliopo kwenye operesheni za ulinzi wa amani katika maeneo hayo wote wanaendelea vizuri na utekelezaji wa majukumu yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa kwa Vijana. Mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa yameendelea kutolewa kwa vijana wa kujitolea na wale wa mujibu wa sheria kwa lengo la kujenga uzalendo, ukakamavu, maadili mema, utaifa pamoja na kutoa stadi za kazi. Katika mwaka 2014/2015, jumla ya vijana 40,082 walipatiwa mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa, kati yao vijana 8,447 ni wa kujitolea na vijana 31,635 ni wa mujibu wa sheria. Mahudhurio hayo ya vijana wa mujibu wa sheria yameongezeka kwa vijana 15,632 ukilinganisha na vijana 16,003 waliohitimu mafunzo hayo mwaka 2013/2014. Hata hivyo, idadi hii bado ni ndogo ikilinganishwa na idadi ya vijana 41,000 waliostahili kujiunga na mafunzo hayo yaani waliohitimu kidato

Nakala ya Mtandao (Online Document)

cha sita. Wito wangu kwa vijana ni kushiriki mafunzo hayo kwani ni ya mujibu wa sheria. Kwa wale ambao hawakushiriki bila ridhaa yetu wataendelea kuwa kwenye orodha yetu ya vijana watoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, dhima ya Jeshi la Kujenga Taifa ni kuwalea vijana wa Kitanzania katika maadili mema, kuwajenga kinidhamu, kuwajengea uzalendo kwa nchi yao, kuwajengea ukakamavu, kufundisha na kuwapa ujuzi na stadi mbambali za kazi ili kuwaandalia mazingira mazuri ya kujijiri mara wamalizapo mkataba wa mafunzo yao. Wakati wa kuandikishwa kujiunga na mafunzo hayo, vijana hujaza na kusaini fomu ya mkataba maalum yenye masharti kwamba kijana awe tayari kurudi nyumbani mara amalizapo mkataba wake.

Hata hivyo, tangu kuanza kwa utaratibu wa mafunzo hayo, baadhi ya wahitimu wamekuwa wakiajiriwa na vyombo vya ulinzi na usalama pamoja na taasisi binafsi kulingana na mahitaji ya vyombo hivyo. leleweke kuwa siyo vijana wote wanaohitimu mafunzo hayo hupata ajira kwenye vyombo na taasisi hizo.

Napenda kutoa rai kwa vijana wanaopata mafunzo ya JKT wazingatie maarifa na ujuzi wanaoupata hususan wa stadi za kazi ili waweze kujijiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza agizo la Mheshimiwa Rais, Amir Jeshi Mkuu kwa vyombo vya ulinzi na Usalama la kuajiri vijana wanaohitimu mafunzo ya JKT, katika mwaka 2014/2015, jumla ya vijana 8,590 wamenufaika na utaratibu huo. Mchanganuo wa ajira katika vyombo hivyo ulikuwa kama ifuatavyo:-

(i) Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania limeajiri vijana 6,531 kati yao wasichana ni 1,233 na wavulana 5,298;

(ii) Jeshi la Polisi vijana 906 wasichana wakiwa 199 na wavulana 707;

(iii) Usalama wa Taifa vijana 22 kati yao wasichana ni wanne (4);

(iv) Jeshi la Magereza vijana 1,107 kati yao wasichana wakiwa 245 na wavulana 862;

(v) Jeshi la Zimamoto vijana 100 kati yao wasichana wakiwa 22 na wavulana 78; na

(vi) TAKUKURU imeajiri vijana 24.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, taasisi na makampuni binafsi kama Benki Kuu ya Tanzania, Baraza la Mitihani, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania,

Nakala ya Mtandao (Online Document)

TANAPA, African Gold Mine na Geita Gold Mines kwa ujumla yameajiri vijana 2,214, tangu utaratibu wa mafunzo ya JKT uliporejeshwa tena mwaka 2011 hadi sasa. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto kuu ya utekelezaji wa mafunzo haya ni ufinyu wa bajeti unaosababisha kushindwa kugharamia huduma za mafunzo kikamilifu na kushindwa kukarabati majengo na miundombinu katika makambi ya Jeshi la Kujenga Taifa. Hata hivyo, baadhi ya changamoto zimeanza kutatuliwa kwa kutumia fedha kidogo zinazopatikana kutokana na vyanzo vya mapato vya ndani ya Jeshi la Kujenga Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, matumizi ya shughuli za maendeleo. Utekelezaji wa shughuli za maendeleo hadi kufikia robo ya tatu ya mwaka wa fedha 2014/2015 kwa ujumla haukuwa mzuri. Mafungu yote matatu yalipokea wastani wa asilimia 29.53 ya bajeti iliyoidhinishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mapokezi hayo, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa limeweza kutekeleza miradi ifuatayo:-

(i) Kuendeleza mradi wa ujenzi wa nyumba 6,064 awamu ya kwanza kwa ajili ya makazi ya wanajeshi;

(ii) Kulipia madeni ya kimkataba, kukarabati majengo pamoja na kuboresha mazingira ya kufanyia kazi na makazi katika makambi na viteule vya JKT;

(iii) Ulipaji fidia kwa baadhi ya maeneo yaliyotwaliwa kwa matumizi ya Jeshi;

(iv) Ujenzi wa Shule ya Mafunzo ya Awali ya Kijeshi Kihangaiko;

(v) Kuendelea na ujenzi wa maghala ya kuhifadha silaha na zana; na

(vi) Kuanza matumizi ya mawasiliano ya kimtandao katika maeneo ya Zanzibar, Pwani na Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa nyumba na makazi ya Wanajeshi. Katika hotuba yangu ya bajeti ya mwaka wa fedha 2014/2015, nililitaarifu Bunge lako Tukufu juu ya kuanza kwa ujenzi wa nyumba 10,000 za kuishi Wanajeshi vikosini. Awamu ya kwanza ya ujenzi wa nyumba 6,064 za makazi ya Wanajeshi vikosini unaendelea vizuri. Nafurahi kulieleza Bunge lako Tukufu kuwa, utekelezaji wa mradi unaendelea kwa kasi kubwa.

Aidha, tarehe 20 Disemba, 2014, Rais na Amiri Jeshi Mkuu, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete aliweka Jiwe la Msingi kwenye ujenzi wa nyumba

Nakala ya Mtandao (Online Document)

552 zinazojengwa Monduli, Mkoani Arusha kuwakilisha mradi wa ujenzi wa nyumba 6,064 katika Mikoa tisa (9) hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ununuzi wa zana na vifaa vya kijeshi. Katika mwaka 2014/2015, Serikali iliendelea kuliimarisha Jeshi kwa kulipatia zana na vifaa vya kisasa. Jeshi lilipokea zana na vifaa mbalimbali kwa ajili ya ulinzi wa anga, nchi kavu na majini. Kutokana na zana na vifaa hivyo, Jeshi letu hivi sasa lina uwezo mkubwa wa kutekeleza majukumu yake. Mpango huu wa ununuzi wa zana za kisasa na bora ni endelevu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Uzalishaji Mali la SUMAJKT. Shirika la Uzalishaji Mali la JKT la SUMAJKT limeendelea kutekeleza shughuli zake katika misingi ya kibiashara. Shughuli hizo zinahusu ujenzi, uhandisi, viwanda, kilimo, biashara, utalii na mradi wa uuzaji matrekta na Kampuni ya Ulinzi Binafsi ya *SUMAJKT Guard Ltd.*

Mheshimiwa Spika, SUMAJKT kupitia Idara ya Ujenzi iitwayo *National Service Construction Department* inatekeleza miradi ya ujenzi katika sehemu mbalimbali nchini. Katika mwaka 2014/2015, jumla ya miradi 39 ya ujenzi imetekelezwa. Aidha, kupitia Idara ya Viwanda na Kilimo, SUMAJKT lilifanikiwa kutengeneza samani mbalimbali katika kiwanda chake cha samani Chang'ombe-Dar es Salaam. Samani hizo ziliuzwa kwenye Idara na Taasisi za Serikali na watu binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2014/2015, SUMAJKT kupitia sekta ya kilimo iliendelea na uzalishaji wa mbegu bora za mazao pamoja na uzalishaji wa mifugo. Aidha, Shirika lilishirikiana na *Tanzania Investment Bank (TIB)* kuboresha kilimo cha umwagiliaji cha zao la mpunga katika kikosi cha Chita kilichopo Wilaya ya Kilombero Mkoani Morogoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, SUMAJKT imeendelea kuyauzia mbegu bora makampuni ya mbegu ya *Agricultural Seeds Agency (ASA), TANSEED, Tropical Seed Company Ltd, Southern Highland Seed Growers Ltd, Kibo Seed na SUBA Company* iliyoingia nayo mikataba. Hata hivyo, katika utekelezaji wa mikataba hii, kumejitokeza changamoto kwa makampuni hayo kutolipa madeni kwa wakati hali inayosababisha shirika kushindwa kufikia malengo yake. Hadi sasa jumla ya Sh.908,716,976.00 hazijalipwa na makampuni hayo. SUMAJKT limeshachukua hatua za kisheria ya kuyafikisha Mahakamani makampuni inayoyadai. Aidha, SUMAJKT limesajili Wakala wake wa Mbegu ambao linaitwa *SUMAJKT Seed Company Ltd* wenye usajili Na.09818 ya tarehe 3 Februari, 2015 ili kuweza kusambaza kwa wingi na unafuu mbegu bora kwa wakulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kujipanua zaidi kibiashara, SUMAJKT kupitia Kampuni yake ya Ulinzi ya *SUMAJKT Guard* imeendelea kutoa huduma

za ulinzi katika Idara za Serikali na sekta binafsi ikiwemo; vituo vya kuzalisha umeme vya Kihansi na Mtera Mkoani Morogoro, Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM), Wizara ya Fedha, CRDB, UBA, Migodi ya STAMIGOLD, Chuo cha Madini Nzega na Chunya, TEMESA - Kivukoni na Busisi/Kigongo Mwanza na TPDC. Hadi sasa kampuni imeajiri walinzi 1,850, ikiwa ni ongezeko la walinzi 182 ukilinganisha na idadi ya walioajiriwa hadi kufikia Juni, 2014.

Mheshimiwa Naibu Spika, SUMAJKT limeendelea kuendesha na kusimamia mradi wa matrekta kwa niaba ya Serikali kuanzia mradi ulipozinduliwa tarehe 7 Oktoba, 2010 ukiwa na lengo la kuongeza uzalishaji wa mazao ya kilimo kwa kuongeza matumizi ya mashine za kisasa ili kuinua kipato cha wananchi, kuhamasisha matumizi bora ya matrekta, *power tillers*' na zana mbalimbali za kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia mwezi Machi, 2015 SUMAJKT kupitia mradi huu lilifanikiwa kuuza matrekta 1,841 na zana 2,929 zenye thamani ya Sh.65,550,428,807.00 kwa njia ya mkopo. Hata hivyo, ukusanyaji wa fedha za mkopo huo ambao ni utekelezaji wa awamu ya kwanza ya mradi ulifikia Sh.31,059,800,870.00 sawa na asilimia 47.4 ya thamani ya mali iliyouzwa. Awamu ya pili ya mradi huu ilianza Oktoba, 2013 ambapo ilihusisha ununuzi wa matrekta 268 kutoka India kwa thamani ya Sh. 7,046,245,600.00. Awamu hii ya mradi inatarajia kukusanya jumla ya Sh. 8,551,692,701.48 baada ya mauzo yote.

Hadi sasa jumla ya matrekta 232 yameshauzwa kwa wateja kwa thamani ya Sh. 7,609,603,059 sawa na asilimia 89. Napenda kuwakumbusha wadaiwa wote kukamilisha malipo ya matrekta waliyokopa.

Mheshimiwa Naibu Spika, shughuli za Shirika la Mzinga. Kulingana na mpango mkakati wa Shirika wa miaka 15 kuanzia mwaka 2011 - 2026, Shirika la Mzinga lina malengo yafuatayo:-

(i) Kuendeleza uzalishaji wa mazao ya msingi kwa ajili ya ulinzi na usalama wa nchi;

(ii) Kuanzisha kiwanda cha kuzalisha milipuko;

Nakala ya Mtandao (Online Document)

(iii) Kuanzisha kituo cha utafiti wa silaha za kijeshi na kusimika mfumo wa usalama wa kiwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2014/2015, Shirika la Mzinga lilikusudia kukamilisha ujenzi wa mkondo mpya wa risasi na ukarabati wa baadhi ya karakana na mitambo, kugharamia ujenzi wa maghala matatu mapya ya kuhifadhi silaha na kukamilisha uboreshaji wa mitambo ya uzalishaji awamu ya kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na ufinyu wa bajeti, shirika lilipata changamoto katika kutekeleza shughuli zake za msingi. Hata hivyo, kwa kutumia mapato madogo ya ndani, shirika limeendelea na uzalishaji katika mkondo wa risasi katika kaliba mbalimbali na ukarabati wa barabara za ndani na maeneo yanayozunguka shirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, shughuli za Shirika la Nyumbu. Katika mwaka 2014/2015, Shirika la Nyumbu lilipanga kutekeleza shughuli zake za kuendeleza utafiti katika teknolojia ya magari na mitambo ya kijeshi, kuimarisha na kuongeza uwezo wa kuhawilisha teknolojia mbalimbali za utafiti na kukarabati miundombinu ya shirika. Kutokana na ukosefu wa fedha za maendeleo, shirika halikuweza kutekeleza shughuli zake za msingi. Hata hivyo, kwa kutumia mapato madogo ya ndani, shirika lilifanikiwa kufanya ukarabati mdogo wa nyumba za makazi na mitambo ya karakana ya shirika; kununua vifaa vya TEHAMA na kukarabati mfumo wa umeme kiwandani.

Mheshimiwa Naibu Spika, mtandao wa mawasiliano Jeshini. Wizara inatekeleza Mradi wa Mawasiliano Salama ya Kujitegemea Jeshini, ambapo hadi kufikia Machi, 2015 jumla ya minara 131 ilisimikwa Tanzania Bara na Visiwani na vituo (*control centre*) viwili kwa ajili ya kuendesha na kusimamia mawasiliano hayo vilishajengwa Dar es Salaam na Dodoma. Mtandao huu umefanyiwa majaribio wakati wa sherehe za maadhimisho ya Mapinduzi ya Zanzibar tarehe 12 Januari, 2015 ambapo mawasiliano ya kimtandao yaliweza kupatikana katika maeneo ya Zanzibar, Pwani na Dar es Salaam. Kazi ya kuunganisha maeneo mengine ya nchi kwenye mtandao huo inaendelea.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Naibu Spika, kudhibiti uvamizi wa maeneo ya Jeshi, upimaji na ulipaji fidia. Serikali imeendelea kufanya upimaji, uthamini na ulipaji wa fidia wananchi kwa maeneo halali yaliyotwaliwa kwa matumizi ya Jeshi kulingana na upatikanaji wa fedha. Katika mwaka wa fedha 2014/2015, Wizara imefanya upimaji na uthamini katika maeneo ya Mahongole – Makambako, Ilemela – Mwanza, Kimbiji – Temeke, Kikongo Ferry – Mwanza, Kasanga – Rukwa, Mkiwa-Singida na Ntyuka-Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na upatikanaji mdogo wa fedha, Wizara imefanikiwa kulipa fidia katika baadhi ya maeneo yakiwemo Mahongole - Makambako na kwa ardhi ya Shirika la Masista -Kasanga Rukwa, ukilinganisha na malengo ya kulipa fidia katika maeneo yote yaliyofanyiwa uthamini. Pamoja na hatua zinazochukuliwa na Serikali zikiwemo za kisheria, wananchi wanashauriwa kutovamia maeneo ya Jeshi wala kufanya shughuli zozote katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto za utekelezaji wa Mpango na Bajeti katika mwaka 2014/2015. Wizara imeendelea kukabiliwa na changamoto mbalimbali lakini kubwa ikiwa ni kupata kiwango kidogo cha fedha ukilinganisha na bajeti halisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2014/2015, Wizara iliomba Sh.708,731,094,124.00 kwa ajili ya Matumizi ya Maendeleo kwa kuzingatia vipaumbele vyake lakini kiasi kilichoidhinishiwa ni Sh.248,842,500,000.00, sawa na asilimia 35.1 ya mahitaji hayo. Hali hii kwa kiasi kikubwa inaathiri utekelezaji wa shughuli za Mpango wa Maendeleo ya Jeshi, mfano kushindwa kulipa mikopo mbalimbali ya kimikataba.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango wa Mwaka 2015/2016. Mpango na Malengo ya Wizara ya Ulinzi na JKT katika mwaka 2015/2016, ni kuendelea kuimarisha uwezo wa kulinda mipaka ya nchi yetu pamoja na kuimarisha mazingira ya amani na utulivu na nchi nyingine duniani, hususan na nchi jirani. Ili kufikia mpango na malengo hayo, Wizara imekusudia kutekeleza majukumu yafuatayo:-

(i) Kuendelea kuliimarisha na kuliongezea uwezo Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania katika utendaji kivita kwa kulipatia vifaa na zana bora za kisasa pamoja na kutoa mafunzo stahiki kwa Wanajeshi dhidi ya adui wa ndani na nje.

(ii) Kulijengea Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania mazingira mazuri ya kufanyia kazi na makazi ikiwa ni pamoja na kujenga nyumba za kuishi Wanajeshi katika makambi na kuimarisha upatikanaji wa huduma na mahitaji ya msingi

kama vile chakula, tiba, sare, usafiri, maslahi na stahili kwa Wanajeshi na watumishi raia.

(iii) Kuimarisha uwezo wa Jeshi katika utafiti na kuendeleza teknolojia kwa madhumuni ya kuzalisha bidhaa na huduma kwa ajili ya matumizi ya kijeshi na kiraia hapa nchini na nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, shukrani. Kabla sijahitimisha hotuba yangu, napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru wafuatao kwa michango yao katika maandalizi ya taarifa hii ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara yangu; Katibu Mkuu - Bwana Job Masima, Naibu Katibu Mkuu - Bi. Mwintango Rose Shelukindo, Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi - Jenerali Davis Mwamunyange, Mnadhimu Mkuu Luteni - Jenerali Samuel Ndomba, Mkuu wa Jeshi la Kujenga Taifa - Meja Jenerali Raphael Muhuga, Wakuu wa Kamandi za Jeshi la Nchi Kavu - Meja Jenerali Salum Kijuu, Jeshi la Anga - Meja Jenerali Joseph Kapwani na Jeshi la Wanamaji - Meja Jenerali Rogastian Laswai, Meneja Mkuu wa Shirika la Mzinga - Meja Jenerali Charles Muzanila na Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Nyumbu - Brigedia Jenerali Anselm Bahati.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napenda kuwashukuru Wakuu wa Idara na Vitengo (Makao Makuu ya Wizara), Wakuu wa Matawi (NGOME), Wakuu wa Idara (Makao Makuu ya Jeshi la Kujenga Taifa), Maafisa, Askari na Watumishi wa Umma wa Wizara kwa kunipa ushirikiano katika kufanikisha majukumu ya Wizara. Aidha, naishukuru Kamati ya Wizara iliyoandaa hotuba hii na Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali kwa kuchapisha hotuba hii kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuwashukuru wahisani mbalimbali waliotoa michango yao kwa namna moja au nyingine katika kufanikisha maendeleo ya Jeshi. Wahisani hao ni pamoja na Serikali ya Jamhuri ya China ambao wameshiriki katika upanuzi wa uwanja wa ndege Ngerengere na ujenzi wa nyumba za makazi ya Wanajeshi 6,064 kupitia mkopo nafuu kutoka Benki ya EXIM China. Vilevile, naishukuru Serikali ya Ujerumani ambayo imeshiriki katika ujenzi wa vituo vya afya vya Kanda, ukarabati na uboreshaji wa karakana kuu ya Jeshi Lugalo na uboreshaji wa Hospitali Kuu ya Jeshi Lugalo. Nazishukuru pia nchi zifuatazo, kwa ushirikiano tuliokuwa nao katika nyanja za ulinzi pamoja na mafunzo. Nchi hizi ni Afrika Kusini, Bangladesh, Burundi, Canada, China, DRC, Ghana, Falme za Kiarabu, Indonnesia, Kenya, Marekani, Msumbiji, Misri, Namibia, Nigeria, Rwanda, Uganda, Ujerumani, Uingereza, Urusi, Zimbabwe na Zambia. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa umuhimu wa pekee na kwa kupitia Bunge lako Tukufu, naomba kuwasilisha salamu za pongezi maalum za Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu, kwa Wanajeshi wote kwa

Nakala ya Mtandao (Online Document)

kufanikisha Maadhimisho ya miaka 50 ya Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania yaliyofanyika Arusha mwezi Septemba, 2014. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Bajeti ya Mwaka 2015/2016. Makadirio ya Mapato. Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na Taasisi zake haina vyanzo vya uhakika vya mapato vinavyoweza kuchangia kwa kiasi kikubwa katika ukusanyaji wa maduhuli. Hali hii inasababishwa na majukumu ya msingi ya Wizara hii. Chanzo kikuu cha mapato ni makusanyo ya mauzo yanayotokana na nyaraka za zabuni, suala ambalo kwa sasa linashughulikiwa pia na GPSA.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2015/2016, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa inatarajia kukusanya jumla ya Sh.72,606,000/= katika mchanganuo ufuatao:-

- (i) Fungu 38 – NGOME , Sh.11,601,000/=
- (ii) Fungu 39 – JKT, Sh.50,003,000/=
- (iii) Fungu 57 – Wizara, Sh.11,002,000/=

Mheshimiwa Naibu Spika, Matumizi ya Kawaida na Maendeleo. Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa inaomba kuidhinishiwa jumla ya Sh.1,716,301,362,000.00 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na matumizi ya maendeleo ili iweze kutekeleza majukumu yake ya mwaka 2015/2016. Kati ya fedha hizo, Sh.1,477,163,404,000.00 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Sh. 239,137,958,000.00 ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Mchanganuo kwa kila Fungu ni kama ifuatavyo:-

Fungu 38 – NGOME.

- (i) Matumizi ya KawaidaSh.1,163,083,841,000.00
 - (ii) Matumizi ya MaendeleoSh.12,000,000,000.00
- Jumla Sh.1,175,083,841,000.00

Fungu 39 – JKT.

- (i) Matumizi ya KawaidaSh.292,296,992,000.00
 - (ii) Matumizi ya MaendeleoSh.7,000,000,000.00
- Jumla Sh.299,296,992,000.00

Fungu 57 – Wizara.

- (i) Matumizi ya Kawaida Sh.21,782,571,000.00
 - (ii) Matumizi ya MaendeleoSh.20,137,958,000.00
- Jumla Sh.241,920,529,000.00

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, hotuba hii inapatikana pia katika tovuti ya Wizara (www.modans.go.tz).

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. (Makofi)

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

**HOTUBA YA WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA
MHESHIMIWA DKT. HUSSEIN ALI MWINYI (MB)
AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO
NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2015/16 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika**, kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Ulinzi na Usalama, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali kupokea, kujadili na kupitisha Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2015/16.

2. **Mheshimiwa Spika**, kwa muktadha huo, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema, aliyenijalia kuwa na uzima na afya njema na kuniwezesha kuwasilisha hotuba yangu ya bajeti kwa mwaka 2015/16. Aidha namshukuru kwa dharti Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu, wa Majeshi ya Ulinzi ya Tanzania, **Mhe. Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete**, kwa kuendelea kuniamini kuiongoza Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Napenda kurejea ahadi yangu kwa Mhe. Rais na Watanzania wenzangu kuwa nitaendelea kutumia uwezo, nguvu na akili zangu zote kutekeleza majukumu yangu kwa haki, weledi, uaminifu, uadilifu na unyenyekevu wa hali ya juu ili kufanikisha malengo ya Taifa kwa ujumla na Wizara kwa hakika.

3. **Mheshimiwa Spika**, vile vile napenda kutumia fursa hii kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Wasaidizi wake Wakuu Kitaifa, Makamu wa Rais, Mhe. Dkt. Mohamed Gharib Bilal na Waziri Mkuu, Mhe. Mizengo Kayanza Peter Pinda (Mb) kwa kuiongoza nchi yetu vema na kwa usimamizi na utekelezaji mzuri wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2010-2015. Aidha napenda kumpongeza Spika wa Bunge hili Mhe. Anne Semamba Makinda (Mb), Naibu Spika Mhe. Job Yustino Ndugai (Mb) pamoja na Wenyeviti wa Bunge kwa kuendesha vizuri shughuli za Bunge letu. Na kwa namna ya pekee, naungana na wenzangu kukupongeza Mhe. Spika kwa kuchaguliwa kwako kuwa Rais wa Jukwaa la Bunge la Nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC). Namwomba Mwenyezi Mungu azidi kuwapeni nyote baraka, hekima, busara na nguvu za kuendelea kuiongoza Bunge hili katika kutekeleza majukumu yake mengi, mazito na nyeti. Pia

napenda kutoa pongezi na shukrani za dhati kwa wananchi wa jimbo langu la Kwahani kwa kunipa ushirikiano katika kipindi chote cha miaka mitano niliyokuwa mwakilishi wao. Ni imani yangu kuwa tutayaendeleza mafanikio tuliyopata.

4. Mheshimiwa Spika, naomba kutumia nafasi hii kumshukuru tena Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ulinzi na Usalama Mhe. Anna Margareth Abdallah (Mb) na Wajumbe wote wa Kamati hii Tukufu kwa kuendelea kunipa ushirikiano wa kutosha katika kuiongoza Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Kwa uhakika, Kamati hii imekuwa muhimili imara kwetu kwa kipindi chote kwani imesimamia, imeongoza, imeshauri, imefuatilia na imetembelea miradi mbalimbali inayotekelezwa na Wizara na hivyo kujionea yenyewe maendeleo na changamoto tunazokabiliana nazo. Ushauri na maelekezo ya Kamati yamechangia kwa kiasi kikubwa katika maendeleo ya Sekta ya Ulinzi na Usalama hapa Nchini. Na kwa uzito wa kipekee kabisa, na kwa niaba ya wapiganaji shupavu wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania, tunawapongeza na kuwashukuru kwa ziara yenu ya kihistoria mliyoifanya kuanzia tarehe 12-19 Aprili, 2015 kutembelea Wapiganaji wetu walioko nchini DRC. Ziara hiyo imeongeza ari na morali wa kazi kwa wapiganaji wetu wote.

5. Mheshimiwa Spika, ninaungana na wenzangu wote waliotangulia kuwapa pole wale waliopatwa na majanga, pamoja na kufiwa na ndugu, jamaa na wapendwa wao katika matukio mbalimbali yaliyotokea nchini yakiwemo mafuriko na ajali za vyombo vya usafiri yakiwemo mabasi ya abiria. Aidha, nachukua fursa hii kutoa salamu za pole kwako Mhe. Spika, Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wote kwa kuondokewa na mpendwa wetu Mhe. Kapteni mstaafu John Damian Komba, Mbunge wa Jimbo la Mbinga Magharibi. Naomba Mwenyezi Mungu azilaze roho za Marehemu wote mahala pema **Amina.**

6. Mheshimiwa Spika, mwaka 2015 ni mwaka ambao Watanzania watahusika na masuala mengi muhimu yakiwemo kujiandikisha katika Daftari la kudumu la wapiga kura na kushiriki katika Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani. Hivyo nikiwa kama mtanzania, na kwa kuzingatia kuwa Wizara yangu ni wadau wakubwa katika kufanikisha mustakabali wa Taifa letu, naungana na watanzania wengi wenye mapenzi mema na nchi yetu kuwaasa wananchi tushiriki kwa ukamilifu na kwa utulivu mkubwa katika kufanikisha masuala hayo muhimu kwa mustakabari wa Taifa letu.

7. Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo ya utangulizi, napenda sasa kuchukua fursa hii kuwasilisha hotuba yangu ambayo kiujumla imejikita katika maeneo makuu yafuatayo: Malengo na majukumu ya Wizara; Utekelezaji wa Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ulinzi na Usalama, Hali ya Ulinzi na

Usalama, Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya mwaka 2014/15 na Mpango na Makadirio ya Bajeti kwa mwaka 2015/16.

MALENGO NA MAJUKUMU YA WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA

8. **Mheshimiwa Spika**, kama ilivyo katika **Dira** yetu, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa inaendelea kuwa Taasisi iliyotukuka ya kulinda na kudumisha amani na usalama wa Taifa. Vivyo hivyo, tumeendelea kulinda Jamhuri ya Muungano wa Tanzania dhidi ya adui wa aina yoyote kutoka ndani au nje ya nchi na kuhakikisha kuwa Mamlaka ya nchi na maslahi ya Taifa letu yako salama sanjari na **Dhima** yetu.

9. **Mheshimiwa Spika**, katika kufanikisha Dira na Dhima zetu, malengo ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa yameendelea kuwa kama ifuatavyo:

(i) Kuwa na jeshi dogo la Ulinzi wa Nchi lenye taaluma mpya, zana bora, vifaa vya kisasa na mawasiliano salama.

(ii) Kuendeleza mazingira bora ya kufanyia kazi na makazi kwa kuimarisha yaliyopo na kujenga mapya.

(iii) Kuimarisha tafiti za kijeshi katika mashirika ya Mzinga na Nyumbu na kuhawilisha teknolojia mpya.

(iv) Kuendelea kuwajengea vijana wa kitanzania moyo wa uzalendo, ukakamavu, maadili mema na utaifa.

(v) Kuimarisha utayari wa Jeshi la akiba.

(vi) Kuhifadhi na kumiliki maeneo yake ya ardhi kwa ajili ya matumizi ya Jeshi.

(vii) Kuendelea kudumisha amani na usalama kwa kushirikiana na nchi nyingine duniani.

10. **Mheshimiwa Spika**, ili kufikia malengo haya, Wizara itaendelea kusimamia utekelezaji wa majukumu yafuatayo:-

(i) Uandikishwaji wa wanajeshi wenye sifa zinazohitajika kwa jeshi dogo kwa ajili ya Ulinzi wa Taifa na kuwapatia mafunzo na mazoezi ya kinadharia na kivitendo.

(ii) Kuwapatia wanajeshi makazi, zana, vifaa na vitendea kazi vipya, bora na vya kisasa.

(iii) Kusimamia matunzo na matumizi mazuri ya zana, vifaa na vitendea kazi kwa ujumla.

(iv) Kuimarisha mafunzo na mazoezi ya kijeshi ikiwa ni pamoja na shughuli za uendeshaji mafunzo ya ulinzi wa mgambo.

(v) Kuboresha mitaala ya mafunzo ya JKT kwa vijana waliojiunga na mafunzo hayo kwa Mujibu wa Sheria au kwa utaratibu wa kujitolea ili iwaandae vijana hao kuwa wakakamavu, wenye nidhamu na kuwajengea moyo wa uzalendo na mshikamano wa kitaifa katika kutekeleza shughuli za kujitegemea.

(vi) Kuendeleza utafiti na uhawilishaji wa teknolojia za kijeshi na kuzalisha mali kupitia mashirika ya Mzinga na Nyumbu.

(vii) Kuwezesha uzalishaji wa Shirika la Uzalishaji Mali la Jeshi la Kujenga Taifa (SUMAJKT) kuwa wa tija na faida itakayochangia katika uendeshaji wa shughuli za Jeshi la Kujenga Taifa.

(viii) Kushirikiana na Mamlaka za kiraia pale inapobidi katika kukabiliana na majanga na dharura za kitaifa.

(ix) Kuimarisha mazingira bora ya kuishi na kufanyia kazi na

(x) Kuimarisha ushirikiano na nchi nyingine duniani katika masuala ya kijeshi.

UTEKELEZAJI WA MAONI NA USHAURI WA KAMATI YA KUDUMU YA ULINZI NA USALAMA YA BUNGE LA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

11. **Mheshimiwa Spika**, wakati Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ulinzi na Usalama ilipokaa na kujadili Makadirio ya Mapato, Mpango na Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka 2014/15 ilitoa maoni, ushauri na maelekezo kadhaa kwa Wizara hii yaliyolenga kuboresha utendaji na utekelezaji wa majukumu yake. Napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa maoni, ushauri na maelekezo yaliyotolewa yamefanywa kazi na majibu yake yameainishwa katika **Kiambatanisho Namba 1**. Aidha, hoja mbalimbali zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge wakati wa mjadala huo pia zimezingatiwa katika mpango na bajeti ya mwaka 2015/16 ninayowasilisha leo hapa Bungeni.

HALI YA ULINZI NA USALAMA

(i) Ugaidi na Uharamia Duniani

12. **Mheshimiwa Spika**, vitendo vya kigaidi na uharamia vimeendelea kuwa tishio kubwa duniani. Mwelekeo wa matukio ya ugaidi hivi sasa ni matumizi ya mbinu na zana za kisasa ikiwemo teknolojia ya habari na mawasiliano katika kufanikisha malengo yao bila kugundulika kiurahisi. Baadhi ya makundi ya ugaidi yanayoendesha harakati zake maeneo mbalimbali duniani ni pamoja na kundi la “Islamic State in Iraq and Syria (ISIS)”, Boko Haram, Al Qaeda na Al Shabaab. Makundi hayo yanaendesha kampeni za kurubuni na kuandikisha makundi ya vijana kutoka mataifa mbalimbali ili kujiunga nayo, hali ambayo inalifanya tishio la ugaidi kusambaa maeneo mengi duniani na kutokuwa na mipaka. Kutokana na ukubwa wa maeneo ya mipaka ya nchi yetu na kuwepo kwa mipenyo katika mipaka hiyo, upo uwezekano wa makundi ya kihalifu kutoka nje kuingia nchini na kufanya uhalifu ikiwemo kueneza itikadi zenye msimamo mkali (radicalization) pamoja na ugaidi. Tunaendelea kuwatahadharisha wananchi kuwa macho na kuyatolea taarifa matukio yanayotishia usalama wa nchi pindi yanapojitokeza.

13. **Mheshimiwa Spika**, Jeshi letu pamoja na kushirikiana vema na vyombo vingine vya ulinzi vya hapa nchini, pia limeshirikiana na majeshi mbali mbali katika kukabiliana na vitendo vya kigaida kwa kuimarisha doria na kuhakikisha eneo hilo la bahari linakuwa salama pamoja na vyombo vya usafirishaji baharini vinaendelea na shughuli zake bila tishio lolote. Ushirikiano na majeshi mbalimbali umekuwa katika nyanja za mazoezi na operesheni za pamoja ambapo katika kipindi hiki, JWTZ lilifanya operesheni za pamoja katika Bahari ya Hindi na majeshi rafiki ya nchi za Kenya, Msumbiji na Afrika Kusini.

(ii) Hali ya Ulinzi na Usalama katika Nchi za Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati

14. **Mheshimiwa Spika**, hali ya Ulinzi na Usalama katika nchi za ukanda wa Afrika Mashariki na Kati ni shwari. Hata hivyo, ukanda huu umekuwa katika tahadhari ya kiusalama dhidi ya mashambulizi ya kigaidi kutoka kundi la Al Shabab la nchini Somalia. Ingawa kundi hili limekuwa likidai kulenga nchi zenye majeshi katika operesheni za Umoja wa Afrika nchini Somalia “The African Union Mission in Somalia (AMISOM),” mienendo yao imekuwa ikiashiria tofauti. Kwa msingi huo vyombo vyetu vya Ulinzi na Usalama kwa kushirikiana na raia wema vimekuwa macho na nyendo za wafuasi wa kundi hili. Pamoja na hayo, hali ya usalama wa nchi yetu kwa ujumla imeendelea kuwa shwari

15. **Mheshimiwa Spika**, pamoja na hali hiyo kumekuwepo na matukio machache yasiyokuwa ya kawaida na yenye dalili za uhalifu uliopitiliza

(extended crime). Matukio haya yamepelekea mauaji ya askari wa JWTZ na wa Polisi na uporaji wa silaha. Naomba nichukue fursa hii kulifahamisha Bunge lako tukufu kwamba juhudi kubwa zimefanyika na zinaendelea kufanywa na vyombo vyetu vyote vya ulinzi na usalama katika kukabiliana na wahalifu hao na mtandao wao. Tunawashukuru wananchi kwa ushirikiano wao katika kukabiliana na njama za uhalifu huu au kuwezesha wahalifu kukamatwa. Aidha, tunawaasa wananchi wote kuwa macho na maadui hao na kuwaomba waendeleo kushirikiana na vyombo vya ulinzi na usalama kukabiliana nao.

16. Mheshimiwa Spika, vikundi vya uasi vyenye silaha vya “The Democratic Forces for the Liberation of Rwanda (FDLR)”, “The Allied Democratic Forces” (ADF) na “The Lord’s Resistance Army” (LRA), vimesababisha hali ya usalama kuwa tete Mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo. Ingawa Kikundi cha FDLR kilitakiwa kujisalimisha mapema tarehe 02 Januari, 2015 kwa Majeshi ya Umoja wa Mataifa (“United Nations Organization Stabilization Mission in the DR Congo” – MONUSCO) hakikuteketeleza kama kilivyotakiwa kwani hadi kufikia tarehe ya mwisho, ni asilimia 30 tu ya waasi hao walikuwa wamejisalimisha. Kutokana na hali hiyo taratibu za kukikabili Kikundi hicho zinaendelea chini ya Umoja wa Mataifa.

17. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa nchi ya Somalia na Sudan Kusini kumekuwa na hali tete ya Usalama hususan nchini Somalia kutokana na mapambano yanayoendelea baina ya majeshi ya AMISOM na kundi la Kigaidi la Al Shabaab. Aidha, hali ya uhusiano kati ya Serikali ya Sudan Kusini inayoongozwa na Rais Salva Kiir na kikundi kinachomuunga mkono Dkt. Riek Machar aliyekuwa Makamu wa Rais imeendelea kuwa tete. Hata hivyo, mazungumzo ya amani yanayoendelea yameanza kuonesha mwelekeo wa kupatikana ufumbuzi wa uhasama uliopo kati ya pande hizo mbili. Kwa upande wa uharamia wa baharini, hakuna matukio yaliyojitokeza katika mwaka 2014/15. Hata hivyo, vyombo vyetu vya ulinzi vinaendelea kufanya ulinzi mkali kwenye eneo letu.

(iii) Hali ya Usalama wa Mipaka

18. Mheshimiwa Spika, kufuatia juhudi kubwa zinazofanywa na vyombo vyetu vya Ulinzi na Usalama kwa kushirikiana na wananchi, majaribio ya ugaidi na matendo maovu ya biashara za madawa ya kulevya, uhamiaji haramu na ujambazi kwa ujumla yamepungua. Hali hiyo imepelekea hali ya mipaka yetu kuwa shwari. Kwa ujumla hali ya mipaka yetu imekuwa kama ifuatavyo:

(a) Mpaka wa Mashariki

19. Mheshimiwa Spika, katika mpaka huu wenye urefu wa km 1,424, nchi yetu inapakana na nchi za Kenya, visiwa vya Ushelisheli na Komoro na nchi ya

Msumbiji. Hali ya usalama katika mpaka huu imeendelea kuwa shwari hakuna tukio lolote la kihalifu lililotokea katika kipindi hiki.

(b) Mpaka wa Kaskazini

20. **Mheshimiwa Spika**, katika mpaka huu wenye urefu wa kilomita 1,221 nchi yetu inapakana na nchi za Kenya na Uganda. Hali ya usalama katika mpaka huu kwa ujumla ilikuwa shwari. Hata hivyo, matukio ya uharibifu wa alama za mipaka (beacons) na ujenzi holela unaofanywa na baadhi ya watu waishio maeneo ya mipakani kwa lengo la kujipatia ardhi kwa ajili ya kilimo, malisho ya mifugo, biashara na ujenzi wa makazi yameendelea kujitokeza na hivyo kuwa changamoto kubwa kwa usalama wa nchi yetu.

(c) Mpaka wa Magharibi

21. **Mheshimiwa Spika**, mpaka wetu wa Magharibi una urefu wa kilomita 1,220. Katika mpaka huu Tanzania tunapakana na nchi za Burundi, Rwanda na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC). Ingawa hali ya usalama wa mpaka huu kwa ujumla umekuwa shwari, matukio ya ujambazi wa kutumia silaha maeneo ya nchi kavu na katika Ziwa Tanganyika ambayo kwa sehemu kubwa yanafanywa na watu wenye silaha na baadhi yao wana uhusiano na vikundi vinavyohasimiana nchini DRC na wengine wakiwa ni masalia ya waasi kutoka nchini Burundi yameendelea kujitokeza. Katika ujambazi huo makundi hayo yamekuwa yakiwashambulia wavuvi na kuwanyang'anya fedha, bidhaa mbali mbali na vifaa vya uvuvi na hata kuwajeruhi.

22. **Mheshimiwa Spika**, mifano ya karibuni ni mwezi Desemba, 2014 ambapo majambazi wenye silaha za kivita wakiwa wamevaa sare za jeshi la nchi jirani waliwavamia na kuwapora wananchi wetu mali na fedha. Aidha, mwezi Novemba 2014, majambazi yenye silaha za kivita yaliwavamia wavuvi katika Ziwa Tanganyika na kuwapora mashine za boti zao na vifaa mbalimbali vya uvuvi na kumteka mvuvi mmoja wakampeleka nchi jirani na baadaye walimwachia na kumruhusu kurudi nyumbani. Matukio hayo ni kielelezo cha kuwepo kwa tishio la usalama katika mpaka wetu wa Magharibi. Hatua za kukabiliana na matukio hayo zimechukuliwa.

(d) Mpaka wa Kusini

23. **Mheshimiwa Spika**, mpaka wetu wa Kusini una urefu wa kilomita 1,536 ambapo Tanzania tunapakana na nchi za Msumbiji, Malawi na Zambia. Hali ya usalama katika mpaka huu imeendelea kuwa shwari. Pamoja na kwamba hatua ya mwisho ya kufikia usuluhishi mgogoro wa mpaka wetu na Malawi katika ziwa Nyasa bado haijafikia, hali ya kiusalama imeendelea kuwa shwari na wananchi wa pande zote wanaendelea na shughuli zao bila bugudha

yoyote ya kiulinzi. Ombi letu kwa wenzetu wa Malawi ni kutulia na kuipa nafasi fursa ya usuluhishi wa mgogoro huo ikamilike.

MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA MWAKA 2014/15

24. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2014/15 Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ilikadiriya kukusanya mapato ya jumla ya shilingi 60,506,000.00 kutoka katika Mafungu yake matatu ya 38-NGOME, 39-JKT na 57-Wizara. Hadi kufikia mwezi Machi, 2015 Mafungu hayo yalifanikiwa kukusanya mapato ya jumla ya shilingi 47,268,778.00 sawa na **asilimia 78.1** ya makadirio. Makusanyo hayo kwa kiwango kikubwa yamefanikiwa kama ilivyokadiriwa. Hata hivyo kwa upande wa uchangiaji katika Mfuko wa Taifa, makusanyo haya ni madogo kwa vile chanzo chake kikuu ni mauzo ya hati za zabuni, ambapo kwa sasa utangazaji huo unafanywa pia na GPSA na hivyo kufanya mapato yake kupungua.

25. **Mheshimiwa Spika**, katika bajeti ya Mwaka wa Fedha 2014/15 Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa iliidhinishwa jumla ya **shilingi 1,269,076,056,000.00** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Maendeleo katika Mafungu yake matatu. Kati ya fedha hizo, **shilingi 1,020,076,056,000.00** zilitengwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **shilingi 249,000,000,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi ya Maendeleo. Hata hivyo, kufuatia maelekezo ya HAZINA ya kurekebisha vitabu vya bajeti ya mwaka 2014/15, bajeti ya mafungu ilibadilika na kuwa **shilingi 1,312,502,196,000.00** kukiwa na ongezeko la shilingi **43,426,140,000** sawa na asilimia **3.42**. Kati ya fedha hizo shilingi **1,063,659,696,000.00** zilitengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **shilingi 248,842,500,000.00** ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Mchanganuo wa bajeti hiyo kwa kuzingatia mafungu ya Wizara ni ufuatao:-

FUNGU	MATUMIZI		
	KAWAIDA	MAENDELEO	JUMLA
NGOME	839,635,388,000	12,000,000,000	851,635,388,000
JKT	204,566,662,000	7,000,000,000	211,566,662,000
WIZARA	19,457,646,000	229,842,500,000	249,300,146,000
JUMLA	1,063,659,696,000	248,842,500,000	1,312,502,196,000

26. **Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia mwezi Machi 2015, Wizara ilikuwa imepokea jumla ya **shilingi 919,748,922,788.00** sawa na **asilimia 70.07** ya bajeti. Kati ya fedha hizo **shilingi 846,248,922,788.00** sawa na asilimia 92.0 zilitumika kwa shughuli za kawaida ikiwemo kulipa mishahara na posho mbalimbali muhimu. Kwa upande wa Matumizi ya Maendeleo, fedha zilizopokelewa ni shilingi **73,500,000,000.00** sawa na **asilimia 29.53** ya fedha zote zilizoidhinishwa kwa ajili

ya shughuli za maendeleo. Mchanganuo wa Matumizi ya Kawaida na Maendeleo kwa Mafungu yote matatu ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa hadi mwezi Machi, 2015 umeoneshwa katika **Kiambatanisho Namba 2**.

27. **Mheshimiwa Spika**, tathmini ya fedha zilizopokelewa inaonesha kwamba mwenendo wa upatikanaji wa fedha kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida hususan fedha za mishahara na chakula kwa wanajeshi katika kipindi hicho kiujumla ulikuwa ni mzuri kwani fedha hizo zilipokelewa kulingana na makisio ya bajeti. Hata hivyo, fedha za Matumizi Mengineyo hazikutolewa kulingana na bajeti, kwani fedha zilizotolewa hadi Machi, 2015 zilikuwa **asilimia 61.03** ya bajeti yake. Aidha, kwa upande wa shughuli za Maendeleo hadi kufikia mwezi Machi, 2015 fedha zilizotolewa zilikuwa **asilimia 29.53** ya bajeti yake. Kiasi hicho ni kidogo sana ukilinganisha na mahitaji halisi yakiwemo kulipia madeni ya kimikataba ya ndani na nje. Hali hii pia imeathiri kasi ya upatikanaji wa vifaa na utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo.

MAFANIKIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA MWAKA 2014/15

MATUMIZI YA SHUGHULI ZA KAWAIDA

28. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2014/15, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ilifanikiwa kutekeleza shughuli mbali mbali katika kufikia malengo iliyojiwekea. Shughuli hizo ni pamoja na kuwapatia stahili mbali mbali wanajeshi, watumishi wa umma na vijana walioko katika mafunzo ya JKT na kutoa huduma muhimu za chakula, tiba, sare, umeme, maji, simu na mafuta ya uendeshaji wa majukumu ya ulinzi.

29. **Mheshimiwa Spika**, majukumu ya kiulinzi yaliyotekelezwa katika kipindi hicho ni pamoja na kufanyika mafunzo na mazoezi ya kijeshi, mafunzo ya Ulinzi wa Mgambo, upatikanaji wa huduma za afya na tiba kwa maafisa, askari na wananchi, ushirikiano wa kiulinzi na kijeshi na nchi nyingine, ushirikiano na Jumuiya za Kikanda na Kimataifa, ushirikiano wa Jeshi na Mamlaka za Kiraia, Mafunzo ya JKT kwa vijana wa kujitolea na wa Mujibu wa Sheria.

(i) Mafunzo na Mazoezi ya Kijeshi

30. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2014/15 Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania, limeendelea kutoa mafunzo na mazoezi kwa wanajeshi wake ili kulifanya kuwa imara na tayari muda wote kutekeleza majukumu yake ya kiulinzi. Aidha, Jeshi letu liliendelea kushiriki katika mafunzo na mazoezi ya pamoja na nchi marafiki. Miongoni mwa mazoezi hayo yalikuwa ni ya **ZOEZI LA "URUSHAJI NDEGE VITA NA MAONESHU YA ZANA"** katika Kamandi ya Jeshi la Anga lililofanyika Jijini Mwanza kati ya tarehe 23 – 28 Julai, 2014, **ZOEZI LA "VALEDE** lililotekelezwa na **JESHI MAALUM"** (Special Force), mwezi Agosti, 2014

nchini Angola, **ZOEZI LA “USHIRIKIANO IMARA”** lilifanyika nchini Burundi mwezi Oktoba, 2014, **ZOEZI LA “SOUTHERN ACCORD”** lililofanyika nchini Malawi mwezi Oktoba, 2014, **ZOEZI LA UTULIVU AFRIKA** lililofanyika nchini Tanzania mwezi Novemba, 2014 na **ZOEZI LA MIAKA 50 YA JWTZ** lililofanyika mkoani Arusha mwezi Septemba, 2014. Mazoezi ya aina hii mbali na kuliimarisha Jeshi kimedani pia, husaidia sana kuboresha na kuimarisha mahusiano ya majeshi yetu na majeshi ya nchi nyingine.

(ii) Mafunzo ya Ulinzi wa Mgambo

31. **Mheshimiwa Spika**, mafunzo ya ulinzi wa Mgambo kwa wananchi yameendelea kutolewa na Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania. Katika kipindi cha mwaka 2014/15 JWTZ kwa kushirikiana na vyombo vya Usalama limeendesha mafunzo katika ngazi mbalimbali ambapo jumla ya wananchi 14,107 walifuzu. Hili ni ongezeko la wahitimu 623 sawa na asilimia 4.6 ukilinganisha na wananchi waliopata mafunzo hayo mwaka 2013/14. Kati yao waliofuzu mafunzo hayo, wanaume walikuwa 12,732 na wanawake 1,375. Naendelea kutoa wito kwa Viongozi wa ngazi mbalimbali kuhamasisha wananchi kushiriki katika mafunzo haya na pia kutoa huduma stahiki Mahsuszi za hifadhi ya silaha na maeneo ya mafunzo.

(iii) Huduma za Afya na Tiba

32. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi hiki, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa imeendelea kutoa huduma za tiba kwa maafisa, askari, watumishi wa Umma, familia za wanajeshi na wananchi kwa ujumla. Huduma hizo zimekuwa zikitolewa katika Hospitali na Vituo vya tiba vya Jeshi hapa nchini. Aidha, huduma hizo zimeboreshwa baada ya kukamilika kwa mradi wa Ujenzi na ukarabati wa Chuo cha Sayansi za Tiba katika kambi ya Lugalo. Mipango yetu ni kukifikisha Chuo hicho katika hadhi ya kuwa Chuo Kikuu Kishiriki cha Sayansi za tiba cha Muhimbili. Kwa sasa Chuo hicho kina uwezo wa kutoa elimu ngazi ya Stashahada ya juu kwa fani za udaktari msaidizi, uuguzi, maabara na Ufamasia. Mchakato wa kutoa elimu ngazi ya Shahada katika fani za unesi, maabara na afya ya jamii unaendelea vizuri.

33. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi hiki, ajira 200 za wataalam wa tiba zimetolewa ili kukidhi mahitaji ya wataalam katika vikosi vya Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania. Aidha, katika juhudi za kuboresha miundo mbinu ya tiba kwenye vikosi vya Jeshi letu, miradi ifuatayo imekamilishwa ujenzi wa wodi mpya ya kisasa kwenye Hospitali Kuu ya Jeshi-Lugalo, ujenzi wa kituo cha uchunguzi (Diagnostic centre) katika Kikosi cha Jeshi Pemba, ujenzi wa jengo la X-Ray na Ultrasound katika Brigedi ya Songea, ujenzi wa jengo la maabara Kambi ya JKT Chita, upanuzi wa vituo vya utafiti wa ugonjwa wa malaria katika kambi za Jeshi la Kujenga Taifa Mgambo na Rwamkoma na ujenzi wa wodi ya Huduma ya Uzazi na Mtoto (Reproductive Child Health Care-RCH) Mwenge-Dar es Salaam. Pamoja na ujenzi wa wodi hii, kituo hiki kimepata msaada wa vifaa

vya kisasa ikiwemo mashine ya kisasa ya kupimia Kansa ya matiti ambayo ilitolewa na Taasisi ya WAMA tarehe 27 Februari, 2015. Kwa nafasi hii, na kwa niaba ya Wizara naomba kumshukuru tena Mama Salma Kikwete kwa msaada wa mashine hiyo.

(iv) Ushirikiano wa Kiulinzi na Kijeshi na Nchi Nyingine

34. **Mheshimiwa Spika**, ushirikiano kati ya nchi yetu na nchi nyingine katika nyanja za kijeshi ni suala muhimu katika mustakabali wa ulinzi na usalama wetu. Kwa kuelewa hivyo, Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania limeendelea kuwa na ushirikiano mzuri na majeshi ya nchi nyingine hususan katika mafunzo. Katika eneo hili, Jeshi letu limeendelea kupeleka maafisa wa ngazi mbalimbali kusoma katika vyuo vya kijeshi vya nchi marakifi zikiwemo China, Kenya, Uganda, Zambia, Rwanda, Afrika Kusini, Marekani, Ujerumani, Uingereza, Urusi na Falme za Kiarabu. Pia, maafisa kutoka katika baadhi ya Nchi hizi wapo hapa nchini katika vyuo vyetu vya kijeshi kwa mafunzo. Vyuo hivyo ni Chuo cha Maafisa Monduli (TMA), Chuo cha Ukamanda na Unadhimu (CSC) Arusha na Chuo cha Ulinzi wa Taifa (NDC) Dar es Salaam.

(v) Ushirikiano na Jumuiya za Kikanda na Kimataifa

35. **Mheshimiwa Spika**, Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania, limeendelea kushirikiana na Jumuiya za Kikanda na Kimataifa hususan katika Operesheni za ulinzi wa amani chini ya udhamini wa Umoja wa Nchi za Afrika (African Union) na Umoja wa Mataifa kama ifuatavyo: Kikosi kimoja cha Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania kipo Darfur, Sudan maeneo ya Khor-Abeche na Meanawashe, kikosi kingine kipo Mashariki mwa DRC kama sehemu ya MONUSCO "Intervention Brigade (IB)" na Kombania mbili za Polisi Jeshi zipo nchini Lebanon. Aidha, Jeshi linao Maafisa wanadhimu na makamanda kwenye Operesheni za Ulinzi wa Amani nchini Sudan, Sudan Kusini, Ivory Coast, Lebanon, Central Africa Republic na DRC. Luteni Jenerali Paul Ignas Mella aliteuliwa kuongoza Majeshi ya Umoja wa Mataifa katika Jimbo la Darfur, Sudan chini ya "United Nation High Brid Mission in Darfur" (UNAMID). Jeshi letu pia lilipewa heshima ya kuteua mwakilishi maalum wa Umoja wa Afrika katika mgogoro wa Sudan Kusini, ambapo Brigedia Jenerali Sara Thomas Rwambali alikabidhiwa jukumu hilo. Vikosi na maafisa wa Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania waliopo kwenye operesheni za ulinzi wa amani wote wanaendelea vizuri na utekelezaji wa majukumu yao.

(vi) Ushirikiano wa Jeshi na Mamlaka za Kiraia

36. **Mheshimiwa Spika**, katika kusaidiana na Mamlaka za Kiraia katika shughuli mbalimbali za kiraia na utoaji wa misaada, JWTZ kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi lilishiriki

kwa ukamilifu na kwa ufanisi mkubwa katika usambazaji nchini kote wa vitabu 2,500,000 vya masomo ya Sayansi na Hisabati vilivyotolewa msaada kutoka Serikali ya Marekani kupitia Shirika lake la USAID. Vitabu hivyo vilisambazwa kwa shule zote za Sekondari za Serikali Tanzania Bara kwa wakati na kuanza kutumika mwezi Januari, 2015 pale shule zilipofunguliwa. Nachukua fursa hii kuzipongeza Mamlaka za kiraia na taasisi zote kwa kutoa ushirikiano mzuri kwa Jeshi wakati wa kutekeleza majukumu iliyopewa.

37. **Mheshimiwa Spika**, Wizara kupitia JKT imekuwa mstari wa mbele katika kutekeleza zoezi la uandikishaji wa wananchi ili kupatiwa vitambulisho vya Taifa. Katika mwaka 2014/15, jumla ya vijana 1,357 kutoka JKT walishiriki katika zoezi la kuwaandikisha wananchi kwa ajili ya kupatiwa vitambulisho hivyo. Kazi hiyo ilifanyika katika awamu mbili; awamu ya kwanza vijana 1,000 walishiriki katika zoezi hili kwenye mikoa ya Dar es Salaam, Pwani na Morogoro hususan katika Wilaya ya Kilombero kuanzia mwezi Agosti hadi Desemba, 2014. Awamu ya pili ambayo imehusisha vijana 357 inaendelea katika Wilaya ya Bagamoyo mkoa wa Pwani.

38. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwaka 2014/15, Jeshi letu lilishiriki katika kusafirisha msaada wa chakula (mahindi) na dawa uliotolewa na Serikali ya Tanzania kwa nchi ya Malawi kufuatia janga la mafuriko lililoikumba nchi hiyo mapema mwaka 2015. Jeshi kwa kutumia askari na magari yake lilifanikiwa kusafirisha jumla ya tani 1200 za mahindi na tani 60 za dawa za aina mbalimbali kwenda nchini Malawi katika mji wa Karonga. Kazi hiyo ilifanyika kuanzia tarehe 22 hadi 30 Machi, 2015 hivyo napenda kuungana na wananchi wengi kuipongeza Serikali kwa kitendo hicho. Aidha, nalipongeza Jeshi kwa kutimiza jukumu hilo kwa haraka, na pia katika kipindi hicho Jeshi lilisaidia katika ujenzi wa nyumba kwa wananchi wa Kahama walioathirika na mafuriko.

(vii) Mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa kwa Vijana

39. **Mheshimiwa Spika**, mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa yameendelea kutolewa kwa vijana wa kujitolea na wale wa Mujibu wa Sheria wahitimu wa Kidato cha sita. Lengo la mafunzo hayo ni pamoja na kuwajengea uzalendo, ukakamavu, maadili mema, utaifa pamoja na kutoa stadi za kazi. Katika mwaka 2014/15 jumla ya vijana 40,082 walipatiwa mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa, kati yao vijana 8,447 ni wa kujitolea na vijana 31,635 ni wa Mujibu wa Sheria. Mahudhurio hayo ya vijana wa mujibu wa sheria yameongezeka kwa vijana 15,632 ukilinganisha na vijana 16,003 waliohitimu mafunzo hayo mwaka 2013/14. Hata hivyo idadi hii bado ni pungufu ikilinganishwa na idadi ya vijana 41,000 waliostahili kujiunga na mafunzo hayo (wahitimu wa kidato cha sita). Miongoni mwa sababu zilizopelekea upungufu huu, ni kalenda ya awamu ya pili ya vijana kugongana na kalenda ya kuanza mihula ya Elimu ya Juu (mwezi Septemba). Wito wangu kwa vijana ni kushiriki mafunzo hayo kwani ni ya

mujibu. Na kwa wale ambao hawakushiriki bila ridhaa yetu wataendelea kuwa kwenye orodha yetu ya vijana watoro. Wizara inatafuta uwezekano wa kuwawezesha JKT kuchukua kundi hilo la vijana kwa mkupuo mmoja wa Juni hadi Agosti ili kuwawezesha vijana wahitimu wa kidato cha sita waweze kuhudhuria mafunzo hayo na kuwahi muhula wa vyuo vya Elimu ya Juu.

40. Mheshimiwa Spika, dhima ya Jeshi la Kujenga Taifa ni kuwalea vijana wa kitanzania katika maadili mema, kuwajenga kinidhamu, kuwajengea uzalendo kwa nchi yao, kuwajengea ukakamavu, kufundisha na kuwapa ujuzi na stadi mbambali za kazi ili kuwaandalia mazingira mazuri ya kujijiri mara wamalizapo mkataba wa mafunzo yao. Wakati wa kuandikishwa kujiunga na mafunzo hayo vijana hujaza na kusaini fomu ya mkataba maalum yenye masharti kwamba kijana awe tayari kurudi nyumbani mara amalizapo mkataba wake. Hata hivyo, tangu kuanza kwa utaratibu wa mafunzo hayo baadhi ya wahitimu wamekuwa wakijiriwa na Vyombo vya Ulinzi na Usalama pamoja na Taasisi binafsi kulingana na mahitaji ya vyombo hivyo. leleweke kuwa sio vijana wote wanaohitimu mafunzo hayo hupata ajira kwenye vyombo na Taasisi hizo. Napenda kutoa rai kwa vijana wanaopata mafunzo ya JKT wazingatie maarifa na ujuzi wanaoupata hususan wa stadi za kazi ili waweze kujijiri badala ya imani inayoanza kujitokeza kwa baadhi yao kuwa kupitia JKT ni kigezo kikuu cha kuajiriwa Serikalini.

41. Mheshimiwa Spika, Mhe. Rais na Amiri Jeshi Mkuu alikwisha kutoa maagizo kwa vyombo vya Ulinzi na Usalama la kuajiri vijana waliohitimu mafunzo ya JKT. Katika kutekeleza agizo hilo mwaka 2014/15 jumla ya vijana 8,590 walijiriwa na vyombo vya Ulinzi na Usalama kwa mchanganuo ufuatao: Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania liliandikisha vijana 6,531 kati yao wasichana ni 1,233 na wavulana 5,298; Jeshi la Polisi vijana 906 wasichana wakiwa 199 na wavulana 707; Usalama wa Taifa vijana 22 kati yao wasichana ni wanne (4); Jeshi la Magereza vijana 1,107 kati yao wasichana wakiwa 245 na wavulana 862; Jeshi la Zimamoto vijana 100 kati yao wasichana wakiwa 22 na wavulana 78 na TAKUKURU imeajiri vijana 24. Aidha, Taasisi na Makampuni binafsi kama Benki Kuu ya Tanzania, Baraza la Mitihani, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania, TANAPA, African Gold Mine na Geita Gold Mines kwa ujumla yameajiri vijana 2,214, tangu utaratibu wa mafunzo ya JKT yaliporejeshwa tena mwaka 2011 hadi sasa.

42. Mheshimiwa Spika, changamoto kuu ya utekelezaji wa mafunzo haya ni ufinyu wa bajeti unaosababisha kushindwa kugharamia huduma za mafunzo, kikamilifu na kushindwa kukarabati majengo na miundombinu katika makambi ya Jeshi la Kujenga Taifa. Hata hivyo, baadhi ya changamoto zimeanza kutatuliwa kwa kutumia fedha kidogo zinazopatikana kutokana na vyanzo vya mapato ndani ya Jeshi la Kujenga Taifa.

(viii) Mapambano dhidi ya UKIMWI

43. **Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kusimamia kikamilifu mapambano dhidi ya maambukizi ya Virusi vya UKIMWI kwa Maafisa, Askari, Vijana na Watumishi wa Umma na familia zao. Mapambano dhidi ya maambukizi haya yanaendelea kwenye Wizara na Taasisi zake. Baadhi ya mikakati ya mapambano hayo ni pamoja na kutoa elimu kwa wahusika wote kupitia mpango wa Elimu Rika kwa vikundi ili kujadili kwa undani namna ya kujikinga na maambukizi ya UKIMWI; kupitia mpango wa Tohara kwa vijana wa kiume kwenye makambi ya JKT. Mkakati mwingine ni upimaji wa hiari wa VVU kwa maafisa, askari, vijana na watumishi wa Umma na utoaji wa dawa za kufubaisha VVU na lishe kwa wale waliokwishaathirika.

(ix) Utawala Bora

44. **Mheshimiwa Spika**, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa imeendelea kutekeleza dhana ya utawala bora katika maeneo ya kazi kwa kushirikisha watumishi wake katika maamuzi, mapambano dhidi ya rushwa na utekelezaji wa sheria na kanuni za manunuzi ya Umma. Wafanyakazi hushirikishwa katika maamuzi kupitia wawakilishi wao kwa kutoa mawazo na changamoto mbalimbali zinazowakabili wakati wa vikao vya Baraza la Wafanyakazi. Pia, watumishi hushirikishwa kwenye maamuzi kupitia vikao vya Idara na Menejimenti. Katika kuhakikisha kuwa rushwa inadhibitiwa sehemu za kazi, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa imeongeza uwazi katika mawasiliano pamoja na kuendelea kuwa na dawati linaloshughulikia malalamiko ya wafanyakazi. Vile vile, sheria ya manunuzi inazingatiwa wakati wa ununuzi wa vifaa vya ofisi na mahitaji mengine yanayohitaji zabuni. Mada ya Rushwa sasa ni agenda ya kudumu kwenye vikao vyote vya Baraza la wafanyakazi.

MATUMIZI YA SHUGHULI ZA MAENDELEO

45. **Mheshimiwa Spika**, utekelezaji wa shughuli za maendeleo hadi kufikia robo ya tatu ya Mwaka wa Fedha 2014/15 kwa ujumla haukuwa mzuri. Mafungu yote matatu yalipokea wastani wa asilimia **29.53** ya bajeti iliyoidhinishwa. Kwa mapokezi hayo, Wizara yetu imeweza kutekeleza miradi ifuatayo; kuendeleza mradi wa ujenzi wa nyumba 6,064 za makazi ya wanajeshi, kulipia madeni ya kimikataba, kukarabati majengo pamoja na kuboresha mazingira ya kufanyia kazi na makazi katika makambi na viteule vya JKT, ulipiaji fidia kwa baadhi ya maeneo yaliyotwaliwa kwa matumizi ya Jeshi, ujenzi wa Shule ya Mafunzo ya Awali ya Kijeshi Kihangaiko, kuendelea na ujenzi wa maghala ya kuhifadhi silaha na zana na kuzindua mradi wa Mawasiliano ya Kimtandao katika maeneo ya Zanzibar, Pwani na Dar es Salaam.

(i) Ujenzi wa Nyumba na Makazi ya Wanajeshi

46. **Mheshimiwa Spika**, katika hotuba yangu ya bajeti ya mwaka wa fedha 2014/15 nililitaarifu Bunge lako tukufu juu ya kuanza ujenzi wa nyumba 10,000 za kuishi wanajeshi vikosini. Katika ujenzi huo, tumeanza na awamu ya kwanza ya nyumba 6,064 ambapo ujenzi unaendelea vizuri na kwa kasi kubwa. Aidha, tarehe 20 Disemba, 2014 Rais na Amiri Jeshi Mkuu, Mhe. Dkt Jakaya Mrisho Kikwete aliweka jive la msingi kwenye ujenzi wa nyumba 552 zinazojengwa Monduli Mkoani Arusha kuwakilisha mradi wa ujenzi wa nyumba 6,064 katika mikoa tisa (9) hapa nchini. Mapema kabla yake, Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar alizindua ujenzi wa nyumba 320 huko Pemba ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya miaka 51 ya Mapinduzi ya Zanzibar tarehe 5 Januari, 2015.

47. **Mheshimiwa Spika**, sehemu ya kwanza ya ujenzi wa nyumba hizi 6,064 umefanyika katika mikoa ya Dar es Salaam na Pwani. Hadi kufikia Januari, 2015 jumla ya nyumba 2,256 zilizokuwa zikijengwa mkoani Dar es Salaam zilikamilika. Uzinduzi rasmi wa nyumba hizo ulifanywa na Rais na Amiri Jeshi Mkuu, Mhe. Dkt Jakaya Mrisho Kikwete tarehe 10 Januari, 2015 huko Gongo la Mboto ikiwa ni sehemu ya kukamilika kwa ujenzi wa awamu ya kwanza wa nyumba 6,064. Nyumba zote zilizokwisha kamilika zimeshakabidhiwa kwa JWTZ kwa ajili ya matumizi. Ujenzi katika vikosi mbalimbali vya JWTZ na JKT vilivyopo katika mikoa ifuatayo; Pwani (840), Arusha (792), Dar es Salaam (32), Dodoma (592), Kagera (144), Morogoro (616), Pemba (320), Kigoma (160) na Tanga (312) bado unaendelea.

(ii) Ununuzi wa Zana na Vifaa vya Kijeshi

48. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2014/15, Serikali iliendelea kuliimarisha Jeshi kwa kulipatia zana na vifaa vya kisasa. Jeshi lilipokea zana na vifaa mbalimbali kwa ajili ya ulinzi wa anga, nchi kavu na majini. Kutokana na zana na vifaa hivyo Jeshi letu hivi sasa lina uwezo mkubwa wa kutekeleza majukumu yake. Mpango huu wa ununuzi wa zana za kisasa na bora ni endelevu.

(iii) Shirika la Uzalishaji Mali la SUMAJKT

49. **Mheshimiwa Spika**, Shirika la Uzalishaji Mali la JKT (SUMAJKT) limeendelea kutekeleza shughuli zake katika misingi ya kibiashara. Shughuli kuu zinazoendeshwa na shirika hili kwa sasa ni katika nyanja za ujenzi uhandisi, viwanda, kilimo, biashara, utalii, na mradi wa uuzaji Matrekta na Kampuni ya Ulinzi kupitia SUMAJKT Guard Ltd.

50. **Mheshimiwa Spika**, SUMAJKT kupitia Idara ya ujenzi iitwayo “National Service Construction Department” inatekeleza miradi ya ujenzi katika sehemu mbalimbali nchini. Katika mwaka 2014/15 jumla ya miradi 39 ya ujenzi imetekelezwa. Miradi hiyo ni pamoja na ujenzi wa jengo la Kitega uchumi cha KKKT Kisukuru-Dar es Salaam, jengo katika Kanisa Katoliki Kristu Mfalme Tabata-Dar es Salaam, maabara katika baadhi ya shule za Sekondari zilizopo mkoani Kilimanjaro. Aidha, kupitia Idara ya viwanda na kilimo SUMAJKT lilifanikiwa kutengeneza samani mbalimbali katika kiwanda chake cha samani Chang'ombe-Dar es Salaam. Samani hizo ziliuzwa kwenye Idara na Taasisi za Serikali na watu binafsi.

51. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2014/15 SUMAJKT kupitia sekta ya kilimo iliendelea na uzalishaji wa mbegu bora za mazao pamoja na uzalishaji wa mifugo. Aidha, Shirika lilishirikiana na Tanzania Investment Bank (TIB) kuboresha kilimo cha umwagiliaji cha zao la mpunga katika kikosi cha Chita kilichopo Wilaya ya Kilombero mkoani Morogoro. Pia SUMAJKT lilishirikiana na “Tanzania Horticultural Association (TAHA)” ambacho ni Chama Cha Wazalishaji wa mboga na matunda kwa kutoa semina kwa watendaji katika vikosi kuhusu uzalishaji wa mboga, matunda, maua na viungo na namna ya kupata masoko ya ndani na nje ya nchi.

52. **Mheshimiwa Spika**, katika msimu wa 2014/15 SUMAJKT lilifanikiwa kuzalisha mahindi tani 1,160, mpunga tani 136, maharage tani 65.9, mafuta ya kula lita 2,162.9, mboga mboga na matunda tani 588.8. Aidha, katika mwaka huo huo jumla ya ekari 7,353 zililimwa kwa ajili ya uzalishaji wa mazao mbalimbali ya chakula ukilinganisha na ekari 4,390 zilizolimwa mwaka 2013/14. Jumla ya ekari 2,337 zililimwa kwa ajili ya uzalishaji wa mbegu bora ukilinganisha na ekari 1,913 zilizolimwa mwaka 2013/14 ikiwa ni ongezeko la ekari 424.

53. **Mheshimiwa Spika**, SUMAJKT imeendelea kuyauzia mbegu bora makampuni ya mbegu ya Agricultural Seeds Agency (ASA), TANSEED, Tropical Seed Company Ltd, Southern Highland Seed Growers Ltd, Kibo Seed na SUBA Company iliyoingia nayo mikataba. Hata hivyo, katika utekelezaji wa mikataba hii kumejitokeza changamoto kwa makampuni hayo kutolipa madeni kwa wakati hali inayosababisha shirika kushindwa kufikia malengo yake. Hadi sasa jumla ya **shilingi 908,716,976.00** hazijalipwa na makampuni hayo. SUMAJKT limeshachukua hatua za kisheria ya kuyafikisha Mahakamani makampuni inayoyadai. Aidha, SUMAJKT limesajili wakala wake wa mbegu ambalo linaitwa SUMAJKT SEED COMPANY LTD lenye usajili Namba 09818 ya tarehe 3 Februari, 2015 ili kuweza kusambaza kwa wingi na unafuu mbegu bora kwa wakulima.

54. **Mheshimiwa Spika**, katika kujipanua zaidi kibiashara SUMAJKT kupitia kampuni yake ya ulinzi ya SUMAJKT Guard Ltd. imeendelea kutoa huduma za ulinzi katika Idara za Serikali na sekta binafsi ikiwemo; vituo vya kuzalisha

umeme vya Kihansi na Mtera mkoani Morogoro, TANESCO, Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM), Wizara ya Fedha, CRDB, UBA, Migodi ya STAMIGOLD, Chuo cha madini Nzega na Chunya, TEMESA -Kivukoni na Busisi/Kigongo Mwanza na TPDC. Hadi sasa kampuni imeajiri walinzi 1,850, ikiwa ni ongezeko la walinzi 182 ukilinganisha na idadi ya walioajiriwa hadi kufikia Juni, 2014. Aidha, SUMAJKT imetenga maeneo maalum kwa ajili ya uwekezaji katika nyanja ya utalii ambapo shughuli zinazotarajiwa kufanyika ni pamoja na ujenzi wa mahoteli, vivutio sehemu za mapumziko, na kumbi za mikutano. Maeneo hayo yapo Makuyuni (Arusha), Kisiju (Pwani), Mbweni na Ndege Beach (Dar es Salaam.)

55. Mheshimiwa Spika, SUMAJKT limeendelea kuendesha na kusimamia mradi wa matrekta kwa niaba ya Serikali kuanzia mradi ulipozinduliwa tarehe 07 Oktoba, 2010 ukiwa na lengo la kuongeza uzalishaji wa mazao ya kilimo kwa kuongeza matumizi ya mashine za kisasa ili kuinua kipato cha wananchi, kuhamasisha matumizi bora ya matrekta, Power Tillers' na zana mbalimbali za kilimo.

56. Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwezi Machi, 2015 SUMAJKT kupitia mradi huu lilifanikiwa kuuza matrekta 1,841 na zana 2,929 zenye thamani ya **shilingi 65,550,428,807.00** kwa njia ya mkopo. Hata hivyo, ukusanyaji wa fedha za mkopo huo ambao ni utekelezaji wa awamu ya kwanza ya mradi ulifikia **shilingi 31,059,800,870.00** sawa na asilimia 47.4 ya thamani ya mali iliyouzwa. Awamu ya pili ya mradi huu ilianza Oktoba, 2013 ambapo ilihusisha ununuzi wa matrekta 268 kutoka India kwa thamani ya **shilingi 7,046,245,600.00**. Awamu hii ya mradi inatarajia kukusanya jumla ya **shilingi 8,551,692,701.48** baada ya mauzo yote. Hadi sasa jumla ya matrekta 232 yameshauzwa kwa wateja kwa thamani ya **shilingi 7,609,603,059.28** sawa na asilimia 89. Napenda kuwakumbusha wadaiwa wote wa ndani na nje ya jengo lako tukufu kukamilisha malipo ya matrekta waliyokopa.

(iv) Shughuli za Shirika la Mzinga

57. **Mheshimiwa Spika**, kulingana na mpango mkakati wa Shirika wa miaka 15 kuanzia mwaka 2011 hadi mwaka 2026, Shirika la Mzinga lina malengo yafuatayo:- kuendeleza uzalishaji wa mazao ya msingi kwa ajili ya ulinzi na usalama wa nchi; kuanzisha kiwanda cha kuzalisha milipuko; kuanzisha kituo cha utafiti wa silaha za kijeshi na kusimika mfumo wa usalama wa kiwanda (electronic surveillance system). Katika mwaka 2014/15 Shirika la Mzinga lilikusudia kukamilisha ujenzi wa mkondo mpya wa risasi na ukarabati wa baadhi ya karakana na mitambo, kugharamia ujenzi wa maghala matatu mapya ya kuhifadhi silaha na kukamilisha uboreshaji wa mitambo ya uzalishaji awamu ya kwanza.

58. **Mheshimiwa Spika**, kutokana na ufinyu wa bajeti Shirika lilipata changamoto katika kutekeleza shughuli zake za msingi. Hata hivyo, kwa kutumia mapato madogo ya ndani Shirika limeendelea na uzalishaji katika mkondo wa risasi katika kaliba mbalimbali na ukarabati wa barabara za ndani na maeneo yanayozunguka Shirika. Aidha, shirika kupitia kampuni yake tanzu ya Mzinga Holding lilifanikiwa kutekeleza miradi mbali mbali ya kibiashara ikiwa pamoja na ukarabati wa jengo la Mkuu wa Mkoa wa Mtwara, ujenzi wa vyumba vya maabara katika Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo, ujenzi wa 'box caravat' Mabwepande katika Wilaya ya Kinondoni, ujenzi wa kiwanda cha maji ya kunywa na hosteli ya masista Jimbo Katoliki la Bukoba na ujenzi wa kituo cha afya Jimbo Katoliki la Kayanga.

(v) Shughuli za Shirika la Nyumbu

59. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2014/15 Shirika la Nyumbu lilipanga kutekeleza shughuli zake za kuendeleza utafiti katika teknolojia ya magari na mitambo ya kijeshi, kuimarisha na kuongeza uwezo wa kuhawilisha teknolojia mbalimbali za utafiti na kukarabati miundombinu ya Shirika. Kutokana na ukosefu wa fedha za maendeleo, Shirika halikuweza kutekeleza shughuli zake za msingi. Hata hivyo, kwa kutumia mapato madogo ya ndani, Shirika lilifanikiwa kufanya ukarabati mdogo wa nyumba za makazi na mitambo ya karakana ya Shirika; kununua vifaa vya TEHAMA na kukarabati mfumo wa umeme kiwandani.

(vi) Mtandao wa Mawasiliano Jeshini

60. **Mheshimiwa Spika**, Wizara inatekeleza mradi wa Mawasiliano Salama ya Kujitegemea Jeshini (Independent Secured Mobile Communication Network). Hadi kufikia Machi, 2015 jumla ya minara 131 ilisimikwa Tanzania Bara na Visiwani na vituo (Control Centre) viwili kwa ajili ya kuendesha na kusimamia mawasiliano hayo vilishajengwa Dar es Salaam na Dodoma. Mtandao huu

umefanyiwa majaribio wakati wa sherehe za maadhimisho ya Mapinduzi ya Zanzibar tarehe 12 Januari, 2015 ambapo mawasiliano ya kimtandao yaliweza kupatikana katika maeneo ya Zanzibar, Pwani na Dar es Salaam. Kazi ya kuunganisha maeneo mengine ya nchi kwenye mtandao huo inaendelea. Kwenye minara iliyokwishasimikwa hatua za kufikisha umeme wa TANESCO zinachukuliwa ili kuepuka gharama za kutumia jenereta kuendesha minara hiyo.

(vii) Kudhibiti Uvamizi wa Maeneo ya Jeshi, Upimaji na Ulipaji Fidia

61. **Mheshimiwa Spika**, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, itaendelea na utaratibu wake wa kulipatia JWTZ na JKT maeneo ya ardhi kwa ajili ya matumizi yao. Matumizi hayo ni kwa shughuli muhimu kama maeneo ya mazoezi ya Kijeshi na medani, shughuli za ujenzi na shughuli za miradi zinazofanywa na JKT na mashirika ya Mzinga na Nyumbu. Pamoja na mahitaji hayo kuwa makubwa upatikanaji wake hutegemea fedha hususan za fidia. Kama nilivyoahidi, mwaka 2014/15 tumeweza kulipa fidia kwa maeneo ya Mataya – Bagamoyo, Mwakidila – Tanga, Mwantini – Shinyanga, Mahongole – Makambako na Kasanga – Rukwa na upimaji wa maeneo ya Ilemela – Mwanza, Mahungu na Ntyuka-Dodoma. Katika kipindi hiki Wizara haikuweza kulipa fidia kwa baadhi ya maeneo tuliyokusudia katika mwaka 2014/15 kutokana na uhaba wa fedha. Maeneo hayo ni pamoja na Kimbiji – Temeke na Tanganyika Packers – Arusha.

62. **Mheshimiwa Spika**, zoezi la kupima na kulipa fidia maeneo ya Jeshi ni endelevu, ambapo mwaka 2015/16 upimaji na kulipa fidia unategemea kufanyika kwa maeneo ya kilima cha Ilemela, Lukobe na Kigongo Ferry – Mwanza, Kimbiji – Temeke, Ras Nondwa – Kigoma, Ronsoti – Tarime, Tanganyika Packers – Arusha na Kaboya – Muleba. Kimsingi maeneo ya Jeshi yaliwekwa mbali na mijini na vijijini kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo za kistratejia, usalama na uhalisia wa shughuli za kijeshi (military manouvres). Pamoja na maeneo ya Jeshi kuwa mbali na shughuli za kiraia, kumekuwa na mienendo ya baadhi ya wananchi kuvamia maeneo hayo kwa visingizio mbalimbali. Wito wangu kwa wananchi waache tabia ya kuvamia maeneo ya Jeshi kwani pamoja na ukweli kuwa ni hatari lakini pia wanakwaza shughuli za Jeshi.

CHANGAMOTO ZA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KATIKA MWAKA 2014/15

63. **Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kukabiliwa na changamoto mbalimbali lakini kubwa ikiwa ni kupata kiwango kidogo cha fedha ukilinganisha na bajeti halisi. Katika mwaka wa fedha 2014/15 Wizara iliomba **shilingi 708,731,094,124.00** kwa ajili ya Matumizi ya Maendeleo kwa kuzingatia vipaumbele vyake, lakini kiasi kilichoidhinishiwa ni **shilingi 248,842,500,000.00** tu sawa na asilimia 35.1 ya mahitaji hayo. Hali hii kwa kiasi kikubwa imekuwa

ikiathiri utekelezaji wa shughuli za Mpango wa Maendeleo ya Jeshi, mfano kushindwa kulipa mikopo mbalimbali ya kimikataba.

64. Mheshimiwa Spika, changamoto nyingine inayoikabili Wizara ni mtiririko wenyewe wa fedha kutoka Hazina ambao hauzingatii Mpango Kazi wa Wizara. Aidha, fedha hutolewa zikiwa pungufu na bila kuzingatia ratiba ya utekelezaji. Hali hii inasababisha shughuli za Wizara hususan za maendeleo kutotekelezwa kama ilivyopangwa na hivyo kushindwa kukamilisha ujenzi wa majengo na miundombinu katika makambi, kukwama kwa shughuli za viwanda, karakana na shughuli za utafiti. Aidha, Wizara inashindwa kutoa huduma na mahitaji muhimu kwa wanajeshi na watumishi wa umma.

MPANGO WA MWAKA 2015/16

65. Mheshimiwa Spika, mpango na malengo ya Wizara ya Ulinzi na JKT katika mwaka 2015/16 ni kuendelea kuimarisha uwezo wa kulinda mipaka ya nchi yetu pamoja na kuimarisha mazingira ya amani na utulivu na nchi nyingine duniani, hususan na nchi jirani. Ili kufikia mpango na malengo hayo, Wizara imekusudia kutekeleza majukumu yafuatayo:-

- a. Kuendelea kuliimarisha na kuliongezea uwezo Jeshi katika utendaji kivita kwa kulipatia vifaa na zana bora za kisasa pamoja na kutoa mafunzo stahiki kwa wanajeshi dhidi ya adui wa ndani na nje.
- b. Kulijengea Jeshi mazingira mazuri ya kufanyia kazi na makazi ikiwa ni pamoja na kujenga nyumba za kuishi wanajeshi katika makambi na kuimarisha upatikanaji wa huduma na mahitaji ya msingi kama vile chakula, tiba, sare, usafiri, maslahi na stahili kwa wanajeshi na watumishi raia.
- c. Kuimarisha uwezo wa Jeshi katika utafiti na kuendeleza teknolojia kwa madhumuni ya kuzalisha bidhaa na huduma kwa ajili ya matumizi ya kijeshi na kiraia hapa nchini na nje ya nchi.
- d. Kuendelea kuwapatia vijana wa Kitanzania mafunzo ya uzalendo, umoja wa Kitaifa, ukakamavu na kuwaandaa katika uzalishaji na stadi mbalimbali katika makambi ya Jeshi la Kujenga Taifa.
- e. Kuimarisha ushirikiano wa kijeshi na kiulinzi na nchi nyingine duniani kupitia Jumuiya za Kimataifa, Kikanda na ushirikiano na nchi moja moja. Ushirikiano wa Kikanda unahusisha ushirikiano wa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) na Umoja wa nchi za Afrika (AU).

SHUKRANI

66. **Mheshimiwa Spika**, kabla sijahitimisha Hotuba yangu napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru wafuatao kwa michango yao katika maandalizi ya taarifa hii ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara yangu; Katibu Mkuu Bw. Job D. Masima, Naibu Katibu Mkuu Bi. Mwintango Rose Shelukindo, Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi Jenerali Davis A Mwamunyange, Mnadhimu Mkuu Luteni Jenerali Samuel A Ndomba, Mkuu wa Jeshi la Kujenga Taifa Meja Jenerali Raphael M Muhuga, Wakuu wa Kamandi za Jeshi la Nchi Kavu Meja Jenerali Salum M Kijuu, Jeshi la Anga Meja Jenerali Joseph F Kapwani na Jeshi la Wanamaji Meja Jenerali Rogastian S Laswai, Meneja Mkuu wa Shirika la Mzinga Meja Jenerali Dkt. Charles N Muzanila na Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Nyumbu Brigedia Jenerali Anselm A Bahati.

67. **Mheshimiwa Spika**, pia napenda kuwashukuru Wakuu wa Idara na Vitengo (Makao Makuu ya Wizara), Wakuu wa Matawi (NGOME), Wakuu wa Idara (Makao Makuu ya Jeshi la Kujenga Taifa), Maafisa, Askari na Watumishi wa Umma wa Wizara kwa kunipa ushirikiano katika kufanikisha majukumu ya Wizara. Aidha, naishukuru Kamati ya Wizara iliyoandaa hotuba hii na Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali kwa kuchapisha hotuba hii kwa wakati.

68. **Mheshimiwa Spika**, nitakuwa mnyimi wa fadhila endapo sitawashukuru Wahisani mbalimbali waliotoa michango yao kwa namna moja au nyingine katika kufanikisha maendeleo ya Jeshi. Wahisani hao ni pamoja na Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China, ambao wameshiriki katika upanuzi wa uwanja wa ndege Ngerengere na ujenzi wa nyumba za makazi ya wanajeshi 6,064 kupitia mkopo nafuu kutoka Benki ya EXIM China. Vilevile naishukuru Serikali ya Ujerumani ambayo imeshiriki katika ujenzi wa vituo vya afya vya Kanda, ukarabati na uboreshaji wa karakana kuu ya Jeshi Lugalo na uboreshaji wa Hospitali Kuu ya Jeshi Lugalo. Nazishukuru pia nchi zifuatazo kwa ushirikiano tuliokuwa nao katika nyanja za ulinzi pamoja na mafunzo. Nchi hizi ni Afrika Kusini, Bangladesh, Burundi, Canada, China, DRC, Ghana, Falme za Kiarabu, Indonnesia, Kenya, Marekani, Msumbiji, Misri, Namibia, Nigeria, Rwanda, Uganda, Ujerumani, Uingereza, Urusi, Zambia na Zimbabwe.

69. **Mheshimiwa Spika**, kwa umuhimu wa pekee na kwa kupitia Bunge lako Tukufu naomba kuwasilisha salamu za pongezi maalum za Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu, Mhe. Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete kwa wanajeshi wote kwa kufanikisha maadhimisho ya miaka 50 ya Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania yaliyofanyika Arusha mwezi Septemba, 2014. Aidha, kwa kumalizia na kwa niaba ya wanajeshi wote namshukuru sana Rais na Amiri Jeshi Mkuu, Mhe. Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete kwa uongozi wake uliotukuka kwa kipindi cha miaka kumi. Mhe. Rais atakumbukwa na kuenziwa vizazi na vizazi hususan kwetu sisi wanajeshi. Ahadi yetu kwake ni kuwa

tutaendelea kusimama imara, kupokea na kutii amri na maelekezo ya Amiri Jeshi Mkuu.

MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA BAJETI YA MWAKA 2015/16

(i) Makadirio ya Mapato

70. **Mheshimiwa Spika**, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na Taasisi zake haina vyanzo vya uhakika vya mapato vinavyoweza kuchangia kwa kiasi kikubwa katika ukusanyaji wa maduhuli. Hali hii inasababishwa na majukumu ya msingi ya Wizara hii. Chanzo kikuu cha mapato ni makusanyo ya mauzo yanayotokana na nyaraka za zabuni, suala ambalo kwa sasa linashughulikiwa pia na GPSA.

71. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2015/16 Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa inatarajia kukusanya jumla ya **shilingi 72,606,000/=** katika mchanganuo ufuatao:-

Fungu 38 – NGOME	Sh.11,601,000.00
Fungu 39 – JKT	Sh.50,003,000.00
Fungu 57 – Wizara.....	Sh.11,002,000.00

(ii) Matumizi ya Kawaida na Maendeleo

72. **Mheshimiwa Spika**, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa inaomba kuidhinishiwa jumla ya **shilingi 1,716,301,362,000.00** kwa ajili ya Matumizi ya kawaida na matumizi ya maendeleo ili iweze kutekeleza majukumu yake katika mwaka 2015/16. Kati ya fedha hizo **shilingi 1,477,163,404,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **shilingi 239,137,958,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi ya Maendeleo. Mchanganuo kwa kila Fungu ni ufuatao:-

Fungu 38 – NGOME

Matumizi ya Kawaida	Sh. 1,163,083,841,000.00
Matumizi ya Maendeleo	Sh.12,000,000,000.00
Jumla		Sh.1, 175,083,841,000.00

Fungu 39 – JKT

Matumizi ya Kawaida	Sh.292,296,992,000.00
Matumizi ya Maendeleo	Sh. 7,000,000,000.00
Jumla		Sh. 299,296,992,000.00

Fungu 57 – Wizara

Matumizi ya Kawaida	Sh.21,782,571,000.00
Matumizi ya Maendeleo	Sh. 220,137,958,000.00
Jumla		Sh. 241,920,529,000.00

MWISHO

73. **Mheshimiwa Spika**, hotuba hii inapatikana pia katika tovuti ya Wizara (www.modans.go.tz). Naomba kutoa Hoja.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Hoja imetolewa na imeungwa mkono, tunakushukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Dokta Hussein Mwinyi.

Sasa nirekebishe kidogo, nilipokuwa nawatambulisha wageni walioko kwenye jukwaa la Spika, wageni wa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Dokta Hussein Mwinyi, vijana wangu walikuwa ameniandikia kwa makosa, cheo cha Mkuu wa Kamandi ya Wanamaji, ambaye ni Rogastian Shaban Laswai, wakawa wameniandikia kwamba ni Brigedia Jenerali. Naomba kurekebisha ili *Hansard* isome vizuri kwamba jina lake halisi ni Meja Jenerali Rogastian Laswai na siyo Brigedia Jenerali, tunaomba radhi kwa kosa hilo. *(Makofi)*

Sasa naomba nimuite Mwenyekiti wa Kamati ambaye atasoma maoni ya Kamati kwa Wizara zote mbili, Mheshimiwa John Chiligati, karibu sana na una nusu saa.

TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ULINZI NA USALAMA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI NA WIZARA YA JESHI LA ULINZI NA KUJENGA TAIFA KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016 KAMA ILIVYOSOMWA BUNGENI

MHE. CAPT. JOHN Z. CHILIGATI - (K.n.y MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ULINZI NA USALAMA): Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama na kwa mujibu wa Kanuni ya 99(9) na 117(11) cha Kanuni za Kudumu za Bunge, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama kuhusu Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, pamoja na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, juu ya utekelezaji wa bajeti ya Wizara hizo kwa mwaka wa fedha 2014/2015 na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hizo kwa mwaka wa fedha 2015/2016.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilikutana na Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Chikawe na Naibu Waziri wake Mheshimiwa Pereira Silima-, pamoja na Dokta Hussein Mwinyi, Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa nyakati tofauti mwezi wa Mei, 2015 na kupokea Taarifa ya Utekelezaji wa Mipango ya Bajeti ya Wizara hizo kwa mwaka wa fedha 2014/2015 na

Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2015/2016 kwa mafungu matano ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na mafungu matatu ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, kama ifuatavyo:-

Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ni: Fungu 14 - Kikosi cha Zimamoto na Uokoaji; Fungu 28 - Jeshi la Polisi; Fungu 29 - Jeshi la Magereza; Fungu 51 - Wizara ya Mambo Ndani ya Nchi; Fungu 93 - Idara ya Uhamiaji.

Kwa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa: Fungu 57 –Wizara ya Ulinzi na JKT; Fungu 39-Jeshi la Kujenga Taifa na Fungu 38-NGOME.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kwa mujibu wa Kanuni ya 98 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ilikagua miradi ya maendeleo iliyoidhinishiwa fedha na Bunge lako kwa mwaka wa fedha 2014/2015. Katika ziara za ukaguzi wa miradi, Kamati ilibaini kwamba Wizara zote mbili, kiasi kikubwa fedha za miradi ya maendeleo hazikutolewa kama zilivyoidhinishwa na Bunge. Kwa mafano, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Bunge liliidhinisha kiasi cha shilingi bilioni 708.7, lakini hadi kufikia mwezi Machi, 2015, ni shilingi bilioni 248.8 tu ndizo zilikuwa zimetolewa ambayo ni sawa na asilimia 35.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa maagizo ya Kamati kwa mwaka wa fedha 2014/2015. Wakati wa kuchambua bajeti ya Wizara hizi mbili kwa mwaka 2014/2015, Kamati ilitoa maoni na ushauri katika maeneo mbalimbali ili kuboresha utendaji kazi wa Wizara hizi. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba katika baadhi ya maeneo Kamati haikuridhiak na utekelezaji wake, kwa hiyo maeneo hayo yanahitaji kufanyiwa kazi zaidi ili yaweze kuboreshwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni na ushauri wa Kamati. Baada ya uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji wa bajeti ya Wizara hizi kwa mwaka 2014/2015 pamoja na makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hizo kwa mwaka 2015/2016, sasa naomba kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati kwa mafungu yote kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naanzia na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ambayo iko katika ukurasa wa nne wa kitabu chetu cha taarifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kikosi cha Zimamoto na Uokoaji hakijatengewa fedha za miradi ya maendeleo kwa muda wa miaka mitano mfululizo. Kwa mwaka huu wa fedha, Kikosi cha Zimamoto kimetengewa shilingi bilioni 1.5 ili kununua gari la zimamoto na ujenzi wa vituo vidogo vitatu vya zimamoto katika Jiji la Dar es Salaam. Maoni ya Kamati ni kwamba, fedha hizi hazitoshelezi mahitaji halisi ya kikosi hiki. Ukosefu wa fedha za maendeleo zimesababisha mradi mkubwa wa ujenzi wa makao makuu ya kikosi hiki kukwama.

Mheshimiwa Naibu, Spika, ununuzi wa vitendea kazi. Kikosi cha Zimamoto kina upungufu mkubwa wa vitendea kazi kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake. Kwa mfano, kukosekana kwa gari la kuzima moto katika majengo marefu yanayozidi ghorofa kumi na saba (17). Vilevile, kuna ukosefu wa vya kisasa vya uokozi. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kuwa kikosi hiki kinapatiwa fedha za kutosha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya kuzimia moto na uokoaji ili kikosi kiweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Polisi, Fungu - 28. Posho za Askari Polisi. Bajeti iliyotengwa kwa mwaka wa fedha 2015/2016 ni shilingi bilioni 99.7 ambazo zitawezesha Askari kuendelea kulipwa posho ya chakula (*ration allowance*) ya Sh.6,000 tu kwa siku. Kiwango hiki cha posho hakitoshelezi mahitaji ya chakula bora kwa Askari wawapo kazini. Pamoja na kutambua ufinyu wa bajeti unaoikabili Serikali, Kamati inapendekeza kwamba kiwango hicho kiongezwe hadi kufikia Sh.10,000 kwa siku. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kwamba viwango hivi vya posho za Askari viwe vinahuishwa kila mwaka kulingana na hali ya maisha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, adhabu kali kwa wanaosababisha ajali. Kwa kuwa Watanzania wengi wanapoteza maisha kutokana na ajali zinazosababishwa na uzembe wa madereva, ubovu wa vyombo vya usafiri na miundombinu isiyokidhi ongezeko la vyombo vya moto, Kamati inashauri kuwa sheria zifanyiwe marekebisho ili wale wote watakaothibitika kwa makosa ya uzembe wapewe adhabu kali. Aidha, Kamati inashauri kwamba miundombinu ya barabara nchini iendeleo kuboreshwa ili kuendana na ongezeko kubwa la magari na watumiaji wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, ununuzi wa vitendea kazi. Kwa kuwa Jeshi la Polisi linafanya kazi kubwa ya ulinzi wa maisha ya watu na mali zao, linahitaji magari ya kutosha, pikipiki, boti za majini na helkopta kwa ajili ya kufanya doria. Katika mwaka huu wa fedha, Wizara imepanga kununua magari 777 na pikipiki 3,800 kwa matumizi ya Jeshi kwa kutosheleza hadi ngazi ya Kata. Hata hivyo, Kamati inaona kwamba Polisi wanahitaji kuimarisha ulinzi wa majini na angani hivyo Serikali ifanye mpango wa kununua boti na helkopta za kukidhi mahitaji hayo.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Magereza, Fungu - 29. Madeni ya wazabuni na watumishi. Kamati inasikitishwa kwa uwepo wa madeni ambayo mpaka sasa hayajalipwa. Kwa kipindi cha Julai, 2012 hadi Juni, 2014 jumla ya madeni yote yalikuwa ni shilingi bilioni 40.8. Kati ya hayo, madeni ya Askari ni shilingi bilioni 8.8, madeni ya wazabuni ni shilingi bilioni 21.8 na shilingi bilioni 10 ni madeni yahasuyo huduma za umeme, simu pamoja na maji. Kamati inazidi kuishauri na kuisisitiza Serikali kutenga fedha ili kulipa madeni haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ununuzi wa magari. Katika mwaka wa fedha 2014/2015, Serikali iliweza kununua magari saba kwa ajili ya shughuli za utawala. Kwa kuwa kuna umuhimu wa kuwa na magari kwa ajili ya kuwasafirisha wafungwa na mahabusu kwenda mahakamani kila siku, hospitalini na shughuli nyingine za kiutawala, Kamati inaishauri Serikali kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya kununua magari, walau gari moja kwa kila gereza la Wilaya. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti ndogo ya chakula kwa wafungwa. Kamati inashauri kwamba fedha iliyotengwa mwaka huu ya Sh.1,500 kwa mtu kwa siku bado ni ndogo na hata hivyo haitolewi yote. Hivyo Serikali inashauriwa iongeze bajeti ya chakula cha wafungwa magerezani kutoka wastani wa Sh.1,500 ya sasa kwa siku hadi kufikia Sh.3,000 kwa siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo sugu la msongamano magerezani. Kumekuwa na msongamano wa wafungwa na mahabusu magerezani ambapo kwa sasa kuna nafasi 29,552 tu wakati idadi ya wafungwa na mahabusu waliopo gerezani hadi mwezi Machi kwa mujibu wa taarifa ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani aliyotuambia sasa hivi ni 33,027. Idadi hii inazidi uwezo wa magereza kuwahifadhi wafungwa na mahabusu. Kamati inazidi kuishauri Serikali kuchukua hatua zifuatazo:-

(i) Sheria ya *Community Service* itumike katika Mikoa yote 25 ya Tanzania Bara badala ya Mikoa 19 ya sasa ili wahalifu wenye makosa madogo madogo watumikie adhabu zao nje ya magereza.

(ii) Maboresho ya Sheria ya *Parole* yaletwe Bungeni mapema iwezekanavyo ili kupanua wigo wa wafungwa watakaonufaika na sheria hii.

(iii) Wahamiaji haramu wanaokamatwa kwa makosa ya kuingia nchini isivyo halali waendeleo kurudishwa makwao badala ya kuwafunga katika magereza yetu na hivyo kuongeza msongamano magerezani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) walitengewa kiasi cha shilingi bilioni 201. Hadi mwezi Machi mwaka huu ni shilingi bilioni 41.8 sawa na asilimia 20 ndizo zilitolewa. Kamati inaishauri Serikali kwamba fedha zilizobaki zitolewe mapema kwani upungufu huu wa fedha unachelewesha zoezi la utoaji wa vitambulisho kwa Watanzania na hivyo itafanya zoezi hili kutokamilika kwa muda uliopangwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Idara ya Uhamiaji. Hadi kufikia mwezi Machi, 2015 wahamiaji haramu 2,015 wamerudishwa katika nchi zao. Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua hii na inashauri kwamba zoezi hili liwe endelevu na lisimamiwe kwa ukamilifu, hasa katika Mikoa ya mipakani.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wa jumla kwa Wizara ya Mambo ya Ndani. Serikali iboreshe mfumo wa makusanyo ya fedha za *retention*. Kuhusu suala la fedha za *retention*, Kamati inashauri ufuatao:-

(i) Viwango vya *retention* virudishwe vile vya zamani yaani Zimamoto iwe 75% badala ya 49% ya sasa na Uhamiaji irudiwe ile 61% badala ya 45% ya sasa.

(ii) Utaratibu wa fedha za *retention* kuwa ndani ya bajeti ya Idara husika unaondoa motisha kwa idara hizo ya kukusanya maduhuli mengi zaidi. Hivyo, Kamati inashauri kwamba fedha za *retention* ziwe ni nyongeza katika bajeti ya Idara husika hasa katika vyombo vya ulinzi na usalama ambavyo vina mahitaji mahsusi ya zana za kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Jeshi la Polisi hawamo kwenye mfumo wa *retention*, Kamati inashauri kwamba ili kuongeza uwezo wa kununua zana za Jeshi la Polisi na pia kutatua tatizo la ukosefu wa nyumba za Askari, ni muhimu wakaachiwa fedha zote wanazokusanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, maelezo yako katika ukurasa wa kumi wa kitabu cha taarifa yetu. Ili kusimamia vyema jukumu la ulinzi na usalama hapa nchini, Kamati inatoa maoni na ushauri ufuatao:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Fungu 55, Wizara ya Ulinzi na JKT. Kamati imebaini kuwepo kwa madeni makubwa katika mwaka wa fedha 2014/2015 yanayofikia kiasi cha bilioni 483.9. Madeni hayo yanatokana na wazabuni, ankara za maji na umeme. Vilevile madeni ya mikataba pamoja na stahili za askari na watumishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndani ya deni hilo, kuna deni la mkataba la siku nyingi la kampuni ya *Poly Technologies* la shilingi bilioni 187.3. Kamati inaishauri Serikali kulipa madeni hayo kwani kutokufanya hivyo kunasababisha madeni yenye riba kuongezeka na hivyo kuongeza ukubwa na mzigo wa madeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imebaini kwamba vyombo vya ulinzi na usalama vinashindwa kutekeleza miradi ya maendeleo kwa sababu fedha za miradi hiyo hazitolewi zote na kwa wakati. Hali hii inapunguza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya vyombo hivi. Kamati inazidi kuishauri Serikali

ihakikishe fedha zote zinazoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya vyombo vya ulinzi zinapelekwa ili kudumisha ulinzi na usalama wa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilipata nafasi ya kutembelea nchi ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na kukutana na vijana wa Jeshi letu wanaosaidiana na Jeshi la Umoja wa Mataifa (MONUSCO), chini ya Brigedi Maalum. Vijana hao tumekuta wanafanya kazi nzuri dhidi ya vikundi vya waasi. Pamoja na Askari wetu waliopo DRC, pia nchi yetu inao Askari wanaoshiriki kulinda amani huko Darfur -Sudan na Lebanon, nao vilevile wanafanya kazi vizuri. Tunaliomba Bunge kuungana na Kamati kulipongeza Jeshi letu kwa kazi nzuri inayofanywa na vijana wetu nchi za nje, kazi ambayo imeliletea Taifa letu heshima kubwa kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Kamati kwa niaba ya Bunge inatoa masikitiko kwa tukio la hivi karibuni kule DRC ambapo Askari wetu wawili wamepoteza maisha wakiwa katika jukumu la kulinda amani. Tunatoa salamu za pole na rambirambi kwa Jeshi la Wananchi na vilevile kwa familia zilizofiwa na tunaomba Mwenyezi Mungu aziweke roho za vijana hao mahali pema peponi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Fungu 38 - NGOME. Katika mwaka wa Fedha 2014/2015, NGOME iliidhinishwa shilingi bilioni 22 kwa shughuli za maendeleo. Hadi kufikia mwezi Machi mwaka huu walikuwa wamepelekewa shilingi bilioni 1.5 ambayo ni sawa na asilimia 12.5. Kamati inaishauri Serikali kuchukua hatua za haraka kutoa fedha zilizobaki ili shughuli za ulinzi na usalama hapa nchini ziendelee kutekelezwa kama ilivyopangwa na kama ilivyokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Fungu 39 - Jeshi la Kujenga Taifa. Kamati ilielezwa kwamba jumla ya vijana wanaohitajika kujiunga na JKT kwa mujibu wa sheria kwa mwaka huu wa 2015, ni vijana 34,100. Fedha iliyotengwa katika bajeti ya 2015/2016 ni shilingi bilioni 25.7 ambayo inatosheleza kuhudumia vijana 20,000 tu wa mujibu wa sheria na vijana 5,000 wa kujitolea. Kamati inaishauri Serikali iongeze bajeti ili vijana wote 34,100 waliomaliza kidato cha sita wapate fursa hii ya kujiunga na JKT ili kuwaongezea ukakamavu, uzalendo na nidhamu badala ya kuwaacha takriban vijana 14,000 wasijiunge na JKT.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Kujenga Taifa linamiliki Shirika la SUMAJKT lililoanzishwa ili kuzalisha mali kibiashara kwa Sheria ya Mashirika ya Umma ya mwaka 1974. Pamoja na uzalishaji, Shirika hili pia linayo Kampuni ya SUMAJKT ambayo ni mahsusi kwa shughuli za ulinzi. Kamati inaishauri Serikali kwamba kwa kuwa *Suma Guard* inao vijana waliohitimu mafunzo ya kijeshi ni vyema ikatumika kulinda maeneo mbalimbali ya taasisi za umma na miundombinu muhimu badala ya kutumia walinzi kutoka makampuni binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inazidi kusisitiza kwamba Sheria Na.16 ya mwaka 1964 iliyounda Jeshi la Kujenga Taifa iletwe Bungeni ili ifanyiwe marekebisho na iendane na malengo na dhamira ya wakati huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho. Nakushukuru wewe binafsi kwa kunipa fursa hii. Pia namshukuru Mheshimiwa Dokta Hussein Mwinyi, Waziri wa Ulinzi na JKT pamoja na Mheshimiwa Mathias Chikawe, Waziri wa Mambo ya Ndani na taasisi zao zote, kwa ushirikiano wao mkubwa wakati wa kujadili makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama kwa kazi nzuri ya kujadili na kuchambua makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hizi kwa mwaka 2015/2016. Kwa aina ya pekee, nawashukuru kwa ushirikiano mkubwa walionipa kwa kipindi chote cha miaka miwili na nusu ya uhai wa Kamati hii. Orodha ya Wajumbe wa Kamati wanaoshukuriwa yapo ukurasa wa kumi na nne wa kitabu cha taarifa.

Aidha, napenda kuwashukuru kwa dhati Katibu wa Bunge Dokta Thomas Kashilillah, Makatibu wa Kamati Ndugu Onesmo Laulau na Ndugu Peter Magati waliotumikia na kusaidia Kamati hii katika kutekeleza majukumu ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo haya, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na ya Wizara ya Mambo ya Ndani kama yalivyowasilishwa na watoa hoja wote wawili.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ULINZI NA USALAMA KUHUSU
UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI KWA
MWAKA WA FEDHA 2014/2015 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU
MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016
KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

UTANGULIZI:

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa kanuni ya 99(9) pamoja na kanuni ya 117(11) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la April, 2013 na kwa niaba ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ulinzi na Usalama naomba kuwasilisha Taarifa Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015; pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilikutana na Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi Mhe. Mathias Chikawe na Wasaidizi wake tarehe 30 Aprili, 04 na 06 Mei, 2015 na kupokea Taarifa ya Utekelezaji wa Mipango ya Bajeti ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2014/2015 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2015/2016 kwa mafungu matano ya wizara hii kama ifuatavyo:-

- (i) Fungu 14 - Kikosi cha Zimamoto na Uokoaji;
- (ii) Fungu 28 - Jeshi la Polisi;
- (iii) Fungu 29 - Jeshi la Magereza;
- (iv) Fungu 51- Wizara ya Mambo Ndani ya Nchi; na
- (v) Fungu 93 - Idara ya Uhamiaji.

Mheshimiwa Spika, Kwa mujibu wa Kanuni ya 98 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Aprili, 2013, Kamati ilikagua miradi ya maendeleo iliyoidhinishiwa fedha na Bunge lako Tukufu kwa mwaka wa fedha 2014/2015. Katika ziara ya ukaguzi wa miradi, Kamati ilibaini kwamba kwa kiasi kikubwa fedha za miradi hazikutolewa kama zilivoidhinishwa na Bunge.

2.0 UTEKELEZAJI WA USHAURI WA KAMATI KWA MWAKA 2014/2015

Mheshimiwa Spika, wakati wa kupitisha Bajeti ya Wizara hii ya mwaka 2014/2015, Kamati ilitoa ushauri na maoni mbalimbali kwa nia ya kufanikisha malengo ya Wizara. Taarifa ya Mheshimiwa Waziri aliyotoa kwa Kamati inaonesha kwamba kwa kiasi kikubwa Wizara imezingatia ushauri wa Kamati na kuufanyia kazi kama ifuatavyo:-

2.1 Magereza – Fungu 29

(i) **Serikali itenge fedha kwa ajili ya kulipa madeni ya wazabuni na watumishi.**

Mheshimiwa Spika, Agizo hili halikuteklezwa kwani kwa kipindi cha kuanzia Julai, 2012 hadi Juni 2014 jeshi lina madeni yanayofikia shilingi bilioni 40.8. Madeni hayo yanahusu watumishi, wazabuni na huduma za simu na umeme.

(ii) **Serikali itenge fedha za kutosha kwa ajili ya kununua magari walau moja kwa kila gereza**

Mheshimiwa Spika, Katika mwaka 2014/2015 Serikali haikuweza kutenga fedha za kutosha kununua magari kwa kila gereza na badala yake Serikali imenunua magari 7 tu kwa ajili ya shughuli za utawala.

(iii) **Serikali iongeze bajeti ya chakula kwa wafungwa iwe wastani wa shilingi 3,000/= kwa siku**

Mheshimiwa Spika, Serikali katika bajeti ya mwaka 2014/2015 iliongeza bajeti ya chakula cha wafungwa toka shilingi 500/= kwa mtu mmoja kwa siku hadi kufikia shilingi 1,500/= tu, badala ya Shilingi 3000 ambazo zilipendekezwa na Kamati. Hivyo ushauri wa Kamati haukutekelezwa kikamilifu.

(iv) **Katika kutatua tatizo sugu la msongamano magerezani** Kamati iliishauri Serikali kwamba sheria ya “Community Service” itumike Mikoa yote badala ya Mikoa 16 ya sasa; Sheria ya Parole kutazamwa upya ili kupanua wigo na wafungwa wengi zaidi kunufaika; Kamati za kusukuma kesi za ngazi za Wilaya na Mikoa zifanye kazi ya kutembelea magereza na mahakama ili kusukuma kesi zimalizike haraka na Wahamiaji haramu warudishwe kwenye nchi zao badala ya kujazwa kwenye magereza.

Mheshimwa Spika, Kamati ilielezwa ifuatavyo:-

a) Sheria ya “community service” inayoelekeza kwamba wahalifu wenye makosa madogo wapewe vifungo vya nje na wapangiwe kazi za umma kwa sasa inatumika katika mikoa 19 tu, badala ya mikoa yote 25 ya Tanzania Bara.

b) Kuhusu marekebisho ya sheria ya “parole” ni kwamba Rasimu ya mapendekezo ya maboresho katika sheria hii bado hayajaletwa Bungeni ili yafanyiwe kazi.

c) Kuhusu wahamiaji haramu kurudishwa kwenye nchi zao badala ya kujazwa kwenye magereza, Serikali iliarifu kwamba hadi mwezi machi, 2015 Wizara kwa kushirikiana na wabia wa maendeleo imewarudisha katika nchi zao wahamiaji haramu 2,155 ikiwa waethiopia 874, Burundi 749, DRC 192, Rwanda 102, Uganda 107, Kenya 95, Zambia 9, India 11, Nepal 21, Nigeria 8, China 2, Somalia 2, Cameroon 1 na Malawi 1.

2.2 Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi – Fungu 51

(i) Usajili wa Asasi za Kiraia kufanyika kwa umakini

Mheshimiwa Spika, Wizara ilitoa taarifa kwamba imeendelea kuimaraisha taratibu mbalimbali za uhakiki wa vyama vya kijamii na kidini kabla ya kuvisajili. Aidha imeendelea kuboresha kanzidata ya vyama hivi kuwa na kumbukumbu sahihi kwa vyama vyote vilivyosajiliwa ambavyo vipo hai.vilevile, hatua za kuvifutia usajili vyama vinavyokiuka masharti ya usajili kwa mujibu wa sheria zimeanza kuchukuliwa. Jumla ya vyama 24 vimepewa notice ya kusudio la kuvifuta.Zoezi hili limeendelea uchukuliwa kwa vyama vingine zaidi.

Mheshimwia Spika, Kamati inaishauri Serikali kwamba kazi hii iwe ndeleu na isiwe ya msimu.

iii) **Serikali ihakikishe kwamba, fedha zilizobaki kwa ajili ya mradi wa Vitambulisho vya Taifa zinatolewa mapema**

Mheshimiwa Spika, Wizara iliarifu kwamba imeendelea kuwasiliana na kufanya ufuatiliaji wa mara kwa mara katika Wizara ya Fedha ili kuhakikisha kuwa fedha zinazopangwa katika bajeti kwa ajili ya shughuli za Mradi wa Vitambulisho vya Taifa zinatolewa mapema.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa vitambulisho unasuasua na kutia mashaka juu ya kufanikiwa kwa kazi hii.

2.3 Uhamiaji – Fungu 93

Kamati ilishauri kwamba Serikali iangalie uwezekano wa kuiongezea fedha za Bajeti Idara hii ili kujengea uwezo wa kukabiliana na tatizo la wahamiaji haramu. Njia mojawapo ni kwa Serikali kuongeza bajeti ya Idara hii ni kuirejeshea gawio (retention) la 61% kama ilivyokuwa awali.

Mheshimiwa Spika, ushauri wa Kamati haukuzingatiwa kwani bajeti ya 2015/2016 kiwango cha gawio (retention) kwa Idara hii hakikuongezwa na isitoshe Kamati bado inasisitiza tena kwamba retention ya Idara ya Uhamiaji irudi kuwa 61% badala ya 45% ya sasa ili kusaidia operesheni zao na miradi ya maendeleo.

2.4 Jeshi la Zimamoto na Uokoaji – Fungu 14

(i) **Serikali itenge fedha kwa ajili ya maendeleo ili Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kukamilisha miradi yao waliyoianza**

Mheshimiwa Spika, ushauri huu umetokelezwa kwani bajeti ya mwaka 2015/2016 Serikali imetenga kiasi cha shilingi milioni 500 kwa ajili ya ujenzi wa vituo vitatu vya Zimamoto jijini Dar es Salaam na Shilingi Bilioni Moja kwa ajili ya ununuzi wa gari la Zimamoto. Hata hivyo kiwango hiki bado hakitoshelezi mahitaji.

(ii) **Serikali ihakikishe kuwa kikosi hiki kinapatiwa fedha za kutosha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya kuzimia moto na vya uokoaji ili kikosi kiweze kutekeleza najukumu yake kwa ufanisi**

Mheshimiwa Spika, katika bajeti ya mwaka 2014/2015 Jeshi la Zimamoto na Uokoaji limenunua magari mawili (2) ya shughuli za utawala pamoja na

pikipiki 40. Aidha katika bajeti ya mwaka 2015/2016, Serikali imetenga kiasi cha shilingi bilioni 1 kwa ajili ya kununulia gari la kuzimia moto ambayo haitoshelezi kwani hivi sasa kuna majengo marefu yenye ghorofa zaidi ya kumi na saba(17) hali inayohitaji magari yenye uwezo wa kuzima moto kwenye majengo ya aina hii.

3.0 TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MALENGO YA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015

Mheshimiwa Spika, Kabla ya kupitia na kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2015/2016, Kamati ilipitia Taarifa ya utekelezaji wa malengo ya Bajeti ya wizara hii kwa mwaka wa fedha 2014/2015 ili kujiridhisha iwapo mapato yaliyotarajiwa kukusanywa na fedha za matumizi zilizoidhinishwa na Bunge lako tukufu yalifikia malengo yaliyokusudiwa.

3.1 Upatikanaji wa Fedha kutoka Hazina

Mheshimiwa Spika, Katika Mwaka wa Fedha 2014/2015 Bunge lako tukufu kwa mafungu ya Wizara yote liliidhinisha jumla ya shilingi Bilioni 881,740,291,800.00/= kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo. Hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2015, kiasi cha fedha kilichopokelewa ni jumla ya shilingi Bilioni 581.353 sawa na asilimia sitini na tano (65%) ya Bajeti iliyoidhinishwa. Kutokana na mtiririko huu wa fedha ambapo sehemu ya fedha zilizoidhinishwa na Bunge hazikutolewa na Hazina, imeathiri utekelezaji wa malengo ya Wizara na asasi zilizo chini yake.

4.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

Mheshimiwa Spika, baada ya kueleza uchambuzi wa Kamati kuhusu Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya nchi kwa mwaka 2014/2015 pamoja na Makadirio ya mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2015/2016, sasa naomba kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati kwa Mafungu yote matano kama ifuatavyo:-

Kikosi cha Zimamoto na Uokoaji - Fungu 14

a) Fedha za Miradi ya Maendeleo

Mheshimiwa Spika, Kikosi cha Zimamoto na Uokoaji hakijatengewa fedha za miradi ya maendeleo kwa muda wa miaka mitano mfululizo. Kwa mwaka huu wa Fedha Jeshi la Zimamoto limetengewa shilingi Bilioni 1.5 ili kununua gari la Zimamoto na ujenzi wa vituo vitatu vidogo vya Zimamoto katika jiji la Dar Es Salaam. Maoni ya Kamati ni kwamba fedha hizi hazitoshelezi mahitaji halisi ya

kikosi hiki. Ukosefu wa fedha za maendeleo umesababisha mradi mkubwa wa Ujenzi wa makao makuu ya zimamoto kukwama.

b) Ununuzi wa Vitendea Kazi

Mheshimiwa Spika, Kikosi cha Zimamoto kina upungufu mkubwa wa vitendea kazi kwa ajili ya kutekeleza majukumuyake. Mfanomagari yakuzimia moto katika majengo marefu yanayozidi ghorofa kumi na saba (17) pamoja na vifaa vya kisasa vya uokozi. Hivyo Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kuwa kikosi hiki kinapatiwa fedha za kutosha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya kuzimia moto na vya uokoaji ili kikosi kiweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Jeshi la Polisi - Fungu 28

a) Posho ya Askari

Mheshimiwa Spika, bajeti iliyotengwa kwa mwaka wa fedha 2015/2016 ni shilingi 99,704,240,000/= ambayo itawezesha askari kuendelea kulipwa posho ya chakula (ration allowance) ya shilingi 6,000/= kwa siku. Kiwango hiki cha posho hakitoshelezi mahitaji ya chakulabora kwa askari awapo kazini. Pamoja nakutambua ufinyu wa bajeti, Kamati inapendekeza kwamba kiwango hicho kiongezwe hadi kufikia shilingi 10,000 kwa siku. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kwamba viwango hivi vya posho viwe vina huishwa kila mwaka kulingana na hali ya maisha

b) Adhabu Kali kwa Wanaosababisha Ajali

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Watanzania wengi wamekuwa wanapoteza maisha kutokana na ajali zinazosababishwa na uzembe wa madereva, ubovu wa vyombo vya usafiri na miundombinu isiokidhi ongezeko la vyombo vya moto, Kamati inashauri kuwa Sheria zifanyiwe marekebisho ili wale wote watakaothibitika kwa makosa ya uzembe wapewe adhabu kali. Aidha, Kamati inashauri kwamba miundombinu ya barabara nchini iboreshwe ili kuendena na ongezeko kubwa la magari na watumiaji wengine.

c) Ununuzi wa Vitendea Kazi

Mheshimiwa Spika, Kwa kuwa Jeshi la Polisi linafanya kazi kubwa ya ulinzi wa maisha ya watu na mali zao, linahitaji magari, pikipiki, boti na helikopta kwa ajili ya kufanya doria. Katika mwaka huu wa fedha Wizara imepanga kununua magari 777 na pikipiki 3,800 kwa matumizi ya jeshi kwa kutosheleza hadi ngazi ya kata. Hata hivyo Kamati inaona kwamba Polisi wanahitaji kuimarisha ulinzi wa majini na angani hivyo Serikali ifanye mpango wa kununua boti na Herikopta.

Jeshi la Magereza - Fungu 29

a) Madeni ya Wazabuni na Watumishi:

Mheshimiwa Spika, Kamati inasikitishwa kwa uwepo wa madeni ambayo mpaka sasa hayajalipwa. Kwa kipindi cha Julai, 2012 hadi June, 2014 jumla ya madeni yote ni shilingi 40,800,811,910.00. Kati ya hayo, madeni ya watumishi ni Tsh.8,878,979,960.00, madeni ya wazabuni ni Sh.21,885,611,975.00 na shilingi 10,036,219,975.00 ni medeni yavirusu umeme, simu pamoja na maji.

Mheshimiwa Spika, Kamati inazidi kuishauri na kuisisitizia Serikali kutenga fedha ili kulipa madeni haya.

b) Ununuzi wa Magari

Mheshimiwa Spika, Katika mwaka 2014/2015 Serikali imeweza kununua magari saba(7) kwa ajili ya shughuli za utawala. Kwa kuwa kuna umuhimu wa kuwa na magari kwa ajili ya kuwasafirisha wafungwa na mahabusu kwenda mahakamani, mahospitalini na shughuli nyingine za kiutawala, Kamati inaishauri Serikali kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya kununua walau gari moja kwa kila gereza la wilaya.

c) Bajeti Ndogo ya Chakula cha Wafungwa

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri kwamba fedha iliyotengwa ya shilingi 1500 kwa mtu kwa siku bado ni ndogo na hata hivyo haitolewi yote, hivyo Serikali inashauriwa iongeze bajeti ya chakula cha wafungwa magerezani kutoka wastani wa shilingi 1500/= kwa siku kwa mtu mmoja hadi kufikia shilingi 3,000/= kwa siku.

d) Tatizo sugu la msongamano Magerezani

Mheshimiwa Spika, Kumekuwa na msongamano wa wafungwa na mahabusu magerezani ambapo kwa hivi sasa kuna nafasi 29,552 tu wakati wastani wa wafungwa na mahabusu waliopo gerezani hadi mwezi Machi, 2015 ni 33,027. Idadi hii inazidi uwezo wamagereza kuwahifadhi wafungwa na mahabusu. Kamati inazidi kuishauri Serikali kuchukua hatua zifuatazo:-

i) Sheria ya "Community Service" itumike katika Mikoa yote 25 ya Tanzania Bara badala ya Mikoa 19 ya sasa ili wahalifu wenye makosa madogo watumikie adhabu nje ya magereza.

ii) Marekebisho ya Sheria ya *Parole yaletwe Bungeni mapema iwezekanavyo ili kupanua wigo wa wafungwa watakapo nufaika na sheria hii.*

iii) Wahamiaji haramu wanaokamatwa kwa makosa ya kuingia nchini isivyo halali waendeleo kurudishwa makwao badala ya kuwafunga katika magereza yetu nchini na hivyo kuongeza msongamano.

NIDA:

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015 Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa NIDA walitengewa kiasicha shilingi 201,048,980,000.00. Hadi mwezi Machi, 2015 nishilingi bilioni 41,884,000,000/= tu sawa na 20% ndizo zilizotolewa. Kamati inaishauri Serikali kwamba, fedha zilizobaki zitolewe mapema kwani upungufu huu wa fedha unachelewesha utoaji wa vitambulisho na hivyo kutokamilika katika muda uliopangwa.

Idara ya Uhamiaji

Mheshimiwa Spika, Hadi kufikia mwezi Machi, 2015 wahamiaji haramu 2,155 wamerudishwa katika nchi zao. Kamati inaishauri Serikali zoezi hili liwe endelevu na lisimamiwe kikamilifu hasa katika mikoa ya mipakani.

USHAURI WA JUMLA KWA WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI

i) Serikali iboreshe mfumo wa makusanyo ya fedha (Retention)

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la fedha za rentetion Kamati inashauri kwamba:-

i) Viwango vya rentetion virudishwe vya zamani yaani Zimamoto iwe 70% badala ya 49% ya sasa na Uhamiaji iwe 61% badala ya 45% ya sasa.

ii) Utaratibu wa fedha za rentetion kuwa ndani ya Bajeti ya Idara husika unaondoa motisha kwa idara husika ya kukusanya maduhuli, hivyo Kamati inashauri fedha za rentetion ziwe ni nyongeza katika bajeti ya Idara husika hasa katika vyombo vya Ulinzi na Usalama ambavyo vina mahitaji mahususi ya zana za kazi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Jeshi la Polisi hawapo kwenye mfumo wa rentetion, Kamati inashauri kwamba ili kuongeza uwezo wa kununua zana za Polisi na pia kutatua tatizo la ukosefu wa nyumba za askari, ni muhimu wakaachiwa fedha zote wanazokusanya.

5.0 HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati hii kwa umahiri wao katika kuchambua hoja pamoja na kutoa ushauri wa mara kwa

Nakala ya Mtandao (Online Document)

mara ambao umekuwa ukiisaidia Wizara hii kufanya maboresho ya utendaji kazi wake.

Kwa kuwa Bajeti ni ya mwisho kwa uhai wa Kamati naomba kuwatambua kwa majina kama ifuatavyo:

1.Mhe. Anna M. Abdallah, Mb	-	Mwenyekiti
2.Mhe. Dkt. Muhammed Seif Khatib, Mb	-	M/Mwenyekiti
3.Mhe. Brig. Jen. (Mst.) Hassan Ngwilizi, Mb	-	Mjumbe
4.Mhe. Kapt. (Mst.) John Z. Chiligati, Mb	-	Mjumbe
5.Mhe. Mariam Mfaki, Mb	-	Mjumbe
6.Mhe. Dkt. Augustino L. Mrema, Mb	-	Mjumbe
7.Mhe. Cynthia Hilda Ngoye, Mb	-	Mjumbe
8.Mhe. Dr. Donald M. Malole, Mb	-	Mjumbe
9.Mhe. Mhandisi Stella Manyanya, Mb	-	Mjumbe
10.Mhe. Vita R. Kawawa, Mb	-	Mjumbe
11.Mhe. Mussa H. Mussa, Mb	-	Mjumbe
12.Mhe. Rahel Mashishanga Robert, Mb	-	Mjumbe
13.Mhe. Hamad Ali Hamadi, Mb	-	Mjumbe
14.Mhe. Masoud Abdallah Salim, Mb	-	Mjumbe
15.Mhe. Vincent Nyerere, Mb	-	Mjumbe

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuchukua fursa hii kumshukuru Katibu wa Bunge Dkt. Thomas Kasililah na watumishi wote wa Bunge kwa kuisaidia Kamati kutekeleza majukumu yake. Kipekee, nawashukuru Ndugu Peter Magati na Ndugu Onesmo Laulau kwa kuratibu vyema kazi za Kamati hadi taarifa hii ilipoletwa mbele ya Bunge lako tukufu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, sasa naomba Bunge lako tukufu, likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ULINZI NA USALAMA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA KWA MWAKA 2014/2015 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA 2015/2016 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

1.0 UTANGULIZI

1.1 Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni Na. 99(9) na 117(11), Kanuni za Kudumu za Bunge, (Toleo la Aprili 2013), naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama. Kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015 na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016.

1.2 Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa majukumu yake, Kamati ya Kudumu ya Ulinzi na Usalama ilikutana tarehe 27/04/2015 hadi 08/05/2015, katika ukumbi wa Ofisi Ndogo ya Bunge Dar es Salaam kupitia Taarifa ya utekelezaji wa Bajeti na kuchambua kwa kina Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka 2015/2016. Wizara hii ina Mafungu 3 kama ifuatavyo:-

- i) Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa – Fungu 57
- ii) Jeshi la Kujenga Taifa – Fungu 39
- iii) Ngome – Fungu 38

2.0 UTEKELEZAJI WA MAAGIZO YA KAMATI KWA MWAKA 2014/2015

2.1 Mheshimiwa Spika, wakati wa kuchambua Bajeti ya Wizara hii kwa mwaka 2014/2015, Kamati ya Ulinzi na Usalama ilitoa Maoni na Ushauri katika maeneo mbalimbali ili kuboresha utendaji wa kazi wa Wizara hii. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba katika baadhi ya maeneo ushauri wa Kamati umetekelezwa na baadhi haujazingatiwa, hivyo maeneo hayo yanahitaji kufanyiwa kazi zaidi ili yaweze kuboreshwa. Utekelezaji wa ushauri wa Kamati ulikuwa kama ifuatavyo:-

3.0 USHAURI/MAONI YA KAMATI WAKATI ILIPOJADILI MAKADIRIO YA

MAPATO, MPANGO NA BAJETI YA MWAKA 2014/15

Ushauri no.1

Serikali ihakikishe inatenga fedha za kutosha ili kuliwezesha Jeshi na vyombo vyote vya Ulinzi na Usalama kusimamia amani na utulivu nchini.

Serikali iliongeza bajeti ya Wizara katika mwaka 2014/15 kutoka makadirio ya Shilingi **1,296,076,056,000.00** hadi Shilingi **1,312,502,196,000.00** sawa na ongezeko la Shilingi 43,426,140,000.00. Pamoja na ongezeko hilo, upatikanaji wa fedha haukuwa wa kuridhisha ambapo hadi Machi, 2015 Wizara Fungu 57 ilipata 28.66% ya matumizi mengineyo, na 30.67% ya fedha ya maendeleo. Fungu 38 – NGOME ilipata 57.77% ya matumizi mengineyo na 12.5% ya fedha ya maendeleo na Fungu 39 – JKT ilipata 73.9% ya matumizi mengineyo na 21.4% kwa ajili ya fedha ya maendeleo.

Ushauri no.2

Serikali ihakikishe madeni yote ya Wizara ya Ulinzi na JKT ambayo yamekwishahakikiwa yanalipwa na kuwa bajeti mpya ya 2015/2016 inaanza bila kuwa na madeni ya miaka ya nyuma

Katika mwaka wa fedha 2014/15 Wizara imelipa madeni ya Shilingi 2,150,000,000.00 katika Fungu 39 – JKT na kubakiwa na jumla ya madeni ya Shilingi 483,980,463,090.92 ambapo kati ya hizo Fungu 57 – Wizara inadaiwa Shilingi 326,355,414,700.00, Fungu 38: NGOME lina deni la jumla ya Shilingi 85,736,350,379.70 na Fungu 39 – JKT, lina madeni ya Shilingi 71,888,698,111.22, kutoka kwa Wazabuni, ankara za umeme na maji, madeni ya mikataba na stahili za askari na watumishi wa Umma na kodi ya pango. Sambamba na madeni hayo, katika mwaka 2015/16 Wizara imepanga kulipa Shilingi 110,300,235,174.00 katika madeni ya mikataba ya Kimataifa. Hivyo, ushauri unaotolewa ni kuiomba Serikali iongeze ukomo wa bajeti ili kuwezesha ulipaji wa madeni hayo na “commitment” za mwaka wa fedha 2015/16. Kamati inapendekeza Hazina ichukue madeni ya kimkataba ya Kimataifa ili kupunguza mzigo kwa Wizara.

Ushauri no.3

Serikali itenge fedha kwa Wizara kwa ajili ya matengenezo ya barabara za mipaka.

Mheshimiwa Spika, kwa masikitiko makubwa hadi tunaandika taarifa hii, Serikali haijatoa jibu lolote kuhusu kukabidhi kazi za matengenezo ya barabara za mipakani kwa Wizara ya Ulinzi na JKT.

Ushauri no.4

Wizara ianzishe Kitengo Maalum kitakachohusika na upimaji, usimamizi na maendeleo ya ardhi ya jeshi

Mwaka wa fedha 20/12/2013 Serikali ilianzisha Kitengo cha Usimamizi wa Maendeleo ya Miliki .Utekelezaji wa agizo hili ulishafanyika.

Ushauri no.5

Serikali iendelee kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa makazi ya askari ikiwemo ujenzi wa mahanga ya askari kapera.

Kwa sasa Wizara inatekeleza mradi mkubwa wa ujenzi wa nyumba 10,000 nchini ya ufadhili wa Serikali (15%) na mkopo wenye masharti nafuu kutoka Benki ya Exim ya China (80%). Ujenzi katika awamu ya kwanza wa nyumba 6064 unaendelea vizuri katika vikosi mbalimbali na utakamilika mwaka 2017. Pamoja na mradi huu Serikali katika mwaka huu iliweza kugharimia ujenzi wa mabweni kwa ajili ya askari kapera na za wanajeshi waliooa katika vikosi vya 2/691 KJ Tongoni na shule ya Anga ya Kijeshi Tanga.

Ushauri no.6

Vyombo vya Ulinzi na Usalama vitekeleze kwa ukamilifu agizo la Amiri Jeshi Mkuu la kuajiri vijana waliohitimu mafunzo ya JKT.

Agizo la Mheshimiwa Rais lilishaanza kutekelezwa ambapo jumla ya vijana 27,059 waliohitimu mafunzo ya JKT na kati ya hao vijana 18,696 sawa na Asilimia 69 wamefaidika na utaratibu wa ajira katika vyombo vya Ulinzi na Usalama kuanzia mwaka 2011 hadi 2015. Utaratibu wa kutoa ajira katika vyombo vya Ulinzi na Usalama kwa vijana waliohitimu mafunzo ya JKT ni endelevu na kwa sasa Serikali haitoi kibali cha ajira katika vyombo vya Ulinzi na Usalama nje ya waliohitimu JKT.

Ushauri no.7

Serikali iwezeshe mafunzo ya JKT kwa vijana wote wanaomaliza kidato cha 6 na vijana ambao hawatajiunga na mafunzo hayo bila sababu za msingi Serikali iwachukulie hatua za kisheria

Serikali imeendelea kuliwezesha JKT ili liweze kuchukua vijana wote wanaomaliza kidato cha sita. Ili kufikia azma hiyo katika mwaka wa fedha 2014/15, Serikali ilitoa kiasi cha Shilingi **11,000,000,000.00** ambazo ziliidhinishwa kwa ajili ya matumizi kwa vijana wa mujibu wa sheria. Aidha, fedha za maendeleo hazikutolewa katika mtiririko mzuri kwani Serikali iliweza kutoa Shilingi **1,500,000,000.00** sawa na Asilimia 21.4 ya Shilingi **7,000,000,000.00** zilizoidhinishwa kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya makambi kwa lengo la kuongeza uwezo wa kuchukua vijana wengi zaidi.

Fedha zilizotolewa zilitosha kugharimia mafunzo kwa vijana 10,000 tu. Hata hivyo JKT lilifanikiwa kuchukua vijana 31,635 wa mujibu wa sheria ambapo kati yao vijana wa kidato cha sita walikuwa 18,839 sawa na Asilimia 54.7 ya lengo na vijana 12,796 walikuwa ni walimu ambao walichukuliwa baada ya kukosa vijana wa kidato cha sita waliotakiwa kujiunga na JKT awamu ya pili lakini ilishindikana kutokana na mwingiliano wa ratiba ya kujiunga na masomo

katika vyuo vikuu. Lengo lililowekwa katika mwaka 2014/15 lilikuwa ni kutoa mafunzo kwa vijana wote 34,450 watakaomaliza kidato cha sita mwezi Mei, 2015.

Ushauri no.8

Serikali ihakikishe inatenga fedha kila mwaka kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa Chuo cha Ukamanda na Unadhimu (Command and Staff College) Duluti, Arusha.

Katika bajeti ya mwaka 2014/15, Wizara ilitenga kiasi cha Shilingi **2,000,000,000.00** kwa ajili ya ukamilishaji wa viporo vya ujenzi ikihusisha pia kuendeleza ujenzi wa Chuo cha Ukamanda na Unadhimu (*Command and Staff College – CSC*) Duluti – Arusha. Ujenzi wa majengo katika chuo hicho umekuwa ukiendelea kwa lengo la kukamilisha majengo muhimu, ili kuwezesha Chuo kuhama toka Monduli na kuanza kuendesha kozi zake katika eneo la Duluti kuanzia Julai, 2015.

4.0 WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA

Mheshimiwa Spika, ili kusimamia vema jukumu la Ulinzi na Usalama nchini, Kamati inatoa maoni na ushauri ufuatao:-

4.1 Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa – Fungu 57

4.1.1 Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kuwepo kwa Madeni Makubwa katika mwaka wa fedha 2014/2015 yanayofikia kiasi cha **Tsh. 483,980,463,090.92**. Madeni hayo yanatokana na Wazabuni, ankara za maji na umeme, madeni ya Mikataba pamoja na stahili za askari na watumishi. Ndani ya deni hilo kuna deni la Mkataba la siku nyingi la Kampuni ya **Poly Technologies Inc.** la **Tsh.187,377,338,970.00**. Kamati inaishauri Serikali kulipa madeni hayo kwani kutofanya hivyo kuna sababisha madeni yenye riba kuongezeka na hivyo kuongeza ukubwa wa madeni.

4.1.2 Mheshimwia Spika, Kamati imebaini kwamba vyombo vya Ulinzi na Usalama vinashindwa kutekeleza miradi ya maendeleo kwa sababu fedha za miradi hiyo hazitolewi zote na kwa wakati. Hali hii inapunguza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya vyombo hivi. Kamati inazidi kuishauri Serikali ihakikishe fedha zote zinazoidhinishwa na Bunge zinapelekwa ili kudumisha ulinzi na usalama wa nchi yetu.

4.1.3 Mheshimwia Spika, Kamati imekuwa ikipokea malalamiko toka kwa wana Jeshi wastaafu hususani Askari wa kawaida kuhusu Mafao yao ya Uzeeni (Pension) Kamati inaishauri Serikali kuhuhisha malipo ya *Pension* kwa wasitaafu wa Jeshi ngazi zote ambao walistaafu kabla ya mpango mpya wa stahili mpya kutolewa

4.1.4 Mheshimiwa Spika, Kamati ilimepata nafasi ya kutembelea nchi ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na kukutana na vijana wa Jeshi letu wanaosaidiana na Jeshi la Umoja wa Mataifa, MONUSCO chini ya Brigid Maalum ya *Intervention Force Brigade (IFB)* ambao wanafanya kazi nzuri dhidi ya vikundi vya waasi. Pamoja na askari wetu waliopo DRC, pia nchi yetu inao askari wanaoshiriki kulinda amani Darful (Sudan) na Lebanon. Tunaliomba Bunge kuungana na Kamati kulipongeza Jeshi letu kwa kazi nzuri inayofanywa na vijana wetu na inayoiletea heshima nchi yetu kimataifa.

4.2 Fungu 38 – NGOME

Mheshimiwa Spika, Katika mwaka wa Fedha 2014/2015 Ngome ilidhinishiwa shilingi 22,000,000,000 kwa shughuli za maendeleo. Hadi kufikia Machi 31 ni shilingi 1,500,000,000/=tu ndizo zilizotolewa sawa na 12.5%. Kamati inaishauri Serikali kuchukua hatua za haraka na kutoa fedha zilizo bakia ili shughuli za ulinzi wa nchi ziende kama zilivyo kusudiwa.

4.3 FUNGU 39 – JESHI LA KUJENGA TAIFA

4.3.1 Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kwamba jumla ya vijana wanaohitajika kujiunga na JKT kwa mujibu wa Sheria kwa mwaka 2015 ni 34,100. Fedha iliyotengwa katika Bajeti ya 2015/2016 ni Shilingi 25,777,234,000/= ambayo inatosheleza kuhudumia vijana 20,000 tu wa mujibu wa sheria na vijana 5,000 wa kujitolea.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri Serikali iongeze bajeti ili vijana wote wanaomaliza kidato cha sita wapate fursa hii ya kujiunga na JKT ili kuongeza uzalendo na ukakamavu kwa vijana wetu; badala ya kuacha maelfu ya Vijana nje ya utaratibu wa JKT. Aidha, idadi ya vijana 34,100 haijumuishi vijana wanaomaliza vyo ambao pia ni muhimu kwenda JKT kwa mujibu wa Sheria. Kamati inasisitiza kwamba Fedha zote za maendeleo zilizobaki kwa upande wa JKT zitolewe ili vijana wote waweze kujiunga na Jeshi la kujenga Taifa.

4.3.2 Mheshimiwa Spika, Jeshi la Kujenga Taifa linamiliki Shirika la SUMA – JKT lililoanzishwa ili kuzalisha mali kibiashara kwa sheria ya Mashirika ya Umma ya mwaka 1974. Pamoja na uzalishaji, shirika hili pia linayo kampuni ya SUMA GUARD ambayo ni mahsusi kwa shughuli za ulinzi. Kamati inaishauri Serikali kwamba kwa kuwa SUMA GUARD inao vijana waliohitimu mafunzo ya kijeshi, ni vema SUMA GUARD ikatumika kulinda maeneo mbalimbali ya taasisi za umma na miundombinu muhimu badala ya kuajiri ulinzi binafsi.

4.3.3 Mheshimiwa Spika, Kamati inazidi kuisitiza kwamba Sheria namba 16 ya mwaka 1964 inayounda Jeshi la Kujenga Taifa iletwe Bungeni ili kufanyiwa

marekebisho na hivyo kuendana na malengo na dhamira ya wakati huu kwani kwa hivi sasa mambo mengi yameboreshwa katika utendaji wa shughuli za JKT.

5.0 HITIMISHO

5.1 Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipa fursa hii. Pia, namshukuru Mheshimiwa Waziri, Dkt. Hussein Mwinyi, (Mb) pamoja na Mheshimiwa Mathias Chikawe, Mb, Wizara zao na taasisi zao zote kwa ushirikiano wao mkubwa wakati wa kujadili Makadirio, Mapato na Matumizi ya Wizara hizo.

5.2 Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kuwashukuru wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama, kwa kazi nzuri ya kujadili na kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hizi kwa mwaka 2015/2016. Kwa kuwa huu ni mwaka wa mwisho wa uhai wa Kamati hii katika Bunge la Kumi naomba kuwatambua kwa majina kama ifuatavyo:-

1.Mhe. Anna M. Abdallah, Mb	-	Mwenyeki
2.Mhe. Dkt. Muhammed Seif Khatib, Mb	-	M/Mwenyekiti
3.Mhe. Brig. Jen. (Mst.) Hassan Ngwilizi, Mb	-	Mjumbe
4.Mhe. Kapt. (Mst.) John Z. Chiligati, Mb	-	Mjumbe
5.Mhe. Mariam Mfaki, Mb	-	Mjumbe
6.Mhe. Dkt. Augustino L. Mrema, Mb	-	Mjumbe
7.Mhe. Cynthia Hilda Ngoye, Mb	-	Mjumbe
8.Mhe. Dr. Donald M. Malole, Mb	-	Mjumbe
9.Mhe. Mhandisi Stella Manyanya, Mb	-	Mjumbe
10.Mhe. Vita R. Kawawa, Mb	-	Mjumbe
11.Mhe. Mussa H. Mussa, Mb	-	Mjumbe
12.Mhe. Rahel Mashishanga Robert, Mb	-	Mjumbe
13.Mhe. Hamad Ali Hamadi, Mb	-	Mjumbe
14.Mhe. Masoud Abdallah Salim, Mb	-	Mjumbe
15.Mhe. Vincent Nyerere, Mb	-	Mjumbe

Kwa aina ya pekee nawashukuru wajumbe wote kwa ushirikiano mkubwa walionipa kwa kipindi chote cha miaka miwili na nusu ya uhai wa Kamati.

Aidha, napenda kuwashukuru kwa dhati Watumishi wa Bunge Ndg. Onesmo Laulau na Ndg. Peter Magati waliotumikia na kusaidia Kamati hii katika kutekeleza jukumu hilo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Usalama na Taasisi zake kama yalivyowasilishwa na Mtoa Hoja.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Capt. Chiligati kwa kuyaptia maoni ya Kamati iliyoshughulikia Wizara zote mbili, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Sasa ni wakati wa maoni ya Upinzani na ningemuomba Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani juu ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi atangulie, atafuatiwa na Msemaji Mkuu wa Upinzani juu ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Namuona Mheshimiwa Lema, una dakika 20. Nasisitiza dakika 20 na atakayefuata naye ni dakika 20 pia. Karibu sana Mheshimiwa Lema.

MHE. GODBLESS J. LEMA – MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, lakini nitachukua na dakika tano za Msemaji wa Kambi ya Upinzani upande wa Jeshi la Ulinzi na Kujenga Taifa, kwa hiyo nitakuwa na dakika 25.

NAIBU SPIKA: Sawasawa.

HOTUBA YA MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KATIKA WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI, MHE. GODBLESS JONATHAN LEMA (MB), AKIWASILISHA BUNGENI MAONI YA KAMBI YA UPINZANI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA YA WIZARA HIYO, KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016 KAMA ILIVYOSOMWA BUNGENI

MHE. GODBLESS J. LEMA – MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa kuwasilisha Bungeni maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya fedha ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2015/2016.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maslahi ya umma wa Watanzania na watu wa Arusha, napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuwepo hapa leo kuwasilisha maoni na mapendekezo ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya fedha katika Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ya mwaka wa fedha 2015/2016.

Mheshimiwa Naibu Spika, familia yangu inatambua kwamba kuwa Mbunge wa Upinzani katika Taifa linalopuuza utu, demokrasia na haki ni adha kubwa kutokana na kuzungukwa na mazingira yaliyojaa vitisho, kejeli, mateso, matusi na kupandikizwa hofu. Hata hivyo, napenda kumshukuru mke wangu kwa kuwa amekuwa msaada mkubwa sana kwangu katika dua, sala na maombi na hivyo kuifanya kazi hii kuwa ya thamani na nyepesi kwangu. Napenda pia kuwapongeza wanangu Allbless na Terrence kwa ucheshi wao unaoifanya familia nzima kuwa na furaha wakati wote.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii natoa pia shukurani zangu za dhati kabisa kwa Wakurugenzi wote wa *Arusha Development Foundation (ArDF)* kwani ni jana tu ya tarehe 21 Mei, 2015 tumeweza kusaini mkataba wa kuanza ujenzi wa Hospitali ya Mama na Mtoto pamoja na Chuo cha Wakunga huko Burka Jijini Arusha. Namshukuru pia Dkt. Andrew Browning wa *Maternity Africa* pamoja na timu yake yote kwa nia ya dhati kabisa ya kukubali na kutafuta fedha ambazo amekwishazipata kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Mama na Mtoto katika Jimbo letu na nchi yetu, jitihada ambazo tumezifanya sisi wenyewe bila msaada wa mtu yeyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru pia rafiki yangu Hayati Wakili Nyaga Mawala, kwa mchango wake kutoa eneo la ujenzi wa hospitali hiyo. Alikuwa ni mtu mwema na mwenye kupenda watu na maendeleo. Leo hatuko naye wakati kazi hii njema imeanza, lakini mchango wake hautasahaulika kwetu sisi na jamii ya watu wa Arusha na Tanzania hususan kwa afya ya Mama na Mtoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kutoa shukrani zangu za dhati kwa wapiga kura wangu wa Jimbo la Arusha Mjini. Ninajua na wanajua kuwa mwaka huu kutakuwa na Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani. Ushindi kwetu ni jambo la kawaida na kutafakari na uamuzi tumeshafanya, tujandikishe kwa wingi daftari litakapokuja hivi karibuni ili kuthibitisha ushindi usio na hofu. Tumepewa fursa ya mabadiliko kwa kujiandikisha na tutumie wajibu wetu kushawishi ndugu zetu popote walipo ndani ya nchi yetu kujua umuhimu wa jambo hili la uandikishaji kwa ajili ya kuiondoa CCM madarakani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia maudhui ya methali isemayo 'sikio la kufa halisikii dawa' na kwa kuzingatia uhalisia wenyewe kwamba Serikali hii ya Awamu ya Nne inamaliza muda wake; Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kipindi hiki haitatoa tena ushauri kwa kuwa Serikali hii kwani haitakuwepo madarakani tena kuutekeleza ushauri huo, badala yake tutaonesha jinsi ambavyo Serikali hii ya CCM imeshindwa kutekeleza majukumu yaliyopo chini ya Wizara hii kwa muda wote wa miaka 53 ya Uhuru iliyokaa madarakani na kutoa mwelekeo wa nchi na masuala muhimu yatakayotekelezwa na Serikali ambayo inayotokana na Upinzani baada ya ushindi wa kishindo katika Uchaguzi Mkuu wa Oktoba, 2015. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya usalama nchini. Uchochezi wa kidini na kikabila. Kwa mihula yote miwili ya utawala wa Serikali hii ya Awamu ya Nne, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imekuwa ikikemea tabia mbaya na hatari kwa mustakabali wa amani ya nchi ya uchochezi wa kidini na kikabila unaofanywa kwa makusudi na viongozi wa CCM kwa maslahi yao ya kisiasa.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la udini na ukabila limeendelea kuwa hatari kwa ustawi wa amani ya nchi yetu na hili ni janga kubwa ambalo linaratibiwa na Chama Tawala na washirika wake kwa maslahi ya kisiasa. Hivi karibuni tumeshuhudia siasa chafu za rushwa, ukabila na udini zikiibuka nyakati hizi za uchaguzi. Kwa Arusha Mjini, siasa za ukabila zinafanywa na zinaendelea kufanywa na baadhi ya makada wa CCM.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati uchochezi huu wa kidini na kikabila unafanyika, Usalama wa Taifa wanajua, Polisi wanajua lakini hawachukui hatua yoyote. Nadhani wanafikiri kwamba ni mkakati mzuri wa ushindi kwa CCM lakini kumbe ni mkakati unaohatarisha hali ya usalama na amani nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nawataka hao wanaofanya vikao kwenye mazizi ya ng'ombe huko Arusha kwa misingi ya ukabila na kupanga mikakati ya kutoa rushwa ili kushinda Ubunge katika Jimbo wa Arusha kuacha mara moja kufanya hivyo kwani Arusha itaendelea kuhitaji Mbunge mkakamavu na siyo kiongozi wa ukoo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwaahidi wapiga kura wangu wa Arusha Mjini kwamba chama changu na mimi mwenyewe hatuta fanya siasa za rushwa za kuwanunua wapiga kura. Hii ni kwa sababu tunatafuta uhuru kamili wa nchi hii, hivyo hatuwezi kujadili bei ya utu wa binadamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka jana nilieleza katika hotuba yangu kwamba tatizo la udini na ukabila katika taifa hili linaonekana kuendelea kukomaa na ni tatizo ambalo halitamwacha hata mmoja wetu salama. Ni tatizo ambalo hakuna mshindi atakayepatikana. Ni tatizo ambalo hata kama litaisambaratisha nchi, hata wale watakaofanikiwa kuikimbia nchi hawatakuwa salama huko wanakokwenda kwa sababu watakuwa bado na imani zao na chuki hiyo dhidi imani nyingine itaendelea popote watakapokuwepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na hatari inayoweza kutokana na uchochezi wa kidini na kikabila, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, iliitaka Serikali kutafakari upya na kuleta sheria mpya itakayokataza na kuwawajibisha kwa nguvu zote wale wote watakaotaribu hata kwa maneno kueneza chuki au ubaguzi dhidi ya dini, kabila au rangi lakini mpaka sasa jambo hilo halijafanyika. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapenda kwa mara nyingine tena kutoa angalizo kwa Serikali kuchukua hatua za dharura za kukabiliana na athari zinazoweza kutokea kutokana na uchochezi wa kidini na kikabila hasa tunapoelekea katika Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani.

Mheshimiwa Naibu Spika, ajali za barabarani na usalama wa wasafiri. Katika miaka yote kumi ya utawala wa Awamu ya Nne ya Serikali hii ya CCM, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imekuwa ikiitaka Serikali kuchukua hatua

madhubuti za kupunguza matukio ya ajali barabarani ambayo yamepoteza maisha ya wananchi wengi na kuacha wengine wakiwa walemavu. Jambo la kushangaza na kusikitisha ni kwamba kadiri tunavyoipa Serikali ushauri mzuri ndivyo inavyozidi kuzembea na ajali zinazidi kuongezeka. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivi kwa sababu katika kipindi cha Januari hadi Aprili mwaka huu wa 2015 ambao kimsingi ndiyo mwaka wa mwisho wa uhudumu wa Serikali hii ya Awamu ya Nne, ndiyo vifo vingi vimetokea kutokana na ajali za barabarani kuliko miaka ya nyuma. Kwa mujibu wa Taarifa ya Kamanda wa Kikosi cha Usalama Barabarani, Kamishna wa Polisi Mohamed Mpinga, kuanzia Januari zimetokea ajali 823, vifo 273 na majeruhi 876. Mwezi Februari peke yake zimetokea ajali 641, vifo 236 majeruhi 726 na Machi zimetokea ajali 652, vifo 357 na majeruhi 761.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama usafiri wa reli ungeboreshwa na kuwa wa uhakika na kama pia usafiri wa anga ungeboreshwa kwa kuwa na ndege nyingi na hivyo kufanya gharama za usafiri wa anga kupungua na hivyo kumwezesha mwananchi wa kawaida kuzimudu basi ingesaidia sana kupunguza matumizi ya barabara kwa mabasi ya abiria na malori ambayo kimsingi ndiyo yanaongoza kwa ajali za barabarani. Barabara zingetumika tu kwa magari binafsi na ajali za barabarani zingepungua sana. Ni aibu kwa taifa kwamba nchi yenye rasilimali nyingi kama Tanzania bado kusafiri kwa ndege tunaambiwa ni ndoto kama kauli mbiu ya *Fast Jet* inavyosema “*Flying your dream*” (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Polisi wamekuwa wepesi kuwatupia madereva lawama kuwa ni wazembe kila inapotokea ajali, lakini wanasahau kuwa ajali nyingine zinatokea kutokana na miundombinu mibovu na pia ajali nyingine zinasababishwa na Polisi wa Usalama Barabarani wenyewe kwa kupokea rushwa na kuyaruhusu magari mabovu kuendelea na safari. Aidha, utaratibu wa sasa wa kumtaka Askari wa Usalama Barabarani kukamata makosa yasiyopungua thelathini kwa siku na kuyaandikia “*notifications*” na kukusanya faini ya Sh. 30,000/= kwa kila kosa kumekifanya Kikosi cha Usalama Barabarani kuwa kama kitengo cha TRA kwa kukusanya mapato. Inasikitisha kusikia Jeshi la Polisi likisifiwa kwa ukusanyaji wa mapato bila kujali athari zilizotokea baada ya ukusanyaji wa mapato hayo. Hili kwa Arusha kwa kweli wanafanya kazi kubwa kuliko hata TRA. Hatutaweza kuondoa ajali barabarani kwa kuongeza faini, isipokuwa kwa kuboresha miundombinu mingine ya usafirishaji kama vile reli na usafiri wa anga ili kupunguza matumizi ya barabara kiholela.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inapenda kuwaahidi wananchi kwamba Upinzani utakapounda Serikali baada ya Uchaguzi wa Oktoba mwaka huu, suala la usalama barabarani litakuwa ni

mojawapo ya vipaumbele vya kazi za Serikali kwa kuwa Watanzania wamechoka kusikia habari za mauti na ulemavu unaosababishwa na matumizi mabaya ya barabara. Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inawasihi wananchi wote kuwa makini na matumizi ya barabara hasa wale waendesha bodaboda, kwani matumizi barabara yasiozingatia sheria za barabarani yanayofanywa na wananchi ni chanzo kikubwa cha ajali barabarani pia. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukomeshaji wa matumizi na biashara haramu ya dawa za kulevyo. Hii iingie kwenye *Hansard*, siwezi kuizungumzia sana kwa sababu Mheshimiwa Rais alishawahi kusema anawafahamu na sasa kama ameshindwa kuwataja maana yake huyu atakuwa ni Mungu na mimi naogopa kumtaja Mungu hapa. Kwa hiyo, naomba hizi zote ziingie kwenye *Hansard*. (Kicheko)

Mheshimiwa Naibu Spika, uundwaji wa Tume ya Uchunguzi wa Kimahakama (*The Judicial Inquest Commission*) kuchunguza mauaji ya raia yaliyofanywa na vyombo vya dola. Kwa miaka yote kumi ya utawala wa Serikali hii ya Awamu ya Nne, Kambi Rasmi ya Upinzani ilikuwa ikipiga kelele na kulaani sana mauaji ya raia wasio na hatia yanayofanywa na vyombo vya dola hususan Jeshi la Polisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi rasmi ya Upinzani Bungeni, iliitaka Serikali kuunda Tume ya Uchunguzi wa Kimahakama au kwa lugha nyingine Mahakama ya Korona kwa ajili ya kuchunguza vifo vinavyotokana na mateso yanayofanywa na Jeshi la Polisi, kwa mujibu wa Sheria ya Kuchuguzi Vifo vyenye Utata (*The Inquest Act*) lakini mpaka sasa hivi Serikali haijafanya hivyo licha ya Waziri Mkuu kuahidi hapa Bungeni mara kadhaa kwamba Serikali ingeunda Tume hiyo. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kutambua kwamba kumwaga damu isiyo na hatia katika nchi ni laana katika nchi. Hivyo, Serikali iliepushe taifa na laana kwa kuzuia umwagaji damu ya watu wasio na hatia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Serikali hii ya CCM haioni umuhimu wa kuunda Tume ya Kimahakama, Kambi Rasmi ya Upinzani inapenda kuwahakikishia wananchi wote kwamba; tutakapokuwa tumeshika madaraka ya dola mwaka huu, utakuwa ndiyo mwisho wa uonevu unaofanywa na vyombo vya dola dhidi ya raia na zaidi sana hakutakuwa na ya damu ya raia wa nchi hii itakayopotea bure kwa sababu ya uonevu. Hata hivyo, tunawapa pole watu wote ambao ndugu zao wamefikwa na mauti na kwamba huzuni yao na uchungu wao unapewa thamani na Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, uboreshaji wa bajeti ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji. Katika hotuba zote za Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu bajeti ya Wizara

hii, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imekuwa ikiitaka Serikali kuongeza fedha za miradi ya maendeleo katika Wizara hii kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya Zimamoto na Uokoaji kwa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji lakini Serikali haijatilika maanani suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba yetu ya mwaka jana tulieleza na ninakukuu; *“Kwa mujibu wa randama ya Jeshi la Zimamoto, Fungu 14 (uk. 2) katika kipindi cha mwaka wa fedha 2013/2014 hakuna fedha yoyote iliyotengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo kwa Jeshi la Zimamoto”*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa randama hiyo, huu ni mwaka wa tatu mfululizo kwa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kutotengewa fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Kutokana na hali hiyo, Jeshi hilo limeshindwa kuendeleza ujenzi wa jengo la Ofisi ya Makao Makuu – TAZARA, Dar es Salaam, kushindwa kukarabati na kujenga vituo vipya vya zimamoto, kushindwa kununua vitendea kazi mbalimbali vikiwemo vifaa vya maokozi na vifaa vya kuzimia moto.

Mheshimiwa Naibu Spika, sote ni mashahidi wa majanga ya moto, maghorofa kuporomoka, meli kuzama, mafuriko na kila aina ya majanga ambapo Idara ya Zimamoto imekuwa ikishindwa kufanya chochote na hivyo kuwaacha wananchi wakiangamia katika majanga hayo. Kambi Rasmi ya Upinzani inashawishika kuamini kwamba Serikali haina nia njema na usalama wa raia na ndiyo maana haitengi fedha hata senti moja katika miradi ya maendeleo ya Jeshi la Zimamoto. Kama Serikali haioni umuhimu wa Jeshi la Zimamoto ni bora kulifuta kuliko kuliacha wakati haliwezeshwi kufanya kazi yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaungana na wananchi wote waliopata madhila kutokana na majanga mbalimbali ambapo Jeshi la Zimamoto na Uokoaji lilishindwa kuwapatia msaada kutokana na kukosa vifaa vya kutendea kazi. Aidha, tunawaahidi wananchi kwamba endapo tutaingia madarakani, bajeti ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji itaboreshwa ili Jeshi hilo liweze kufanya kazi kwa ufanisi ili kuwaokoa wananchi wakati wa majanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatima ya Vitambulisho vya Taifa. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni iliitaka Serikali kutoa ukomo wa muda, ambapo kila raia wa Tanzania atapatiwa Kitambulisho chake cha Taifa na kuainisha gharama zilizotumika katika mchakato mzima wa kutengeneza vitambulisho vya Taifa. Inasikitisha sana kuona kwamba tangu mchakato huo uanze, Serikali haitoi mrejesho wa namna zoezi hilo linavyoendelea, ni wananchi wangapi wameshapata vitambulisho hivyo, ni lini kila raia wa Tanzania atakuwa amepatiwa kitambulisho chake cha Taifa na ni fedha kiasi gani zimetumika hadi sasa katika mchakato huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Serikali hii ya Awamu ya Nne inaondoka madarakani kabla haijakamilisha mchakato wa kuwapatia wananchi wote Vitambulisho vya Taifa na kwa kuwa fedha nyingi za walipa kodi zimetumika kuanzisha mchakato huo, Kambi Rasmi ya Upinzani inapenda kuwaahidi wananchi kwamba tutakapoingia madarakani katika Uchaguzi Mkuu wa Oktoba, 2015, zoezi hilo litakamilishwa ndani ya kipindi cha mwaka mmoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maboresho ya mazingira na afya za mahabusu na wafungwa magerezani. Kwa miaka yote ya utawala wa Serikali ya Awamu ya Nne, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imekuwa ikiitaka Serikali kuchukua hatua ya kupunguza msongamano wa wafungwa na mahabusu magerezani sambamba na kuboresha lishe na huduma za afya kwa wafungwa na mahabusu. Licha ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuishauri Serikali mara zote hizo, msongamano wa wafungwa na mahabusu magerezani umeendelea kuwa ni tatizo na mateso makubwa, hali kadhalika huduma za afya na lishe kwa mahabusu na wafungwa zimeendelea kuwa duni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Serikali hii imeshindwa kupunguza msongamano wa mahabusu na wafungwa magerezani kwa kubuni adhabu mbadala nje kwa makosa madogo madogo badala ya vifungo na kwa kuwa Serikali hii imeshindwa kufanya upelelezi wa kesi zinazowakabili watuhumiwa wa makosa mbalimbali kwa wakati na hivyo kusababisha msongamano wa mahabusu magerezani ambapo hawazalishi chochote isipokuwa wanaitia hasara Serikali kwa kula bila kufanya kazi, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapenda kuwaahidi wananchi wote kwamba, endapo Upinzani utaingia madarakani msongamano wa wafungwa na mahabusu magerezani utapunguzwa kwa kutoa adhabu mbadala ya vifungo vya nje kwa makosa madogo madogo na kukamilisha upelelezi za kesi mbalimbali kwa wakati ili pia kupunguza msongamano wa mahabusu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni pia inalitaka Jeshi la Polisi kuwa linakamata na kuwatia watu mahabusu wakati uchunguzi wa kina ukiwa umeshafanyika tofauti na sasa ambapo mtu anayehisiwa tu kuwa ni mhalifu anaweza kuwekwa mahabusu na kukaa huko hadi miaka zaidi ya mitano na baadaye kuambiwa kuwa hana hatia. Huu ni uvunjaji wa haki za binadamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, uboreshaji wa mazingira ya kazi kwa Askari Magereza. Kwa mihula yote miwili ya utawala wa Serikali hii ya Awamu ya Nne, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imekuwa ikiitaka Serikali kujenga nyumba za Askari wa Magereza ili kuboresha mazingira yao ya kazi. Aidha, Kambi Rasmi ya iliitaka Serikali hii kuondoa urasimu na utaratibu kandamizi katika Jeshi la Magereza kuhusu mpango wa kujiendeleza kielimu kwa Maafisa wa Magereza

ambapo utaratibu huo ulikuwa unakwenda kinyume na *General Service Order (GSO)* na Sheria nyingine za Kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la msingi kuhusu kujiendeleza kielimu kwa Maafisa wa Magereza lilikuwa ni muda wa kisheria wa miaka miwili ya kukaa kwenye kituo cha kazi baada ya kuajiriwa kwa mara ya kwanza (*first appointment*) kabla ya kuomba ruhusa ya kujiendeleza kimasomo kukiukwa na badala yake waombaji wa nafasi za kujiendeleza kielimu kutakiwa kukaa kwenye kituo cha kazi hadi miaka sita ndipo waruhusiwe kujiendeleza kielimu. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaamini kwamba, mazingira bora ya kazi na maendeleo ya rasilimali watu ni nyenzo muhimu ya utendaji kazi kwa ufanisi si kwa Jeshi la Magereza tu bali kwa sekta na taasisi mbalimbali za Serikali zinazojali weledi na tija kwa watumishi wake. Kwa minajili hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inapenda kuwaahidi Askari Magereza kwamba iko nao bega kwa bega kukabiliana na changamoto zinazowakabili na kwa maana hiyo tutakapochukua nchi mwaka huu Oktoba, Sera ya Maendeleo ya Rasilimali Watu kwa Askari wa Jeshi la Polisi, itaboreshwa ili kutoa fursa nyingi zaidi za kujiendeleza kielimu kwa Maafisa wa Jeshi la Polisi na Magereza na halikadhalika mazingira ya kazi kwa Askari wa Jeshi la Polisi na Magereza ikiwa ni pamoja na kuwajengea nyumba nzuri zenye staha yataboreshwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, maboresho ya posho ya chakula (*ration allowance*) kwa Jeshi la Polisi. Kufuatia ugumu wa maisha ya Askari wetu wa Jeshi la Polisi, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwa miaka yote ya utawala wa Serikali ya Awamu ya Nne, imekuwa ikiitaka Serikali kuongeza posho ya chakula (*ration allowance*) kwa Askari wa Jeshi la Polisi ili walau posho hiyo ishabihiane na posho ya Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) ili waweze kukabiliana na ugumu wa maisha. Kwa mujibu wa Kumbukumbu Rasmi za Bunge (*Hansard*), Waziri wa Fedha wa wakati huo Marehemu William Mgimwa, alikubali posho ya chakula ya Sh.225,000/= kwa mwezi sawa na Sh.7,500/= kwa siku kwa kila Askari. Taarifa tulizo nazo ni kwamba, posho hiyo haijalipwa mpaka leo, licha ya Serikali kuahidi kuwalipa posho hiyo. Hata hii posho ya Sh.7,500/= kwa Polisi wanaowatii kwa kiwango hicho bado ni ndogo sana. Katika mazingira kama haya ambapo Serikali inaahidi ndani ya Bunge hili kupandisha posho za chakula za Askari Polisi halafu haitekelezi, inataka tuishauri nini tena?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa hoja ya kupandisha *ration allowance* kwa Askari wetu wa Jeshi la Polisi ilianzishwa na Kambi ya Upinzani Bungeni na kwa kuwa kwa miaka yote ya utawala wa Serikali ya Awamu ya Nne, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imekuwa ikiwatetea Askari wa Jeshi la Polisi ili walipwe posho ya chakula kwa siku kwa kila Askari; na kwa kuwa kwa mihula yote miwili ya utawala wa Serikali ya Awamu ya Nne, Serikali imeshindwa kutekeleza ahadi yake yenyewe iliyoitoa hapa Bungeni kwamba ingepandisha posho hiyo, hivyo basi Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapenda kuchukua

nafasi hii kuwaahidi Askari wote walio chini ya Jeshi la Polisi kwamba endapo Upinzani tutaingia madarakani Oktoba, 2015, posho hiyo itapandishwa haraka iwezekanavyo kwa kuwa ni Sera ya Upinzani kuboresha maslahi yao na maslahi yenu. Ili kutimiza azma hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inalitaka Jeshi la Polisi nchini kukataa kutumika kiasiasa na Serikali ya CCM kuukandamiza Upinzani na badala yake wafanye kazi kwa kuzingatia sheria na taratibu zinazotumika kuongoza utendaji wa Jeshi hilo. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, udhibiti wa fujo na mauaji kuelekea Uchaguzi Mkuu wa 2015. Kwa miaka yote kumi ya utawala wa Serikali hii ya Awamu ya Nne, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ilipigia kelele sana na kulaani mauaji ya raia yenye sura ya kisiasa. Tulisema mauaji haya yana sura ya kisiasa kwa sababu waliouwawa ni viongozi wa Vyama vya Siasa vya Upinzani na mauaji hayo yalitokea vipindi vya chaguzi mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, itakumbukwa kwamba katika Uchaguzi mdogo wa Ubunge katika Jimbo la Igunga aliuwawa kiongozi wa CHADEMA aliyejulikana kwa jina la Mbwana Masoud na pia aliyekuwa Mwenyekiti wa CHADEMA Kata ya Usa River, Msafiri Mbwambo, naye aliuwawa kwa kukatwa shingo na watu wasiojulikana mara baada ya Uchaguzi Mdogo wa Ubunge katika Jimbo la Arumeru Mashariki na watu hao walikamatwa lakini baadaye waliweza kukamatwa wakiwa na pingu katikati ya Maaskari. Itakumbukwa pia kwamba Wabunge wa CHADEMA, Mheshimiwa Highness Kiwia wa Jimbo la Ilemela na Mheshimiwa Salvatory Machelili wa Jimbo la Ukerewe, walinusurika kifo baada ya kujeruhiwa vibaya kwa mapanga na watu wanaosadikiwa kutumwa na viongozi wa CCM Mkoani Mwanza. Pia Mheshimiwa Rose Kamili ambaye mpaka sasa yuko kwenye matibabu alipigwa vibaya huko Iringa wakati wa Uchaguzi wa Kalenga. Inasikitisha kwamba shambulio hilo dhidi ya Wabunge hao lilitokea mbele ya Maafisa wa Polisi ambao hawakusaidia chochote.

Mheshimiwa Naibu Spika nimelazimika kukumbusha masuala haya ili Serikali ijipange vizuri na kuliagiza Jeshi la Polisi kuwalinda raia, wafuasi wa vyama vya siasa, wagombea wa nafasi mbalimbali za uongozi kwa haki na usawa hasa katika kipindi hiki ambapo taifa linaelekea kwenye Uchaguzi Mkuu. Endapo Jeshi la Polisi litaendelea kutumika kisiasa na kuwaacha “green guards” wa CCM kufanya fujo kwenye mikutano ya kampeni ya Vyama vya Upinzani, basi Vyama vya Upinzani vitalazimika kuchukua jukumu la kujilinda vyenyewe na uwezo huo tunao. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya vyama vya siasa vinavyounda UKAWA, napenda kutoa tahadhari kwa CCM kwamba, endapo wamepanga njama zozote zile kuhujumu Vyama vya Upinzani na UKAWA katika Uchaguzi Mkuu wa Okotoba, 2015, njama hizo zitadhibitiwa ipasavyo.

Napenda kuwahakikishia CCM kwamba, upinzani wa sasa hivi una nguvu kuliko wakati mwingine wowote, hivyo wasijaribu kupanga hujuma yoyote dhidi ya wizi wa kura kwani hujuma hizo zitawafanya kuwa wafungwa watarajiwa. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho. Kwa kuwa taifa linaelekea kwenye Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani na kwa kuwa kipindi cha uchaguzi ni kipindi ambacho amani ya nchi yetu inatakiwa kulindwa kwa nguvu zaidi kuliko vipindi vingine, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapenda kutoa angalizo kwa Serikali kuhusu mambo mawili muhimu ili kunusuru amani ya nchi yetu kuelekea Uchaguzi Mkuu. Masuala hayo ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kutochezea haki ya mwananchi kujiandikisha kuwa mpiga kura. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inarudia na kusisitiza tena kwamba, mzaha katika jambo hili hautavumilika kwani haki haiombwi, inadaiwa.

Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatoa rai kwa wananchi wote kujitokeza kwa wingi kujiandikisha katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura ili waweze kuamua nani atakuwa kiongozi wao kwenye Uchaguzi Mkuu wa Oktoba, 2015. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inamkumbusha kila mwananchi atambue kwamba, *"Kura yako ni maisha yako, nenda kajandikishe sasa."* (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kutofanya mzaha na uwepo wa Tume Huru ya Uchaguzi. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatambua makundi makubwa na mgogoro mkubwa mlio nao ndani ya chama chenu, hivyo tunarudia tena kuionya Serikali kutofanya mzaha na jambo la Tume Huru ya Uchaguzi kwani, linaweza kuingiza nchi katika machafuko makubwa.

Tunapenda kurudia tena rai yetu kwa Serikali: *"Tunataka Tume Huru ya Uchaguzi, si kwa sababu tunataka kushinda uchaguzi bali ni kwa sababu tunataka kulinda imani ya mpiga kura ili kulinda amani ya nchi yetu"*.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba sasa niwaonye kwamba, kwenye uandikishaji unaoendelea nchi nzima ni vyema daftari hili likaenda kwa ufasaha. Hii biashara ya kuruka vitongoji, vijiji na kata ili muonekane mme-cover maeneo yote itaweza kuleta shida. Nisingependa baada ya Serikali yenu kutoka madarakani mje muiwe wafungwa watarajiwa.

Ningependa muwe raia wazuri tutakaowahudumia vizuri kama wastaafu. Hili jambo ambalo mnafanya nalo mizaha, mnapeleka BVR mahali kisirisiri linaweza likaleta shida kubwa sana. Tanzania ya sasa, siyo Tanzania ya jana.

Ndiyo maana hata watu wenye ulemavu wameweza kugoma na kuonesha kwamba wako tayari kwa mabadiliko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana na Mungu akubariki, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

HOTUBA YA MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KATIKA WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI, MHE. GODBLESS JONATHAN LEMA (MB), AKIWASILISHA BUNGENI MAONI YA KAMBI YA UPINZANI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA YA WIZARA HIYO, KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

Inatolewa chini ya Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, toleo la Aprili, 2013.

1. UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, kwa maslahi ya umma wa Watanzania na watu wa Arusha, napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuwepo hapa leo, kuwasilisha maoni na mapendekezo ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya fedha katika Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka wa fedha 2015/2016

Mheshimiwa Spika, familia yangu inatambua kwamba kuwa Mbunge wa Upinzani katika Taifa linalopuuzwa utu, demokrasia na haki ni adha kubwa kutokana na kuzungukwa na mazingira yaliyojaa vitisho, kejeli, mateso, matusi na kupandikiziwa hofu. Hata hivyo napenda kumshukuru Mke wangu, kwa kuwa amekuwa msaada mkubwa sana kwangu katika dua, sala na maombi na hivyo kuifanya kazi hii kuwa ya thamani na nyepesi kwangu. Napenda pia kuwapongeza wanangu Allbless na Terrence kwa ucheshi wao unaoifanya familia nzima kuwa na furaha wakati wote.

Mheshimiwa Spika, leo hii natoa pia shukurani zangu za dhati kabisa kwa Wakurugenzi wa Arusha Development Foundation (ArDF) kwani ni jana tu, tarehe 21 Mei 2015 ambapo tumeweza kusaini Mkataba wa kuanza Ujenzi wa Hospitali ya Mama na Mtoto pamoja na Chuo cha Wakunga huko Burka Jijini Arusha. Namshukuru pia Dkt. Alex Browning pamoja na timu yake yote kwa nia ya dhati kabisa ya kukubali na kutafuta fedha ambazo amekwisha zipata kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Mama na Mtoto katika Nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, namshukuru pia rafiki yangu, hayati Wakili Nyaga Mawalla kwa mchango wake wa kutoa eneo la ujenzi wa hospitali hiyo. Alikuwa mtu mwema na mwenye kupenda watu na maendeleo, leo hatuko naye

wakati kazi hii njema inaanza, lakini mchango wake hautasaulika kwetu Sisi na Jamii ya watu wa Arusha na Tanzania, hususan kwa Afya ya Mama na Mtoto.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kutoa shukrani zangu za dhati kwa wapiga kura wangu wa Jimbo la Arusha Mjini. Ninajua na wanajua kuwa mwaka huu kutakuwa na Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani. Ushindi kwetu ni jambo la kutafakari na uamuzi tumeshafanya tujiandikishe kwa wingi daftari litakapokuja hivi karibuni ili kuthibitisha ushindi usio na hofu. Tumepewa fursa ya mabadiliko kwa kujiandikisha na tutumie wajibu wetu kushawishi ndugu zetu popote walipo ndani ya nchi yetu kujua umuhimu wa jambo hili la uandikishaji kwa ajili ya kuiondo CCM madarakani.

Mheshimiwa Spika, Kwa kuzingatia maudhui ya methali isemayo **‘Sikio la kufa Halisikii Dawa’**, na kwa kuzingatia uhalisia wenyewe kwamba Serikali hii ya awamu ya nne inamaliza muda wake; Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kipindi hiki haitatoa tena ushauri kwa kuwa Serikali hii haitakuwepo madarakani tena kuutekeleza ushauri huo, na badala yake tutaonesha jinsi ambavyo Serikali hii ya CCM imeshindwa kutekeleza majukumu yaliyopo chini ya Wizara hii kwa muda wote wa miaka 53 ya Uhuru iliyokaa madarakani; na kutoa mwelekeo wa nchi na masuala muhimu yatakayotekelezwa na Serikali mpya inayotokana na Upinzani baada ya ushindi wa kishindo katika uchaguzi Mkuu wa Oktoba mwaka huu wa 2015.

2. HALI YA USALAMA NA AMANI YA NCHI YETU

2.1. Uchochezi wa Kidini na Kikabila

Mheshimiwa Spika, kwa mihula yote miwili ya Utawala wa Serikali hii ya awamu ya nne, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imekuwa ikikemea tabia mbaya na hatari kwa mustakabali wa amani ya nchi ya uchochezi wa kidini na kikabila unaofanywa kwa makusudi na viongozi wa CCM kwa maslahi yao ya kisiasa.

Mheshimiwa Spika, Tatizo la Udini na ukabila limeendelea kuwa hatari kwa ustawi wa amani ya nchi yetu, na hili ni janga kubwa ambalo linaratibiwa na Chama tawala na washirika wake kwa maslahi ya kisiasa. Hivi karibuni tumeshuhudia Siasa chafu za rushwa, ukabila na udini zikiibuka nyakati hizi za Uchaguzi. Kwa Arusha Mjini, siasa hizi za ukabila zinafanywa na zinaendelea kufanywa na baadhi ya makada wa CCM.

Mheshimiwa Spika, wakati uchochezi huu wa kidini na kikabila unafanyika, Usalama wa Taifa wanajua, Polisi wanajua lakini hawachukui hatua yoyote. Nadhani wanafikiri kwamba ni mkakati mzuri wa ushindi kwa CCM lakini kumbe ni mkakati unao hatarisha hali ya usalama na amani nchini. Ninawataka hao wanaofanya vikao kwenye mazizi ya ng'ombe kwa misingi ya kikabila na

kupanga mikakati ya kutoa rushwa ili kushinda Ubunge katika Jimbo wa Arusha kuacha mara moja kufanya hivyo kwani Arusha itaendelea kuhitaji Mbunge mkakamavu na sio Kiongozi wa Ukozi.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwaahdi wapiga kura wangu wa Arusha Mjini kwamba Chama changu na Mimi mwenyewe hatuta fanya Siasa za rushwa za kuwanunua wapiga kura. Hii ni kwa sababu tunatafuta uhuru kamili wa nchi hii, hivyo hatuwezi kujadili bei ya UTU wa mwanadamu.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana nileleza katika hotuba yangu kwamba *“tatizo la udini na ukabila katika taifa hili linaonekana kuendelea kukomaa, na ni tatizo ambalo halitamwacha hata mmoja wetu salama. Ni tatizo ambalo hakuna mshindi atakayepatikana. Ni tatizo ambalo hata kama litaisambaratisha nchi, hata wale watakaofanikiwa kuikimbia nchi hawatakuwa salama huko wanakokwenda kwa sababu watakuwa bado na imani zao na chuki hiyo dhidi imani nyingine itaendelea popote watakapokuwa”*.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hatari inayoweza kutokana na uchochezi wa kidini na kikabila, Kambi Rasmi ya Upinzani iliitaka Serikali kutafakari upya na kuleta sheria mpya itakayokatiza na kuwawajibisha kwa nguvu zote wale wote watakaribu hata kwa maneno kueneza chuki au ubaguzi dhidi ya dini, kabila au rangi. Lakini mpaka sasa jambo hilo halijafanyika. Kambi Rasmi ya Upinzani inapenda kwa mara nyingine tena kutoa angalizo kwa Serikali kuchukua hatua za dharura za kukabiliana na athari zinazoweza kutokea kutokana na uchochezi wa kidini na kikabila hasa tunapoelekea katika Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani.

2.2. Ajali za Barabarani na Usalama wa Wasafiri

Mheshimiwa Spika, katika miaka yote kumi ya utawala wa awamu ya nne ya Serikali hii ya CCM; Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imekuwa ikiitaka Serikali kuchukua hatua madhubuti za kupunguza matukio ya ajali barabarani ambayo yamepoteza maisha ya wananchi wengi na kuacha wengine wakiwa walemavu. Jambo la kushangaza na kusikitisha ni kwamba; kadiri tunavyoipa Serikali ushauri mzuri ndivyo inavyozidi kuzembea na ajali zinazidi kuongezeka.

Mheshimiwa Spika, nasema hivi kwa sababu kwa kipindi cha Januari hadi Aprili mwaka huu wa 2015 ambao kimsingi ndio mwaka wa mwisho wa uhudumu wa Serikali hii ya awamu ya nne, ndio vifo vingi vimetokea kutokana na ajali za barabarani kuliko miaka ya nyuma. Kwa mujibu wa Taarifa ya Kamanda wa Kikosi cha Usalama Barabarani Kamishna wa Polisi Mohamed Mpinga, *“Kuanzia Januari zimetokea ajali 823 vifo 273 majeruhi 876, mwezi Februari zimetokea ajali 641, vifo 236 majeruhi 726 na Machi zimetokea ajali 652, vifo 357 na majeruhi 761”*

Mheshimiwa Spika, Kama usafiri wa reli ungeboreshwa na kuwa wa uhakika, na kama pia usafiri wa anga ungeboreshwa kwa kuwa na ndege nyingi na hivyo kufanya gharama za usafiri wa anga kupungua na hivyo kumwezesha mwananchi wa kawaida kuzimudu basi ingesaidia sana kupunguza matumizi ya barabara kwa mabasi ya abiria na malori ambayo kimsingi ndiyo yanaongoza kwa ajali za barabarani. Barabara zingetumika tu kwa magari binafsi na ajali za barabarani zingepungua. Lakini ni aibu kwa taifa kwamba Nchi yenye rasilimali nyingi kama Tanzania bado kusafiri kwa ndege tunaambiwa ni ndoto kama kauli mbiu ya Fast jet inavyosema *“Flying your dream”*

Mheshimiwa Spika, Polisi wamekuwa wepesi kuwatupia madereva lawama kuwa ni wazembe kila inapotokea ajali. Lakini wanasahau kuwa ajali nyingine zinatokea kutokana na miundo mbinu mibovu, na pia ajali nyingine zinasababishwa na polisi wa usalama barabarani wenyewe kwa kupokea rushwa na kuyaruhusu magari mabovu kuendelea na safari. Aidha, utaratibu wa sasa wa kumtaka askari wa usalama barabarani kukamata makosa yasiyopungua thelathini kwa siku na kuyaandikia “notification” na kukusanya faini ya shilingi 30,000/= kwa kila kosa kumekifanya kikosi cha usalama barabarani kuwa kama kitengo cha TRA kwa kukusanya mapato. Inasikitisha kusikia Jeshi la polisi likisifiwa kwa ukusanyaji wa mapato bila kujali athari zilizotokea baada ya ukusanyaji wa mapato hayo.

Mheshimiwa Spika, hatutaweza kuondoa ajali barabarani kwa kuongeza faini, isipokuwa kwa kuboresha miundombinu mingine ya usafirishaji kama vile reli na usafiri wa anga ili kupunguza matumizi ya barabara.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapenda kuwaahidi wananchi kwamba endapo Upinzani utaunda Serikali baada ya Uchaguzi wa Oktoba mwaka huu, suala la usalama barabarani litakuwa ni mojawapo ya vipaumbele vya kazi za Serikali kwa kuwa watanzania wamechoka kusikia habari za mauti na ulemavu unaosababishwa na matumizi mabaya ya barabara. Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inawasihi Wananchi wote kuwa makini na matumizi ya barabara hasa wale waendesha boda boda, kwani matumizi barabara yasiozingatia sheria za barabarani yanayofanywa na wananchi ni chanzo kikubwa cha ajali barabarani pia.

3. UKOMESHAJI WA MATUMIZI NA BIASHARA HARAMU YA DAWA ZA KULEVYA NCHINI

Mheshimiwa Spika, kwa miaka yote kumi ya utawala wa Serikali hii ya CCM, Kambi Rasmi ya Upinzani ilipiga sana kelele kuhusu wimbi kubwa la matumizi na biashara haramu ya dawa za kulevya nchini lilivyokuwa linazidi

kuangamiza nguvu kazi ya taifa. Licha ya Serikali hii ya CCM kupitia Rais Jakaya Kikwete kukiri kwamba inawafahamu kwa majina wanaohusika na biashara hiyo, bado hakuna hatua za wazi zilizochukuliwa dhidi ya wahusika hao.

Mheshimiwa Spika, Serikali hii ya CCM inaweza kujitetea kwamba ina mkakati wa kukomesha biashara haramu ya dawa za kulevya na ndio maana ikaleta Bungeni Muswada wa Sheria ya Udhhibiti na Usimamizi wa Dawa za Kulevya ya mwaka 2014 uliojadiliwa na kupitishwa na Bunge katika Mkutano wa Bunge uliopita. Lakini katika maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu muswada wa sheria hiyo tulionesha jinsi ambavyo sheria hiyo haiwezi kudhibiti biashara haramu ya dawa za kulevya: Sababu za kusema hivyo zilikuwa ni kama ifuatavyo: nanukuu:

1. *Adhabu kali sana zilizotajwa katika muswada huu, zinaweza kuvutia mazingira ya rushwa hususan katika vyombo vilivyopewa mamlaka ya upekuzi na ukamataji wa watuhumiwa wa dawa za kulevya na pia katika mahakama zetu.*

Mheshimiwa Spika, ni vema kutambua kwamba biashara hii ya dawa za kulevya ni biashara ya fedha nyingi na mara nyingi wahusika ni matajiri. Hivyo ikiwa mtuhumiwa amekamatwa; na kwa mujibu wa makosa yake anajua kwamba anakabiliwa na kifungo cha miaka 30 gerezani au faini ya shilingi milioni 200, yuko radhi kutoa hata milioni 50 kwa afisa aliyemkamata ili asimfikishe kwenye vyombo vya sheria. Na kwa jinsi hali ya maisha ya watumishi wa umma ilivyo duni, ni jaribu kubwa sana kwa afisa mkamataji kukataa shilingi milioni 50 aliyopewa kama rushwa ili asimfikishe mtuhumiwa mahakamani.

2. *Katika mazingira ya rushwa vilevile, mahakimu wanaweza kutoa adhabu za faini pekee bila kifungo kwa watuhumiwa wa dawa za kulevya watakaopatikana na hatia chini vya masharti ya sheria inayopendekezwa, jambo ambalo linaweza kusababisha biashara ya dawa za kulevya kuendelea kushamiri na kukomaa hapa nchini. Hii ni kwa sababu wafanya biashara wa dawa za kulevya wana uwezo wa kifedha wa kulipa faini hizo bila ugumu wowote.*

3. *Kuendelea kutoza faini kwa mtu anayepatikana na hatia ya kujihusisha na dawa za kulevya, ni sawa na kuhalalisha biashara hiyo kwani ni sawa na mfanya biashara kulipia kodi au ushuru wa biashara yake.*

4. *Serikali kukubali kupokea faini na kumwachia mtu aliyepatikana na hatia ya kujishughulisha na baiashara ya dawa za kulevya, haina tofauti na kupokea rushwa (iliyogeuzwa jina na kuitwa faini) ili kumwachia mfanyabiashara wa dawa za kulevya kuendelea kuangamiza kizazi cha taifa hili.*

Mheshimiwa Spika,

Kambi Rasmi ya Upinzani iliendelea kuonesha wasiwasi wake juu ya uwezo wa sheria hiyo, kukomesha biashara ya dawa za kulevya hapa nchini kwa sababu Tanzania ilikuwa na Sheria ya Kuzuia Biashara Haramu ya Dawa za Kulevya ya Mwaka 1995, tumekuwa na Tume ya Kudhibiti Dawa za Kulevya chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, tumekuwa na Polisi miaka yote lakini viwango vya uingizaji na usafirishaji wa dawa za kulevya vimekuwa vikiongezeka. Kwa uhalisia huu ni dhahiri kwamba; tatizo sio sheria bali ni kukosekana kwa utashi wa Serikali kushughulikia jambo hilo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali hii ya CCM ya awamu ya nne imeshindwa kukomesha matumizi na biashara haramu ya dawa za kulevya, na kwa kuwa imejulikana sasa kuwa Serikali haina Mpango Kabambe wa kukomesha biashara haramu ya dawa za kulevya hapa nchini, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inawaahidi wananchi kwamba; endapo vyama vya upinzani vitafanikiwa kushinda Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 2015 na kuunda Serikali, vita dhidi ya matumizi na biashara haramu ya dawa za kulevya nchini itakuwa ni kipaumbele katika kazi za Serikali.

4. UUNDWAJI WA TUME YA UCHUNGUZI WA KIMAHAKAMA (THE JUDICIAL INQUEST COMMISSION) KUCHUNGUZA MAUAJI YA RAIA YALIYOFANYWA NA VYOMBO VYA DOLA

Mheshimiwa Spika, kwa miaka yote kumi ya utawala wa Serikali hii ya awamu ya nne, Kambi Rasmi ya Upinzani ilikuwa ikipiga kelele na kulaani sana mauaji ya raia wasio na hatia yanayofanywa na vyombo vya dola hususan Jeshi la Polisi.

Mheshimiwa Spika Kambi rasmi ya Upinzani Bungeni, iliitaka Serikali kuunda Tume ya Uchunguzi wa Kimahakama au kwa lugha nyingine Mahakama ya Korona kwa ajili ya kuchunguza vifo vinavyotokana na mateso yanayofanywa na jeshi la Polisi, kwa mujibu wa sheria ya kuchunguza vifo vyenye utata (*The Inquest Act*) lakini mpaka sasa hivi Serikali haijafanya hivyo licha ya Waziri Mkuu kuahidi hapa Bungeni mara kadhaa kwamba Serikali ingeunda tume hiyo.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kutambua kwamba kumwaga damu isiyo na hatia katika nchi ni laana katika nchi. Hivyo, Serikali iliepushe taifa na laana kwa kuzuia umwagaji damu ya watu wasio na hatia.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali hii ya CCM haioni umuhimu wa kuunda Tume ya Kimahakama, Kambi Rasmi ya Upinzani inapenda kuwahakikishia wananchi wote kwamba; endapo upinzani utashinda na

kutwaa madaraka ya dola, utakuwa ndio mwisho wa uonevu unaofanywa na vyombo vya dola dhidi ya raia na zaidi sana hakutakuwa na ya damu ya raia wa nchi hii itakayopotea bure kwa sababu ya uonevu. Hata hivyo tunawapa pole wote ambao ndugu zao wamefikwa na mauti na kwamba huzuni yao na uchungu wao unapewa thamani na Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni.

5. UBORESHAJI WA BAJETI YA JESHI LA ZIMA MOTO NA UOKOAJI

Mheshimiwa Spika, katika hotuba zote za Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu bajeti ya Wizara hii, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imekuwa ikiitaka Serikali kuongeza fedha za miradi ya maendeleo katika wizara hii kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya zima moto na uokoaji kwa Jeshi la Zima Moto na Uokoaji lakini Serikali haijatilika maanani suala hili.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba yetu ya mwaka jana tulieleza; na ninakukuu: *“Kwa mujibu wa Randama ya Jeshi la Zimamoto, fungu 14 (uk. 2) katika kipindi cha mwaka wa fedha 2013/14 hakuna fedha yoyote iliyotengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo kwa Jeshi la Zima Moto.*

Mheshimiwa Spika,

Kwa mujibu wa Randama hiyo, huu ni mwaka wa tatu mfululizo kwa Jeshi la Zima Moto na Uokoaji kutotengewa fedha kwa ajili ya miradi ya Maendeleo. Kutokana na hali hiyo, Jeshi hilo limeshindwa kuendeleza ujenzi wa jengo la Ofisi ya Makao Makuu – TAZARA, Dar es Salaam, kushindwa kukarabati na kujenga vituo vipya vya zimamoto, kushindwa kununua vitendea kazi mbalimbali ikiwemo vifaa vya maokozi na vifaa vya kuzimia moto.

Mheshimiwa Spika,

Sote ni mashahidi wa majanga ya moto, maghorofa kuporomoka, meli kuzama, mafuriko na kila aina ya majanga ambapo idara ya zima moto imekuwa ikishindwa kufanya chochote na hivyo kuwaacha wananchi wakiangamia katika majanga hayo. Kambi Rasmi ya Upinzani inashawishika kuamini kwamba Serikali haina nia njema na usalama wa raia na ndio maana haitengi fedha hata senti moja katika miradi ya maendeleo ya Jeshi la Zima Moto. Kama Serikali haioni umuhimu wa Jeshi la Zima Moto ni bora kulifuta kuliko kuliacha wakati hailiwezeshi kufanya kazi yake”.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaungana na wananchi wote waliopata madhila kutokana na majanga mbalimbali ambapo Jeshi la Zima Moto na Uokoaji lilishindwa kuwapatia msaada kutokana na kukosa vifaa vya kutendea kazi. Aidha, tunawaahidi wananchi kwamba endapo tutaingia madarakani, bajeti ya Jeshi la Zima Moto na Uokoaji itaboreshwa ili Jeshi hilo liweze kufanya kazi kwa ufanisi ili kuwaokoa wananchi wakati wa majanga.

5. HATIMA YA VITAMBULISHO VYA TAIFA

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ikiitaka Serikali kutoa ukomo wa muda, ambapo kila raia wa Tanzania atapatiwa Kitambulisho chake cha Taifa na kuainisha gharama zilizotumika katika mchakato mzima wa kutengeneza vitambulisho vya Taifa.

Mheshimiwa Spika, inasikitisha sana kuona kwamba tangu mchakato huo uanze, Serikali haitoi mrejesho wa namna zoezi hilo linavyoendelea, ni wananchi wangapi wameshapata vitambulisho hivyo, ni lini kila raia wa Tanzania atakuwa amepatiwa kitambulisho chake cha Taifa, na ni fedha kiasi gani zimetumika hadi sasa katika mchakato huo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa serikali hii ya awamu ya nne inaondoka madarakani kabla haijakamilisha mchakato wa kuwapatia wananchi wote vitambulisho vya taifa, na kwa kuwa fedha nyingi za walipa kodi zimetumika kuanzisha mchakato huo, Kambi Rasmi ya Upinzani inapenda kuwaahidi wananchi kwamba tutakapoingia madarakani katika uchaguzi mkuu wa Oktoba, 2015 na kuingia madarakani, zoezi hilo litakamilishwa ndani ya kipindi cha mwaka mmoja.

6. MABORESHO YA MAZINGIRA NA AFYA ZA MAHABUSU NA WAFUNGWA MAGEREZANI

Mheshimiwa Spika, kwa miaka yote ya utawala wa Serikali ya awamu ya nne, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imekuwa ikiitaka Serikali kuchukua hatua ya kupunguza msongamano wa wafungwa na mahabusu Magerezaji sambamba na kuboresha lishe na huduma za afya kwa Wafungwa na Mahabusu.

Mheshimiwa Spika, licha ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuishauri Serikali mara zote hizo, msongamano wa wafungwa na mahabusu magerezani umeendelea kuwa ni tatizo, hali kadhalika huduma za afya na lishe kwa mahabusu na wafungwa zimeendelea kuwa duni.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali hii imeshindwa kupunguza msongamano wa mahabusu na wafungwa magerezani kwa kubuni adhabu mbadala za nje kwa makosa madogomadogo badala ya vifungo, na kwa kuwa Serikali hii imeshindwa pia kufanya upelelezi wa kesi zinazowakabili watuhumiwa wa makosa mbalimbali kwa wakati na hivyo kusababisha msongamano wa mahabusu magerezani ambapo hawazalishi chochote isipokuwa wanaitia hasara Serikali kwa kula bila kufanya kazi, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapenda kuwaahidi wananchi wote kwamba, endapo Upinzani utaingia madarakani msongamano wa wafungwa na mahabusu magerezani utapunguzwa kwa kutoa adhabu mbadala ya vifungo vya nje kwa

makosa madogo madogo, na kukamilisha upelelezi za kesi mbalimbali kwa wakati ili pia kupunguza msongamano wa mahabusu.

Mheshimiwa Spika, Kambi rasmi ya Upinzani Bungeni pia inalitaka Jeshi la Polisi kuwa linakamata na kuwatia Watu mahabusu wakati uchunguzi wa kina ukiwa umeshafanyika tofauti na sasa ambapo mtu anayehisiwa tu kuwa ni mhalifu anaweza kuwekwa mahabusu na kukaa huko hadi miaka zaidi ya mitano na baadae kuambiwa kuwa hana hatia, huu ni uvunjaji wa haki za Binadamu.

7. UBORESHAJI WA MAZINGIRA YA KAZI KWA ASKARI MAGEREZA.

Mheshimiwa Spika, kwa mihula yote miwili ya utawala wa Serikali hii ya awamu ya nne, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imekuwa ikiitaka Serikali kujenga nyumba za Askari wa Magereza ili kuboresha mazingira yao ya kazi. Aidha, Kambi Rasmi ya iliitaka Serikali hii kuondoa urasimu na utaratibu kandamizi katika Jeshi la Magereza kuhusu Mpango wa kujiendeleza kielimu kwa maafisa wa Magereza ambapo utaratibu huo ulikuwa unakwenda kinyume na General Service Order (GSO) na sheria nyingine za kazi.

Mheshimiwa Spika, tatizo la msingi kuhusu kujiendeleza kielimu kwa maafisa wa magereza lilikuwa ni muda wa kisheria wa miaka miwili ya kukaa kwenye kituo cha kazi baada ya kuajiriwa kwa mara ya kwanza (first appointment) kabla ya kuomba rufusa ya kujiendeleza kimasomo kukiukwa na badala yake waombaji wa nafasi za kujiendeleza kielimu kutakiwa kukaa kwenye kituo cha kazi hadi miaka sita ndipo waruhusiwe kujiendeleza kielimu.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaamini kwamba mazingira bora ya kazi, na maendeleo ya rasilimali watu ni nyenzo muhimu ya utendaji kazi kwa ufanisi si kwa Jeshi la Magereza tu bali kwa sekta na taasisi mbalimbali za Serikali zinazojali weledi na tija kwa watumishi wake. Kwa minajili hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inapenda kuwaahidi askari Magereza kwamba iko nao bega kwa bega kukabiliana na changamoto zinazowakabili, na kwa maana hiyo iwapo upinzani utachukua madaraka ya nchi, sera ya maendeleo ya rasilimali watu kwa askari wa Jeshi la Polisi itaboreshwa ili kutoa fursa nyingi zaidi za kujiendeleza kielimu kwa maafisa wa Jeshi la Polisi na Magereza, na halikadhalika mazingira ya kazi kwa Askari wa Jeshi la Polisi na Magereza ikiwa ni pamoja na kuwajengea nyumba nzuri zenye staha yataboreshwa.

8. MABORESHO YA POSHO YA CHAKULA (RATION ALLOWANCE) KWA JESHI LA POLISI

Mheshimiwa Spika, kufuatia ugumu wa maisha ya Askari wetu wa Jeshi la Polisi, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, kwa miaka yote ya utawala wa Serikali ya awamu ya nne, imekuwa ikiitaka Serikali, **kuongeza** posho ya chakula (Ration allowance) kwa askari wa Jeshi la Polisi ili walau posho hiyo ishabihiane na posho ya Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) ili waweze kukabiliana na ugumu wa maisha. Kwa mujibu wa kumbukumbu rasmi za bunge (hansard) Waziri wa Fedha wa wakati huo Marehemu William Mgimwa alikubali posho ya chakula ya shilingi 225,000/= kwa mwezi sawa na shilingi 7,500/= kwa siku kwa kila askari. Taarifa tulizo nazo ni kwamba posho hiyo haijalipwa mpaka leo, licha ya Serikali kuahidi kuwalipa posho hiyo.

Mheshimiwa Spika, katika mazingira kama haya ambapo Serikali inahidi ndani ya Bunge hili kupandisha posho za chakula za askari Polisi halafu haitekelezi, inataka tuishauri nini tena?

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa hoja ya kupandisha "*ration allowance*" kwa askari wetu wa Jeshi la Polisi ilianzishwa na Kambi ya Upinzani, na kwa kuwa kwa miaka yote ya utawala wa Serikali ya awamu ya nne Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imekuwa ikiwatetea askari wa Jeshi la Polisi ili walipwe posho ya chakula ya shilingi 7,500/= kwa siku kwa kila askari; na kwa kuwa kwa mihula yote miwili ya utawala wa Serikali ya awamu ya nne, Serikali imeshindwa kutekeleza ahdadi yake yenyewe iliyoitoa hapa Bungeni kwamba ingepandisha posho hiyo, hivyo basi Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapenda kuchukua nafasi hii kuwahidi Askari wote waliopo chini ya Jeshi la Polisi kwamba endapo Upinzani utaunda Serikali baada ya ushindi katika uchaguzi mkuu wa Oktoba, 2015, posho hiyo itapandishwa haraka iwezekanavyo kwa kuwa ni sera ya Upinzani kuboresha maslahi ya askari wa Jeshi la Polisi. Ili kutimiza azma hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inalitaka Jeshi la Polisi Nchini kukataa kutumika kiasiasa na Serikali ya CCM kuukandamiza upinzani na badala yake wafanye kwazi kwa kuzingatia sheria na taratibu zinazotumika kuongoza utendaji wa Jeshi hilo.

9. UDHIBITI WA FUJO NA MAUJAJI KUELEKEA UCHAGUZI MKUU WA 2015.

Mheshimiwa Spika, kwa miaka yote kumi ya utawala wa Serikali hii ya awamu ya nne, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ilipigia kelele sana na kulaani mauaji ya raia yenye sura ya kisiasa. Tulisema mauaji haya yana sura ya kisiasa kwa sababu waliouwawa ni viongozi wa vyama vya siasa vya Upinzani na mauaji hayo yalitokea vipindi vya chaguzi mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Itakumbukwa kwamba katika Uchaguzi mdogo wa Ubunge katika Jimbo la Igunga aliuwawa kiongozi wa CHADEMA aliyejulikana kwa jina la Mbwana Masoud, na pia aliyekuwa Mwenyekiti wa CHADEMA Kata ya Usa River, Msafiri Mbwambo, naye aliuwawa na watu wasiojulikana mara baada ya Uchaguzi Mdogo wa Ubunge katika Jimbo la Arumeru Mashariki.

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa pia kwamba wabunge wa CHADEMA, Mhe. Highness Kiwia wa Jimbo la Ilemela na Mhe. Salvatory Mchemuli wa Jimbo la Ukerewe walinusurika kifo baada ya kujeruhiwa vibaya kwa mapanga na watu wanaosakiwa kutumwa na viongozi wa CCM mkoani mwanza. Inasikitisha kwamba shambulio hilo dhidi ya wabunge hao lilitokea mbele ya maafisa wa polisi ambao hawakusaidia chochote.

Mheshimiwa Spika nimelazimika kukumbusha masuala haya ili Serikali ijipange vizuri na kuliagiza Jeshi la Polisi kuwalinda raia, wafuasi wa vyama vya siasa, wagombea wa nafasi mbalimbali za uongozi kwa haki na usawa hasa katika kipindi hiki ambapo taifa linaelekea kwenye Uchaguzi Mkuu. Endapo Jeshi la Polisi litaendelea kutumika kisiasa, na kuwaacha **“green guards”** wa CCM kufanya fujo kwenye mikutano ya kampeni ya vyama vya Upinzani, basi vyama vya Upinzani vitalazimika kuchukua jukumu la kujilinda vyenyewe.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya vyama vya siasa vinavyounda UKAWA, napenda kutoa tahadhari kwa CCM kwamba, endapo wamepanga njama zozote zile kuhujumu vyama vya UKAWA katika uchaguzi Mkuu wa Okotoba, 2015, njama hizo zitadhibitiwa ipasavyo. Napenda kuwahakikishia CCM kwamba Upinzani wa sasa hivi una nguvu kuliko wakati mwingine wowote, hivyo wasijaribu!!!

10. HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, Kwa kuwa taifa linaelekea kwenye Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani, na kwa kuwa kipindi cha uchaguzi ni kipindi ambacho amani ya nchi yetu inatakiwa kulindwa kwa nguvu zaidi kuliko vipindi vingine; Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapenda kutoa angalizo kwa Serikali kuhusu mambo mawili muhimu ili kunusuru amani ya nchi yetu kuelekea Uchaguzi Mkuu. Masuala hayo ni kama ifuatavyo:

i. Kutochezea Haki ya Mwananchi Kujiandikisha kuwa Mpiga Kura:

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inapenda kurudia na kusesitiza tena kwamba mzaha katika jambo hili hautavumilika kwani haki haiombwi, inadaiwa. Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatoa wito kwa wananchi wote kujitokeza kwa wingi kujiandikisha katika Daftari la Kudumu la Wapiga kura ili waweze kuamua nani atakuwa kiongozi wao kwenye uchaguzi

Mkuu wa Oktoba, 2015. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inamkumbusha kila mwananchi atambue kwamba **“Kura yako ni Maisha yako, Nenda Kajandikishe Sasa”**

ii. Kutofanya Mzaha na Uwepo wa Tume Huru ya Uchaguzi:

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inarudia tena kuionya Serikali kutofanya mzaha na jambo hili kwani linaweza kuiingiza nchi katika machafuko makubwa. Napenda kurudia tena rai yetu kwa Serikali: **“Tunataka Tume Huru ya Uchaguzi, si kwa sababu tunataka kushinda uchaguzi bali ni kwa sababu tunataka kulinda Imani ya Mpiga Kura ili kulinda amani ya nchi yetu”**.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha.

Godbless Jonathan Lema (Mb)

MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI NA WAZIRI KIVULI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI

Imesomwa leo, tarehe 22 Mei, 2015

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Godbless Lema, Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Sasa ninaomba nimuite Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kwa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Masoud na atatumia robo saa tu.

HOTUBA YA MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KATIKA WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA, MHE MASOUD ABDALLA SALIM (MB) AKIWASILISHA BUNGENI MAONI YA KAMBI YA UPINZANI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO, KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016 KAMA ILIVYOSOMWA BUNGENI

MHE. MASOUD ABDALLA SALIMU - MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA: Mheshimiwa Naibu Spika, ifuatayo ni hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2015/2016 ambayo inatolewa chini ya Kanuni ya 99 (9), ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Aprili, 2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuendelea kunijalia afya njema na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge hili Tukufu kutoa maoni ya Kambi Rasmi

ya Upinzani Bungeni kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka wa fedha 2015/2016.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwapongeza viongozi wote wa UKAWA nikianza na Mwenyekiti wa UKAWA, Mheshimiwa Freeman Aikaeli Mbowe, ambaye pia ni Kiongozi wa Upinzani Bungeni, Wenyeviti Wenza Waheshimiwa Prof. Ibrahim Lipumba (CUF), Dkt. Emmanuel Makaidi (NLD) na James Mbatia (NCCR – Mageuzi); Makatibu Wakuu wa vyama vinavyounda UKAWA, Waheshimiwa Maalim Seif Sharrif Hamad (CUF) ambaye pia ni Makamu wa Kwanza wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Katibu Mkuu wa CUF, Dkt. Wilbroad Slaa (CHADEMA), Mosena Nyambabe (NCCR – Mageuzi) na Tozi Matwange (NLD) kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kuwaunganisha Watanzania katika harakati za kuleta mabadilko ya kweli ya kisiasa kwa mustakabali mwema wa taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuwashukuru wapiga kura wangu wa Jimbo la Mtambile kwa kuendelea kuniamini na kunipa ushirikiano. Kwao wote nasema ahsanteni sana na Mwenyezi Mungu awabariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa masuala yote yanayohusu utendaji wa Wizara hii yanategemea sana Mwongozo wa Sera na Sheria ya Ulinzi wa Taifa na kwa kuwa Sera na Sheria ya Ulinzi wa Taifa ni ya zamani tangu mwaka 1966 hivyo imepitwa na wakati na kwa kuwa tangu mwaka 2008 Serikali iliahidi kuiboresha Sera na Sheria ya Ulinzi ili iendane na wakati, hivyo basi Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka kujua ni lini mchakato wa kuboresha Sera na Sheria ya Ulinzi utamalizika?

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Kujenga Taifa na ajira kwa vijana wanaohitimu mafunzo ya JKT. Kwa miaka yote kumi ya utawala wa Awamu ya Nne ya Serikali hii, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imekuwa ikiishauri Serikali kuwaajiri vijana wanaojiunga na programu ya mafunzo ya JKT kwa hiari pindi wanapohitimu mafunzo hayo. Kwa kuwa tulifahamu kwamba ni vigumu sana vijana wote waliopata mafunzo ya JKT kupata ajira ya moja kwa moja katika Jeshi la Kujenga Taifa au katika taasisi nyingine za kijeshi, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni iliishauri Serikali kuanzisha Idara ya Mafunzo ya Ufundi ndani ya JKT itakayokuwa inaratibiwa na VETA ili vijana wanaojiunga na JKT wapatiwe mafunzo ya ufundi na wanapohitimu wapewe vyeti vya VETA, ili waweze kutumia vyeti hivyo kutafuta ajira katika sekta mbalimbali ikiwa watakosha ajira Jeshini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali hii ya CCM ilipuuza wazo hili zuri la Upinzani na matokeo yake ni kwamba vijana hao waliopatiwa mafunzo ya JKT na kukosa ajira wameanza kuwa tishio kwa Serikali. Ushahidi kwamba vijana

hao sasa ni tishio, ni maandamano yao yaliyofanyika mapema mwaka huu wakishinikiza kuonana na Rais kumweleza kilio chao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa hoja ya kuwaajiri vijana wanaopata mafunzo ya JKT ni hoja ya Upinzani na kwa kuwa kwa miaka yote kumi ya utawala wa Awamu ya Nne, Serikali hii ya CCM imeshindwa kutatua tatizo la ajira kwa vijana wanaohitimu mafunzo ya JKT, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapenda kuwaahidi wananchi kwamba endapo vyama vinayounda UKAWA vitashinda katika uchaguzi Mkuu wa Oktoba, 2015 *inshallah* na kuunda Serikali, utaoji wa ajira kwa vijana wanaohitimu mafunzo ya JKT utakuwa ni kipaumbele katika Serikali ya UKAWA. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, JKT na utunzaji wa mazingira. Kwa miaka yote kumi ya utawala wa Serikali hii ya Awamu ya Nne, Kambi Rasmi ya Upinzani imekuwa ikiishauri Serikali kutumia nguvu kazi iliyoko katika Jeshi la Kujenga Taifa katika utunzaji wa mazingira ili kukabiliana na mabadiliko ya Tabianchi ambayo yanafishia uhai na ustawi wa wananchi. Katika kufanikisha jambo hili, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ilitoa pendekezo kwa Jeshi la Kujenga Taifa kuendesha Operesheni Maalum ya kupanda miti nchi nzima kwa kushirikiana na wananchi. Aidha, tulipendekeza zoezi hilo lifanywe na vijana wanaojiunga na JKT kama sehemu ya mafunzo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, licha ya kurudia pendekezo hili mara nyingi, Serikali bado haijaonesha utayari wa kutekeleza pendekezo hili. Kwa sababu hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapenda kuwaahidi wananchi kwamba endapo upinzani utaingia madarakani *inshallah* 2015, nguvu iliyoko katika Jeshi la Kujenga Taifa itatumika ipasavyo katika utunzaji wa mazingira na katika miradi mbalimbali ya maendeleo. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, utunzaji wa silaha za milipuko. Kutokana na milipuko katika ghala za silaha iliyotokea katika Kambi za Jeshi za Mbagala na Gongo la Mboto, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ilipiga kelele sana na kuitaka Serikali kutofanya mzaha na masuala ya usalama katika Kambi za Jeshi kwa kisingizio kwamba fedha hazitoshi. Aidha, tuliikumbusha Serikali kwamba ni muhimu kujiweka tayari kukabiliana na maafa yote mara tu yatokeapo kwa kuwa maafa na ajali hutokea ghafla bila taarifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa randama ya Fungu 38 – Ngome, ukurasa wa 58), fedha ambazo ziliidhinishwa kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa maghala ya silaha kwa mwaka wa fedha 2012/2013 na 2014/2015 ni Sh.10,000,000,000 na fedha zinazoombwa kwa mwaka wa fedha 2015/2016 kwa kazi hiyo ni Sh.4,500,000,000. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kulieleza Bunge hili ni maghala mangapi mapya ya silaha yamejengwa na ni mangapi yamefanyiwa ukarabati.

Mheshimiwa Naibu Spika, maboresho ya hospitali za Jeshi. Mwaka jana Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni iliitaka Serikali kuongeza bajeti ya kuhudumia hospitali za Jeshi kutoka shilingi bilioni 2.4 zilizokuwa zimeidhinishwa na Bunge hadi kufikia shilingi bilioni 10 ili kufanya upanuzi na kuboresha huduma za utabibu katika hospitali za Jeshi hasa zile za Lugalo-Dar es Salaam na Bububu-Zanzibar kwa kuwa hospitali hizo zinatoa pia huduma kwa raia wa kawaida tena kwa takriban asilimia 80.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Fungu 38 (Ngome), ukurasa wa 54, fedha zinazoombwa kwa ajili ya kuhudumia hospitali za Jeshi ni shilingi bilioni 4.9 ikiwa ni sawa na ongezeko la shilingi bilioni 2.5. Hizi ni fedha zilizoidhinishwa, haijulikani kama zitatolewa zote kwa kuwa Serikali hii imekuwa hodari wa kutotekeleza bajeti inayoidhinishwa na Bunge. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni haina hakika kama kiasi cha shilingi bilioni 4.9 zinaweza kufanya upanuzi wa hospitali za Jeshi katika kanda mbalimbali sambamba na kufanya manunuzi ya madawa na vifaa tiba katika hospitali za Jeshi zilizopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, migogoro ya mipaka ya ardhi katika Jeshi la Wananchi. Ni ukweli usiopingika kwamba kuna baadhi migogoro ya mipaka ya ardhi kati ya maeneo ya Jeshi na maeneo ya makazi ya wananchi. Migogoro hii imesababisha uhasama na kudorora kwa mahusiano baina ya Wanajeshi na wananchi wanaoishi karibu na maeneo ya Jeshi. Aidha, migogoro hii imesababisha baadhi ya vikosi vya Jeshi kuwavunjia wananchi nyumba zao kwa madai kwamba wamejenga katika maeneo ya Jeshi. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni iliishauri Serikali katika miaka ya nyuma kutenga bajeti maalum kwa ajili ya kupitia upya mipaka ya Jeshi na wananchi katika maeneo yale yenye migogoro na kuiweka bayana ili wananchi watambue maeneo ya Jeshi na hivyo kutoyaingilia lakini mpaka sasa zoezi hilo halijafanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ipo migogoro mingine ya ardhi kati ya Jeshi na Wwananchi ambapo Jeshi ndilo linaingilia maeneo ya makazi ya watu. Kwa mfano, katika Wilaya ya Ilemela – Mwanza, Kikosi cha 601 cha JWTZ kimeingilia mitaa halali ya Lukobe na Buduku ambayo ni makazi ya wananchi na Jeshi lilikiri kwamba, liliingilia maeneo hayo kwa kuwa linayahitaji lakini hakuna mpango wowote wa kuwafidia wananchi uliofanyika. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuwafanyia tathmini wakazi wa mitaa hiyo ili walipwe fidia waweze kuondoka. Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuvielekeza vikosi mbalimbali vya Jeshi vyenye migogoro ya aina hiyo na wananchi kuwashirikisha wananchi endapo kuna utata wa mpaka ili wafikie suluhu kwa pamoja ili kudumisha ujirani mwema na mahusiano mazuri badala ya kuwavunjia wananchi nyumba, na kuwapiga bila kuwasikiliza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, madeni ya wazabuni wanaotoa huduma Jeshini. Katika mwaka wa fedha 2014/2015, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni

iliitaka Serikali kulipa madeni yote ya wazabuni wanaotoa huduma katika vikosi mbalimbali vya Jeshi. Kwa taarifa ambazo Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inazo, madeni hayo hayajalipwa na yamezidi kuongezeka jambo ambalo linasababisha wazabuni washindwe kuendelea kutoa huduma Jeshini. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kulieleza Bunge hili imelipa madeni hayo kwa kiasi gani na ina mkakati gani wa kutolimbikiza madeni kwa wazabuni?

Mheshimiwa Naibu Spika, wastaafu wa Jeshi la Wananchi. Kwa mihula yote miwili ya utawala wa Serikali hii ya Awamu ya Nne, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni iliitaka Serikali kuwajali wastaafu wa Jeshi la Wananchi kama sehemu ya kuenzi utumishi wao uliotukuka kwa taifa. Katika hotuba yangu kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2014/2015 nilielezea kwa kina suala hili na nanukuu:-

“Mheshimiwa Naibu Spika, maisha ya Wanajeshi wetu wastaafu yanasikitisha licha ya kulitumikia taifa hili kwa muda mrefu, kwa uadilifu na uzalendo mkubwa. Hata hivyo, hali zao za maisha zimekuwa duni, mbaya na kubakia ombaomba ambayo hailingani na utumishi wao walioufanya kwa uadilifu na uzalendo wa hali ya juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Serikali imewatelekeza Wanajeshi wastaafu na kuwaacha mitaani bila kujua ni kitu gani cha kufanya, tayari wameanzisha umoja wao unaojulikana kama Muungano wa Wanajeshi Wastaafu Tanzania (MUWAWATA).

Mheshimiwa Naibu Spika, Wanajeshi hawa wastaafu ni Jeshi la Akiba (Reserved Army). Kambi Rasmi ya Upinzani inahoji na kuitaka Serikali kutoa mkakati wa Serikali wa kuweza kuboresha maisha ya Wanajeshi wastaafu na hasa kwenye viwango vya pensheni kwa maafisa na askari wa kawaida toka Private hadi Brigedia General”.

Mheshimiwa Naibu Spika, imekuwa ni desturi kuwapa heshima kubwa na kutoa risala yenye maneno mazuri wakati wa mazishi yao lakini walipokuwa hai hawakusifiwa wala hawakupata haki zao stahili. Kwa mfano risala inasema kuwa Marehemu alikuwa hodari shupavu na jasiri, mwaminifu na mtiifu, yeye ni mfano wa kuigwa, atakumbukwa na atathaminiwa kwa kazi nzuri aliyoifanya. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, imekuwa ni desturi kuwapa heshima kubwa na kutoa risala yenye maneno mazuri wakati wa mazishi yao lakini walipokuwa hai hawakusifiwa wala hawakupata haki zao stahili. Kwa mfano, risala inasema kuwa Marehemu alikuwa hodari shupavu na jasiri, mwaminifu na mtiifu, yeye ni mfano wa kuigwa, atakumbukwa na atathaminiwa kwa kazi nzuri aliyoifanya.

Kambi Rasmi inahoji mbona sifa hizo haziendani na jinsi wanavyotendewa wakiwa hai? Je, Serikali ina mpango gani wa kutunza familia za marehemu waliotumikia Jeshi? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, mapitio ya utekelezaji wa bajeti ya 2014/2015 na uchambuzi wa makadirio ya matumizi ya fedha kwa mwaka 2015/2016. Kwa miaka yote kumi ya utawala wa Serikali ya Awamu ya Nne, kipindi hiki bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Kujenga Taifa imeandikwa vibaya na inakiuka misingi ya kibajeti kuliko miaka mingine ya fedha. Randama za Mafungu yote matatu yaani Fungu 57 (Wizara ya Ulinzi na JKT), Fungu 39 (JKT) na Fungu 38 (Ngome) hayaoneshi utekelezaji wa bajeti ya mwaka wa fedha 2014/2015. Kwa hiyo, haifahamiki ni fedha kiasi gani zilizotolewa na Hazina kwa ajili ya utekelezaji wa bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kwa mwaka huo hadi kufikia Machi, 2015 ili kuweza kukokotoa kiasi cha fedha ambacho bado hakijatolewa. Ukitazama makadirio ya fedha za miradi ya maendeleo katika randama ya Fungu 38 – Ngome yameandikwa kwa tarakimu kamili jambo linaloibua hisia kwamba yamebuniwa na kuandikwa tu bila kuwa na mchanganuo mahsusi. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kutoa maelezo mbele ya Bunge hili kwa nini haijatoa mrejesho wa utekelezaji wa bajeti ya 2014/2015 na kwa nini imekiuka *principles* za uandaaji wa bajeti kwa kuweka makadirio ya kubuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, naomba kuwasilisha na *ishallah* mwaka 2015 ni mwaka wa UKAWA, Mungu atubariki kuunda Serikali Mpya inayotarajiwa na Watanzania wote. Ninashukuru sana. (Makofi)

HOTUBA YA MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KATIKA WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA, MHE MASOUD ABDALLA SALIM (MB) AKIWASILISHA BUNGENI MAONI YA KAMBI YA UPINZANI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO, KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

Inatolewa chini ya Kanuni ya 99 (9), ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Aprili, 2013

1. UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, awalili ya yote napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuendelea kunijalia afya njema na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge hili kutoa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka wa fedha 2015/2016.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwapongeza viongozi wote wa UKAWA nikianza na Mwenyekiti wa UKAWA, Mhe. Freeman Aikaeli Mbowe (Mb) ambaye pia ni Kiongozi wa Upinzani Bungeni, Wenyeviti wenza Waheshimiwa Prof. Ibrahim Lipumba (CUF), Dr. Emmanuel Makaidi (NLD) na James Mbatia (NCCR – Mageuzi); Makatibu wakuu wa vyama vinavyounda UKAWA, Waheshimiwa Maalim Seif Sharrif Hamad (CUF) ambaye pia ni Makamu wa Kwanza wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zainzibar, Dr. Wilbroad Slaa(CHADEMA) , Mosena Nyambabe (NCCR – Mageuzi) na Tozi Matwange (NLD) kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kuwaunganisha wataanzania katika harakati za kuleta mabadiliko ya kweli ya kisiasa kwa mustakabali mwema wa tafa letu.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuwashukuru wapiga kura wangu wa Jimbo la Mtambile kwa kuendelea kuniamini na kunipa ushirikiano. Kwao wote nasema asanteni sana na Mwenyezi Mungu awabariki.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa masuala yote yanayohusu utendaji wa Wizara hii yanategemea sana mwongozo wa Sera na Sheria ya Ulinzi, na kwa kuwa Sheria na Sera ya Ulinzi ni ya tangu mwaka 1966 hivyo imepitwa na wakati, na kwa kuwa tangu mwaka 2008 Serikali iliahidi kuiboresha Sera na Sheria ya Ulinzi ili iendane na wakati, Hivyo basi Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka kujua ni lini mchakato wa kuboresha sera na sheria ya Ulinzi utamalizaka?

2. JESHI LA KUJENGA TAIFA (JKT)

Ajira kwa Vijana wanaohitimu Mafunzo ya JKT

Mheshimiwa Spika, kwa miaka yote kumi ya utawala wa awamu ya nne ya Serikali hii, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imekuwa ikiishauri Serikali kuwaajiri vijana wanaojiunga na programu ya mafunzo ya JKT kwa hiari pindi wanapohitimu mafunzo hayo.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni iliieleza Serikali kwamba mategemeo ya vijana hao wanapojiunga na JKTni kupata ajira pindi wamalizapo mafunzo. Aidha, tulitoa angalizo kwamba kuwapatia vijana hao mafunzo ya kijeshi ikiwa ni pamoja na kutumia silaha za moto, na hatimaye kuwaacha mtaani bila kazi ni hatari kwa usalama wa raia kwani wanaweza kujihusisha na vitendo vya kihalifu, na kwa kuwa wana mafunzo ya kijeshi ni vigumu kukabiliana nao.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa JKT peke yake haina uwezo wa kuwaajiri vijana wote wanaojiunga na Jeshi hilo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni iliitaka Serikali kutoa kipaumbele cha ajira kwa vijana hawa pindi inapotangaza nafasi za kazi katika jeshi la Polisi, Magereza, Uhamiaji na Jeshi la Wananchi – JWTZ. Tulishauri kwamba, wakati Serikali inajiri watumishi katika majeshi haya, basi

mtumishi aliyepitia JKT awe na sifa ya ziada (added advantage) ya kuajiriwa ili kutoa motisha kwa vijana wengi kujiunga na JKT kwa hiari na kupata mafunzo mbalimbali ikiwemo nidhamu na uzalendo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa tulifahamu kwamba ni vigumu vijana wote waliopata mafunzo ya JKT kupata ajira ya moja kwa moja katika Jeshi la Kujenga Taifa, au katika taasisi nyingine za kijeshi, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni iliishauri Serikali kuanzisha Idara ya Mafunzo ya Ufundi ndani ya JKT itakayokuwa inaratibiwa na VETA, ili vijana wanaojiunga na JKT wapatiwe mafunzo ya ufundi, na wanapohitimu wapewe vyeti vya VETA, ili waweze kutumia vyeti hivyo kutafuta ajira katika sekta mbalimbali ikiwa watakosa ajira jeshini.

Mheshimiwa Spika, Serikali hii ya CCM ilipuuza wazo hili zuri la Upinzani na matokeo yake ni kwamba vijana hao waliopatiwa mafunzo ya JKT na kukosa ajira wameanza kuwa tishio kwa Serikali. Na ushahidi kwamba vijana hao sasa ni tishio, ni maandamano yao yaliyofanyika mapema mwaka huu wakishinikiza kuonana na Rais kumweleza kilio chao.

Mheshimiwa Spika, kama alivyofanyiwa Ulimboka, kiongozi wa vijana hao alitekwa katika mazingira ya kutatanisha na kuteswa na madai ya vijana hao wa JKT yamezimwa kimyakimya kana kwamba hakuna tatizo lolote.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa hoja ya kuwaajiri vijana wanapata mafunzo ya JKT ni hoja ya Upinzani, na kwa kuwa kwa miaka yote kumi ya utawala wa awamu ya nne Serikali hii ya CCM imeshindwa kutatua tatizo la ajira kwa vijana wanaohitimu mafunzo ya JKT, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapenda kuwaahidi wananchi kwamba endapo vyama vinayounda UKAWA vitashinda katika uchaguzi Mkuu wa Oktoba, 2015 na kuunda Serikali, utaoji wa ajira kwa vijana wanaohitimu mafunzo ya JKT utakuwa ni kipaumbele katika Serikali ya UKAWA.

2.2. JKT NA UTUNZANJI WA MAZINGIRA

Mheshimiwa Spika, kwa miaka yote kumi ya utawala wa Serikali hii ya awamu ya nne, Kambi Rasmi ya Upinzani imekuwa ikiishauri Serikali kutumia nguvu-kazi iliyoko katika Jeshi la Kujenga Taifa katika utunzani wa mazingira ili kukabiliana na mabadiliko ya Tabia Nchi ambayo yanatishia uhai na usitawi wa wananchi. Katika kufanikisha jambo hili, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ilitoa pendekezo kwa Jeshi la Kujenga Taifa kuendesha Operesheni Maalum ya kupanda miti nchi nzima kwa kushirikiana na wananchi. Aidha, tulipendekeza zoezi hilo lifanywe na vijana wanaojiunga na JKT kama sehemu ya mafunzo yao.

Mheshimiwa Spika, licha ya kurudia pendekezo hili mara nyingi, Serikali bado haijaonesha utayari wa kutekeleza pendekezo hili. Kwa sababu hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapenda kuwaahidi wananchi kwamba endapo upinzani utaingia madarakani, nguvu iliyoko katika Jeshi la Kujenga Taifa itatumika ipasavyo katika utunzaji wa mazingira na katika miradi mbalimbali ya maendeleo.

3. UTUNZAJI WA SILAHA ZA MILIPUKO

Mheshimiwa Spika, kutokana na milipuko katika ghala za silaha iliyotokea katika Kambi za Jeshi za Mbagala na Gongo la Mboto, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ilipiga kelele sana na kuitaka Serikali kutofanya mzaha na masuala ya usalama katika Kambi za Jeshi kwa kisingizio kwamba fedha hazitoshi. Aidha tuliikumbusha Serikali kwamba ni muhimu kujiweka tayari kukabiliana na maafa mara tu yatokeapo kwa kuwa maafa na ajali hutokea ghafla bila taarifa.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa randama ya fungu 38 – Ngome, (uk. 58) fedha ambazo ziliidhinishwa kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa maghala ya silaha kwa mwaka wa fedha 2012/13 na 2014/15 ni shilingi bilioni 10, na fedha zinazombwa kwa mwaka wa fedha 2015/16 kwa kazi hiyo ni shilingi bilioni 4 na milioni 500. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kulieleza Bunge hili ni maghala mangapi mapya ya silaha yamejengwa na ni mangapi yamefanyiwa ukarabati.

4. MABORESHO YA HOSPITALI ZA JESHI

Mheshimiwa Spika, mwaka jana Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni iliitaka Serikali kuongeza bajeti ya kuhudumia hospitali za Jeshi kutoka shilingi bilioni 2.4 zilizokuwa zimeidhinishwa na Bunge hadi kufikia shilingi bilioni 10 ili kufanya upanuzi na kuboresha huduma za utabibu katika hospitali za jeshi hasa zile za Lugalo – Dar es Salaam na Bububu – Zanzibar kwa kuwa hospitali hizo zinatoa pia huduma kwa raia wa kawaida tena kwa takriban asilimia 80.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa fungu 38 (Ngome) uk.54. fedha zinazombwa kwa ajili ya kuhudumia hospitali za jeshi ni shilingi bilioni 4.9 ikiwa ni sawa na ongezeko la shilingi bilioni bilioni 2.5. Hizi ni fedha zilizoidhinishwa, haijulikani kama zitatolewa zote kwa kuwa Serikali hii imekuwa hodari wa kutotekeleza bajeti inayoidhinishwa na Bunge.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni haina hakika kama kiasi cha shilingi bilioni 4.9 zinaweza kufanya upanuzi wa hospitali za Jeshi katika kanda mbalimbali sambamba na kufanya manunuzi ya madawa na vifaa tiba katika hospitali za Jeshi zilizopo.

5. MIGOGORO YA MIPAKA YA ARDHI KATI JESHI NA WANANCHI

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usioplingika kwamba kuna baadhi migogoro ya mipaka ya ardhi kati ya maeneo ya Jeshi na maeneo ya makazi ya wananchi. Migogoro hii, imesababisha uhasama na kudorora kwa mahusiano baina ya wanajeshi na wananchi wanaoishi karibu na maeneo ya Jeshi. Aidha, migogoro hii imesababisha baadhi ya vikosi vya Jeshi kuwavunjia wananchi nyumba zao kwa madai kwamba wamejenga katika maeneo ya Jeshi.

Mheshiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni iliishauri Serikali katika miaka ya nyuma kutenga bajeti maalum kwa ajili ya kupitia upya mipaka ya Jeshi na Wananchi katika maeneo yale yenye migogoro na kuiweka bayana ili wananchi watambue maeneo ya Jeshi na hivyo kutoyaingilia lakini mpaka sasa zoezi hilo halijafanyika.

Mheshimiwa Spika, ipo migogoro mingine ya ardhi kati ya Jeshi na wananchi ambapo Jeshi ndio linaingilia maeneo ya makazi ya watu. Kwa mfano, katika Wilaya ya Ilemela – Mwanza, kikosi namba 601 cha JWTZ kimeingilia mitaa halali ya Lukobe na Buduku ambayo ni makazi ya wananchi na Jeshi lilikiri kwamba liliingilia maeneo hayo kwa kuwa linayahitaji lakini hakuna mpango wowote wa kuwafidia wananchi uliofanyika. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuwafanyia tathmini wakazi wa mitaa hiyo ili walipwe fidia waweze kuondoka. Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuvielekeza vikosi mbalimbali vya jeshi vyenye migogoro ya aina hiyo na wananchi kuwashirikisha wananchi endapo kuna utata wa mpaka ili wafikie suluhu kwa pamoja ili kudumisha ujirani mwema na mahusiano mazuri badala ya kuwavunjia wananchi nyumba, na kuwapiga bila kuwasikiliza.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inashangaa kuona kwamba katika fedha za maendelo katika fungu 38 – Ngome hakuna fedha zilizotengwa kwa ajili ya kupima maeneo yanayomilikiwa na Jeshi la Wananchi au kulipa fidia kwa maeneo ya wananchi yatakayochukuliwa na Jeshi la Wananchi. Tunashangaa kwa sababu katika fungu hili ndipo Jeshi la Wananchi na Jeshi hili ndilo lenye migogoro ya mipaka ya ardhi na wananchi kuliko majeshi mengine. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka kujua kama migogoro ya ardhi kati ya Jeshi na Wananchi haipo katika programu ya kushughulikiwa katika mwaka wa fedha 2015/16.

6. MADENI YA WAZABUNI WANAOTOA HUDUMA JESHINI

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2014/2015, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni iliitaka Serikali kulipa madeni yote ya wanajeshi na wazabuni wanaotoa huduma katika vikosi mbalimbali vya Jeshi.

Mheshimiwa Spika, kwa taarifa ambazo Kambi Rasmi ya Upinzani inazo, madeni hayo hayajalipwa na yamezidi kuongezeka jambo ambalo linasababisha wazabuni washindwe kuendelea kutoa huduma Jeshini.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kulieleza Bunge hili imelipa madeni hayo kwa kiasi gani na ina mkakati gani wa kutolimbikiza madeni kwa wazabuni?

7. WASTAAFU WA JESHI LA WANANCHI

Mheshimiwa Spika, kwa mihula yote miwili ya utawala wa Serikali hii ya awamu ya nne, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni iliitaka Serikali kuwajali wastaafu wa Jeshi la Wananchi kama sehemu ya kuenzi utumishi wao uliotukuka kwa taifa. Katika hotuba yangu kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya wizara hii kwa mwaka wa fedha 2014/2015 nilielezea kwa kina suala hili, nanukuu:

“Mheshimiwa Spika, maisha ya wanajeshi wetu wastaahafu yanasikitisha licha ya kulitumikia taifa hili kwa muda mrefu, kwa uadilifu na uzalendo mkubwa. Hata hivyo hali zao za maisha zimekuwa duni, mbaya na kubakia ombaomba ambayo hailingani na utumishi wao walioufanya kwa uadilifu na uzalendo wa hali ya juu.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa serikali imewatelekeza wanajeshi wastaahafu na kuwaacha mitaani bila kujua ni kitu gani cha kufanya, tayari wameanzisha umoja wao unaojulikana kama Muungano wa Wanajeshi Wastaafu Tanzania (MUWAWATA).

Mheshimiwa Spika, wanajeshi hawa wastaafu ni jeshi la akiba (Reserved Army). Kambi Rasmi ya Upinzani inahoji na kuitaka serikali kutoa mkakati wa serikali wa kuweza kuboresha maisha ya wanajeshi wastaafu na hasa kwenye viwango vya pensheni kwa maofisa na askari wa kawaida toka private hadi Brigedia General”.

Mheshimiwa Spika, imekuwa ni desturi kuwapa heshima kubwa na kutoa risala yenye maneno mazuri wakati wa mazishi yao lakini walipokuwa hai hawakusifiwa wala hawakupata haki zao stahili. Kwa mfano risala inasema kuwa Marehemu alikuwa hodari shupavu na jasiri, mwaminifu na mtiifu, yeye ni mfano wa kuigwa, atakumbukwa na atathaminiwa kwa kazi nzuri aliyofanya.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi inahoji mbona sifa hizo haziendani na jinsi wanavyotendewa wakiwa hai? Je, Serikali ina mpango gani wa kutunza familia za marehemu waliotumikia Jeshi?

8. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA 2014/2015 NA UCHAMBUZI WA MAKADIRIO YA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2015/16

Mheshimiwa Spika, kwa miaka yote kumi ya utawala wa Serikali ya awamu ya nne, kipindi hiki bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Kujenga taifa imeandikwa vibaya na inakiuka misingi ya kibajeti kuliko miaka mingine ya fedha iliyopita.

Mheshimiwa Spika, Mosi, Randama za Mafungu yote matatu yaani fungu 57 (Wizara ya Ulinzi na JKT), fungu 39 (JKT) na fungu 38 (Ngome) hayaoneshi utekelezaji wa bajeti ya mwaka wa fedha 2014/2015. Kwa hiyo haifahamiki ni fedha kiasi gani zilizotolewa na hazina kwa ajili ya utekelezaji wa bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kwa mwaka huo hadi kufikia Machi, 2015 ili kuweza kukokotoa kiasi cha fedha ambacho bado hakijatolewa. Randama zimeonesha fedha ziliyoidhinishwa kwa mwaka wa fedha 2014/15 lakini hazioneshi fedha zilizotumika.

Mheshimiwa Spika, Jambo la Pili ambalo ni upungufu katika maandalizi ya bajeti ya Wizara hii ni kutoa makadirio ya jumla yasiyokuwa na mchanganuo. Kwa mujibu wa misingi ya uandaaji wa bajeti, na kwa mujibu wa Naibu waziri wa fedha Mhe. Mwigulu Nchemba wakati akiichambua bajeti mbadala ya Upinzani kwa mwaka wa fedha 2012/13 kabla hajateuliwa kuwa Naibu Waziri wa fedha, ni makosa kutoa makisio ya bajeti kwa tarakimu kamili (Mfano. 6,000,000/=, 7,000,000/= nk) Tarakimu za namna hiyo zinaonesha kwa makadirio hayo ni ya kubuni na hayajakotolewa kwa mchanganuo mahsusi.

Mheshimiwa Spika, ukitazama makadirio ya fedha za miradi ya maendeleo katika randama ya wizara fungu 38 – Ngome uk. 56, 57 na 58 katika yameandikwa kwa tarakimu kamili jambo linaloibua hisia kwamba yamebuniwa na kuandikwa tu bila kuwa na mchanganuo mahsusi. Hali kadhalika randama ya wizara fungu 39 (JKT) - Item 280200 (uk.13), Item 430400 (uk.17) nk.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kutoa maelezo mbele ya Bunge hili kwa nini haijatao mrejesho wa utekelezaji wa bajeti ya 2014/15 na kwa nini imekiuka **principles** za uandaaji wa bajeti kwa kuweka makadirio ya kubuni.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, naomba kuwasilisha.

Mhe. Masoud Abdalla Salim (Mb)

**MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI
NA WAZIRI KIVULI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA**

Imesomwa leo tarehe 22 Mei, 2015

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Masoud, Msemaji wa Kambi ya Upinzani juu ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa hotuba hiyo.

Waheshimiwa Wabunge, sasa tunaingia kwenye awamu ya uchangiaji kwa ujumla wake. Watakaotufungulia awamu hii ni Mheshimiwa Yahya Kassim Issa na Mheshimiwa Deogratias Ntukamazina atafuatia. Mheshimiwa Yahya, dakika saba.

MHE. YAHYA KASSIM ISSA: Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa kupata nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kwanza ni kuhusu ajira zetu kuandamana na uwezo. Kuna tatizo ambalo linajitokeza mara nyingi hasa kule Zanzibar, wale Askari walioko bandarini (*marine*) kwa kweli uwezo wao wa uogeleaji ni mdogo. Walikuwepo Askari wenye uwezo baada ya kuletwa boti mpya wameondolewa. Napenda wale viongozi waelewe kwamba, haya tunayoyasema labda tunayazungumza tu lakini ni mambo ambayo yanajitokeza katika utendaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa tumelalamika kwa kiasi kikubwa kutokana na vifo vilivyotokea, hivi karibuni tunajua Zanzibar vilitokea vifo lakini suala moja lililosababisha ni uwezo wa Askari kuogelea. Askari hawajui kuogelea tunawaweka sehemu zile wale wanaojua baada ya kuja boti mpya tumewatoa wote. Naomba kiongozi aliangalie suala hili kwa uangalifu kabla matatizo mengine hayajitokeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ambalo napenda nizungumzie ni fursa ya kujiendeleza kielimu. Zanzibar kwa kweli kuna matatizo. Hivi sasa kwa kweli watu wanatafuta taaluma mbalimbali na wengine wanajiunga na Jeshi hili Polisi, uwezo wanao lakini umaskini unawafanya watafute ajira kwanza halafu waweze kujiendeleza, haya ndiyo yanayojitokeza lakini wakati mtu anapoomba nafasi ya kujiendeleza anazuiliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunao watu kama hao, OC anakubali kwamba huyu muache akajiendeleze hana pingamizi, RPC anakubali kwamba huyu muache akajiendeleze, barua inafika Makao Makuu inazuiliwa, kwa kweli siyo jambo la busara. Sisi tunahitaji vijana wenye uwezo na wenye taaluma, tukienda hapo ndipo tutafika mahali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hili ndilo linalosababisha siku zote tuseme kwamba tunaonewa, kumbe sisi wenyewe ndiyo tunawabana watoto wetu. Kwa hiyo, fursa hizi tunaomba zikubalike ili watoto wetu waende kusoma. Huyu kijana ilikuwa tayari ameshapeleka pesa kule Uganda matokeo yake sisi

tumemzuia ina maana amepata hasara vilevile muda umepita kwa kweli hakufanikisha.

Kwa hiyo, naomba masuala haya tuyaangalie kwa jicho la rehema ili tuweze kufanikisha suala hili la upatikanaji wa elimu kwa watumishi hawa. (Makofi)

Nalishukuru sana Jeshi la Polisi katika upandishaji wa vyeo, wamejitahidi kwa kiasi fulani, lakini ingekuwa vizuri watu wakaenda kwa *intake*, kikundi kimetoka na kwa muda uliowekwa, tuhakikishe muda haupiti vijana wanakwenda kwenye mafunzo. Tatizo linalojitokeza ni moja; kuna askari wameumia kazini, kweli mafunzo yapo ya vitendo na pia yako mafunzo ya darasani, kwa hiyo, hawa walioumia ambao baadhi ya shughuli za vitendo hawaziwezi, wasikomae kuwa wao ndiyo wamekosa haki kwa sababu wameumia kazini. Fursa ya kuwapatia mafunzo darasani bila shaka na wao tunaweza kuwapandisha kutokana na uwezo wao. Siyo kwamba wakae eti hawafai, hili ninaomba vilevile lichukuliwe hatua na tuweze kufanikisha. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu, kuna mambo ambayo ninaomba vilevile yaangaliwe. Kwa mfano, askari wetu wakipewa likizo hawapewi fedha. Hili siyo jambo la busara, hebu tujitahidi mbona hatujasikia hapa Jeshi linalalamika isipokuwa hawa polisi tu! Maana yake tunawaweka mahala pabaya. Jeshi sijasikia hapa kulalamika wala husikii malalamiko yao, siku zote tunazungumza haya kwa Jeshi la Polisi. Naomba hili liangaliwe vizuri. (Makofi)

Kutolipa kwa wakati madeni ya uhamisho hili ni tatizo. Siku zote tunazungumza haya siyo jambo la busara, hebu turekebisheni kwa nini wenzetu wale wanakuwa tofauti na sisi. Hii lazima siri itatoka tu kwa sababu mtoto wako mmoja anaweza kuwa polisi, mtoto mmoja anaweza kuwa mwanajeshi, haya wanaweza kuzungumza, kwa hiyo, haya masuala tuyarekebishe.

Askari wanapofanya kazi nje ya Mkoa vilevile hawapati kitu na mara nyingi kule Zanzibar ndiyo malalamiko haya yanatokezea sana, kwa hiyo, Kamishna jitahidi sana, wewe ni mpya ndiyo kwanza umeingia, jitahidi haya mambo myaangalie kwa uangalifu zaidi ili kuweza kufanikisha. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Misafara ya Viongozi, tunajua kuwa askari wanaridhiana kwa muda fulani mpaka saa sita anakuja mwenzie, lakini katika misafara utaona anachukua muda mrefu sana mpaka saa kumi na mbili pengine afike kwao usiku, lakini hakuna chochote anachopatiwa. Hakuna *disturbance allowance* yoyote anayopatiwa, yeye inakuwa kafanya kazi kwa Bwana tu. Mimi ninadhani mambo haya tuyarekebishe.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana na leo ni Siku ya Ijumaa, kwa hayo machache ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Yahya Kassim Issa. Mheshimiwa Deogratius Ntukamazina, atafuatiwa na Mheshimiwa Agripina Buyogera!

MHE. DEOGRATIUS A. NTUKAMAZINA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Nianze kwa kuipongeza Wizara ya Mambo ya Ndani, kwa kazi nzuri ambayo imekuwa ikiifanya tangu Uhuru ya kulinda amani katika nchi yetu; ninawapongeza sana.

Nina mambo manne tu kwa sababu muda hautoshi. La kwanza ni jepesi lakini ni muhimu sana kwa Wilaya ya Ngara na mawili ya mwisho ni mazito.

La kwanza, ninadhani Wizara ya Mambo ya Ndani ingekuwa na vipaumbele, Wilaya ambazo ni vipaumbele; kwa mfano, Wilaya ya Ngara inapakana na nchi mbili za Rwanda na Burundi na Mheshimiwa Waziri anajua kwamba, Burundi haijawahi kutulia tangu Uhuru. Huyu kijana mdogo anayeitwa Nkuruzinza, anafanya matendo ambayo hayafanani na jina lake. Jina lake ni zuri sana, maana ya Nkuruzinza ni habari njema kwa Kiswahili au good news kwa Kiingereza, lakini ninashangaa analeta matatizo katika nchi yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Wilaya ya Ngara, Vyombo vya Usalama vina matatizo makubwa sana ya kuwa na nyenzo za kufanyia kazi. Magereza, Polisi na Uhamiaji wana magari mabovu, wanapewa bajeti ndogo ya mafuta, wanabaki kuombaomba kwa Mkurugenzi wa Halmashauri. Kwa mfano, Magereza wanadaiwa sana na Idara ya Maji na TANESCO. Mimi nilifikiri Wizara ya Mambo ya Ndani ingehakikisha Wilaya za pembezoni kama Ngara ambazo zinapakana na hizo nchi, wangepewa kipaumbele hivi Vyombo vya Usalama wa Taifa vikapewa nyenzo za kufanyia kazi.

Jambo la pili, Mheshimiwa Waziri anajua kwamba, kuanzia mwaka 2012 na Katibu Mkuu hajabadilika, Wizara ya Mambo ya Ndani iliahidi kuchangia ujenzi wa Nyumba za Polisi wa Kituo cha Murusagamba, ambacho kinapakana na Burundi. Kwa muda mrefu polisi wa kituo hicho hawana magari, wanafanya kazi asubuhi mpaka jioni wanakwenda kulala Mkoa wa Kigoma, Wilaya ya Kibondo, katika Kijiji cha Nyabibuye. Kutokana na hali hiyo, kumewepo na ujambazi mkubwa sana unaosababishwa na watu kutoka Burundi kwa sababu wanajua usiku hakuna polisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tangu 2012 walinahidi kuwa watachangia, baada ya hapo nikawamasisha wananchi wamechangia vifaa vingine, ningomba Mheshimiwa Waziri utukumbuke ututekelezee ahadi ya mwaka

2012. Hayo ni mambo ya kwanza mawili, nilisema ni mepesi lakini ni muhimu kwa Jimbo la Ngara, sasa nije kwa mambo mazito.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamwomba ndugu yangu Chikawe, kwa kuwa Mambo ya Ndani imekuwa ikilinda amani tangu Uhuru mpaka sasa, ninamwomba yeye ni Msimamizi Mkuu wa Amani, aendelee kuhakikisha kwamba, vitendo ambavyo vinaweza kuleta vurugu katika nchi yetu vinakomeshwa. Kabla sijaendelea, nitoe mfano wa Rais mmoja mstaafu wa Namibia, jina lake la kwanza ni gumu, anaitwa Hifikepunye Pohamba, juzi juzi alipewa zawadi ya Mo Ibrahim, yule tajiri mkubwa wa Sudani anayetoa tuzo kwa Viongozi waliofanya vizuri katika Utawala Bora.

Nikajjuliza kwa nini Pohamba amepata zawadi? Nikafuatilia mambo mazuri aliyoyafanya, nikakuta cha kwanza alipoingia madarakani, Vyama Vya Upinzani pamoja na wananchi wa Namibia walifikiri atakuwa mtu mbaya, kwa sababu amekuwa *hand-picked* na Sam Nujoma, ambaye alikuwa anatuhumiwa kwa kunyanyasa Vyama Vya Upinzani. Alipoanza kazi akasema, mimi ninataka utawala wa pamoja, yaani *collective leadership*, akaanza kuwa na mawasiliano ya karibu na Vyama vya Upinzani. Akafanya *consultation* na Vyama Vya Upinzani, akafanya *Consultation* na Viongozi wa Dini kwa sababu alijua makundi hayo mawili ni muhimu sana katika kulinda amani.

Ninasema hivyo kwa sababu hivi karibuni kumetokea tabia kwa baadhi ya Viongozi wa Serikali, kuwabeza au kutumia lugha ambayo haifai kwa Viongozi wa Dini. Ninaomba sana Viongozi wa Serikali wajue kuwa, Viongozi wa Dini ni watu muhimu sana. Ukishawasema vibaya Viongozi wa Dini, unatumiza sisi Waumini na ujue kwamba sisi Waumini tunawatii zaidi na kuwaheshimu Viongozi wa Dini kuliko tunavyoiheshimu Serikali. Kwa mfano, Kiongozi wa Kanisa Katoliki, Baba Mtakatifu au Papa, anaheshimiwa na Viongozi wa Kimataifa wote *including* Rais wa Marekani, kwa sababu nyuma yake kuna wafuasi bilioni moja na laki tatu. Hivyo hivyo Maaskofu na Mashehe, wana wafuasi wengi nyuma yao, ambao wanawatii kuliko wanavyoitii Serikali. Kwa hiyo, ninaomba sana Viongozi wa Serikali wasije wakatumia lugha mbaya kwa Viongozi wa Dini, kwa sababu watatumiza sisi Waumini na itakuwa ni kuleta vurugu katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ambalo ni muhimu, nirudie niliyoyasema juzi katika swali langu kwamba, ninaomba na Waziri Chikawe rafiki yangu hakuwepo, niliuliza swali nikasema, kwa muda mrefu sana Watu wa Ngara tumenyanyaswa sana na tumebaguliwa na Idara ya Uhamiaji. Kabla sijawa Mbunge nimekuwa nikienda kugombana na Kamishna wa Uhamiaji kwa nini anawanyanyasa Watu wa Ngara na kuwabagua hasa wanapotaka kusafiri kwenda nje! Wanapojaza fomu za kupata *passport* wanaambiwa hawana uhakika na Urai wao, kwa sababu kuna mwingiliano mkubwa na Warundi na Wanyarwanda. Sasa nikauliza kwani Ngara sisi ndiyo tuko mpakani yetu; mbona

Watu wa Masasi wanapakana na Msumbiji hawabaguliwi? Mbona watu wa Songea wanapakana na Malawi hawabaguliwi? Mbona watu wa Tarime wanapakana na Wakenya hawabaguliwi? Watu wa Tanga na Mombasa hawabaguliwi; kwa nini Ngara tunabaguliwa?

Bahati nzuri rafiki yangu Chikawe ni msomi, anajua kwamba ...

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa, muda hauko upande wako. Ninakushukuru sana.

Mheshimiwa Agripina Buyogera, atafuatiwa na Mheshimiwa Esther Matiko!

MHE. AGRIPINA Z. BUYOGERA: Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia machache katika Wizara hizi mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ridhaa yako, kwanza, ninaomba niwape pole wapiga kura wangu wa Kijiji cha Nyamidaho, ambapo kuna mfanyabiashara mmoja amevamiwa na majambazi usiku na amepigwa risasi ameuawa na mwingine yuko hospitalini. Ninaomba Mungu awape faraja na niliombe Jeshi la Polisi lishughulikie suala hilo hatimaye wahusika waweze kupatikana.

Awali ya yote, ninaomba nianze na Jeshi la Wananchi hususan JKT. Ninaomba nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri, mtu akifanya vizuri ni lazima nimpongeze. Bunge lililopita nililalamika sana kuhusu iliyokuwa Kambi ya Wakimbizi sasa hivi ni JKT pale Mtabila, ambao wako Jimboni kwangu. Walikuwa na mgogoro mkubwa sana na Kijiji cha Mgombe juu ya mpaka, lakini kwa kweli tangu wakati ule, sasa hivi hata kama bado hawajaweka mipaka halisi, lakini vurugu ile ya Jeshi kuwasumbua Wananchi wa Kijiji cha Mgombe imetulia. Ninaomba nikushukuru na nimshukuru mhusika wa JKT ambaye ametambulishwa yuko pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba juhudi hizi ziendeele na Wizara mpange fedha ili kwenda kubaini mipaka halisi, ikiwezekana muweke uzio. Kambi ile ndiyo kwanza imeanza, hatuna sababu ya kulimbikiza matatizo na baadaye kuleta madhara kwa Watanzania bila sababu za msingi.

Mheshimiwa Waziri hili uliangalie, utupangie fedha pale Mtabila ili usituchonganishe na Wanajeshi wetu, ambao leo wako wanafanya kazi nzuri ya kujenga Grand High School pale Kasulu. Ukileta mahusiano mazuri, ninaamini Jeshi litakuwa na ubora zaidi na wananchi wataendelea kuliheshimu. Kwa upande wa Jeshi, ninaomba niseme hayo na niwape pole kwa kupangiwa fedha na zisitolewe.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Naibu Spika, hii Serikali kila Wizara inalalamika, Bunge tunapitisha Bajeti hapa lakini pesa hazipelekwi kwa walengwa ni kwa sababu gani? Unashangaa kama Wizara zingine zinalalamika mpaka Jeshi? Jeshi ambalo linaheshimika ulimwenguni kote, Jeshi la Tanzania, leo mnawanyima fedha mnataka nini? Ndiyo maana ninaungana na Hotuba ya Kambi ya Upinzani, kwa kweli Hotuba ya Upinzani muipitie vizuri ili yale yaliyozungumzwa muweze kuyarekebisha.

Leo hii kama mnawanyima fedha Jeshi; mnategemea nini na wakati mnaona mambo yanayotokea Burundi? Jeshi ndiyo mpango mzima, kama Jeshi lisingekuwepo leo Rais anayetajwa hapa asingekuwepo. Kwa hiyo, ninaomba fedha za Jeshi mhakikishe Serikali mnatekeleza kama ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba niende Jeshi la Polisi. Jeshi la Polisi ninawashukuru kwa kupanga mpango mkakati wa kutengeneza Uwanja wa Ndege wa Kasulu. Kwa kweli lilikuwa ni jambo linalosikitisha sana, Kasulu hatunufaiki na chochote wakati ndiyo Wilaya tunayopokea wakimbizi miaka yote. Ninaomba, nimewahi kufika Wizarani na kuomba gari la Kituo cha Makere. Leo mnaona ujambazi unafanyika huko, askari wangu pale hawana vitendea kazi, wakimbizi wanapita kupitia huko Kitanga kwa kuwa mpaka uko wazi. Mtu wa haraka wa kumkimbilia ni polisi, sasa polisi wanategemea gari kutoka Wilayani na Wilaya ile ni kubwa, unamkuta OCD ana gari moja ambalo ni zima, lakini mnetuwekea gari pale Kituo cha Makere, lingeweza kusaidia kukimbia pale Kagera Nkanda, kukimbia hapo palipofanyika ujambazi Nyamidaho na maeneo mengine.

Ninakuomba Mheshimiwa Waziri Chikawe, ninakuheshimu sana, unisaidie hili. Haiwezekani nipige kelele miaka mitano kesho kutwa tunavunja Bunge hutaki kunielewa kwa nini? Hakuna kama mama Dunia hii, fanya kweli bwana!

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naomba Wizara ya Mambo ya Ndani, Kitengo cha Uhamiaji, sasa hivi wakimbizi wanaingia Wilaya ya Kasulu na Kambi ya Wakimbizi iko Jimboni kwangu. Naomba mtumie utulivu, mtumie utaalamu wenu mliosomea, msituchanganye wakati huu tunakwenda kwenye uchaguzi; msianze kutukarahisha Wananchi wa Tanzania halisi mkatuita Warundi. Ninaomba tabia hiyo isijitokeze, kutuletea vurugu bila sababu za msingi, kama mambo haya hamkuyasomea msemi kuliko kwenda kutushindisha polisi, kesho mnatupeleka Mahakamani tunaonekana ni raia! Mheshimiwa Chikawe umenisikia.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho ...

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, ndiyo lilikuwa la mwisho hilo Mheshimiwa Agripina.

MHE. AGRIPINA Z. BUYOGERA: Ninaunga mkono Hotuba ya Msemaji wa Upinzani. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Esther Matiko, atafuatiwa na Mheshimiwa Idd Azzan!

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru. Ninamshukuru pia Mwenyezi Mungu, kwa kunipa uhai siku ya leo na kuweza kuchangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na Jeshi la Polisi kwa upande wa Askari Magereza. Ni dhiri na Kambi ya Upinzani imeainisha ndugu zetu hawa Askari wa Magereza, Mfumo wao wa Uendeshaji ni kama vile enzi za ukoloni. Ninasema haya kwa sababu utakuta kwa mfano, Askari Magereza amefanya kosa, akifanya kosa anapewa adhabu anakatwa robo ya mshahara wake. Huyo askari Magereza anasimamishwa kwa miaka mitatu asiende kujiendeleza. Ndani ya miaka mitatu ya kutumikia adhabu yake, hatakiwi kupandishwa cheo. Kikubwa zaidi, posho za ujuzi za Askari Magereza hazibadiliki. Posho au fedha wanazopewa haziendani na elimu yao, ukiangalia pia kiwango kidogo wanachopata kati ya cheo na cheo. Kwa hiyo, ukiangalia mfumo mzima wa ndugu zetu hawa Askari Magereza, hauko sawa. Ninaomba wapitie na wao waweze kuwarekebisha.

Ninakumbuka mwaka 201 pia tulibadilisha tukapendekeza posho ya chakula wanayopewa, lakini mpaka leo hii bado wanaendelea kupewa shilingi 180,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine ni mrundikano wa mahabusu kwenye Magereza yetu. Jana tulizungumzia kwamba, ni bora wale wenye kesi za jinai ndogo ndogo wapewe dhamana. Leo hii ukienda kwa mfano Gereza la Tarime, utakuta uwezo wa cell ni kati ya watu 27 wamezidi sana inatakiwa wawe na watu 40, lakini leo wanachukua kati ya watu 100 na 110. Kwa hiyo, unaweza ukaona ni kwa kiasi gani hawa watu wanaweza kupata maambukizi ya magonjwa.

Kikubwa zaidi, kwenye cell hizo hizo, mathalani hiyo ya Trime niliyoisema, unakuta kuna watoto wadogo kati ya miaka 12 na 14 nao wanachanganywa humo humo kwa watu wazima na wanarundikwa kwenye cell watu 100 mpaka 110. Ukiangalia unakuta huwatendei haki hawa watoto wadogo kati ya miaka 12 na miaka 14. Ninaomba Serikali iangalie, aidha, iwatengee cell yao watoto wenyewe au iangalie ni adhabu gani mbadala hawa watoto waweze kutumikia. Kwanza, unakuta ni mahabusu, waweze hata kukaa nje na makosa waliyotenda na yepi kuliko kwenda kuwarundika na watu wazima.

Kingine kikubwa zaidi, chakula wanachopewa mahabusu au wafungwa ni maharage siku zote, kinyume kabisa na Sheria ya Chakula cha Mahabusu. Kwa hiyo, ninaomba waangalie, kama ni fedha wapeleke, ndugu zetu wapate chakula stahiki kulingana na Sheria, maana tumeona hata kwenye Ripoti ya CAG fedha nyingi zinapigwa, wazipeleke huko ziweze kuwapa chakula mbadala.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu kingine ni nyumba za askari. Wakati ninachangia Bajeti ya Waziri Mkuu nilisema Nyumba za Askari Magereza zinasikitisha. Nilisema siku ile kwamba, hazifai hata kuishi binadamu, nilimaanisha leo hii ukienda Magereza mbalimbali nchini na hususan nikatoa mfano wa Gereza la Tarme, hauwezi ukakaa binadamu.

Kwa hiyo, nashauri tutenge fedha na kwa mpito huu kwa sababu nimesema bainadamu hawezi kukaa kwenye nyumba zile za Magereza, wapewe posho ya pango kwa muda, zile nyumba ziondolewe kabisa, zijengwe nyumba za kisasa ambazo hazitatumia eneo kubwa, kwa sababu ardhi yao siyo kubwa sana. Ukijenga nyumba za kisasa za maghorofa, ndugu zetu wale watapata makazi ya kisasa, waweze kufanya kazi katika mazingira mazuri, lakini pia kutakuwa na matumizi mazuri ya ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine, nizungumzie sasa kuhusiana na Jeshi la Polisi. Katika Kijiji cha Gibaso, Kata ya Kwihanchi Wilaya ya Tarime, wananchi hawamtaki OCS wa pale Ndugu Mdee, kwa sababu amejivika Ukada wa Chama cha Mapinduzi. Anawapiga risasi wananchi ambao wana mlengo wa Chama cha Upinzani. Amepiga wengi na kesi zipo na RPC wa Tarime nimeshamfikishia hiyo kesi anaijua. Ninashukuru RPC Mambosasa mliyemleta sasa hivi, angalau anaendana na dhana dhima ya kujua ni nini wajibu wa Jeshi la Polisi. Kwa hiyo, tunaomba mumhamishe OCS wa Gibaso haraka sana iwezekanavyo, wananchi hawamtaki.

Mheshimiwa Naibu Spika, niye kwenye Jeshi la Wanachi. Fidia, tangu nimekuwa Mbunge humu ndani nimekuwa nikizungumzia fidia ya Watu wa Lonoti na Msati, ambao tuliwakaribisha mwaka 1973, baada ya kuwa yametokea mafuriko kwenye kambi yao ya kule Nyandoto. Mwaka 2007 wakaona ni vyema watwae ile ardhi. Kuanzia mwaka 2007 mpaka leo, wale wananchi walizuiliwa kufanya shughuli zao za kimaendeleo, hawajengi, hawalimi wala hawafanyi chochote.

Mwaka 2014 Mheshimiwa Waziri alisema wametenga bajeti wawalipe fidia, juzi wakati tunaongea akasema Serikali haikumpa bajeti ambayo tulikuwa tumetenga. Nikajiuliza hizi fedha ambazo ni misamaha ya kodi na nini, maana tulimtengea bilioni mia saba tu anasema amepewa milioni mia saba tu wakati huo huo wale ndugu wanazidi kuteseka kule! Kama hamna fedha, muwaache

wale wananchi waendeleo kuendeleza maeneo yao, mpaka mtakapokuwa mmepata fedha za kuwafidia ndiyo muwaondoe.

Hapo hapo katika Jeshi la Wananchi, JKT imetoa eneo la Kulutambe na Kubitereri. Hawajalipwa fidia wale ndugu, mpaka leo zaidi ya hekta 393, hawajafanyiwa chochote kile, ndiyo yalikuwa makazi yao, walikuwa wanachungia pale na kulima, kwa hiyo wame-*paralyze* kabisa na shughuli za kiuchumi. Naomba na hilo nalo kwenye bajeti ambayo tunaenda kukupitishia leo, utuhakikishie kwamba, utaenda kutoa fidia, ili wale wananchi, unajua kabisa Jeshi la Wananchi lilivyo; hawataki wananchi waingiliane nao. Wakienda wanapata matatizo, wananyanyaswa, tunaomba hao wananchi wahamishwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kuhusu madeni ya wazabuni kwenye Jeshi la Wananchi. Kweli kabisa Watanzania wanaotoa huduma za uzabuni kwenye Mashirika au Taasisi mbalimbali nchini hasa Jeshi la Polisi, wamekuwa wakidai fedha nyingi. Unakuta mtu anadai hata shilingi bilioni nane, kumi na tano na unajua kabisa wanakopa hizo hela ili waweze kwenda kuendesha hiyo biashara. Tunawaweka njia panda na ndiyo maana hata huduma zinasitishwa sasa hivi, tunaomba mtoe kipaumbele ili hao wazabuni walipwe fedha zao. (Makofi)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Ester Matiko. Mheshimiwa Iddi Azzan, atafuatiwa na Mheshimiwa Khatibu Said Haji na Mheshimiwa Hamad Ali Hamad!

MHE. IDDI M. AZZAN: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Naomba nianze kwa ninukuu maneno aliyoyasema hivi juzi na yaliandikwa na Gazeti la Mtanzania la Jumatano la Tarehe 20 Mei. Mwanazuoni na Msomi mkubwa hapa nchini, Dkt. Issa Shivji anasema: “Hatuwezi kujifariji kuwa sisi ni kisiwa cha amani wakati leo kuna viashiria vya kuvunjika kwa amani nchini.”

Niliona nitangulize kuyasema hayo, kwa sababu wakati nachangia kwenye Taarifa za Kamati tarehe 4 Februari, niliyasema maneno haya. Kwa masikitiko makubwa sana, Serikali haikujibu na Mjumbe wa Kamati ya Ulinzi na Usalama, Kapteni Mstaafu Chiligati, alinijibu kwa dharau na kwa kebeh! Nimeona niyazungumze, lakini narudia tena yale niliyoyasema kwamba, viashiria vya kuvunjika amani katika nchi yetu vipo na vinaonekana. Matokeo ambayo yamejitokeza hivi karibuni ya ugaidi, ujambazi kupita kiasi yapo na yanaonekana.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Katika majibu yake aliniambia, kwa sababu niliomba JKT ama Jeshi kuishauri Serikali, ione uwezekano wa kutumia Vyombo hivyo viwili kusaidiana na Jeshi la Polisi. Kwa sababu polisi wamezidiwa ama kwa sababu hawana vitendea kazi au kwa sababu ni wachache. Majeshi haya yote yapo kwa ajili ya kulinda Watanzania, lakini nilichojibiwa nikaambiwa na Kapteni Mstaafu kwamba, Wanajeshi wamefundishwa kupiga risasi kichwani na kifuani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maneno haya yalinisikitisha sana na kuonyesha kwamba maneno haya hayakuwa na ukweli, kulitokea tukio la kigaidi Tanga, wanajeshi walitumwa kwenda kupambana na magaidi wale. Sasa leo wasimame waniambie wanajeshi wetu waliwapiga risasi za kichwani na kifuani magaidi wangapi zaidi ya maaskari wetu watano kujeruhiwa na mmoja kuuawa? *(Makofi)*

Waniambie vile vile huko nje tunakolinda amani katika nchi za nje, wanajeshi wetu wamewapiga watu wangapi risasi za kifuani na kichwani?

Katika taarifa ya Waziri, miongoni mwa kazi ambazo Jeshi la Wananchi wanafanya ni pamoja na kushirikiana na Mamlaka za Kiraia pale inapobidi, katika kukabiliana na majanga na dharura za Kitaifa.

Jeshi halifanyi kazi ya kupiga risasi kichwani na kifuani tu, wana mambo mengi wanayoyafanya, wanafundishwa mambo mengi sana. JKT wanafundishwa mpaka kilimo, wanafundishwa stadi za maisha, lakini jeshi linafundishwa pia kukabiliana na adui ambaye hana silaha. Leo mnasema jeshi letu limefundishwa kupiga risasi kifuani na kichwani!

Mheshimiwa Naibu Spika, yalinisikitisha sana maneno hayo na niliona niseme.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye mchango wangu sasa, naomba kabisa katika Wilaya ya Kinondoni ama Polisi Mkoa wa Kinondoni, tunakabiliwa na hali mbaya sana ya uhalifu. Nawapongeza sana askari wa Mkoa huu wa Kipolisi Kinondoni pamoja na RPC wetu Wambura, kwa kazi nzuri wanayoifanya kupambana na uhalifu huo pamoja na kwamba, hawana vitendea kazi na askari ni wachache.

Hatuna vitendea kazi kwa maana ya magari, lakini aibu zaidi ni kwamba, hata mafuta ya kwenda kutia kwenye hayo magari mabovu tuliyokuwa nayo ikifika tarehe 15 ya mwezi, mafuta yamekwisha, Mkoa ule unakuwa hauna fedha za mafuta kwa ajili ya magari ya polisi. Sasa hii ni aibu!

Bajeti yenu mwaka 2014 ilikuwa bilioni mia tisa, leo mna mia nane. Badala ya kupanda juu bajeti inazidi kurudi chini, hali ya uhalifu inaongezeka! Naomba

Serikali ilianganalie kwa umakini na ianganalie Polisi Kinondoni kutokana na hali halisi ilivyo. Wilaya hii ina watu wengi sana na ina uhalifu kuliko maeneo mengine yoyote. Matukio mengi ya uhalifu yapo Kinondoni, lakini hatuna vitendea kazi.

Bahati mbaya sana ninyi Viongozi wote mnaishi Kinondoni na ninyi nyote mnatakiwa mlindwe na askari hao hao wachache! Sasa unajiuliza askari wangapi watalinda wananchi na askari wangapi watakwenda kulinda Viongozi? Mabalizi wamejaa Kinondoni, Mawaziri mpo Kinondoni na mambo mbalimbali yote yapo Kinondoni. Lindo moja linachukua askari sita kwa saa 24. Sasa jiulize malindo yapo zaidi ya mia moja tunatumia maaskari wangapi? Askari wangapi watakwenda kukabiliana na uhalifu?

Naiomba sana Serikali ianganalie uwezekano wa kuisaidia Wilaya hii ya Kinondoni kwa maana ya kuwapatia vitendea kazi, kuwapatia askari wa kutosha, lakini kuangalia pia uwezekano wa kuongeza posho za askari. Askari unamlipa shilingi laki moja na nusu kwa mwezi itamsaidia kitu gani?

Bajeti tunayoipitisha hapa leo, ya mwaka tunaoumalizia ipo juu kuliko hii ambayo tunaipitisha ipo chini. Waheshimiwa Wabunge na Kamati ya Ulinzi na Usalama kwenye Taarifa yenu mmesema, kama kweli tuna uchungu na hali ambayo inaendelea hivi sasa ya uhalifu, basi tukubaliane leo hii hapa, Bajeti hii ya Wizara ya Mambo ya Ndani, kama pesa hazikuongezwa angalau zilingane na za Mwaka wa Fedha 2014//15, basi ni vyema tusipitishie bajeti hii ili tujue kwamba Serikali imeshindwa. *(Makofi)*

Huwezi kupitisha bajeti ndogo namna hii na uhalifu unazidi kushamiri. Naomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu tuungane na natoa hoja kwenye hili kwamba bajeti hii isipite kama pesa hazitaongezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante Mheshimiwa Iddi Azzan. Bahati mbaya waliokuunga mkono bado ...! *(Kicheko)*

Umesikika Mheshimiwa Iddi Azzan, ahsante sana. *(Kicheko)*

Mpo wote wawili na Mheshimiwa Hamad? Basi nakupeni dakika nne, nne, kwa sababu ni dakika saba mnagawana wawili.

MHE. KHATIB SAID HAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, zinatoshia hizo. Mimi nianze kwa kusema kwamba, namshukuru sana Rais Jakaya Kikwete, wakati analihutubia Bunge hili kwa mara ya kwanza, kati mambo aliyoyaongea hapa ni kwamba, atahakikisha amani ya nchi yetu hususan Zanzibar inaimarika. Jitihada zake zilionekana kwa kusimamia usalama na amani katika muda wote huu.

Mimi nataka kumwuliza Mheshimiwa Rais kupitia ninyi Watendaji wake, shida ya Rais kwa amani katika Visiwa vya Zanzibar ilikuwa ni wakati wa utawala wake tu; maana yake baada ya utawala wake hana haja ya kuiona Zanzibar inabakia katika hali ya usalama na utulivu?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini nasema hivi? Kuna viashiria kadhaa ambavyo vinaelekeza Zanzibar kwenda katika janga kubwa la umwagaji wa damu. Haya yanaandaliwa kwa makusudi na watawala wa upande wa CCM Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, Zanzibar tuna Serikali ya Umoja wa Kitaifa, lakini Viongozi Wakuu wawili; Mheshimiwa Rais na Mheshimiwa Seif Sharif Hamad, bado wanasimamia falsafa ya Rais Kikwete ya kuona Zanzibar inabakia katika amani yake. Zanzibar kuna genge la kihuni linalolindwa na bunduki, linasimamia uhalifu wa kuifanya Zanzibar iingie katika matatizo makubwa. Nasema na ninasema kwa ushahidi, haiwezekani kutokea katika nchi, Makamu wa Rais wa Nchi anaenda kufanya mkutano halali wa Chama cha Siasa, anatokea muhuni anatoa amri kwa Jeshi la Polisi anazuia Mkutano wa Makamu wa Rais wa Nchi, haijatokea Duniani!

Hili nasema ni genge la kihuni linafaa lilaaniwe. Maana yake ni kwamba, hawamthamini Makamu wa Rais ambaye amechaguliwa na watu na amewekwa pale kwa mujibu wa sheria. Hii inaashiria kwamba, Wafuasi wa Makamu wa Rais, tungekuwa hatuna akili na tungekuwa akili na ndogo kama wengine, tayari nchi ile sasa hivi ingekuwa imeingia kwenye machafuko.

Tumeendelea kustahimili tukijua kwamba, Rais Kikwete ndiyo mwenye dhamana ya Jeshi la Polisi. Jeshi la Polisi linatumika kupokea amri za kihuni, kufanya uhuni, kuvizuia vyama vya halali vya kisiasa kufanya shughuli za kisiasa!

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hili jambo tukiendelea kunyamaza hapa tunakoelekea siyo kuzuri.

Nataka niseme suala lingine, hivi ninavyozungumza pamoja na heshima kubwa Watanzania wanayoipa Jeshi la Wananchi la Tanzania, tayari linajiingiza Jeshi la Wananchi wa Tanzania katika mambo ya kisiasa Zanzibar. Hivi ninavyozungumza, karibia mwezi mzima, Jeshi la Wananchi kwa kutumia magari yao, wamekuwa Wakipokea vijana kutoka Tanga na Dar es Salaam, wanawaweka kwenye Makambi ya Jeshi kuandikisha kupata uraia wa Zanzibar. *(Makofi)*

Huu ni uhuni mwingine unaofanywa na yote haya yanafanywa kwa amri ya mtu mmoja anayeitwa ni Mbunge wa Kitope, Seif Ali Idd. Nasema wazi

kabisa, hatuwezi kuvumilia! Mheshimiwa Seif Ali Idd anafikia hadi kusema kwamba, Jimbo la Kitope hakuna ruhusa Vyama vya Siasa kuingia. Kule Pemba kwenye Jimbo langu Wana-CCM hawazidi 200, lakini Seif Ali Idd anakuja na anatamba anafanya mkutano. Nimzuie akome kuja kwenye Jimbo langu Seif Ali Idd. Kwa heri.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Khatib Said Haji, tunakushuru, sijui sauti imeenda wapi hii!

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa!

NAIBU SPIKA: Aah, bahati mbaya ameshakaa. Taarifa imechelewa kidogo. Mheshimiwa Hamad Ali Hamad!

MHE. HAMAD ALI HAMAD: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Naomba niseme kwamba mwezi Julai 2010, Wizara ya Mambo ya Ndani kupitia Jeshi la Polisi, waliwaajiri Watanzania katika ajira ya mkataba ya miaka miwili.

Baada ya kumaliza mkataba wao wa miaka miwili, ni jambo ambalo ninashindwa kuamini lakini ni ukweli kabisa kwamba, wajiriwa hawa walitoka katika Mkoa wa Rukwa, Mkoa wa Mtwara na Zanzibar. Inasikitisha na ni jambo la ajabu sana, wale wa kutoka Tanganyika wote, Mikoa yote miwili niliyoitaja ya Rukwa na Mtwara, wamelipwa stahili zao baada ya kumaliza mkataba wao. Wale wa Zanzibar mpaka ninavyozungumza hapa bado ni nenda rudi, wamechoka, wamejichokea, hawana hata nauli za kufuatilia, hawajalipwa stahili zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nataka niliulize Jeshi la Polisi; huu ni ule mkakati na mwendelezo wa Tanganyika iliyovaa koti la Muungano katika kuhakikisha wanaidhalilisha Zanzibar na Wazanzibari au ni kitu gani?

Naomba Mheshimiwa Waziri utakapokuja uwaambie Wazanzibari hawa ambao wametoa jasho lao kuitumikia nchi yao; ni lini watalipwa stahili zao na kama hawalipwi ni kwa nini msiwalipe au ndiyo mmewatoa kwenye Muungano huu?

Hivi wana sababu gani hawa wanapokataa kusema hawataki Muungano wanakosa gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie suala la askari polisi ambao wamepandishwa vyeo kuanzia mwaka 2012 na hadi sasa hawajapata nyongeza ya mishahara itokanayo na vyeo walivyopandishwa. Ni jambo la ajabu, inakuwaje mtu unampa *promotion* ya cheo bango tu unambandikia bango begani halafu hakuna masilahi, anaweza kujidai vipi kwamba

ameongezwa cheo kama hakuna masilahi? Hakuna hiyo fedha? Mpaka sasa hivi hamjawapa nyongeza ya mishahara yao hiyo baada ya kupandishwa vyeo. Naomba mtakapokuja pia muwape uhakika askari hawa ni lini kupitia bajeti hii mtawapa malimbikizo ya nyongeza za mishahara zitokanazo na hivyo vyeo?

Mheshimiwa Naibu Spika, namna ambayo polisi wanatumika kama silaha ya kuihami CCM hasa kwa upande wa Zanzibar. Polisi sasa kinyume na sheria, kinyume na utaratibu, wamekuwa watiifu kwa Chama cha Mapinduzi, wanatumiwa kama silaha ya kuinusuru CCM ambayo tayari haina manusura tena kwa mwelekeo wanaokwenda nao, lakini wamethubutu hata kutangaza kipindupindu cha kisiasa kule Zanzibar. Wameweka *quarantine* kinyume na Sheria ya Vyama vya Siasa Namba Tano.

Wametengeneza sheria, sijui wameiokota wapi, lakini wanasema ni marufuku vyama vya siasa kutoka Mkoa mmoja au Wilaya moja kuingia Wilaya nyingine na wafuasi wao kwenda kushiriki kwenye mkutano; ni jambo la ajabu sana! Hatuelewi wamepata wapi na wana uwezo upi wa kubadilisha sheria zilizokwishatengenezwa na nchi hii ndani ya Katiba. Wao wanazibadilisha kwa sababu tu wameagizwa na Chama cha Mapinduzi, haiwezekani!

Polisi mnaonekana ndani ya mashati tuliyowanunulia sisi wananchi kwa kodi zetu, mmeweka mashati ya kijani humo ndani, mnakitumikia Chama cha Mapinduzi, hili halikubaliki na ninawaomba sana muache huo utaratibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie suala la *retention*.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)*

NAIBU SPIKA: Muda hauko upande wako Mheshimiwa Hamad.

MHE. HAMAD ALI HAMAD: Nashukuru. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Faida Bakar!

MHE. FAIDA MOHAMMED BAKAR: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi na mimi ya kuchangia hoja hizi hapa. Kwanza, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema. Napenda pia kuwashukuru akina mama wa Mkoa wa Kusini Pemba, kwa mashirikiano yao makubwa wanayonipatia na wao ndiyo walionituma hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napenda kumshukuru Jemedari Mkuu Rais wetu Jakaya Mrisho Kikwete na Rais Dkt. Shein wa Zanzibar, kwa jinsi

wanavyoiongoza nchi hii kwa amani na utulivu. Ingawa Wapinzani hawapendi amani hiyo na utulivu, maana wao wamezoea vita, lakini Viongozi wetu hawa wamejizatiti katika kuleta maendeleo ya nchi hii kwa amani na utulivu. *(Makofi)*

Nashangaa Wapinzani kusimama hapa leo ...

MBUNGE FULANI: CUF?

MHE. FAIDA MOHAMMED BAKAR: Aaah, Wapinzani wote. Wamesema kwamba eti 2015 Oktoba watachukua ushindi, *never!* Hiyo haiwezekani, CCM itaendelea. CCM itaendelea kushinda katika nchi hii kwa sababu Sera zake zinaeleweka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia hoja sasa. Nyumba za Askari Polisi; kama tunavyojua Askari Polisi wa Nchi hii wanafanyakazi kubwa sana katika nchi hii, siyo usiku siyo mchana, siyo shida siyo raha, mvua na jua, wanalinda amani ya nchi hii, lakini askari wengi hawana makazi mazuri hasa kule Pemba. Mheshimiwa Naibu Waziri alishakuja, naomba Mheshimiwa Waziri uje, Mheshimiwa Chikawe uje uangalie askari wako wanavyokaa katika zile nyumba. Pale Mkoani zile nyumba hazistahili kukaa na askari wengi wanakaa uraiani na siyo vizuri askari kukaa uraiani. Naomba sana nyumba za askari ziboreshwe ili waweze kufanya kazi kwa ufanisi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Vituo vya Polisi pia navyo hasa kule Pemba Mkoa wa Kusini Pemba, Kengeja na pale Mkoani, kile Kituo cha Mkoani kiko sehemu mbaya sana. Mlima unaporomoka kila siku na mvua kama mnavyoziona. Ninaomba sana mtupie jicho Kituo cha Polisi cha Mkoani na Kituo cha Polisi cha Kengeja ili kuweza kuwaboresha kituo kile kiwe kizuri, waweze kufanya kazi zao kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ajira kwa Askari wa Jeshi na Askari Polisi. Vijana wapo wengi kule Pemba ambao wana maadili mazuri, wamesoma vizuri na ni vijana ambao wako katika nchi yao, kwa hamasa na utulivu na wamesoma vizuri, lakini hapo nyuma walikuwa hawaajiriwi. Watu wanatoka sehemu wanaletwa Pemba kuajiriwa kwa majina yao, wale vijana wa Kipemba hawapati ajira. Nashukuru sasa tumepata uongozi mzuri, tunaye Mkuu wa Mkoa wetu pale Mheshimiwa Mwanajuma Majid na vilevile tanaye Mkuu wa Wilaya wa Chake Chake vilevile ni Mwanamke dada yangu Hanuna Ibrahim na Mkuu wa Wilaya ya Mkoani kaka yangu Hemed Suleiman, najua sasa hili wameshaliona watalifanyia kazi, kwa sababu tunawaamini wanafanya kazi nzuri kwa ushirikiano na wananchi wao. Nawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia posho za askari hasa Askari Polisi na Magereza. Askari Magereza wanajitahidi kulinda wafungwa, ni

kazi kubwa sana, lakini posho zao ni ndogo hazilingani na askari wengine wa Jeshi la Ulinzi. Kwa nini Askari hawa wa Polisi na Mgereza wanapatiwa posho ndogo? Naomba sana Askari hawa Polisi na wao wapate posho kubwa kwa sababu maisha ni magumu. Kila siku tukisimama hapa tunatetea posho za Askari Polisi, lakini kwa nini Serikali inafanya hivi?

Naomba sana Mheshimiwa Naibu Spika, Askari Polisi tuwaangalie na wao wanalinda nchi hii kwa amani na utulivu jamani. Tusingeweza kukaa sisi katika nchi hii, lakini hawa ndiyo wanaotufanya tukae katika nchi hii kwa amani na utulivu tukaleta maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile naomba kuongelea haki za warithi wa marehemu askari. Wapo askari wengi, nimepata hayo malalamiko, wazee wao wamekufa ama waume zao au wake zao wamekufa, lakini haki zao zinacheleweshwa kutolewa. Naomba hili hebu liangalieni, Mheshimiwa Pereira ninakujua ni mchapakazi mzuri, Mheshimiwa Chikawe ninakujua ni mchapakazi mzuri, hebu liangalieni hili. Maafisa wenu waambieni waliangalie hili ili mlete usawa kwa kila askari hapa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupandishwa vyeo kwa askari na nyongeza za mishahara yao; kuna askari wengi tu wa zamani hawapandishwi vyeo wanapandishwa wapya na hatujui sababu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana. Naomba kuunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Faida, ahsante sana. Mheshimiwa Machali, ajiandae Mheshimiwa Amina Makilagi atamalizia!

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru nami kwa kunipa fursa niweze kuchangia Hotuba hizi za Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na Wizara ya Mambo ya Ndani.

Awali ya yote, naomba niseme tu kwamba, ninaipongeza Serikali hii ya CCM kwa kuendelea kuwalipa mishahara kiduchu hasa Jeshi la Polisi, kwa sababu hii inaweza ikaja kuwafanya askari wetu watambue na waone kwamba, Chama cha Mapinduzi hakiwajali kamwe na kipo kwa ajili ya kuwatumia wakati wanahitaji kupitisha mambo ambayo yana masilahi kwao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa najaribu kupitia Kitabu hiki cha Pili ambacho kinaonesha matumizi ya kawaida ikiwemo mishahara ya askari wetu au majeshi yote kwa maana ya Jeshi la Ulinzi na Kujenga Taifa na Jeshi la Polisi. Nimeangalia kwa upande wa Jeshi la Ulinzi kidogo Serikali naona imewakumbuka kwa sababu nimeona kuna nyongeza ya takribani bilioni 213

ambazo zinaongezeka. Kwa upande wa Jeshi la Polisi bado ninaona Serikali hii haijali kazi kubwa ambayo imekuwa inafanywa na Jeshi la Polisi ya kuendelea kutulinda raia wa nchi hii.

Naomba nitoe wito kwa Serikali; Serikali ninaleta swali moja kwenu; ni kwa nini bado mnaendelea kuwalipa ujira tofauti Askari Polisi pamoja na Jeshi la Ulinzi wa Nchi yetu? Ukiangalia kwa upande wa Magereza, nyongeza za mshahara kwa mujibu wa rekodi ambazo zipo kwenye vitabu hivi siyo nzuri. Sasa kazi kwenu Askari Polisi ambao tunakwenda kwenye uchaguzi mwaka huu, muangalie mpime, mwendeleee kukikumbatia Chama cha Mapinduzi ambao wanawatumia kama mabango ya makampuni ya kibiashara au mfanye mabadiliko sasa na kuona hawa jamaa wameshindwa, tunapowaambia wameshindwa na wala hawawajali ni kwa kutumia rekodi ambazo zinajitokeza kwenye vitabu hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiangalia kwa upande wa Askari wa Jeshi la Wananchi, pamoja na nyongeza hiyo ambapo nimeona kuna ongezeko la bilioni 213, bado kazi ambayo wanafanya Jeshi la Wananchi wanastahili kuendelea kuangaliwa kwa jicho pevu, waweze kulipwa zaidi kwa sababu ni kazi ngumu. Tunapata taarifa wanatupigia simu askari wetu ambao wanafanya kazi huko DRC, tunapata taarifa kwa askari ambao wapo huko Sudani na kwingineko, mazingira ni magumu. Kwa hiyo, ni wajibu kwa Serikali ambayo iko makini, kuendelea kuwaangalia na kuwakumbuka Askari Magereza wote ambao wanashughulika na kurekebisha mienendo ya wananchi ambao walitenda makosa mbalimbali ili kuweza kuwa-*shape* waje kuwa raia wema hapo baadaye.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kazi ya Jeshi la Polisi kuhakikisha pia waangalie Uhamiaji, waangalie Askari wa Jeshi la Zimamoto, malipo haya yanaonesha tofauti kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa napitia Taarifa ya Kamati ya Ulinzi na Usalama, wamesema kwenye ukurasa wao mmoja kwamba, posho ya shilingi elfu sita kwa siku haitoshi. Niungane na Kamati na mtazamo wao na *position* ambayo wameichukua. Sijui pengine Serikali itusaidie, hivi hii posho ya shilingi elfu sita ndiyo mnawalipa Askari wa Jeshi la Wananchi; Polisi wanalipwa hiyo shilingi elfu sita; Magereza wanalipwa shilingi elfu sita; Uhamiaji; na Zimamoto wanalipwa shilingi elfu sita au kuna tofauti pengine labda Jeshi la Wananchi wana kiwango chao kama ilivyokuwa huko nyuma? Nitaomba Kauli ya Serikali kuhusiana na viwango hivi vya posho.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mtazamo wangu, nilikuwa nafikiri kiwango ambacho kimependekezwa na Kamati cha kuweza kuwalipa walau shilingi elfu kumi kwa siku, itakuwa ni kiwango kizuri. Serikali fikirieni haya masuala ya

kuwaangalia askari hawa yamekuwa ya muda mrefu, tangu tumekuwa Wabunge hapa kila tukija na kupitia Taarifa za Kamati, Taarifa za Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani na michango ya Wabunge kwa nyakati tofauti, wamekuwa wakisisitiza kuwaangalia askari hawa pasipo kuweka misingi ya ubaguzi. Ninaomba *position* ya Serikali mtaongeze itoke shilingi elfu sita kwenda shilingi elfu kumi au hamtaongeze?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu tunaona tunawashauri sisi Wapinzani, masuala ya kuendelea kutenga pesa nyingi za *hospitality*, pesa za vitafunwa kwenye maafisi, tuzitoe huko wakati mwingine tuzipeleke kwenye maendeleo. Sasa maendeleo ni pamoja na maisha ya askari wetu. Askari wanalalamika wakiwemo wa Jimbo langu, wanalalamika kutokupandishwa vyeo kwa wakati, wanalalamika kupandishwa vyeo kwa misingi ya ubaguzi, wanalalamika kuidai Serikali pesa kwa ajili ya uhamisho, matibabu na hata wanapopandishwa vyeo kama ambavyo wachangiaji wengine wamezungumza, unambandikia cheo askari anajikuta amepata amepata nyota, lakini humlipi stahili zake. Haya ni mambo gani? Mambo ya namna hii yanakatisha tamaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeangalia niende kwa upande wa Askari wa Shirika la Reli. Askari wanaofanya kazi kwenye Shirika la Reli nchini wana malalamiko mengi kuhusu kutokulipwa posho zao mbalimbali. Naomba nipate kauli ya Serikali, askari wanaofanya kazi kwenye Shirika la Reli nchini, maana nimeona hata pesa mmezipunguza kwenye kitabu hiki. Ukiangalia rekodi ya mwaka jana na kiwango ambacho pengine mmetenga kwa ajili ya *allowance* ambazo askari hawa wa Kitengo cha Shirika la Reli wanastahili kulipwa zimepungua. Naomba mnisaidie; hivi Askari hawa mmeweza kuwalipa madai yao yaliyokuwepo huko nyuma?

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nina taarifa nina-*declare interest* kama Waziri Kivuli wa Uchukuzi, wanatupigia simu na wanatueleza kila siku. Nitaomba nipate kauli ya Serikali ni lini matatizo haya yatatatuliwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani mpaka tupate ufafanuzi kutoka Serikalini. Ahsante. (Makofi)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Machali kwa kuunga mkono hoja. Mheshimiwa Amina Makilagi!

MHE. AMINA N. MAKILAGI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja hii muhimu kwa mustakabali wa nchi yetu. Awali ya yote, naomba niungane na wenzangu kumshukuru Mwenyezi Mungu,

Mungu muweze wa yote, aliyetuwezesha kukutana katika Bunge letu Tukufu na leo tunajadili hoja nzito sana kwa maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mara baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu na kabla sijajielekeza katika kuchangia mambo ambayo nimechagua kuyatilia mkazo, naomba nizungumze na wanangu; nizungumze na Lema na mwenzake Machali na wengine wote. Huwa sina tabia ya kuongea na Wabunge Vijana, lakini leo ngoja nitoe elimu kwa watoto wangu kwa sababu kazi ya mama siku zote ni kuelimisha vijana, kazi ya mama siku zote ni kulea familia na leo naomba nitimize wajibu wangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niongee na vijana kwamba, kupitia Kambi ya Upinzani wamesema kwamba, Serikali ya CCM inachochea udini, ukabila na inachochea mambo mbalimbali. Wameeleza kwamba, hii Serikali ya CCM haijali askari hata kuongeza masilahi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwaambie askari wa nchi yetu kwamba, wasidanganyike. Wangukuwa na dhamira njema, hii bajeti ni ya mwisho, tunaelekea kwenye uchaguzi, itakwenda mpaka mwaka kesho; kama kweli dhamira ni njema na kweli mna uchungu na askari hawa, leo mngekuja na bajeti mbadala, mngekuja na mipango mbadala. Kwa bahati nzuri mnasema kwamba, mtakabidhiwa nchi hii, tulitaka kuona ripoti yenu ya leo inakuja na bajeti mbadala, mara baada pengine Watanzania kama wangewaamini mwezi Oktoba 2010 mngejengaje nyumba za askari, mngeboreshaje masilahi yao, mngeongezaje posho, vyanzo vya pesa mngevipata wapi. Leo mngewaambia Watanzania na askari wangewasikia na mimi ningewaamini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ya kuwapaka uji kwenye mdomo wakati leo mnawatukana, mnawaaita watu wa ajabu ajabu, halafu mnakuja kuwadanganya. Nataka niwaambie na bahati nzuri na mimi ni mdau, ni mtoto wa askari tena baba na mama, nimelelewa kambi ya *Field Force*. Kwa bahati njema watoto wa askari na askari wenyewe ni waelewa sana na msije mkajidanganya kwamba, askari wanawaelewa, walishawajua siku nyingi kwamba, ninyi mnawadanganya, hamna mapenzi nao na mngekuwa na mapenzi nao hata katika ile Mifuko yenu ya Jimbo mngeonesha mfano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maana hata kutengeneza gari wakati mwingine OC-CID anakwamba kwa pancha kwenda kushughulikia uhalifu, Mbunge upo wala hufanyi chochote. Wakati mwingine hata service ya gari inashindikana. huwezi kutumia Mfuko wako wa Jimbo hata kuchangia chochote. Mnatumia fedha nyingi mnazopewa hata na watu wasioitakia

mema nchi hii kwenda kufanya maandamano yasiyokuwa na tija na wanawalinda hata bila kuwa na kinyongo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu muda unaniacha, naomba nizungumzie suala la ajali za barabarani. Wanasema eti Serikali ya CCM haina uchungu na wananchi. Nataka niwaambie, msiwadanganye Watanzania, kama kweli mna uchungu na ajali za wananchi barabarani ni mara ngapi hata mmeshiriki hiyo misiba? Ajali za barabarani zinatokea mpo kwenye maandamano hatuwaoni hata katika msiba mmoja, hata katika kutoa pole. Bahati nzuri katika taarifa ya Waziri amezungumza vizuri hatua zinazochukuliwa na Serikali.

Ningependa kusikia katika Taarifa yenu, mnahamasisha jamii yote kwa pamoja tushirikiane na Serikali kuhakikisha tunapunguza ajali za barabarani, kwa sababu mbali na sababu zinazotokea, lakini hata na sisi wananchi wakati mwingine tunachangia kwa sababu gari linakimbizwa na wewe uko mle wala huchukui hatua yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba wasidanganye na askari naomba mtusikilize, endeleeni kuwa na imani na Serikali yenu hii, msidanganyike na watu hawa. Juzi hapa Mzee Lipumba na wenzake walipofanyiwa kashikashi kidogo, mliwasikia walivyowatukana hadi matusi ya nguoni. Mimi nilikuwa nimekaa hapa kwenye kiti, kama mtoto wa askari nilijisikia vibaya sana. Nimeona wazazi wetu wanavyohangaika kwenda kuwalinda huko vichochozoni mpaka usiku, mpaka saa ngapi mnatoka salama, leo mnawaita majina ya ajabu ajabu! Basi niishie hapo, elimu imetoshia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nizungumzie mambo machache yafuatayo:-

Naomba niipongeze Serikali kwa kazi yake nzuri sana inayofanya ya kuendelea kuimarisha ulinzi na usalama na mpaka watu sasa leo wanathubutu wanazungumza. Naona kiongozi hapa mmoja anasimama anamwita Kiongozi wa Nchi muhuni! Wapo hapa na hawamkamati, lakini nchi zingine huthubutu!

Naomba niwaombe askari wetu endeleeni kuwa na moyo wa uvumilivu, endeleeni kuwa hivyo hivyo. Ninawaomba sana hata katika kulinda usalama wa nchi yetu msitumie nguvu sana, kwa sababu ndiyo nia yao, mnapopiga mabomu wao wanashangilia, kwa sababu yale mabomu pia yanahatarisha na watu wengine. Lengo lao siku moja hapa na sisi amani yetu ya Tanzania isitokee. Muendeleo kuwavumilia, tumieni busara na ninajua maarifa mnayo na mimi ninayajua kwamba mnaweza mkatuliza ghasia, mnaweza mkadumisha amani bila kutumia nguvu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niipongeze sana kazi njema inayofanywa ya kuboresha masilahi ya askari. Nimeshuhudia kuna nyumba nyingi za polisi zinajengwa Dar es Salaam na katika maeneo mbalimbali. Mimi mwenyewe ni familia ya askari ninalala katika nyumba hizo, tunashukuru. Naiomba Serikali iongeze bidii. Uwezo wa kufanya hivyo tunao, kama ambavyo tumeboresha kwenye kujenga mashule na bahati nzuri tuna rasilimali. Zamani mimi nilipokuwa kwenye Jeshi nilikuwa ninaona, kulikuwa kuna Kitengo cha Ujenzi, askari wenyewe walikuwa wanajenga nyumba, wanawezeshwa fedha kidogo tu. Kile kitengo kiko wapi?

Ninaomba Serikali ikiboreshe kile Kitengo, ikijengee uwezo, nyumba za askari tujenge askari wenyewe kwa sababu uwezo tunao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie mishahara ...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana.

MHE. AMINA N. MAKILAGI: Muda umekwisha?

NAIBU SPIKA: Ahsante, muda umeisha.

MHE. AMINA N. MAKILAGI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naunga mkono hoja, mwaka 2015 CCM itashinda, tena kwa kishindo! *(Makofi)*

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mwongozo wa Spika!

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Bahati mbaya sana muda haupo upande wetu. Ninakushukuru sana Mheshimiwa Amina Makilagi, mtoto wa *Barracks* huyu. Baba na Mama *Field Force* unafikiri mchezo! *(Kicheko/Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, muda haupo upande wetu kabisa, kwa hiyo, ningepomba nitishe shughuli za Bunge hadi saa kumi kamili jioni ya leo. Ahsanteni sana.

*(Saa 7.55 mchana Bunge lilisitishwa hadi saa 10.00 jioni)
(Saa 10.00 jioni Bunge lilirudia)*

Hapa Mwenyekiti (Mhe. Mussa A. Zungu) Alikalia Kiti

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Hati ifuatayo iliwasilishwa Mezani na:-

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI (K.n.y. WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA):

Randama za Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika kwa mwaka wa fedha 2015/2016.

HOJA ZA SERIKALI

**Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2015/2016
Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi**

na

**Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2015/2016
Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa**

(Majadiliano yanaendelea)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tunaanza na wachangiaji wetu wa jioni na nafikiri walishapangwa asubuhi na Mheshimiwa Naibu Spika. Kwa hiyo, tunaanza na Mheshimiwa Lekule Laizer; hayupo. Mheshimiwa Godbless Lema, ajiandae Mheshimiwa Joseph Selasini!

MHE. GODBLESS J. LEMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nianze kwa kuwapa pole sana Wakazi wa Wilaya ya Rombo, kwa sababu anapotoka Mkuu wa Wilaya hadharani na kutoa tamko alilolitoa ya kwamba, Wanawake wa Rombo wana *import* wanaume kutoka Kenya kwa ajili ya kufanya nao biashara ya ngono na huyo DC mpaka leo bado yuko kazini; kama tunaongelea usalama wa nchi hii, ni pamoja na kuzuwia watu wajinga na wapumbavu kama DC wa Rombo, aliyetoka na kauli chafu ya udhalilishaji wa kiwango cha juu ya Taifa, siyo tu wakazi wa Rombo! Udhalilishaji wa kiwango cha juu wa Taifa kwamba, Rombo sasa wanawake wanachukua wanaume Kenya, kwa hiyo, watoto wanaozaliwa Rombo wote wana uraia wa Kenya na huyu DC bado yuko kazini! Hivi ni viashiria vya uchochezi na uvunjifu wa amani mkubwa sana. Nitashangaa sana kama Serikali itaendelea kumwacha huyu DC mjinga kuendelea kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya ya Rombo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wachangiaji wengi wamesema hapa na mimi nimesema kwenye Hotuba yangu; Jeshi la Polisi ambalo ni nguzo muhimu sana katika usalama wa nchi, wanapokosa masilahi bora, wanapokuwa

wanaombewa posho ya 7,000/= ya chakula, kwenye Hotuba yangu mimi niliruka kiwango cha 7,000/= cha chakula; ni aibu kwamba, leo kila Mbunge anafahamu huwezi kupata chakula hata cha 10,000/= katika hoteli zinazotuzunguka mijini. Leo bado tunapigania posho ya Jeshi la Polisi ya chakula iwe takribani 220,000/=! Taifa linapita kwenye majaribu makubwa sana ya ulinzi na usalama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunaona kuna *attempt* za ugaidi. Leo tunaona kuna *attempt* kubwa za biashara ya madawa ya kulevya. Unapokuwa na Polisi ambaye anaweza aka-*compromise integrity* yake tu kwa sababu ya njaa na Serikali msione umuhimu wa kumlinda Polisi, tena Polisi mdogo wa nchi hii!

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo wachangiaji wamechangia hapa kwamba, kuna mahali Polisi ambao wako mipakani wanaopaswa kuzuwia waingiaji haramu, hawana hata gari! Polisi wa nchi hii wanaishi maisha magumu sana. Kimsingi, Polisi wa nchi hii wanaishi maisha kama vibaka, isipokuwa tu wamevaa *uniform*, ni kwa sababu Serikali haiwajali, mishahara yao ni midogo, hawawezi hata kulinda familia zao. Ndiyo maana nchi hii unakuja ku-*realise* kwamba, Polisi anazaa polisi na mtoto wa polisi naye anazaa polisi! Kwa sababu, ndiyo kazi ambazo Askari Polisi anaweza akamwachia mtoto wake urithi, kwa sababu ni kazi ambazo kwa kweli wana kazi kubwa, wana kazi ngumu, lakini mishahara yao ni midogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tahadhari, tunapokuwa na Jeshi linalonung'unika dhidi ya njaa, tunapokuwa na Jeshi linalonung'unika dhidi ya maisha yao, tunapokuwa na Jeshi ambalo halimudu kupeleka watoto shule, tunapokuwa na Jeshi ambalo matibabu yao ni mgogoro; maana yake ni kwamba, mnatengeneza kundi la majambazi ama kundi la wahalifu ambalo limevaa *uniform* na siku moja wakigeuka nchi hii inaweza ikawa ni mahali pabaya sana pa kuishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe sana kuelekea Uchaguzi Mkuu tunaona mmeongeza magari ya kuwasha, mmeongeza *Land Rover* kwa ajili ya kudhibiti watu kwenye uchaguzi, fujo kwenye uchaguzi hazitadhibitiwa na wingi wa polisi. Fujo kwenye uchaguzi zitadhibitiwa na uchaguzi utakaokuwa na mazingira huru na haki. Kukiwepo na mazingira ya uhuru na haki mnaweza mkalinda uchaguzi hata kwa kutumia ma-*miss* acha polisi. Kama kutakuwepo na *grounds* ambazo ziko *fair*, mnaweza msitumie hata kirungu kimoja kupiga mtu, lakini kuongeza magari ya kivita, magari ya ku... *(Makofi)*

(Hapa Sauti ilikatika ghafla)

... kama mna mkakati. Hii ni mikakati ya kuiba kura!

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2010 niliwaambia watu wangu waje na silaha zote halali ambazo wanaweza kuja nazo kuchunga kura. Niliambiwa kwamba, natishia usalama wa Mkoa, nikasema hapana hazitatumika, zitatumika tu kuzuwia mwizi wa kura. Kimsingi, hazikutumika kwa sababu wizi wa kura haukuwepo. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali isiongeze magari ya polisi, Serikali nisiongeze vijana wengi wa polisi, Serikali isiongeze wapiganaji. Serikali ifanye utafiti ni wapi inakosea katika msingi wa kuendesha nchi katika Utawala Bora, unaojali demokrasia na haki. Tukiwa na utawala wa haki, tukiwa na uchaguzi utakaofuata misingi ya haki, hakika ni kwamba, Mheshimiwa Waziri Chikawe, *my brother*, hautapiga risasi moja wala bomu moja halitatumika. Kwa hali ilivyo hata mkiongeza Polisi wa Irani, mkaongeza Polisi wa Kongo, uchaguzi wa mwaka huu tunataka uwe halali. Siyo kwa sababu tunataka kushinda, ila tunataka ku-*gamble* peace ya nchi hii iwe na thamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hali ilivyo sasa na uandikishaji unavyoendelea, Mheshimiwa Waziri naomba unielewe, inawezekana kabisa kutatokea idadi ya nusu ya watu nchi nzima watakuwa hawajaandikishwa. Hili *group* la watu wakiamini kiongozi wao aliyeshindwa ilitokana na idadi kubwa ya watu kutokuandikishwa, mtaanza kutengeneza magenge ya watu watakaofikiria demokrasia siyo *alternative* na wataanza kutafuta njia nyingine ya kutafuta ukombozi. Vilevile ni hatari sana Serikali ikiwapeleka watu kufikiria kwamba, demokrasia siyo njia ya ukombozi, isipokuwa njia nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, amani ya nchi hii itavurugika. Amani ya nchi hii haitajengeka kwa porojo na propaganda za kwenye magazeti na *television!* Amani ya nchi hii itajengeka kwa sababu ya kuwa na utawala unaodumu katika haki... *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Rage!

T A A R I F A

MHE. ISMAIL A. RAGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumpa taarifa Msemaji aliyemaliza kuongea kwa mujibu wa Kifungu Namba 68(7), asitumie lugha ya kuudhi ndani ya Bunge. Kama anataka kupima aangalie wakati tulipofanya uchaguzi, Kata 27 wametumia *chopper* 3, wamepata Madiwani watatu! Katika kura za Serikali za Mitaa tumewapiga vizuri sana. Wanajeshi wetu na Askari Polisi wetu wanafanya kazi nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa aangalie kauli yake. Upinzani ni kutoa hoja siyo kutoa lugha ya kutukana na ya kujidhalilisha. (Makofi)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Lema muda wako umeisha, nakuomba ukae.

Mheshimiwa Selasini!

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii niyapongeze Majeshi yetu yote; Jeshi la Wananchi, Jeshi la Polisi, Jeshi la Magareza, JKT, Jeshi la Uhamiaji na vilevile Jeshi letu la Zimamoto, kwa kazi wanayoifanya katika mazingira mbalimbali, mazingira magumu, lakini katika moyo wa kulihudumia Taifa letu. Pamoja na pongezi hizo, niseme kwamba, miongoni mwao na kama binadamu, lazima kuna baadhi ya wapiganaji na askari walioingia katika Majeshi hayo ilhali siyo mahali pao na hawa ndiyo tunaowalalamikia. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ningepomba sana Viongozi wa Vyombo hivi, waangalie baadhi ya Watendaji katika Majeshi haya ambao wanachafua sifa nzuri za haya Majeshi na kuwaondoa haraka iwezekanavyo. Jambo la ajabu kumkuta Askari wa Jeshi la Wananchi anapigana mtaani na raia! Jambo la ajabu kumkuta Askari Polisi anapigana hovyohovyo na raia au amelewa hovyohovyo na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nizungumze zaidi kuhusu Jimbo langu. Nataka nimfahamishe Waziri kama alikuwa hana taarifa, lakini nina hakika Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani anajua. Pale Rombo, wananchi wa Rombo wanajenga kwa nguvu zao, kwa kujitolea na kwa kushirikiana na Mbunge wao, Kituo cha Polisi Mahida, Kituo cha Polisi Mengwe, Kituo cha Polisi Kirongo Chini, Kituo cha Polisi Useri na kwa kusaidiana na Mbunge, Polisi wamekamilisha ujenzi wa Bwalo lao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Jengo la Polisi pale Mkuu Mjini, *Central Police*, linavuja kiasi kwamba, hata wananchi wanapoitwa kwa ajili ya kuandika mashauri yao, mvua ikinyesha wanavujiwa! Nimemuahidi *OCD* nitampa 5,000,000/= kabla ya mwisho wa mwezi Juni; ninaomba Mheshimiwa Waziri utusaidie pamoja na fedha hizo, kukarabati lile jengo, ili liweze kuwahudumia wananchi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika bajeti ya mwaka 2013/2014, nimekuwa nikizungumza kwamba, Askari Polisi pale Rombo pamoja na Askari Magareza, majengo wanayoishi yanalitia aibu Jeshi la Polisi. Tunasikia ujenzi wa majumba

ya Polisi mijini kwenye miji mikubwa, Dar es Salaam, Arusha na kadhalika, lakini kwenye Mawilaya, kama Wilaya ya Rombo, hakuna kinachoendelea! Tusaidieni, ili Polisi wapate amani, wawe na furaha wanapotoka kazini na kwenda kuwatumikia wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo ziko posho mbalimbali za askari hawa. Hili ninalizungumza kwa nchi nzima; hazitolewi kwa wakati na hazitolewi kabisa! Wakati mwingine mimi napata mawazo Polisi wanapotumia nguvu isiyotakiwa kwa raia, labda pengine kwa sababu ya hasira na uchovu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nawaomba sana, muangalie uwezekano wa kupeleka posho stahiki za Askari Polisi na za Majeshi mengine kwa wakati. Kwa sababu hainiingii akilini kumkuta Askari anauza *chips* ili aweze kupata namna ya kuisaidia familia yake! Haiingii akilini nimkute askari yuko baa anaendesha baa apate namna ya kujikimu! Hayo sisi tunayaweza, askari hawayawezi! Kwa sababu gani fedha zao hazipelekwi kwa wakati?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiacha hilo acha nizungumze suala hili la posho, limepigwa kelele sana. Hivi jamani kweli Serikali hamwoni umuhimu wa kutoa posho stahiki kwa Askari Polisi, Askari wa Magereza, Askari wa Uhamiaji na kadhalika? Posho inayotolewa, tumepiga kelele sana ni ndogo, iongezwe walau mpaka 10,000/=. Hiki kigugumizi ni cha nini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningependa kusema, pamoja na kazi nzuri ambayo Jeshi la Polisi inafanya, naomba Jeshi la Polisi wajitahidi kutojiingiza katika mitego ya wanasiasa. Juzi Naibu Waziri wa Fedha alisimama hapa akasema kwamba, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam wanafunzi wamegoma kwa sababu ni kweli Serikali haijawapelekea fedha. Sisi tukategemea kwamba, fedha zingepolekwa ili wananchi hawa waishi kwa amani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii Bunge linapoendelea wanafunzi wa UDOM wamepigwa sana na Jeshi la Polisi! Kisa ni kidogo tu, wanadai fedha za kujikimu, wanadai fedha za chakula waishi kama watoto wetu wanavyoishi. Hivi ninavyozungumza, Chuo cha Mifugo – Tengeru, watoto wamejikusanya wanataka kuingia mtaani. Vyuvo nvyote vina sintofahamu! Sijui Askari Polisi mnaona fahari gani kwenda kuwapiga watoto, miongoni mwao ni watoto wenu. Hata kama ni kuzuwira fujo, hivi fujo haiwezi kuzuilika bila kutumia marungu? Bila kutumia mitutu ya bunduki? Hakuna namna nyingine yoyote ya kuweza kuwa-*contain* wale watoto wakaeleza shida zao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili siyo zuri kabisa. Tunaenda kwenye nchi za wenzetu, tunaona migomo inavyokuwa *treated*, jinsi ambavyo Majeshi

ya wenzetu yanavyozuwia migomo kama hii ya wanafunzi ambao hawana kisu, hawana jiwe, hawana chochote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sana jambo hili liangaliwe; hiyo migomo askari watafute namna ya kuishughulikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, ningependa kurudia yaliyosemwa na wenzangu; nchi iko katika sintofahamu, tunasikia hadithi za ugaidi, tunasikia habari ya udini na kadhalika. Ninaomba sana fedha zilizotengwa kwa ajili ya Vyombo vya Ulinzi na Usalama zipelekwe, ili sote tuweze kujihakikishia ulinzi wa nchi yetu, amani ya nchi yetu, badala ya kupeleka fedha katika Majeshi haya kwa kudunduliza na hivyo kuyafanya yashindwe kufanya kazi zake sawasawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kusema kwamba, kuna wafanyabiashara ambao wanapeleka vitu katika Majeshi yetu, wana-supply vyakula na kadhalika. Ninaomba vilevile deni hili la ndani lilipwe, ili Magereza yahudumiwe vizuri na haya Majeshi yetu yahudumiwe vizuri na vilevile hawa wafanyabiashara wapewe fedha zao ambazo nyingine ni za mikopo kwenye mabenki. Wengine nasikia wameshapata *pressure* wakafa kwa sababu ya kudaiwa na mabenki. Mabenki yanataka kuuza vile vitu ambavyo wameweka rehani kama dhamana. Sasa hii ni aibu kwa Serikali. Ninaomba sana hili liangaliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, niseme kwamba, haya yaliyotokea katika Jimbo langu la Rombo kweli yanasikitisha na yanatia uchungu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Yussuf Salim, ajiandae Mheshimiwa Laizer!

MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN: Mheshimiwa Mwenyekiti, *Bismillah Rahman Rahim*. Namshukuru Mwenyezi Mungu na mimi kupata nafasi jioni hii kuchangia Wizara mbili zilizo mbele yetu. Hizi ni Wizara muhimu sana, lakini kwa masikitiko makubwa zimepangwa siku moja ili tushindwe kuchangia kwa ukamilifu. Kwa uwezo wa Mungu tutajitahidi tuzungumze machache na ninadhani yataeleweka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianza katika Wizara ya Ulinzi katika ukurasa wa 9 na wa 10, Hotuba ya Waziri amezungumzia masuala ya ugaidi na mambo yanayofanana na hayo. Naye amezungumza vizuri namna gani tunaweza sasa kupambana na vita hiyo. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri hapa sasa inatuonesha kwamba, Dunia imeondokana na ile vita ya *conventional* na sasa tunaenda katika *convetional war!* Kwa hiyo, ni lazima Watanzania tujipange kukabiliana

na vita hii. Tutawezaje kujipanga na vita hii kama hatutakuwa na mpango madhubuti ambao utaingia katika Sera ya Taifa ya *National Defence Force* ambayo itatuwezesha kukabiliana na vita ya namna hii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima tuwe na Sera ya Kitaifa ambayo itatuwezesha kuingia kukabiliana na vita ya namna hii, vinginevyo, tutakuwa tunajidanganya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuwezesha kukabiliana na vita hii ni lazima tuwe na kikosi kizuri sana ambacho ni *Special Force*. *Special Force* ambayo imetayarishwa vizuri, ina mafunzo ya kisasa, ina vifaa vya kisasa, ina masilahi mazuri na wametayarishwa kizalendo kwelikweli. Kama ulivyosema mwenyewe kwamba, vita hii inapiganwa katika mambo haya kisasa ya teknolojia ya kisasa ya TEHAMA. Kwa hiyo, ni lazima tuwe na kikosi ambacho kinakuwa kimepangwa vizuri kweli kweli; vinginevyo, tutashindwa.

Umezungumza katika ukurasa 33 kwamba mmenunua vifaa katika Mwaka wa Fedha Uliopita, lakini sina hakika kama vifaa hivyo viko *special* au vimetayarishwa *special* kwa ajili ya hawa *Special Forces*.

Tutoe mfano kwa wenzetu tu hapa Kenya, juzi hapo Garissa, Westgate, lakini tuchukulie Mungu ayaepushe mbali, sasa hivi tuvamiwe hapa; je, *Special Force* wetu wana helicopter za kuja kutuokoa hapa? Wana ndege ambazo zitawafikisha hapa kwa wakati kuja kutokuoa? Kwa hiyo, lazima jeshi letu lijipange kisasa kukabiliana na vita ya kisasa ambayo iko duniani, *otherwise*, tutaingia katika matatizo makubwa.

Sikuona katika kitabu hiki, Tanzania sasa hivi tunapeleka vijana wetu wengi nchi za nje katika kulinda amani. Tumewapeleka hapo Kongo katika *Chapter Six*, ile ni vita, lakini sijaona kwamba askari wetu angalau wale ambao wamekuwa *assigned* kwenda pale wamewekewa *insurance*. Inaumiza sana, tunaletewa maiti tu hapa katika masanduku, lakini je, vijana wetu hawa wana *insurance*? Kwa hiyo, kama hawana *insurance* ninaloomba vijana hawa waingie katika *insurance* ili wakienda vitani wajue masilahi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisikitike sana na Jeshi la Ulinzi na Mheshimiwa Waziri upo hapo na kama Mkuu wa Majeshi yupo ananisikia. Tunasikitika sana Jeshi letu kwa heshima iliyonayo, lakini kama alivyosema kaka yangu Iddi Azzan, kuna viashiria ndani ya nchi yetu vya kuvunjika kwa amani na viashiria hivi viko waziwazi na kwa ushahidi wa kutosha kule Zanzibar. Kama Mheshimiwa Waziri unafahamu ama hufahamu, jeshi lako kwa kutumia magari yake na makambi yake, yanawachukua vijana kutoka katika Ofisi za Chama cha Mapinduzi na kuwapeleka katika kambi zao kuandikishwa kupewa Vitambulisho vya

Uzanzibari Mkaazi. Tunaliomba sana Jeshi la Wananchi wa Tanzania, amani ya nchi yetu isije ikaingia katika mikono yao. *(Makofi)*

Tunawaomba sana, tunawaheshimu sana, wawe waadilifu na wahakikishe wanafuata Sheria Namba Tano, hawatakiwi kujiingiza katika masuala ya kisiasa. Sina hakika kama Mheshimiwa Waziri na Mkuu wa Majeshi mnaelewa hali ile, lakini kwa Zanzibar ipo wazi na ushahidi tunao. Linalotusikitisha zaidi ni kutaka kugombanishwa kati ya pande mbili za Muungano, vijana halisi wa kizanzibari hawapewi Vitambulisho vya Uzanzibari, badala yake wanachukuliwa vijana kutoka Tanganyika na kuletwa pale kujiandikisha kupewa Vitambulisho vya Uzanzibari Mkaazi ili waingie katika Daftari la Wapiga Kura. Ieleweke kwa Watanzania wote kwamba, zumari ikilia Zanzibar huchoza walioko Bara, amani ikichafuka Zanzibar na Tanganyika pia hakuna amani. Tunaliomba Jeshi la Wananchi wa Tanzania katika hili lihakikishe haliingii hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije sasa katika Wizara ya Mambo ya Ndani. Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani, kuna kijana Pemba anaitwa Said Ali Abdallah, ameondoshwa Pemba ameletwa Zanzibar kwa kusema tu kwamba, CCM Zanzibar inauliwa na Balozi Seif Ali Iddi. Vitendo vyake anavyovifanya ndiyo vinavyoiua CCM Zanzibar. Kijana huyo amehamishwa Pemba ameletwa Zanzibar anateswa. Kwa hiyo, tunakuomba Mheshimiwa Waziri suala hili ulifuatilie.

Inashangaza kusema Jeshi la Polisi halina uwezo wa kuhudumia shughuli hizi, mimi nakataa katakata; kwa sababu kuna vitendo vinatokea, wamepigwa wananchi wetu siku ya tarehe 29 wanatoka katika mkutano Makunduchi, wameumizwa wengine wako India sasa hivi wanatibiwa, imechomwa moto ofisi yetu ya Jimbo hakuna mtu yeyote aliyekamatwa. Jeshi la Polisi wanasema wanashindwa kufanya hivyo, lakini juzi tu, wiki moja iliyopita, Mkoa wa Kusini Pemba, RPC ameibiwa kuku wake baada ya saa mbili tu wezi wamekamatwa. Kwa hiyo, ni dhahiri kwamba, uwezo upo...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Laizer, ajiandae Mheshimiwa Njwayo!

MHE. MICHAEL L. LAIZER: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie Wizara hii. Natanguliza kusema kwamba, naunga mkono bajeti za Wizara zote mbili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na ujenzi wa Makao Makuu ya Wilaya ya Longido. Wilaya ya Longido haijawahi kujengewa jengo lolote tangu tupate

Uhuru. Majengo yaliyoko pale ni ya kikoloni, hakuna jengo liloongezwa, sasa utashangaa kama Makao Makuu ya Wilaya haina majengo hata Ofisi ya Makao Makuu pale Polisi hawana.

Nawapongeza sana Polisi wa Logido, siku hizi wamechanga wenyewe na kuanza kujenga jengo kubwa, ofisi kubwa. Naomba Serikali iwasaidie iwaongeze nguvu kwa ajili ya kujenga jengo hilo ili polisi waweze kuwa na ofisi hata *lockup*, waweze kuwa na majengo mazuri kama hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni nyumba za polisi katika Kata ya Gelaibomba. Wananchi wamejitahidi sana wamejenga Kituo cha Polisi, kimemalizika lakini hakuna hakuna nyumba za askari. Nawapongeza Makao Makuu ya Polisi, Makao Makuu ya Arusha, walisaidiana na wananchi kujenga hilo mpaka likamalizika, ni jengo nzuri lakini hakuna nyumba za polisi, naomba Wizara hii itusaidie kujenga nyumba polisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni mishahara wa polisi. Naomba sana tuwaangalie polisi, ni watu muhimu, wanafanya kazi saa 24, wanaitwa wakati wa vita na majambazi wakituvamia tunawaita polisi. Nadhani watu wengine wote wanakimbia kujificha, polisi tu ndiyo wanakuja kupambana na hao majambazi. Naomba sana tuone umuhimu wa kuwaongezea mishahara na posho zao ili waweze kufanya kazi kwa uaminifu. Tunasema kila siku polisi wanakula rushwa, ikizungumziwa rushwa ni Polisi na Mahakama, basi tuwaangalie. Mimi nadhani ni kwa ajili ya mishahara midogo ambayo haitoshi. Naomba mishahara ya polisi pamoja na posho tuwaongeze ili waweze kufanya kazi kwa ufanisi. *(Makofi)*

Jambo lingine ni vitendea kazi katika Wilaya ya Longido. Wilaya ya Longido ni Wilaya ya mpakani, tunapakana na Kenya, kwa mpaka mrefu sana kuanzia Rombo mpaka Lake Natron, ni kilomita 360, urefu wa mpaka huo. Kuna kituo kimoja tu cha Namanga, sasa hicho kituo hakiwezi kufanya kazi katika mpaka ule kwa sababu ni mrefu. Majambazi wengi wanaotoka huko pamoja na maharamia wote wanapita katika mpaka wa Longido kuingia Tanzania. Kwa hiyo, naomba vitendea kazi viongezwe katika ukanda huo, pamoja na polisi wa kutosha, ili waweze kufanya doria katika mpaka ule. Naomba tuongezewe vitendea kazi pamoja na pikipiki na magari.

Wakati huu wa uchaguzi tuko katika kipindi mgumu, ili kuondokana na tuhuma kwamba polisi wamechukua rushwa, naomba waongezewe posho ili waweze kufanya kazi hii kwa ufanisi.

Jambo la mwisho, ni vijana wanaochaguliwa kujiunga na Jeshi la Polisi. Tunashukuru kila Wilaya wana nafasi, lakini uchaguzi unaofanyika katika Wilaya yangu siyo sahihi; na ndiyo maana katika Wilaya za wafugaji huwaoni wafugaji wakiwa katika Jeshi la Polisi, kuna upendeleo mkubwa sana. Mnafahamu

kwamba, Wamasai ni jasiri wanaweza kuingia katika Jeshi la Polisi lakini hawapo na uchaguzi unaofanyika kwa ajili ya kujiunga na Jeshi la Polisi una ubaguzi mkubwa. Wale watu wanaokuja kufanya *interview* wanakuja na majina, unakuta watu wa Longido wanaoijiunga ni watatu, watu wengine wametoka katika wilaya zingine, wanakuja na majina. Kwa hiyo, kuna upendeleo mkubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nafasi hizi katika wilaya zetu na sisi tujiunge na jeshi kulinda Watanzania. Sisi tuko imara kabisa kuulinda nchi. Tunaomba nafasi hizo zitolewe kwa upendeleo kwa sababu tumekaa miaka mingi hatujawahi kuhesabiwa katika Jeshi hili Polisi, tumekaa tu kuwa walinzi wa nyumba zenu. Tukilinda nyumba zenu mnatuamini, msituamini kwa ulinzi wa nyumba tu, tunaweza kuulinda na nchi. Kwa hiyo, naomba usifanyike ubaguzi tena katika jambo hili. Kama ni wa Longido, kama Simanjiro, kama ni Ngorongoro, wachaguliwe vijana katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Njwayo!

MHE. JUMA A. NJWAYO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi jioni hii niungane na Wabunge wenzangu kuchangia Hotuba za Bajeti za Wizara mbili zilizoko mbele yetu. Awali ya yote, napenda kwanza kutoa shukrani za dhati kwa Wananchi wa Jimbo la Tandahimba, kwa kunipa ushirikiano katika kipindi chote cha uwakilishi wangu kwao. Imani yangu ni kuwa, wataendelea kuniamini ili niweze kuendeleza au kushirikiana kwa mafanikio tuliyoapata. Naomba kuwapongeza Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Dkt. Hussein Ali Mwinyi na Waziri wa Mambo ya Ndani ndugu yangu Mwanasheria Wakili Mathias Meinrad Chikawe, kwa kazi nzuri wanazozifanya kwa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa pamoja na Wizara ya Mambo ya Ndani. *(Makofi)*

Baada ya kusema haya, kama maelezo yangu ya awali, nina maoni na ushauri kwa Serikali kama ifuatavyo:-

La kwanza, Jeshi la Zimamoto ni muhimu sana kwa ajili ya kupunguza vifo, majeruhi, uharibifu wa mali kwa njia ya moto, mafuriko, ajali za barabarani, kimbunga na kadhalika. Pamoja na jukumu hili la msingi na zito walilionalo, jeshi hili halijapewa kipaumbele nchini. Mifano ni mingi lakini mimi nitasema michache tu; wakati vinahitajika vituo 152 nchini, yaani vifike mpaka Mawilayani, wana vituo 52 tu. Wakati yanahitajika magari 280, wana magari 53 tu. Katika bajeti hii wametengewa gari moja tu. Ndugu zangu nilitangulia kusema, jukumu la msingi walilionalo Jeshi hili la Zimamoto na Uokoaji. Kwa nini tunafanya hivi? Ni vizuri tukaweka mkakati wa makusudi wa kuhakikisha

tunasaidia jeshi hili, kwa sababu tukiwekeza kwenye jeshi hili tutapunguza matatizo mengi kama ambavyo awali nimesema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo langu la pili nataka kuipongeza Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, kwa kuwa na mpango wa kuanzisha Chuo cha Sayansi ya Tiba pale Lugalo. Mimi naamini Chuo hiki licha ya mafunzo, lakini kitafanya utafiti wa mambo mbalimbali ya tiba pamoja na ulinzi, kitajaribu kutoa elimu ya fani ya tiba kwa raia na askari. Rai yangu basi, Serikali pamoja na Wizara hii ijitahidi kuhakikisha kila kambi nchini inapata vifaa vya tiba vya uhakika ili si tu wananchi, lakini na askari wanapopata maradhi au ndwele, waweze kupata tiba ya uhakika. Si hivyo tu, kituo kile kisaidie, ikitokea madaktari au wauguzi wamegoma, wao wa-*take over*, maana itasaidia sana, wakiwa na wataalam wengi wa kutosha wanaingia mara moja kuziba tatizo lililoko. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni la NIDA. Hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani, ukurasa wa tisa na ukurasa wa 42, amejaribu kueleza mambo mengi yanayofanywa na NIDA kwa sasa; uandikishaji, idadi na mambo mengi. Mimi nina shida sana; hivi ni lini NIDA itakamilisha zoezi la kutoa vitambulisho kwa Watanzania waliojiandikisha tangu 2012?

Leo kuna Watanzania wengi wanalalamika, wakienda kwenye ofisi hizo walizojiandikishia wanaambiwa nenda kwenye Kata. Ninaye ndugu yangu mmoja siyo lazima nimtaje, amekuwa akilalamika kila siku akienda, tena huyo alifanya kazi vizuri, alikuwa daktari Wizara ya Afya pale, amestaafu sasa, Mtanzania mpenda nchi yake, anataka kitambulisho tu cha Uraia wa Tanzania. Wako wengi watu hawa, kila siku nenda rudi, wanaambiwa nenda kwenye Kata, njoo baada ya miezi miwili! Jamani tumalize tatizo, Watanzania wanataka vitambulisho vyao, walishapewa risiti walipojiandikisha mwanzoni, lakini vitambulisho vyenyewe hawapati. Tutafute dawa, tutafute ufumbuzi, tusiwasumbue Watanzania, wanaacha kazi zao kwa sababu ya kufuatilia vitambulisho tu. (Makofi)

Mheshimiwa Waziri, nadhani hilo ni jambo dogo mno wala hatuna sababu. Nilikuwa nafuatilia fuatilia walipokuwa wanapita watu wa NIDA kufanya *sensitization* kwenye Mikoa au Mawilaya, kumekuwa na tatizo pia, unakuta wale wadau waliowaita kuwapa semina za *sensitization* wanakaa pale hawana posho. Posho wanapata baada ya siku tatu, nne au tano, mnaanza kugombana hatufanyi kwa sababu posho haipo; why?

Tutafute dawa ya mambo yetu ili kazi inapofanyika na kila stahili inayotakiwa ipatikane wakati huo huo badala ya kungoja. Kama mjuavyo, haki inayocheleweshwa mwajua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninalo jambo lingine, kule jimboni kwangu liko eneo linaita Chiumo. Chiumo ni Shamba la Magereza, linalomilikiwa na Magereza wakati ule ikiwa Wilaya ya Newala. Shamba lile liko muda mrefu, Magereza walikuwa wanalima pale kwa muda mrefu, lakini baadaye ni kama wameli-condemn hivi, hakuna kinachoendelea pale. Watanzania wa Kata ya Mkolea na Maundo, wana tatizo la ardhi. Kama Magereza wanaona hawana sababu ya kuendelea kufanya shughuli za kilimo pale, wawaachie wananchi wale wa Mkocha, Mkolea na Maundo wafanye kazi, badala ya kung'ang'ania tu. Watu wanataka...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Mwaiposa, ajiandae Mheshimiwa Chatanda!

MHE. EUGEN E. MWAIPOSA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia hoja ambayo iko mbele yetu. Niungane na wachangiaji waliotangulia, kuwapongeza Mawaziri wa Wizara zote mbili na Watendaji katika Wizara hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi zangu hizo, napenda kuchangia jambo linalohusiana na hali ya maaskari. Katika Jimbo la Ukonga, eneo hilo la Ukonga lina wakazi wengi ambao ni askari. Mimi ninataka kuchangia kuhusiana na hali zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka sasa hali za maaskari hasa Askari Polisi, Askari Magereza na FFU siyo nzuri, bado wana makazi duni sana na wengine au wengi wao bado wanaishi uraiiani. Nafikiri ni mara ya pili kuongelea jambo hili katika Bunge lako Tukufu. Naendelea kuiomba sana Serikali iangalie ni namna gani inaweza kuboresha makazi pamoja na hali halisi ya maisha ya askari. Tunajua kabisa kwamba, usalama tulionao sasa hivi ni kwa sababu jeshi letu pamoja na askari wetu, wako kazini usiku na mchana. Sasa kama hatutawatendea haki ya kuhakikisha mishahara yao na maeneo yao wanayoishi yameboreshwa, tunaweza tukafikiria tuna ulinzi mzuri lakini baadaye tukajikuta hatuna ulinzi mlinzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili la mishahara limekuwa ni la muda mrefu. Hivi sasa kwa mfano, *Staff Sergeant* aliyepandishwa cheo mwaka huu anapata mishahara sawa sawa na *Staff Sergeant* aliyepandishwa cheo hicho hicho kwa miaka mitano. Watu hawa wanapandishwa vyeo lakini mishahara yao haipandi. Tunajua kabisa kwamba, kwenye majeshi kuna nidhamu ya hali ya juu na *seniority* kwao ni kitu muhimu sana. Sasa kama kuna askari ambao wana vyeo vinavyofanana, kinacho-matter pale ni *seniority*, lakini *seniority* hii kwa hali

halisi haiendani na mishahara yao. Ninamwomba sana Mheshimiwa Waziri ahakikishe jambo hili linarekebishwa ili askari hawa waweze kupata haki zao za msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hilo niwapongeze sana askari hawa na Serikali kwa jinsi ambavyo wanashirikiana na wananchi katika suala zima la ulinzi shirikishi. Ulinzi shirikishi ni jambo ambalo limesaidia sana kuweka hali kuwa tulivu katika maeneo mengi ya wananchi. Ninaomba sana, vijana hawa ambao wengine wanapata ajira kutokana na watu wengine kushindwa kulinda, wapatiwe vifaa kama vile mabuti au viatu, lakini hata virungu pamoja na pikipiki kwa ajili ya kuwasaidia kufanya shughuli zao katika maeneo ya jamii wanakoishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashauri sana waendeleo kutumia kwa kiwango kikubwa wale waendesha pikipiki. Hawa wanaoendesha pikipiki wakitumika vizuri wanaweza wakawa walenzi wazuri sana wa Taifa letu. Kwa sababu wao mara nyingi ndiyo wanaobeba watu, wanasikia wanaongea nini, hata mara nyingine huwa wanawabeba wahalifu. Kwa hiyo, wakishirikishwa vizuri katika ulinzi shirikishi ni moja kwa moja tunaweza tukawa na uhakika kwamba, ulinzi wa raia na mali zao unaweza pia ukachangiwa na watu hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitazungumzia suala la mahusiano kati ya Jeshi hili la Polisi na Raia. Kumekuwepo na malalamiko makubwa, ni kweli kwamba, askari hawa wanafanya kazi nzuri, lakini saa nyingine wanashindwa kuelewa kwamba, kuna hata utaratibu tu ule wa kumwelekeza mtu anapokosea mahali, siyo lazima apate adhabu au anyanyasike. Ninawaomba waendeleo kuwa watunza amani wazuri na hasa hawa bodaboda. Bodaboda wanakamatwa na hawa askari hasa wale ambao siku hizi wanaoitwa tigo. Wanawasumbua na kuwanyanyasa sana waendesha bodaboda, naomba hawa vijana wanafanya kazi ngumu, lakini wanafanya kazi katika mazingira magumu pia. Niwaombe sana askari, hebu wajaribu kuwaelimisha badala ya kuchukua muda wao mwingi kuwashika vituoni pamoja na kuchukua fedha za rushwa ambazo kwa kweli zinawanyanyasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo limeongelewa ni suala la *NIDA*. Vitambulisho ni muhimu sana ili kuweza kumjua raia ni yupi na asiye raia ni yupi, lakini mradi huu umechukua muda mrefu sana. Ninaiomba Serikali, ninajua kabisa kwamba tatizo ni fedha, naomba sana Serikali ijaribu kuangalia ni namna gani inawekeza katika Mradi huu ili wananchi waweze kupata vitambulisho ambavyo vitawasaidia sana kujitambulisha mahali popote pale ambapo wanatakiwa kufanya hivyo. Bila kuwa na kitambulisho inakuwa ni shida sana na nchi yetu ni kweli kabisa watu wamekuwa wanaingia na kutoka, huwezi kujua ni nani Mtanzania na nani siyo Mtanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaiomba Serikali na kuishauri kwamba, vitambulisho ni muhimu sana kupita maelezo. Uhakikishe kwamba, Bajeti hii itakapopita hapa sasa, Kitengo hiki au Mradi huo unapata fedha za kutosha ili wananchi waweze kuondokana na usumbufu wa kuambiwa nenda rudi vitambulisho bado havijawa tayari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi ya hapo labda niendeleo kusema kwamba, Jeshi letu tunalipongeza linafanya kazi nzuri. Majeshi haya ya Polisi na Majeshi mengine wanafanya kazi nzuri. lakini wanahitaji sana kupewa ushirikiano ili kuhakikisha ulinzi katika nchi hii unaimarika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nashukuru kwa kupata nafasi, lakini niseme pia kwamba ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Chatanda, ajiandae Mheshimiwa Shibuda!

MHE. MARY P. CHATANDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia Hotuba iliyo mbele yetu, iliyowasilishwa na Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi pamoja na Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Aidha, naomba nitangulie kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianza na Hotuba ya wenzetu wa Upinzani, iliyosomwa na Godbless Lema, ndugu yangu rafiki yangu, juu ya hali ya usalama na amani ya nchi yetu. Katika kile kitabu, ukurasa wa nne, ameeleza suala la uchochezi wa kidini na kikabila na kuitamka kwamba, Serikali ya CCM ndiyo inayofanya uchochezi wa kidini na kikabila.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwaambie Watanzania kwamba, ndugu yangu Lema kauli anazozitoa siyo za kweli bali ni za uchochezi mkubwa, ni za uzandiki mkubwa. Nchi yetu hii ya Tanzania wananchi wake wanaishi wako huru, wanakwenda wanaishi mahala popote pale wanapotaka, hawaulizwi ukabila wala hawaulizwi wewe ni dini gani. Nikitolea mfano ni pamoja na yeye mwenyewe Godbless Lema, Lema amechaguliwa Mkoa wa Arusha hususan Halmashauri ya Jiji la Arusha, waliomchagua ni Watanzania wanaoishi Jiji la Arusha, makabila yote yaliyoko pale na wala siyo kabila lake yeye. *(Makofi)*

Sasa kitendo cha kusema Serikali ya Chama cha Mapinduzi ndiyo inayoendeleza au inayozungumzia suala la ukabila na udini, ndugu yangu huyu nilikuwa nafikiri kama inawezekana kwa sasa afike mahala ajitambue; kwa sababu nimemwona hapa tena baadaye anapiga jalamba la kuwaomba walewale Waarusha na Wamasai wale, waliomchagua kipindi kilichopita kwamba anataka tena kurejea. Sasa anaji-*contradict* na kauli zake. Unaendaje kuwaomba watu ambao tayari wana mambo ya ukabila! Kwa hiyo, nimwombe

asiwe mwongo, asiwe mnafiki. Wananchi wa Arusha walimpa kura wakiwemo hao Wachaga, wakiwemo Waarusha, wakiwemo Wamasai, wakiwemo Warangi, wakiweko kule Wasambaa wamejaa chungu nzima. Ndugu yangu ananisaidia anasema mpaka na Wanyiramba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile amesema katika maelezo yake kwamba, polisi hawawalindi wanawafanyia vibaya na nini. Kwa hiyo, wao safari hii watahakikisha wana uwezo wa kujilinda. Sasa naomba nimwambie asitingishe kiberiti, kiberiti kimejaa na wala asimtukane mkunga uzazi ungalipo. Jeshi hili la Polisi ndilo litakalomlinda. Hilo Jeshi lake lisilo na anuani wala *address* wala halitafanya kitu chochote ndani ya Vyombo vyetu vya Ulinzi na Usalama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nilikuwa nampasha tu rafiki yangu hiyo, naomba sasa angalau niweze kuipongeza Serikali kwa kuwa na Vyombo madhubuti vya Ulinzi na Usalama kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya pamoja na changamoto nyingi walizonazo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wamekuwa na changamoto mbalimbali kama vile kutopewa bajeti ambayo wameiomba na kutengewa na Bunge hili. Naomba Serikali, kwa Majeshi yetu haya tunapokuwa tumepitisha bajeti yao, ni vizuri fedha zao wakapewa zote. Tunapochwa kuwapa fedha zote kama walivyoomba, tunaviza shughuli ambazo walikuwa wamezipanga kuzitekeleza. Kwa hiyo, naiomba Serikali, katika bajeti ya 2014/15, fedha ambayo ilikuwa imebakia basi waweze kuwapa kabla ya kumaliza huu mwezi Juni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nizungumzie tatizo la makazi ya askari. Kama walivyosema wenzangu, pamoja na jitihada za Serikali za kuanza kujenga makazi ya askari, lakini bado nyumba zile hazitoshelezi. Naiomba Serikali iongeze juhudi ya kujenga nyumba hizo ili kusudi askari wetu waweze kuondokana na kukaa kwenye maeneo ya nje, kwa maana ya mitaani ili warudi wakae sehemu moja ambapo ni maeneo ya askari wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata zile nyumba walizonazo zimechakaa. Kwa hiyo, niiombe Serikali vilevile angalau tuweze kuwakarabatia zile nyumba ambazo wanaishi sasa ili waweze kukaa mahala pazuri na hatimaye waweze kufanya kazi vizuri. Maana unapolala pazuri, ukamka pazuri, basi ujue kwamba wewe ukienda ofisini unaenda kufanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nizungumzie suala la Jeshi la Magereza. Jeshi la Magereza lina rasilimali watu wa kutosha. Jeshi hili Serikali ikiliwezesha, linaweza likafanya kazi kubwa ya kuzalisha na hatimaye likajilisha lenyewe na hatimaye likauza ziada ambayo inaweza ikaisaidia Serikali kwa maana ya maduhuli. Sasa niiombe Serikali, ili kuondokana na matatizo

waliyonayo, Serikali iweke utataribu wa kuyawezesha Majeshi yetu hasa Jeshi la Magereza kwa sababu wana Magereza ya Kilimo, waweze kuwapatia zana za kilimo zilizo bora ikiwemo pembejeo. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Shibuda!

MHE. JOHN S. MAGALLE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata fursa hii ili nami niweze kuchangia mawazo katika hizi Wizara mbili. Awali ya yote, naomba kutumia fursa hii kumwomba Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani pamoja na Naibu Waziri na IGP na Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama, tuweze kuwa na faragha ya kutafakari mambo muhimu ambayo yanasababisha migomo ya kifikiria katika baadhi ya makundi yaliyo katika Wilaya ya Maswa na sehemu za Kanda ya Ziwa hususan wanganga wa jadi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namtakia kheri Mheshimiwa Chikawe katika safari yake ya matumaini mema ya mwaka 2015, ambayo bado ni siri, lakini nakushauri usimsahau Naibu Waziri wako kuwa katika mawazo ya fikra za watu wa kuwa Waziri Mkuu. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kukiri kwamba, Wizara hii ina kazi kubwa sana ya utumishi kwa masilahi ya Watanzania. Napenda kumpongeza IGP na kumpongeza pia DCI aliyeteuliwa na vilevile napenda kuwashauri tu kupitia Wizara hii kwamba, ni vyema vilevile tukawa tunawakumbuka wastaafu. Naomba kumpongeza Mheshimiwa Mstaafu IGP Mwema na DCI Manumba. Kupitia hali hii basi naomba kuwaomba Viongozi wote wa Serikali na Taasisi mbalimbali hata sisi Wabunge, tunapokuwa na Mbunge amemaliza muda wake, si vibaya kuwa unapitapita unamsalimia unamwachia ndondondo hujaza kibaba. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakumbusha kwamba, ukiona kuna maendeleo mahali popote ujue kuna watu waliosagika. Kwa hiyo, wastaafu tuwaenzi na hususan wajane wao, inapotokezea basi tusiwe tunawasahau, kwani kwenye misiba huwa tunajitokeza sana kusema wameacha pengo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ya Mambo ya Ndani imekondeana hususan katika huduma zake za mikoani. Barabara chakavu zinachakaza sana Wizara hii. Naomba kushauri ya kwamba, wakati umefika Kamati ya Ulinzi na Usalama ikate rufaa kwa Rais kuhusu ceilings zinazotolewa ili waweze kufikiriwa, kwa sababu magari yanapoharibika panakuwa hakuna njia yoyote tunalaumu Jeshi la Polisi. Vilevile naomba Wizara hii ikae na TAMISEMI muwe na ubunifu na ugunduzi wa jinsi gani TAMISEMI wanaweza kuchangia masuala ya Jeshi la Polisi kupitia vipato vyao vya wilayani.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, dini zinatuhimiza na zinatukumbusha kuwa waadilifu wa maadili. Napenda kusema ya kwamba, katika Jeshi la Polisi kuna vijana wanakuwa na mihemuko ya tabia chafu ambazo zinachafua Jeshi la Polisi. Nashauri pawepo watoa nasaha wa kuwasaidia hawa vijana. Tukumbuke ya kwamba, kila ujana una haki zake na una mihemuko yake, sasa fukuza fukuza inakuwa haiwajengi vijana. Nashauri wale ambao wanakuwa na ulevi wa madaraka, wawatafutie watu wa kuwasomesha, kuwapa nasaha ili waondokane na mawazo potofu yanayosababisha kuaibisha Jeshi la Polisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuhimiza taasisi zote za Wizara hii zipende kuwa na sare ya kuheshimiana na viongozi wengine. Naomba kuhimiza ya kwamba, Makao Makuu ya Jeshi la Polisi wana sare ya kuheshimiana na Mihimili yote, wanaheshimiana sana na viongozi wa taasisi mbalimbali. Basi mikoani na katika wilaya, suala hilo liwepo, Wabunge wasionekane kwamba ni wachafuzi wa kisiasa wanaingilia Jeshi la Polisi. Tujenge makutano ya fikra, umoja wa mawazo patanifu, kwa masilahi ya kujenga uongozi na Utawala Bora na kuchochea ustawi na maendeleo ya usalama wa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza sana hongera za taasisi zote za Wizara hii na napenda kushauri ya kwamba, pamekuwepo na tabia mbaya ya kuhisi ya kwamba utambulisho wa waganga wa jadi ni vibuyu. Napenda kutambulisha ya kwamba, vibuyu siyo utambulisho wa mganga ramli na mganga wa ramli chonganishi. Vibuyu kwa ukweli ndiyo vyombo vya sayansi na teknolojia asilia vya kuhifadhi dawa. Narudia vibuyu ni sayansi na teknolojia asilia ya kuhifadhi dawa. Vilevile pembe za wanyama zinazohifadhi dawa, hizo huwa ni friji dawa za chanjo zisiharibike. Kwa hiyo, naomba kusema ya kwamba, tusiwe tunafikiria kwamba hayo ni mabaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba vilevile pawepo na ziara ya Mheshimiwa Waziri ya kutembelea maeneo yetu ili aje asikilize matatizo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ajali, naomba pawepo utafiti wa kuhusu upatanifu kati ya ardhi na matairi yanayotumika kwenye magari mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nizungumzie Wizara ya Ulinzi. Naomba kulipongeza Jeshi la JKT kwa kuwa kiotesho cha kuotesha mbegu ya vijana ambao wanakuwa wamefuliwa dhidi ya mawazo potofu na kuwa ni chachu ya mawazo mapya. Napongeza JKT kwa kuchukua vijana toka maeneo mbalimbali na kunyumbulisha mtazamo mpya. Sasa ningeomba Jeshi la Wananchi pamoja na JKT, aidha Wizara ya Ulinzi pamoja na Ofisi ya Waziri Mkuu, ni vyema tukawa na programu maalum ya kuotesha zinduko la kuhakikisha tunakuwa na operesheni safisha maono potofu katika jamii.

Natambua maono ya imani potofu za mauaji ya vikongwe, mauaji ya *albino* yako hususan katika mtandao wa Kabila la Wasukuma. Naomba basi JKT ipewe fursa ya kujenga mapinduzi ya fikra na kujenga mageuzi ya mawazo potofu kwa kuwaweka programu maalum itakayokuwa inaondoa aibu ya mauaji haya ambayo nashukuru ya kwamba, hivi sasa yamekuwa yakipungua. Napenda kusema ya kwamba, tushauri sisi Bunge na Serikali tuwe na mapinduzi ya kifikra kuisaidia JKT kupata kipato cha kutosha kuweza kufanya operesheni mbalimbali. Aidha, mang'amuzi yaliyopo hivi sasa, ukitaka kuelewa Wasukuma toka Kanda ya Kaskazini hadi Ziwa Victoria, kutoka Ziwa Victoria hadi Ziwa Tanganyika na Ziwa Nyasa, utakuta Wasukuma wapo. Ukitoka Mto Mara hadi Mto Kagera utakuta Wasukuma wapo. Haya yote yanakuwa na tambazi kutokana na Wasukuma. Kwa hiyo basi, ninaomba ya kwamba, tuwe na Programu ya Operesheni Uamusho Dhidi ya Mila Potofu.

Wizara ya Ulinzi, Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zote, tuungane kutafuta pesa ya kuhakikisha Operesheni Uamusho Dhidi ya Imani Potofu iwaguse zaidi watu wa maeneo hayo. Wawekwe kwenye maeneo maalum ya JKT, pawe na mnyumbuliko kwa vijana wa leo kwani vijana wa leo ndiyo wazee wa kesho na wazee wa leo ndiyo wazee wa kesho. Kwa hiyo, nawaombeni wote tuwe na umoja wa mitazamo tuweze kujenga mapinduzi ama fikra dhidi ya imani potofu. Ahsanteni. *(Makofi)*

MICHANGO KWA MAANDISHI

MHE. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na kumpongeza Waziri, Mheshimiwa Dkt. Hussein Mwinyi na Watendaji wote wa Wizara, kwa Hotuba yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze Serikali kwa kurudisha tena mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) kwa ajili ya kujenga ukakamavu na uzalendo kwa vijana wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni mmoja wa Wabunge waliohudhuria mafunzo hayo katika Kambi ya Msange JKT Tabora. Nikiri kuwa mafunzo ni mazuri sana, lakini zipo changamoto zinazolikabili Jeshi hili, ambazo tungeomba Serikali ifanye maboresho. Kwa mfano, maboresho kwa baadhi ya makambi kupanua mabweni na miundombinu.

Wahitimu wa Mafunzo ya JKT Serikali iliwaahidi kuwapatia kazi katika taasisi mbalimbali kama Bandari, Wanyamapori na kazi mbalimbali katika majeshi yetu.

Ushauri wangu kutokana na malalamiko yanayojitokeza, ni vyema hata Halmashauri zetu zote zingekuwa na utaratibu wa kuwatumia wahitimu hawa wa JKT.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Serikali yetu ihakikishe wastaafu wetu wa jeshi wanapatiwa malipo yao kwa wakati na ikiwezekana yaboreshwe ili kuwapatia heshima na kuendelea kuwaenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na migogoro mikubwa sana ya muingiliano wa mipaka kati ya makambi yetu na wananchi. Je, ni makambi mangapi bado hayajawa na hati za kumiliki ardhi?

Je, nini mkakati wa Serikali kuhusiana na wananchi walioingia katika mipaka ya jeshi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. JOHN P. LWANJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri, kwa Mpango mzuri wa Bajeti ya 2015/16 na utekelezaji wa Mpango 2014/15.

Hivi sasa ni zaidi ya miaka mitano sasa tangu Serikali itoe ahadi ya kujenga Kambi ya Jeshi la Kujenga Taifa Wilaya ya Manyoni eneo la Kijiji cha Sanjaranda, Tarafa ya Ifigi.

Wataalamu wa Jeshi la JWTZ wakishirikiana na Kamanda wa Mkoa na Wilaya ya (Mgambo) wamefika mara kadhaa Kijijini Sanjaranda na kuwapa matumaini makubwa wananchi na vijana ambao wanatamani sana kambi hiyo ianzishwe ili kuwapatia ufundi stadi na hivyo kuweza kujiajiri.

Mkoa wa Singida hauna Kambi hata moja na tulitarajia Kambi ya Sarajaranda ingetoe uwiano na mgawanyo na Kambi za JKT kimikoa. Naomba kupata majibu ya kuridhisha ni kwa nini Kambi hiyo haijaanza na itaanza lini?

Naipongeze JWTZ kwa kazi nzuri ya ulinzi wa mipaka ya nchi yetu na kazi nzuri ya ulinzi DRC na maeneo mengine chini ya Umoja wa Afrika na UN.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MHE. BEATRICE M. SHELUKINDO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Dkt. Hussein Mwinyi, kwa kazi nzuri anayoifanya na Hotuba nzuri pia. Ninampongeza Katibu Mkuu na Watendaji wote. Aidha, kwa namna ya pekee ninampongeza CDF pamoja na *Chief of Staff* na Watendaji wote, kwa kazi nzuri wanayoifanya hususan katika JKT.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo, ninapenda kutoa mchango wangu kama ifuatavyo:-

Kwanza, mafunzo ya mgambo yamekuwa yakitolewa katika Kata mbalimbali za Wilaya ya Kilindi. Jambo la kushangaza ni kwamba, mafunzo hayo ni hiari lakini kule Kilindi ni lazima, utake usitake na ikibidi hata kwa kushurutishwa. Nimepokea malalamiko mengi toka kwa Wananchi na nilifika ofisini kwako kutoa taarifa. Ninaomba utaratibu uwekwe wazi.

Pili, ninashauri badala ya mafunzo ya ukakamavu, wange-introduce hata mafunzo ya ujasiriamali ili kujiongezea vipato kama ilivyo JKT.

Tatu, nilipongeze Jeshi kwa kujali afya ya Watumishi wake. Nikiwa nchini India, nimeshuhudia Wanajeshi wa ngazi zote wakipatiwa matibabu mbalimbali bila ubaguzi. Hii ni motisha kubwa kwao.

Nne, suala la matrekta. Wakati matrekta yameletwa sisi kama Halmashauri ya Wilaya ya Kilindi tulifika na kutaka kuchukua 50 tuliambiwa tsubiri. Je, ni lini yatafika tuweze kupatiwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naomba tuendeleo kuwapa mazingira mazuri Wanajeshi hususan wa ngazi za chini ili tuwe na Jeshi imara ambalo litakuwa imara wakati wowote litakapohitajika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja.

MHE. GREGORY G. TEU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri na Watendaji wake wote, kwa kwa kazi nzuri inayofanyika ya ulinzi wa Taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kufahamu ule utaratibu wa kurejesha uwepo wa Kambi ya JKT iliyokuwepo katika Wilaya ya Mpwapwa miaka ya nyuma chini ya uangalizi wa Kambi kubwa ya Makutupora Mkoani Dodoma. Kambi hii ilikuwepo katika eneo la Kikombo - Mayawile. Je, itarejeshwa lini?

Kambi hii ilikuwa na msaada mkubwa wa kutunza vyanzo vya maji vya Mayawile pamoja na kilimo na ufugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha

MHE. ABDALLAH HAJI ALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, ninapenda kumshukuru Mungu, muweza wa mambo yote. Ninaanza kutoa maelezo yangu kuhusiana na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

Ninapenda kuipongeza Serikali kwa kuridhia kurejesha tena Mafunzo ya JKT kwa vijana wanaomaliza Kidato cha Sita. Mafunzo haya yanawasaidia sana vijana wetu kuwaweka katika hali ya nidhamu, uzalendo, kujituma na kujitegemea na kujenga upendo miongoni mwao, lakini pia kuipenda nchi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taifa lenye nidhamu ndilo linalopiga hatua za maendeleo. Bila nidhamu katika nchi ni vurugu; hivyo, ninakiri kwamba, mafunzo ya JKT kwa vijana wetu ni yenye thamani na ninaiomba Serikali iyaboreshe kwa kuongeza makambi ili vijana wengi wapate nafasi ya kujiunga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu kwa Serikali itilie mkazo mafunzo haya kwa kuwapa stadi za ufundi ili wamalizapo mafunzo hayo waweze kujitegemea ili kuondokana na ile dhana kwamba, wakikosa ajira huyatumia mafunzo yao kijeshi kwa uhalifu kama ujambazi.

Kumekuwa na malalamiko ya siku nyingi kuhusiana na ajira katika Vyombo vya Ulinzi hususan kutokea Zanzibar kwamba, nafasi za ajira za jeshi na hata zile za polisi, hazitolewi ipasavyo. Inadaiwa kwamba, zinachakachuliwa na baadaye walengwa haziwafikii na badala yake kupewa watoto wa wakubwa ambao haziwahusu nafasi hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaishauri Serikali isimamie haki hii ili ugawaji wa ajira za Jeshi la Polisi uende kwa waliokusudiwa ili kuondoa malalamiko yasiyokuwa ya lazima. Sote tunajenga nyumba moja kwa nini tugombe vito?

MHE. NYAMBARI C. M. NYANGWINE: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie nafasi hii kumpongeza Waziri na Watendaji wengine wa Wizara hii, kwa uchapaji kazi wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi la Wananchi limetwaa maeneo ya Ronsonti na Msati kwa nguvu. Mheshimiwa Waziri nasisitiza kuwa, eneo hilo la Msati na Ronsonti lilichukuliwa na Wanajeshi wa Kambi ya Nyandoto toka 1973, wakati ambapo wananchi walifanya wema kuwakaribisha hao wanajeshi kuweka vifaa vyao wakati wa mafuriko ya Mto Mori. Naomba Waziri ahimize Watendaji wa Wizara hii kuhakikisha kuwa, wanawalipa fidia wananchi ambao walinyang'anywa maeneo yao na Jeshi hili ama sivyo nashauri wanajeshi wayaachie maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo haja ya Jeshi la Wananchi na Jeshi la Kujenga Taifa kusaidia kuimarisha ulinzi na usalama wa raia kutokana na tishio la ugaidi Duniani. Wanajeshi washirikishwe kulinda maeneo yenye msongamano na watu wengi kama vile shule, vyuo, masoko, *malls* na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo haja ya J.K.T kuzalisha mazao ya chakula na biashara ili kuondoa tatizo la njaa hapa nchini. Makambi ya JKT yatumike kuzalisha mazao ya chakula kwa wingi na hata biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. SAID A. ARFI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi linaendelea na ujenzi wa makambi mapya na programu za mafunzo na kupelekea maafisa kadhaa kuchukuliwa kama wakufunzi au kazi mahususi na kuwatenganisha na familia zao kwa muda mrefu. Jambo hili husababisha msongo wa mawazo kwa wanandoa, kuhatarisha uhai wa ndoa, ulezi na malezi ya watoto na pia kuongeza maambukizi ya UKIMWI kwa wanandoa. Wizara ina mpango gani mahususi kukabiliana na changamoto hii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba katika hitimisho Serikali itoe kauli juu ya tatizo hili, kuwafariji wahusika wake na watoto na kuwathibitishia Serikali imesikia kilio chao. Nashukuru sana.

MHE. MKIWA A. KIMWANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nianze kwa kumpongeza Waziri kwa kuonesha umahiri wake katika Wizara hii ya Ulinzi na wa nchi yetu na mipaka ya nchi yetu, pia kuwa na Jeshi la Kujenga Taifa ambalo ni imara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wilaya ya Ilemela Mkoani Mwanza kuna maeneo ambayo Jeshi letu la Wananchi wa Tanzania limeyachukua kwa ajili ya shughuli zao za kikazi. Hatulikatai suala hilo, lakini basi kuna mambo ambayo hayahitajiki kuona yanaendelea. Mfano, eneo la Mitaa ya Nyanguku na Lukobe yaliyoko Kata ya Kahama, Wilaya ya Ilemela, kuna Kambi ya Jeshi la Wananchi, Kikosi cha 601, ambayo ilichukua nafasi au eneo la wananchi. Tangu ichukue eneo hilo, yapata miaka 15 hadi sasa, hakuna hata kitu kimoja miongoni mwa wakazi hao kinachoruhusiwa kuendelezwa kwenye maeneo hayo kwa muda huo wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitendo hicho kimewafanya wananchi wa mitaa hiyo kushindwa kuendeleza kitu chochote kile. Baadhi ya familia nyumba zao zinabomoka, hawaruhusiwi hata kuinua ukuta ulioanguka, hivyo basi, kupelekea watoto kuchukuliwa na fisi kwa nyakati tofauti, nyoka kuingia ndani kwa kuwa baadhi ya nyumba kuta zimeanguka na siyo ruhusa kuziba tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnamo tarehe 6 Machi 2015 tulifika ofisini kwako kwa ajili ya kuomba watu hawa wapate kuthaminiwa makazi na mali zao. Maafisa wako waliahidi baada ya wiki mbili watafika kufanya survey na kuangalia kazi ya uthamini ilivyofanyika. Hadi leo hawajaja na hali ya mvua zinazoendelea Mwanza ni hatari. Mbaya zaidi katika maeneo hayo kuna silaha

za kivita ambazo ni hatari kwa wakazi hao. Naitaka Wizara hii ifuatilie uhakiki na uthamini mapema ili kuepusha yaliyotokea Mbagala na Gongolamboto yasije yakatokea Lukobe na Buduku. Pia wananchi waweze kujiendeleza kimakazi, kilimo na mambo mengine mengi ya kimsingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maisha ni uhai, hatuhitaji kuhatarisha maisha ya watu kwa wanyama kama fisi, nyoka na wengine kutoa maisha ya watu kwa linalowezekana. Ahsante.

MHE. SYLVESTER MASSELE MABUMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri wake pamoja na Katibu Mkuu na Timu yake yote ya Watendaji, kwa namna wanavyotekeleza majukumu yao kwa Taifa kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majukumu makubwa ya Wizara hii pamoja na mambo mengine, ni kulinda usalama wa raia na mali zao, kutoa huduma za zimamoto na uokoaji na kadhalika.

Je, Wizara ina mpango gani kuimarisha ulinzi katika katika Vituo vya Polisi kwani tumeshuhudia katika siku za karibuni askari wetu wakiuawa na watu wahalifu? Vile vile tumeshuhudia silaha zikiporwa vituoni na hivyo kuweka rehani maisha ya askari na raia wema hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, askari wetu wameendelea kuishi katika makazi duni, nyumba hazina viwango. Je, Serikali itazifanyia lini ukarabati wa kina ili nyumba wanazokaa maafisa na wapiganaji wetu zifikie viwango?

Nyumba zilizopo Mwera Wilaya ya Kati, Mkoa wa Kusini Unguja, zinahitaji ukarabati mkubwa. Pia kwa kuwa Mwera ndiyo Ofisi Kuu ya Polisi Mkoa wa Kusini, Wilaya ya Kati, nashauri Serikali ipeleke *computer* za kutosha, *photocopier* na *printers* za kuweza kukidhi mahitaji ya Mkoa na Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kujua ni lini Serikali itaanza kujenga jengo linaloendana na hadhi ya Kituo cha Traffic cha Mwembe Mchomeke kilichopo katika Jimbo la Dole. Kituo hiki kina jengo dogo sana lenye hadhi ya *police fast*, Ikini majukumu yake ni makubwa. Naomba kujua kama Setikali ina mpango wowote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda vilevile kujua Serikali itamaliza lini kulipa madeni wanayodai askari polisi wote hapa nchini? Askari wetu wanadai malimbikizo ya likizo, uhamisho, yote haya yanawafanya wawe wanyonge, lakini majukumu wanayowakabili ni makubwa, kwa mfano, kusimamia Uchaguzi Mkuu ujao mwezi Oktoba 2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa unyenyekevu kabisa naiomba Wizara ya Mambo ya Ndani iongeze ulinzi kwa Viongozi wa Dini na nyumba za ibada kule Zanzibar hasa kipindi hiki tunapoelekea kwenye Uchaguzi Mkuu Oktoba 2015. Ombi hili ninalileta kutokana na dalili mbaya zinazotokana na vitisho kutoka kwa wapambe, viongozi wa siasa wa chama kimojawapo cha siasa huko Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakusudia kukamata mshahara wa Mheshimiwa Waziri kama sitapatiwa maelezo kuhusu ukarabati wa nyumba za maafisa na wapiganaji pale Mwera, ujenzi wa Kituo cha Polisi Mwembe Mchumeke na ulipaji wa madai yote ya askari wanaoidai Serikali na madeni ya Wizarani ya wote waliotoa huduma kwa Wizara ya Mambo ya Ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MHE. ABAS Z. MTEMVU: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii adhimu kuzungumza kuhusiana na mchango wangu nilioutoa baada ya Hotuba iliyotolewa na Mheshimiwa Waziri Mkuu, ambapo nilizungumzia kuhusiana na suala la usalama barabarani (*Traffic*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wanataka kujua kama Askari wa Usalama Barabarani wanalipwa posho za dharura za kujikimu wakati wa maafa kama mvua za masika zilizonyesha mfululizo tangu mwezi wa nne mpaka mwezi wa tano ambapo zilisababisha askari hao kutokuonekana barabarani na kusababisha foleni kubwa za magari ambayo iliwaletoa wananchi usumbufu mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wanataka kujua kama maaskari hao wanapatiwa vifaa vinavyokidhi shughuli za usalama barabarani wakati wa maafa ili kuepusha madhara hayo makubwa ya msongamano wa magari katika kipindi cha maafa hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MHE. ALI KHAMIS SEIF: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Kusini Pemba umejengwa na Wilaya ya Mkoani na Chake-Chake.

Masafa kutoka Mji wa Mkoani mpaka Mjini Chake-Chake ni karibu kilomita 30.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati mbaya magari ya abiria yanasimamishwa karibu mara tano yanapotoka Mkoani kwenda Chake-Chake. Pia, magari hayo yanaporejea Wilayani Chake-Chake kwenda Mkoani yanasimamishwa mara tano.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, usimamishwaji huo unafanywa na Askari wa Usalama Barabarani mara tatu na mara mbili ni kwenye Vituo vya Polisi vya Mkoani, Mtambile na Chake-Chake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina mashaka hata kidogo na usimamishwaji unaofanywa na Askari wa Usalama Barabarani, mashaka yangu yako kwenye huu usimamishwaji kwenye Vituo vya Polisi ambapo kama ni amri ipo muda mrefu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwepo wa amri hii sioni kama unasaidia kuimarisha ulinzi na usalama kwa vile magari binafsi na ya mizigo yanasimama kwenye Vituo vya Polisi kwa upekuzi. Hivyo basi, kama utaratibu huo ni kudhibiti uvunjifu wa usalama wa eneo husika kwa kutokaguliwa magari binafsi na mizigo, wabaya wote wangelitumia magari hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu huu ni kuwasumbua Wananchi. Mkoa wa Kaskazini Pemba hakuna utaratibu huu na halijatokea tamko la uvunjifu wa sheria kwa sababu magari ya abiria hayakupelekwa. Hali ilivyo sasa ni mazoea tu lakini hali halisi utaratibu huo haupunguzi uhalifu na uvunjifu wa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wagonjwa na wazazi wengi wanapopelekwa hospitali hutumia magari ya abiria badala ya gari la wagonjwa (*Ambulance*). Kwa amri ilivyo inabidi gari lisimame kwenye Kituo cha Polisi na wakati mwingine huchukua muda kuruhusiwa na Polisi hasa wakati wa usiku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu; amri ya magari ya abiria kulazimika kusimama kwenye vituo iondolewe. Pale Jeshi la Polisi linapohisi kuna wasiwasi wa usalama, waweke vizuizi vya barabarani (*road block*), waachiwe Askari wa Usalama Barabarani wafanye kazi zao za kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jambo la kusikitisha sana hali ya makaazi ya Askari Polisi Mkoani ni mbaya mno. Ujenzi wa nyumba unafanywa toka wakati wa Ukoloni. Tokea tupate Uhuru wetu halikujengwa jengo lolote la kuishi askari na jengo la ofisi.

Kwa kuwa hakuna ujenzi wowote uliofanywa baada ya Uhuru itakuwa ni dhambi tukisema ni bora wakati wa Ukoloni kuhusiana na majengo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara inieleze kwa bajeti ya mwaka ujao 2015/2016 ni kiasi gani kimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za kuishi askari wetu na ofisi zao.

MHE. ALLY K. MOHAMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Mambo ya Ndani ina Vituo vya Polisi ambavyo viko Mwambao mwa Ziwa Tanganyika vya

Wampembe, Namaji na Kabwe. Vituo hivyo havina usafiri wa uhakika kabisa, naomba Wizara iwafikirie sana kwa kuwasaidia hata pikipiki.

Pia, kuna Kata ambazo zina uhalifu mkubwa sana mpaka hata matukio ya kuuwana na pia uvamizi wa mara kwa mara kwa raia toka DRC Congo katika Vijiji vya Korongwe na Karungu na kupora mali zao. Vijiji vilivyopo Mwambao mwa Ziwa Tanganyika kama Kijiji cha Swaila, Makao Makuu ya Kata ya Mkwamba, wananchi wako tayari kujenga Vituo vya Polisi kwa kushirikiana na Wizara yako ili kupunguza uhalifu na kulinda mali za raia wema.

Suala zima la kuchukua silaha za wenye silaha halali. Wanafika Kituo cha Polisi na kuchukua *list* ya wenye silaha na kuchukua silaha, hadi leo hawajarudisha silaha zao. Ukienda Maliasili wanasema hawahusiki. Je, nani anahusika au kuna mradi mpya hakuna kumiliki silaha kihalali maana hata wakimkuta mmiliki halali hana kosa lolote hapewi silaha yake? Hayo yamefanyika Mkoa wa Rukwa tena wanavamiwa saa saba za usiku.

MHE. INNOCENT R. SEBBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kunipa nafasi ya kuchangia Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Nimpongeze Waziri kwa kazi nzuri inayofanywa na Wizara yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipende kuchangia kuhusu Jeshi la Polisi. Jeshi letu la Polisi kwa upande wa Wilaya yetu ya Kyerwa, Mkoa wa Kagera wanafanaya kazi katika mazingira magumu sana. Majengo yote ni mabovu sana, kipindi cha mvua wananyeshewa na kuangukiwa na paa. Hawana vitendea kazi kama gari hali ya ambayo inawapa wakati mgumu kutimiza wajibu wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wilaya yetu ya Kyerwa hali ya usalama ni mbaya sana baada ya baadhi ya watumishi wa vyombo vya ulinzi na usalama kutumiwa na wahamiaji haramu wa nchi jirani ya Rwanda na Uganda kwa maslahi ya nchi hizo. Watumishi wasio waaminifu wamekosa uzalendo pia wamekiuka maadili ya kazi yao. Tunaomba Wilaya ya Kyerwa iangaliwe kwa ukaribu sana, maana Rwanda na Uganda wanatumia pesa nyingi sana wakitumia wanasiasa kwa maslahi ya nchi zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Kerwa wanaishi kwa hofu kubwa baada ya kushuhudia kikundi cha zaidi ya vijana 300 wakifundishwa mafunzo ya kijeshi na wanaowafundisha ni wanajeshi waliopewa jeshini na wengine inasemekana ni askari wenye asili ya Rwanda. Pia baadhi ya vijana waliopewa mafunzo ni wahamiaji haramu toka Rwanda na Uganda, yote hayo vyombo vya ulinzi vinajua na wala hakuna hatua zilizochukuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba wakati wa kuhitimisha Waziri awaeleze wananchi wa Kyerwa ni hatua zipi zitachukuliwa ili hawa wananchi waweze kurudisha imani kwa vyombo vya ulinzi na usalama pia wahakikishiwe usalama wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. ENG. ATHUMANI R. MFUTAKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia 100.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kesi ya kulawiti Tabora ipelekwe Mahakamani. Tarehe 20 Januari, kuamkia tarehe 21 Januari, 2015 pale Tabora Isevy/Mjini, Cheyo, kijana Dotto Selemani alilawitiwa na Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Uyui. Mwenyekiti huyo jina limeandikwa gazeti la Jambaleo la tarehe 19 Mei, 2015, ni Mussa Rashid Ntimizi. Taarifa za uhalifu huu ziliripotwa na gezeti la Mwananchi tarehe 27 Januari, 2015, ukurasa wa 8. Naomba Bunge lipate taarifa ya kesi hii na RPC aeleeze kwa nini haijafika Mahakamani?

Sasa ni miezi takribani minne imeshapita. Kijana Dotto ni mkaanga *chips*, anatokea familia maskini, kutopeleka kesi hii Mahakamani ni kumlinda mtoto anayejijita ni wa tajiri, eti kwa kuwa wana shilingi bilioni moja kwa kuuza nyumba Dar es Salaam. Japo mara kadhaa Mussa Ntimizi amekamatwa Tabora Mjini, Mabama na kupelekwa kituo cha Wilaya ya Uyui- Isikizya lakini huachiwa siku hiyo hiyo. Dotto ana haki, ilindwe, isimamiwe na ipatikane. Naomba Mussa Ntimizi pelekwe Mahakamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vituo vya polisi Kata ya Igalula. Vijiji vya Kata za Lutende, Miyenze, Goweko, Nsololo, Kizengi, Tura vinahitaji vituo vya polisi. Kituo cha Loya kimekamilika bado ufunguzi. Tunashukuru kata za Kigwa na Igalula vituo vipo na vinatoa huduma. Mawe, tofali, mchanga wananchi tuko tayari kuchangia. Serikali itupatie vifaa vya viwandani, rangi, sementi na nondo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawasilisha.

MHE. JOHN P. LWANJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu wake kwa kuwasilisha mpango mzuri wa bajeti ya mwaka 2015/2016 na utekelezaji wa mpango wa mwaka 2014/2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, nalipongeza Jeshi la Polisi chini ya IGP wake kwa kazi nzuri wanayoifanya kulinda raia na mali zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri mambo yafuatayo:-

Nakala ya Mtandao (Online Document)

(i) Ulinzi shirikishi. Wananchi wapatiwe elimu ya kutosha ili waweze kukubali dhana nzima ya ulinzi shirikishi na waweze kushiriki kikamilifu. Aidha, polisi kata wapatiwe usafiri (pikipiki) ili waweze kufanya kazi kwa ufanisi zaidi.

(ii) *Whistleblowers*. Kwa sasa wananchi hawashirikiani na polisi kufichua wahalifu kutokana na polisi kutokuwa na siri kwa kuwasaliti *whistleblowers* pale wanapotoa taarifa kwa polisi. Polisi haohao hawatunzi siri na kuwafanya watoa taarifa kubainika kwa wahalifu. Jeshi la Polisi litunze siri na lifanye kazi kisayansi.

(iii) Kubambikiza kesi. Mpaka sasa kuna malalamiko kwamba wananchi wanabambikiziwa kesi ili polisi wapate miradi ya kujipatia mapato haramu kwa njia ya rushwa. Jeshi la Polisi lipambane na watumishi wake wasiowaaminifu na hivyo kulichafua jina zuri la jeshi hilo lililokuwa nalo tangia uhuru mwaka 1961. Lifanye operesheni maalum kuwabaini na hata kuendesha kura ya maoni ya siri kwa wananchi na ndani ya jeshi lenyewe kuwabaini watumishi hao. Wale watakaolalamikiwa zaidi na wananchi watoswe ili kulisafisha jeshi letu.

(iv) Watuhumiwa kuachiwa haraka bila sababu za msingi na hata pale ambapo uchunguzi bado unafanyika na hivyo kuwafanya raia wema waonekane hawana ubavu wa kupambana na watuhumiwa na pia dhana ya rushwa kutawala hata kwa kesi ndogo ndogo.

(v) Mafunzo magerezani. Nashauri magereza iwe na utaratibu wa kutoa mafunzo ya nadharia kwa wafungwa darasani na wakihitimu wapatiwe vyeti au barua za uhitimu wa mafunzo hayo kama utambulisho wanapotoka magerezani kwenda uraiani.

(vi) Benki ya magereza. Nashauri magereza ianzishe benki kwa ajili ya wafungwa na ije na utaratibu wa malipo kwa wafungwa wanapofanya kazi maalumu za ujenzi na kazi zingine za ujasiriamali ndani na nje ya magereza. Mapato yapatikanayo sehemu ilipwe magereza na sehemu ilipwe wafungwa kwenye akaunti zao katika benki hiyo ili ziweze kusaidia familia zao. Mpango huu wa kuwa na Benki Maalumu ya wafungwa uko nchi ya Peru. Nashauri maafisa wahusika wa magereza waende kujifunza hilo huko Peru.

(vii) Naiomba Serikali itenge fedha za kutosha ili kuvipatia vituo vyote vya polisi usafiri wa uhakika ili kuviwezesha kufanya doria na kufuatilia wahalifu na upelelezi wa kesi. Kituo cha Itigi na Mitundu, tarafa ya Itigi, Wilaya ya Manyoni vinahitaji msaada wa haraka kuvipatia usafiri wa uhakika pamoja na kituo cha polisi cha Ukimbu (Kayui). Gari lililotolewa kwa kituo cha polisi Itigi ni bovu tunahitaji gari jipya na pikipiki mbili kila kituo.

(viii) Ujenzi wa kituo kipya cha polisi Itigi unasuasua. Naiomba Serikali itenge fedha za kutosha kujenga kituo hicho. Waziri Mkuu alichangia shilingi

milioni mbili mwaka 2010 lakini hadi sasa kazi iko *level* ya msingi tu. Hii ni kwa sababu wananchi wameelemewa na michango mingine mingi ya maendeleo kama elimu, kwa mfano maabara na madarasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawasilisha.

MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutoa mchango wangu kwa Wizara hii, nathubutu kusema kwamba Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania haijawa kabisa na utayari wa kuweka Muungano huu wa Tanganyika na Zanzibar katika hali ya kuonekana na kuaminika kuwa ni Muungano wa nchi mbili huru kwani katika kujadili masuala ya Muungano kumekuwa na tabia ya kuibana mijadala yake. Haiwezekani Wizara nyeti za ulinzi yaani Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa zijadiliwe kwa kulipua huku ikijulikana kwamba hizi ni Wizara za Muungano. Imekuwa ni tabia iliyozoeleka kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutotoa kipaumbele kwa Wizara zinazohusika na mambo ya Muungano jambo ambalo halionyeshi nia njema katika kukuza na kuboresha Muungano wa Tanganyika na Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuonyesha kwamba Muungano huu ni wa kweli na wa dhati katika kuteua vyeo vya *IGP* ndani ya kipindi cha miaka hamsini ya Muungano wetu ni mara ngapi au kipindi kipi ambacho Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania amewahi kuteua *IGP* kutoka Zanzibar kama mshirika wa Muungano huu angalau kwa mwaka mmoja tu, naamini halijapata kutokea. Hii ni sura halisi inayoonyesha kuinyong'onyeza Zanzibar na kuonekana dhahiri kwamba ni koloni la Watanganyika na sio mshirika wa Muungano wa Tanganyika na Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuwemo kwa Wabunge kutoka Zanzibar katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni sehemu ya kiini macho cha kuonyesha kwamba kuna Muungano wa Tanganyika na Zanzibar licha ya kukatishwa tamaa katika kuyajadili masuala ya Muungano katika ustahiki wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na matatizo ya kushtumiana ndani ya Jeshi la Polisi na kwa sababu ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kutofautilia baadhi ya shutma hizo kuna tabia ya kuwakosesha haki zao baadhi ya askari wanaotuhumiwa kutenda kosa kwa kuwafukuza kazi bila ya vielelezo. Mfano ni kufukuzwa kinyume cha sheria Coplo Muhidin Kombo Ali D5003 aliyefukuzwa kazi kwa tuhuma za kupoteza vielelezo vya watu walituhumiwa kuwa wauza unga (madawa ya kulevya). Cha kusikitisha ni kwamba vielelezo hivyo havikuwepo bali ilikuwa ni vya kubuni tu kwa maneno. Askari D5003 Coplo Muhidin Kombo Ali alivuliwa *rank* ya Coplo Septemba, 2004 na wala hakuna barua yoyote aliyopewa ya kuteremshwa cheo au kufukuzwa kwake bali hukumu yake ilikuwa ya maneno matupu.

Je, kwa nini mwenzake ambaye walishukiwa pamoja kwa kosa hilo hilo alitakiwa arejee kazini? Je, si dhahiri kwamba hili lilijengwa kwa sababu ya kutakiwa Askari D5003 Coplo Muhidin Kombo Ali afukuzwe kazi tu. Je, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi inaridhika na hukumu kama hizo ambazo hazina vielelezo wala ushahidi wowote? Siamini kwamba kuna nia ya Serikali kuwakosesha watu haki zao lakini kuna baadhi ya watendaji wa Jeshi la Polisi ambao wanatumia nafasi zao katika kuwakosesha watu walio chini yao haki zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, askari D5003 Coplo Muhidin Kombo Ali alifukuzwa kazi tarehe 14 Oktoba, 2005 na mwenzake Massoud Ali kurejeshwa kazini ambapo Massoud Ali alifanyiwa hivyo katika kushirikishwa na tuhuma hizo ili ipatikane njia tu ya kufukuzwa D5003 Coplo Muhidin Kombo Ali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni matumaini yangu kwamba Wizara husika italifuatilia suala hili ili mfukuzwa bila barua yoyote D5003 Coplo Muhidin Kombo Ali, apatiwe haki zake anazostahili. Si vyema kuwatumia baadhi ya askari kama watu wasiokuwa na maana na kuwahujumu kwa kuwaandalia kesi zisizostahili. D5003 Coplo Muhidin Kombo Ali, ni mkazi wa Pandani, Wilaya ya Wete, Mkoa wa Kaskazini Pemba. Naamini suala hili litafuatiliwa ili kumpatia haki zake zote anazostahili.

MHE. RASHID ALI OMAR: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nachukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia kuwepo katika Bunge lako Tukufu nikiwa mzima wa afya hadi leo ambapo tunaelekea ukingoni ili kumaliza muda wa miaka mitano toka mwaka 2010 - 2015 tukiwa salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii na mimi niweze kuchangia hotuba hii ya bajeti ya mwaka 2015/2016 ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Kwanza natoa pongezi zangu za dhati kwako kwa kuliongoza Bunge muda wote ambao ulikuwepo katika kiti, tunakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, nachukua fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa Jeshi la Polisi kwa kusimamia ulinzi na usalama wa mali za raia na raia wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachoshangaza na kuleta masikitiko makubwa ni juu ya Jeshi la Polisi kutosimamia demokrasia nya nchi hii badala yake kujielekeza upande mmoja wa Chama Tawala kama wakala na kuwanyanyasa wananchi kinyume na sheria za nchi. Tumeshuhudia kipindi chote cha miaka mitano hii ya Bunge lako Tukufu hali ya utulivu na amani imevurugwa sana kisiasa na Jeshi la Polisi kufuata matakwa ya Chama cha Mapinduzi na Serikali zake, Serikali ya SMZ na Serikali ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania kwa kuweka vizuizi na kuwashambulia Wapinzani kinyume na Sheria

ya Vyama Vingi vya Siasa. Tumeshuhudia Jeshi la Polisi likivamia mikutano na maandamano halali ya Vyama vya Upinzani na kusababisha mauaji na kuwajeruhi raia ambao hawana hatia.

Naomba niishauri Serikali ya Jamhuri ya Muungano katika kipindi hiki cha kuelekea uchaguzi, Chama cha Mapinduzi kielewe kwamba Vyama vya Upinzani vina haki sawa na chama hicho kinachotawala waanze kutoa maelezo kwa jeshi hilo nalo lijirekebishe ili kutunza hazina iliyopo ya amani na utulivu kinyume na nchi nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho naomba niieleze Serikali ya Chama cha Mapinduzi, Watanzania wote awe mwanachama, awe mwananchi wa kawida au awe kiongozi, wote tunahitaji amani, vita haina macho, tujiandae kila mmoja kutetea amani kwa kumpatia kila mtu haki yake.

MHE. ZARINA S. MADABIDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naunga mkono hoja. Naipongeza sana Serikali ya CCM kwa kazi nzuri inayoifanya kuhakikisha usalama wa wananchi. Tanzania imekuwa nchi kimbilio la wakimbizi kwa zaidi ya miaka arobaini; hii inaonesha ni jinsi gani nchi yetu imekuwa ni kisiwa cha amani. Katika nchi nane zinazozunguka Tanzania, nchi tano zimekuwa na matatizo ambayo yote yametokea katika kipindi cha uchaguzi au yanayokuwa na uhusiano na masuala ya siasa. Hivyo, naomba sana tunavyoelekea kwenye uchaguzi mkuu ni lazima Jeshi la Polisi liwe na utayari wa kutosha kuhakikisha linalinda amani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, makazi ya Polisi. Napongeza jitihada ya Serikali kujenga nyumba kwa ajili ya askari. Nyumba za polisi za zamani zina hali mbaya sana na kama pale karibu na kwangu wanaishi kwenye *fullsuit* ya mabati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania inaweza kabisa kuishinda rushwa ambayo ni muhimu sana vyombo vyetu vya dola iwe haipo. Niombe tuige mfano wa nchi za wenzetu wamefanya nini; kutoa mishahara inayokidhi mahitaji na akiba, hii itasaidia kumlazimisha Askari kufikiria mara mbili umuhimu wa ajira yake iwapo atafukuzwa kazi. Hii mishahara iendane na makazi mazuri, mikopo ya maendeleo yao binafsi kama ya kujenga nyumba binafsi, usafiri na elimu ya watoto. Adhabu kali sana kwa askari yeyote atakayekamatwa na rushwa ikiwa ni pamoja na kufukuzwa kazi, kupoteza maslahi yote ikiwa ni pamoja na haki za kustaafu na vilevile kupelekwa Mahakamani. Adhabu hizi ukichanganya na mishahara mizuri sana na makazi mazuri yatamfanya askari awaze mara mbili kabla hajakubali rushwa. Ni pale tu vyombo vyetu vya usalama watakapokataa rushwa ndiyo jamii kwa ujumla itaweza kupiga vita ya kweli ya rushwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya jela na mahabusu ni mbaya sana na vinapingana na haki za binadamu. Ukienda kumwona mtuhumiwa aliyeko rumande utalia na inaweza kukuletea hata *pressure*. Huwezi kusema kama ni mahali walipo binadamu. Ni suala lisilopingika kuwa, hutegemei kizuizi kiwe kama hoteli lakini ni utu tu, kumweka binadamu katika mazingira ya kiutu. Sasa hivi kuna sehemu nyingine za magareza kama Segerea utasema ni wanyama ndiyo walio hapo. Magereza hata kwa wale waliohukumiwa ni sehemu ya mafunzo na si sehemu ya mateso. Kuna vitendo vingi vya unyanyasaji wa hali ya juu. Naomba Serikali ilianganalie hili.

MHE. DKT. HAJI H. MPONDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kulipongeza Jeshi la Polisi kwa ujumla katika kulinda usalama wa raia na mali zao pamoja na changamoto zinazowakabili ikiwapo upungufu wa fedha na Askari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, nichukue nafasi hii kumpongeza *RPC* wa Mkoa wa Morogoro, Afande Paul kwa jitihada zake binafsi kwa kushirikiana na uongozi wa Mkoa na wadau wengine katika kudhibiti uvunjifu wa amani unaotokana na migogoro ya ardhi baina ya wafugaji na wakulima. Katika udhibiti huo wa migogoro inayoendelea ya ardhi (wafugaji/wakulima) pamoja na Jeshi kuanzisha programu ya kilimo na ufugaji salama, baadhi ya askari katika Jeshi la Polisi, Mkoani Morogoro nao wanakuwa kisababishi au chanzo cha migogoro hiyo ya wafugaji na wakulima kwa ukiukwaji wa maadili ya utendaji wao wa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kumeonesha katika matukio mbalimbali baadhi ya Maaskari hao hasa Wakuu wa Vituo vya Polisi hususan Kituo cha Mtimbira na Lupiro na Askari wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai kujihusisha na rushwa, hivyo kusababisha kutoa upendeleo kwa wale watuhumiwa wenye fedha hasa wafugaji. Nashauri *RPC* Morogoro awaangalie/awasimamie au kufanya uchunguzi kwa askari hao ili kubaini ukweli na kuchukua hatua stahiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiwango cha posho ya chakula kwa Askari (*Ration Allowance*) kiongezeke hadi kufikia Sh.15,000/= kwa siku badala ya Sh. 6,000/=.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa 100% na kusesitiza Serikali kupeleka kwa wakati mwafaka fedha zote za miradi ya maendeleo inayoidhinishwa na Bunge hili katika bajeti hii. Ahsante.

MHE. JUMA A. NJWAYO: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kwanza kutoa shukrani za dhati kwa wananchi wa Jimbo la Tandahimba kwa kunipa ushirikiano katika kipindi cha miaka mitano kama mwakilishi wao. Ni imani yangu kuwa wataendelea kuniamini ili tuyaendeleze mafanikio tuliyoyapata.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo ya awali, napenda pia kuwapongeza Waziri wa Mambo ya Ndani, Mheshimiwa Mathias Chikawe na Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Dkt. Hussein Mwinyi, pamoja na vyombo vyote vya ulinzi na usalama nchini kwa kazi nzuri zinazotekelezwa.

Napenda kutoa ushauri ufuatao:-

Jeshi la Zimamoto ni muhimu sana kwa ajili ya kupunguza vifo, majeruhi, uharibifu wa mali kwa njia ya moto, mafuriko, ajali za barabarani, kimbunga na kadhalika. Pamoja na jukumu hilo la msingi nchi yetu haitoi kipaumbele na hivyo kuwekeza kwa jeshi hilo. Mifano ni mingi kama nchi nzima inahitaji vituo 152, lakini kuna vituo 52 nchi nzima, mahitaji ya magari ni 280, lakini katika bajeti ya mwaka 2015/2016 imepangiwa gari moja tu, ni kwa nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, napenda kupongeza mpango wa kuanzisha Chuo Kikuu Kishiriki cha Sayansi za Tiba, Lugalo na Ukarabati kwa ajili ya kutoa elimu ya fani za tiba. Rai yangu ni kuwa, Wizara ijitahidi kufanya haraka kukamilisha chuo na pia kufanya mafunzo na utafiti wa tiba kwa askari na raia ikiwa ni pamoja na kupeleka huduma hizi muhimu kwa kambi zetu zote ili askari wasipate tabu wapatapo maradhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri NIDA ikamilishe zoezi la kutoa vitambulisho kwa waliojiandikisha. Mfano, wale waliojiandikisha 2012/2013 hawajapata vitambulisho badala yake ni kuwaelekeza kurudi mara kwa mara kwenye ofisi za Kata. Tafizo ni nini? Kama ni fedha basi waongezewe fedha za kutosha ili tumalize usumbufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, Serikali kupitia Idara ya Magereza ione uwezekano wa kutoa kwa wananchi shamba la Magereza la Chumo ambalo limeachwa kwa muda mrefu bila kuendelezwa. Wananchi wa Kata ya Maundo na Mkoreha wana uhitaji mkubwa sana wa ardhi ya kilimo. Kama Magereza hawana cha kuwekeza wapewe wenye shida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Mambo ya Ndani ikumbuke kuwa, Tandahimba inahitaji Ofisi za OCD na DPO, Halmashauri imewapa viwanja, kwa nini wanasita kuweka kwenye mpango wa ujenzi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. DESDERIUS J. MIPATA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa mchango ufuatao:-

Polisi Wilayani Nkasi wanafanya kazi katika mazingira magumu sana kwani hawana mafuta ya kuwawezesha wamudu operesheni mbalimbali za kiusalama. Wakati mwingine hali hii huweza kuhatarisha haki na usalama wa wanyonge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha ya uendeshaji haitoshi kiasi kwamba, magari yanakosa fedha ya kununulia matairi ya gari. Hii ni aibu kwa jeshi muhimu kama hili. Nikiwa Mbunge wa Jimbo la Nkasi Kusini nimekuwa napewa ushirikiano wa Polisi jambo ambalo linatia faraja, nawashukuru. Kwa sababu ya kutambua hayo nimechangia Sh. 5,000,000/= katika ujenzi wa Kituo cha Kijiji cha Mpasu. Naiomba Serikali ituongeze fedha za kumaliza jengo lililokwisha anzishwa na wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Nkasi iko mpakani na mpaka wake ni mrefu sana unaunganisha nchi za Burundi na Kongo. Tunahitaji Askari, vitendea kazi na fedha. Pia Askari wa Nkasi wanakaa katika nyumba ambazo hazijakamilika, naomba zikamilike kwa kutoa fedha zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Nkasi kuna hali ya hewa nzuri, ingawa ipo dhana inayojengeka ya kuwaleta Watumishi wenye matatizo kama adhabu. Dhana hiyo inatakiwa ife. Polisi ni muhimu na Serikali iwalipe fedha za posho na marupurupu mengine ambayo ni haki yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru kwa kuendelea kutuunga mkono.

MHE. AHMED A. SALUM: Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na kukua kwa Jiji la Dar es Salaam kumekuwa na tatizo kubwa la nyumba nyingi kuungua moto na mara nyingi kikosi cha zimamoto kinashindwa kufika kwa wakati kuzima moto kwenye eneo husika.

Ushauri, naomba Serikali iongeze fedha na juhudi ili kikosi hiki kipate kuwa cha kisasa na kuwa na vifaa vya kisasa ili kiweze kufanya kazi ya uzimaji moto kwenye matukio husika kwa wakati na haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Operesheni Tokomeza askari waliweza kufanya vitendo ambavyo havikuwa vya maadili ya Jeshi la Polisi au Jeshi. Kwa mfano, kuna mtu anaitwa Mashiri mwenyeji wa Kata ya Didia, Wilaya ya Shinyanga alikuwa na mifugo yake katika Kijiji cha Lumbe, Wilaya ya Kaliua, Mkoa wa Tabora alinyang'anywa mifugo yake ng'ombe 254. Hivyo, alichukua hatua za kisheria ikiwemo kumletea Mheshimiwa Waziri Wassira ambaye alikuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mahusiano na Uratibu na Mheshimiwa Wassira alipokea malalamiko hayo kwa maandishi, lakini mpaka leo hajalipwa mifugo yake. Napenda kujua Serikali imechukua hatua gani mpaka kuwalipa fidia wale wote walionyang'anywa mali zao kutokana na Operesheni Tokomeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri, naiomba Serikali ijaribu kuwafidia wote waliopoteza mali zao au kunyang'anywa kutokana na Operesheni Tokomeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi la Polisi wana uhaba mkubwa sana wa nyumba za kuishi na kufanya Jeshi la Polisi kutokufanya kazi zao vizuri. Nashauri Serikali ijenge nyumba za Jeshi la Polisi ili kuondoa tatizo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na naunga mkono hoja.

MHE. AMINA A. CLEMENT: Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi pamoja na Naibu wake, pia siwezi kuwasahau Askari na Watendaji wote kwa kazi zao za kila siku wanazozifanya za kutulinda raia pamoja na mali zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwakumbusha ndugu zangu wa Jeshi la Polisi kuwa, kuna wimbo wanaotakiwa waimbe kila siku kabla ya kuanza kazi zao za kila siku. Ule wimbo siyo wimbo tu wa kujifurahisha ila ile ni ahadi au kiapo. Je, ni kwa nini Askari wetu hawafuati yale maneno yaliyomo katika kiapo kile na kuyatendea haki katika utekelezaji wake?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Wizara pamoja na Serikali yetu wauimbe ule wimbo wa askari na urekodiwe kwenye vyombo vya habari ili wananchi wote wauielewe na inapotokea askari kukiuka angalau moja katika kiapo kile japo kwa bahati mbaya, mwananchi anaweza kukukumbusha kile kiapo badala ya kugombana na kujibizana maneno ya kashfa, hii itasaidia askari wetu kukumbuka wajibu wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza sana sana aliyetunga shairi lile na pia naomba mtu huyu kama yupo hai atendewe haki ya kuzawadiwa kwa shairi zuri sana la kuwaasa askari wetu, kama hayupo katika dunia hii basi akumbukwe kwa wema wake kwa usia mzuri aliowatungia Askari wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya majengo wanayoishi Askari wetu bado yamezekwa kwa mabati ya asbestos na bati hizi Serikali inajua kama ni hatari kwa afya za binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri ajibu hapa kwenye Bunge lako, ni lini nyumba hizo zitafanyiwa ukarabati na kuezuliwa bati hizo ambazo ni hatari sana kwa afya za binadamu zinazosababisha *cancer* inayoitwa *asbestosis*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba pia Mheshimiwa Waziri awaambie wale wote wanaotumia maji ya mvua yanayopita katika bati hizi ni hatari kwa matumizi ya binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante.

MHE. HAMAD ALI HAMAD: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze na watumishi wa Jeshi la Polisi ambao walistaafishwa mwaka 2010 Mei, lakini kwa kuwa walikuwa bado wana afya njema waliongezewa miaka miwili ya ajira ya mkataba kuanzia Julai, 2010 hadi Juni, 2012 ambapo walimaliza mkataba wao. Jambo la kusikitisha ni kwamba, waajiriwa hawa walikuwa toka Rukwa sita, Mtwara watano na Zanzibar 34.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo linalosikitisha kwa watu hawa ni kwamba, wale wote kutoka Tanganyika walilipwa mafao yao baada ya kumaliza mkataba, lakini hadi leo sasa ni miaka mitatu wale wote kutoka Zanzibar hawajapewa stahili zao. Hii ni nini au ni ule mkakati wa Watanganyika waliovaa koti la Muungano wa kuwadhalilisha Wazanzibari?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri awaeleze watu hawa ni lini watalipwa haki zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupandishwa vyeo. Vijana Askari ambao walipandishwa vyeo tangu mwaka 2012 hadi leo hawajapata nyongeza zao za kupandishwa vyeo, sambamba na hilo kuna Maafisa ambao walimaliza mafunzo ya ngazi ya nyota moja na baada ya kurudi katika mikoa yao tu walipokea taarifa za kustaafishwa kazi, ni jambo linalosikitisha sana. Nashauri Serikali kwamba kwa kuwa Magereza wana sheria ya Ofisa chini ya umri wa miaka 60 hawezi kustaafishwa, naomba Polisi nao sheria iletwe na kwa wakati huu pia ambapo sheria bado, basi ubinadamu utumike wapewe nafasi ya kuendelea na kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Polisi wanavyotumiwa na CCM kudhalilisha Vyama vya Upinzani. Inashangaza kwamba kila jambo linalotokea la viashiria vya vurugu vinahusishwa na Viongozi na wafuasi wa Vyama vya Upinzani, lakini hata pale Wapinzani pamoja na mali zao wanapohujumiwa bado Polisi hawachukui hatua zozote na kwamba huwageuzia kibao hao hao Wapinzani waliohujumiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, Mkutano wa CUF Makunduchi, 29 Machi, ulivyohujumiwa kwa kupigwa vibaya kwa wafuasi waliokuwa wakirudi mkutanoni, lakini Polisi hakuna waliyemkamata na kumtia hatiani, kuchomwa ofisi za CUF na CCM Tumbatu Unguja, walikamatwa CUF pekee na CCM wanapeta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Mkutano wa Kitope, Polisi walitumia nguvu isiyo ya kawaida kuhakikisha kwamba wanakidhi kiu ya CCM ya kwamba CUF hawafanyi mikutano yao hadi leo unyanyasaji huo unaosimamiwa na Polisi bado unaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulipuliwa ofisi ya CUF Kisauni. Tangu Ofisi ya Jimbo la Kisauni ya CUF ilipolipuliwa katika eneo la Kisauni Unguja hadi leo hakuna mtu aliyetiwa hatiani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, naelewa kuwa makosa ya barabarani ni lazima yaendane na maonyo pamoja na faini kwa makosa yanayosababishwa na uzembe, lakini imekuwa kawaida kwa askari wa barabarani kutoza faini hata kwa makosa ambayo yanaweza kupewa onyo kwa dereva. Wananchi wanatambuaje makosa yenye kupewa onyo na ya kutozwa faini? Nchi nyingi zina utaratibu huo wa kuainisha makosa hayo kwa uwazi, kwa nini askari wanatumia mwanya huo kutoza faini kwa makosa yenye kustahili onyo na kuchochea mazingira ya rushwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kuna tabia ya maaskari kutembea na vitabu vya makosa maarufu kama *notification books* na huwa wagumu kutoa risiti ama stakabadhi za malipo kwa walipaji. Hii inaleta malalamiko kuwa askari hawa huwa wana vitabu vyao. Kwa nini Jeshi la Polisi sasa lisiwe na mfumo kama wa kielektroniki utakaomwezesha mtenda kosa kulipia kosa lake na kupewa stakabadhi papo kwa papo? Kama zilivyo mashine za EFD?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini Jeshi la Polisi lisiwe na uwezo wa kujenga Vituo vya Polisi lakini liwe na uwezo wa kununua magari ya anasa kama *Range Rover*? Kwa mfano, hivi karibuni imeonekana gari aina ya *Range Rover* ikiwa na namba za PT 1538, haya ni matumizi yasiyo na tija kwa Jeshi la Polisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu wa kupekua ama kukamata watuhumiwa siku hizi Polisi imeshindwa kusimamia maadili yake na hata kuonesha baadhi ya Askari Polisi wakiwakamata na kuwapiga wanawake huku baadhi ya maungo yao ya siri yakionekana. Hii imetokea wakati wa dhoruba ya kuzuia mkutano wa CUF hivi karibuni, askari wale walionekana hata kwenye *video* na Vyombo vya Habari wakiwadhalilisha mama zetu ikiwemo kumpiga mmoja wa akinamama kwenye titi lake. Je, Askari wale wamechukuliwa hatua? Kama laa, watachukuliwa hatua gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Polisi wanaotumia pikipiki; Polisi wengi wamekuwa wanajihusisha na vitendo vya rushwa hasa Polisi wanaotumia

pikipiki na wamekuwa wakifanya hivi hasa pale wanapokutana na waendesha bodaboda ama magari ya abiria na kusababisha usumbufu mkubwa. Je, Jeshi la Polisi lina utaratibu wa kuwaratibu Polisi wanapokua katika doria zao?

MHE. SAID A. ARFI: Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la makazi na usafiri kwa Askari Polisi na Magereza. Uchache na uchakavu wa nyumba zilizopo za Askari Polisi na Magereza hususan Mpanda Mjini. Aidha, tatizo hili ni kwa Mkoa mzima wa Katavi ukizingatia Mkoa huu ni miongoni mwa Mikoa mipya minne, hakuna miundombinu ya kutosheleza kama Mkoa, pia vitendea kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, malimbikizo ya posho/uhamisho na madaai mengineyo kuchukua muda mrefu kulipwa, uwiano wa ukubwa wa Mkoa na mgao wa uendeshaji hususani mafuta bado ni tatizo na uchakavu wa magari yaliyopo katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri, ukurasa wa 46.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu wakimbizi 162,156 waliopewa uraia hivi karibuni, naomba kauli ya Serikali kwa kuwa uandikishaji wapiga kura unaendelea hivi sasa Mkoa wa Katavi na wakimbizi hawa ni raia na wana haki za kikatiba wataandikisha kama wapiga kura na wanayo haki ya kugombea? Kwa nini eneo lililokuwa ni la makazi halikutenga maeneo ya kutosha ya uandikishaji, kuna kituo kimoja tu katika eneo la Katumba ambalo sasa idadi ya Watanzania imeongezeka mara dufu. Naomba sana katika hitimisho, Mheshimiwa Waziri aweke bayana suala hili la uandikishaji kwa hawa raia waliokuwa wakimbizi kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.

MHE. NYAMBARI C. M. NYANGWINE: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutumia nafasi hii kutoa maoni kuhusu Wizara hii kama ifuatavyo:-

Pongezi kwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Watendaji wengine wa Wizara na hususan viongozi wa Jeshi letu la Polisi kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, rushwa katika Jeshi la Polisi; rushwa imekithiri katika Jeshi la Polisi hususan Trafiki wa barabarani. Imekuwa ni kawaida kuomba na kupokea rushwa bila hata aibu. Pia Askari wa Uhamiaji nao wanahusika. Askari wanaohusika na upelelezi wa makosa mbalimbali. Upelelezi haufanyiki na badala yake rushwa inafanya kazi. Tubadilike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uonevu wa Jeshi la Polisi Wilayani Tarime. Polisi wanawapiga hovyoy raia wa Tarime, wanawabambikia kesi za ajabu ajabu na wanapokea rushwa hadharani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na mwekezaji wa Mgodhi wa North Mara amewaonea vya kutosha wananchi wa Nyamongo, Nyamwaga na vijiji vingine vya jirani. Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani na IGP wana taarifa hiyo. Naomba majibu sahihi namna ya kuondoa adha hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mauaji ya raia yasiyo na hatia hasa Nyamongo, madeni ya wazabuni; nashauri Serikali ifanye kila linalowezezana ili iweze kuwalipa wazabuni hasa wale wa magereza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haja ya uzalendo na uadilifu kufundishwa kwa wananchi, Polisi na hata Polisi Jamii. Hii itasaidia sana kupunguza malalamiko toka raia hadi Polisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haja ya kulifanya Jeshi letu la Polisi kuwa la kisasa. Jeshi letu la Polisi liwezeshe vyombo vya kisasa ili liweze kutenda kazi yake kwa ufanisi wa hali ya juu. Kunahitajika vyombo vya kisasa vya sayansi na teknolojia ili kulifanya jeshi letu la Polisi lifanye kazi kulingana na wakati wa sasa au uliopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uhalifu, vitisho, wizi, ujambazi na udanganyifu ni vitendo ambavyo vile vile inabidi Jeshi la Polisi lijipange ili kukabiliana navyo kwani hali hizi zote husababisha kutoweka kwa amani, usalama na utulivu katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la wahamiaji haramu; ni tatizo katika nchi yetu, naishauri Serikali iimarise ulinzi katika maeneo ya mipakani. Pia raia hasa Viongozi wa Vijiji/Vitongoji na Mitaa wapewe elimu ya uzalendo ili kuwatambua kuwabaini na kuwakamata wahamiaji na kuwapeleka katika vyombo vya dola.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. MARY P. CHATANDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naunga mkono hotuba ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kuwa na vyombo imara na madhubuti vya ulinzi na usalama kwa kazi nzuri wanayoifanya mbali ya changamoto wanazokabiliana nazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokupewa bajeti zao zote kama walivyoidhinishiwa ni kuwaviza kutekeleza majukumu waliyojipangia. Hivyo, niitake Serikali kuwapatia fedha yote iliyobaki katika bajeti ya mwaka 2014/2015 inayoishia Juni waweze kutekeleza majukumu yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, makazi ya askari bado hayatoshi mbali na juhudi ya Serikali kujenga nyumba ambazo hazitoshi na hata zile zilizopo zinahitaji ukarabati ili ziwe na hadhi ya kuishi askari. Kwa mfano, nyumba za askari zilizopo Korogwe ni za mkoloni, niombe nyumba hizo zikarabatiwe ili zifanane na usafi wa askari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi la Magereza; Jeshi hili lina rasilimali watu kubwa ya kuwezesha Jeshi la Magereza kujitegemea. Nishauri Serikali kupitia rasilimali waliyonayo iwawezeshe kuwapatia vitendea kazi magereza ya kilimo wapewe mtaji zikiwemo zana za kilimo, pembejeo na kadhalika. Kwa kufanya hivyo, Serikali itakuwa inawekeza na Jeshi la Magereza litajilisha lenyewe na ziada kuuzia Serikali na kupata maduhuli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halikadhalika JKT wakiwezesha wataweza kufanya uzalishaji mkubwa ukiwemo ufundi wa fenicha au bidhaa mbalimbali tunazoziona kwenye maonyesho na kuingizia Serikali mapato kupitia maduhuli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na Serikali ione uwezekano huo wa kuwezesha Magereza na JKT ili waweze kujitegemea.

MHE. KHERI ALI KHAMIS: Mheshimiwa Mwenyekiti, Polisi Jamii. Polisi jamii tangu imeanzishwa imewezesha kupunguza uhalifu kwa kiasi kikubwa lakini vijana wanaofanya kazi hiyo wanavunjwa moyo.

Moja, wanapowapeleka wahalifu kituoni hawapati ushirikiano, wanapuuzwa. Polisi wanaona kama vile wanawaongezea kazi.

Pili, wanapopeleka ombi la kuwapatia msaada wa Askari ili wafanye operesheni Mitaani, hawapatiwi na wanapofanya operesheni wanapigwa na kuumizwa hadi kupelekea kulazwa hospitali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu ni kwamba; moja, Polisi Jamii wanapopeleka wahalifu vituoni wanapokelewa kama wanavyopokelewa Askari Polisi na kukamilisha taratibu zote za Polisi.

Pili, Polisi Jamii wanapoomba msaada wa kupatiwa Askari kwa ajili ya operesheni maalum, basi wapatiwe ili wapate ulinzi stahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Polisi Jamii ni Kamisheni kama ilivyo Kamisheni nyingine kama vile *FFU*, Upelelezi na nyinginezo, lakini Polisi Jamii Askari wake hawalipwi mafao kama wanavyolipwa Askari katika Kamisheni nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu kwa Serikali ni kwamba, Kamisheni ya Polisi Jamii ipatiwe mafao stahili na Bunge liarifiwe ni lini mafao hayo yataanza kulipwa kama wanavyolipwa askari katika Kamisheni nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ni vizuri Askari Polisi kupandishwa cheo kama tunzo kwa utendaji mzuri wa kazi na kama kakamilisha vigezo vingine. Lakini kumekuwa na utaratibu wa kuwaacha Askari ambao wanakuwa mstari wa mapambano dhidi ya uhalifu. Pamoja na kutopandishwa vyeo, Askari hao wamekuwa wakitishwa na wahalifu na kuambiwa kwamba hawatapata vyeo maisha yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri kwamba Askari ambao wamekaa muda mrefu bila kupandishwa vyeo, majalada yao yapitiwe na kuchunguzwa, iwapo kuna makosa yoyote waliyofanya ambayo yamepelekea kutopandishwa vyeo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka huu wa 2014/2015 kumekuwa na ajali za kutisha zilizopoteza maisha ya Watanzania wengi. Wengi wa wahanga wa ajali pamoja na mambo mengine unachangiwa na:-

Moja, magari kupakia abiria zaidi ya idadi iliyoidhinishwa na *SUMATRA*; pili, magari kutokuwa na mikanda; na tatu, abiria kutofunga mikanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Askari wa Usalama Barabarani wafanye ukaguzi wa magari ili kuhakikisha kwamba: moja, abiria waliomo ndani ya gari ndiyo walioidhinishwa na *SUMATRA*; na pili, viti vya magari vyote view na mikanda na abiria wote wafunge mikanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. BEATRICE M. SHELLUKINDO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi kwa hotuba nzuri na kazi ngumu ya Wizara hii. Aidha, nampongeza Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Watendaji Wakuu na Watendaji wote Wilayani. Kipekee nampongeza *IGP* Mangu na Makamishna wote na Mkurugenzi Mkuu wa Uhamiaji Bwana Ambokile na Watendaji wake wote kwa kazi nzuri wanazofanya. Nawapongeza kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, amani ya nchi yetu ni wazi inatokana na mchango mkubwa wa sekta hizi. Tumeshuhudia Askari wanafanya kazi katika mazingira magumu, mvua, mafuriko, jua na vyote vyao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Kilindi ina takriban miaka 12 lakini hadi leo haina Kituo cha Polisi cha Wilaya, tuna *Police Post. Store* imegeuzwa kuwa mahabusu, hakuna hewa. Nyumba nazo ni vibanda ambavyo kwa uzito wa kazi wanayofanya Askari hawa inasikitisha. Nimekuwa nikiahidiwa kuwa Wizara itajenga kituo mwaka hadi mwaka. Naomba sasa Kituo hicho kipewe kipaumbele kwani zipo Wilaya zimeanza baada yetu, tayari zina Vituo vya Polisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na jioografia ya Wilaya ya Kilindi na ukubwa wake, pamoja na Mahakama kuwa Wilaya jirani, takriban kilometa 122, magari yamekuwa chakavu sana. Naomba tupatiwe magari ili kukidhi shida hii na kuwawezesha maaskari kufika kwenye matukio kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vitendea kazi navyo ni muhimu kama komputa na kadhalika. Pamoja na OCD na Polisi wote wa Wilaya ya Kilindi, hufanya kazi katika mazingira magumu wakiwa na makazi duni. Naomba basi angalau watembelewe mara kwa mara ili kuwatia moyo hata kama siyo kutoka Makao Makuu, basi kutoka Mkoani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, kutokana na mazingira magumu ya Kilindi na kwa sababu Wilaya iko pembezoni, Askari wetu wapatiwe posho maalum. Hii pia itazuia tamaa ya rushwa na pia kuwapa motisha kufanya kazi zao kwa bidii zaidi na uadilifu zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, lakini nikisisitiza ujenzi wa kituo.

MHE. AMINA N. MAKILAGI: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nakushukuru wewe na pia nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuchangia sekta hii muhimu ya ulinzi na usalama wa raia na mali zao na ulinzi na usalama wa nchi yetu. Mara baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu, naomba nijielekeze katika kutoa ushauri katika maendeleo machache niliyoyachagua kuyatilia mkazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango na ushauri wangu ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuipongeza Serikali kwa kazi nzuri ya kuhakikisha nchi na raia wa Tanzania wanaendelea kuishi kwa usalama. Nawapongeza sana Mawaziri na Watendaji wote wa Wizara hizi kwa kazi nzuri na ngumu wanayoifanya ya kuhakikisha ulinzi, usalama wa nchi raia na mali zao unaendelea kuimarika siku hadi siku.

Pamoja na pongezi, naomba kushauri kwamba Serikali iendeleo kuimarisha ulinzi na usalama katika nchi na raia wa Tanzania ili kuondoa viashiria vyote vya uvunjifu wa amani.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda Mawaziri watakapokuja hapa watuambie; je, anayo taarifa kuwa wapo baadhi ya watu wa hapa nchini wameanza kutoa mafunzo ya kivita kwa vijana wetu? Kama anazo taarifa: Je, Serikali imejipangaje kudhibiti hali hiyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kazi nzuri inayoendelea kutendwa na kutoa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa kazi za vyombo vya usalama, bado fedha zinazotengwa na zinazotolewa hazitoshi kutekeleza majukumu ya vyombo vya usalama na matokeo yake wanashindwa kukarabati vitendea kazi kama vile magari, vyombo vya majini, mafuta ya magari ili kukabiliana na majanga ya moto, kununua magari na vifaa vya uokozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Serikali itenge na kutoa fedha zote zilizoidhinishwa kwa ajili ya utekelezaji wa kazi za vyombo vya ulinzi na usalama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuishukuru sana Serikali katika kuendelea kuboresha maslahi ya Askari katika vyombo vyote vya ulinzi na usalama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi hizo, naomba kushauri yafuatayo:-

- (a) Maslahi ya mshahara wa Askari yatazamwe upya, posho iongezeke toka kiwango cha sasa hadi kufikia Sh. 10,000/= kwa mwezi;
- (b) Nyumba za Askari ziboreshwe;
- (c) Utaratibu wa posho za Askari wanaofanya kazi katika mazingira magumu uangaliwe upya;
- (d) Utaratibu wa Askari kupandishwa vyeo uangaliwe upya;
- (e) Utaratibu wa posho na maslahi wa Askari wanaopandishwa madaraka uangaliwe upya.
- (f) Vilevile napenda kujua, Mheshimiwa Waziri atakapohitimisha hotuba yake atuamabie Serikali imejipangaje kuboresha maslahi ya Askari wetu? Kwani matatizo yao yanajirudia kila mwaka;
- (g) Gharama za umeme na maji kwa askari wetu nani anayelipa? Ni wao wenyewe au Serikali?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili Jeshi la Magereza lijiendeshe kiuchumi, nashauri Serikali itoe nyenzo kwa Magereza ili iweze kujiendesha; wapatiwe zana za kilimo, stahiki za kazi na vitendea kazi ili wazalishe mali na mali hizo

ziweze kuwahudumia wafungwa na hata wafungwa wanapotoka Gereza watoke na kitu kipya walichojifunza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa juhudi mbalimbali za kupunguza vifo vya wanawake katika Mikoa ya Mara, Wilaya ya Butiama na Mikoa mbalimbali hapa nchini. Naomba hizi jitihada ziendeleo za kudhibiti vitendo hivi vya kinyama. Napenda kumsikia Mheshimiwa Waziri anasema nini juu ya kudhibiti vitendo hivyo na kukomesha vitendo hivyo vya mauaji ya albino, vikongwe, walemavu na wanawake wasio na hatia?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna baadhi ya wanasiasa wamekuwa wakisikika kutoa kauli zinazoashiria uvunjifu wa amani. Napenda kusikia: Je, Serikali inajua na imejipangaje kudhibiti hali hiyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi la Kujenga Taifa. Naishukuru Serikali kwa kuimarisha na kurudisha mafunzo ya JKT kwa vijana wetu. Naomba kambi za mafunzo ziimarishwe ili kuongeza vijana wanaojiunga kwa ajili ya kuwajengea uwezo na kujifunza stadi za kazi. Nashauri kuwa, kambi hizi za JKT zijengwe katika mipaka yote nchini kwa ajili ya ulinzi na usalama wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. YUSSUF HAJI KHAMIS: Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii adhimu kumshukuru *Allah* kwa uhai na afya njema kwa sote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu utahusu vitambulisho vya Taifa kwa mamlaka inayohusika.

Pamoja na taarifa iliyopo ndani ya kitabu cha Hotuba ya Waziri kwamba vimetolewa katika Mikoa ya Dar es Salaam na Zanzibar na kwamba tayari vimeanza kutumika, naomba Wizara iangalie kwa umakini mkubwa sana, kwasababu watu wanasumbuliwa sana kupata vitambulisho hivyo. Hivi sasa na bado watu wengi hawajapata vitambulisho hivyo katika zoezi hili la vitambulisho. Mamlaka husika imewafuata watu katika Sheiya mbalimbali kuandikisha na kupiga picha, lakini kuwapatia vitambulisho ambapo ni *point* ya mwisho, wamekwenda kuwapa watu wachache sana, waliobaki wafuatie katika Wilaya zao kupitia Masheha na kusababisha usumbufu mkubwa wa kufuatilia pasipo mafanikio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara ifuatilie kwa kina jambo hili ili kuwaondolea usumbufu wananchi na kila mmoja apate haki yake Kikatiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumzia mikakati ya kupambana na mishahara hewa katika Jeshi la Polisi. Mimi binafsi naungana na mkakati huu

mia kwa mia kwasababu ni ufiadi miongoni mwa ufiadi. Lakini zoezi hili kwa kiasi kikubwa limeathiri watu ambao hawahusiki hasa Zanzibar. Kwa kuwa Wazanzibar wengi majina yao yameingiliana na kufanana sana kuanzia jina la kwanza mpaka jina mwisho.

Watu kama hawa wameingia katika usumbufu mkubwa wa kuzuliwa mishahara yao kwa takribani miezi miwili sasa, hawapati mishahara eti inaonekana kama mtu mmoja na ka- *forge*. Pamoja na kupeleka vielelezo mbalimbali kama vyeti vya kuzaliwa, vyeti vya skuli lakini bado wanasumbuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali ishughulikie mapema suala hili kwa maslahi ya Taifa.

MHE. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara kwa kuwasilisha bajeti yao.

Pamoja na unyeti wa Wizara hii, Serikali imekuwa haitengi Bajjeti ya kutosha ukilinganisha na majukumu mazito waliyonayo Askari wetu. Wizara hii ina changamoto ambazo naomba Serikali mtupatie majibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Askari wetu wanaishi katika mazingira magumu sana, nyumba ni chakavu sana, zilijengwa katika enzi ya Mkoloni, lakini pamoja na hilo, nyumba zenyewe hazitoshelezi kuishi Askari wote kambini na baadhi ya Askari wana madeni uraiani. Mbaya zaidi kuna Askari ambao wana madeni hata ya pango na kusababisha kudhalilika Uraiiani wanakoishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kuhusu ujenzi wa Ofisi za Polisi Wilayani Kilolo. Ninavyojua Mjini alipo DC ndipo Kamati yote ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya inatakiwa iwepo, lakini Wilaya ya Kilolo OCD ofisi yake ipo tofauti na yalipo Makao Makuu ya Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya hii siyo mpya, ina zaidi ya miaka 10 toka ihamishwe wananchi wanapata usumbufu mkubwa sana kufuata huduma hiyo. Askari wote wa Kilolo hawana nyumba za kuishi. Ni nini mkakati wa Setikali kuhusu Ofisi za Wilaya hii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Gereza Kuu la Iringa kuna changamoto nyingi, lakini kubwa ni msongamano wa wafungwa na mahabusu. Gereza lina uwezo wa kuchukua watu 228 lakini kuna wafungwa 452. Gereza halina eneo maalumu kwa ajili ya watoto. Wafungwa hawana mashati, masweta, mablanketi hayatoshi na hivyo kukabiliwa na ugonjwa wa *pneumonia*. Pia wana gari moja tu ambalo halitoshelezi kutoa huduma zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Gereza la Mgagao Iringa linatumia majengo ya iliyokuwa Kambi ya Wakimbizi wa Afrika ya Kusini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, historia ya Makambi yaliyoachwa na Wakimbizi yamekuwa yakikabidhiwa kwa Taasisi za Elimu au Makambi ya JKT kama Kambi ya Mazimbu Morogoro, Mpwapwa, Kanembora na Kasulu. Kwa nini Mgagao tu ndiyo liwe Magereza? Mnakumbusha nini historia ya Mandela? Naomba Serikali itoe kipaumbele na kubadili matumizi ya eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee Jeshi la Zimamoto Iringa. Naipongeza Serikali kwa kutuletea Askari 36 ambao wameweza kufungua vituo katika Wilaya ya Kilolo na Mufindi lakini Askari hawa wanafanya kazi katika mazingira magumu sana, hawana nyumba za kuishi na wala hawapatiwi *Housing Allowance*, hawana *uniform* kwani wanashona kwa pesa yao wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkoa wetu una gari moja tu zima, wakati tunao uwanja wa ndege na msitu mkubwa katika Wilaya ya Mufindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Mji wa Iringa unakua sana. Kumekuwa na matukio ya moto ya mara kwa mara, yakiwemo Mabweni ya shule katika Jimbo la Isimani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wetu umekuwa na ajali za mara kwa mara katika barabara kuu iendayo Mlima Kitonga ambao huwa unasababisha kuziba kwa barabara kwa muda mrefu, hivyo kunahitajika gari la uokozi yaani *crane* ya kunyayua makontena. Pia kunahitajika *ambulance* ya kubeba majeruhi wa ajali mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu madeni ya Wazabuni kwa Jeshi la Polisi; tatizo hili ni kubwa sana kiasi kwamba limekuwa likisababisha hata Wazabuni kutaka kusitisha huduma kwa vyombo vyetu hivi. Pia Wazabuni wetu wengi wamechukua mikopo Benki na kutishiwa kuchulikiwa ardhi zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali itoe mkakati wa kulipa haya madeni ambayo ni mabilioni ya pesa.

MHE. HUSSEIN MUSA MZEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Naipongeza Wizara ya Mambo ya Ndani kwa juhudi zake za kulinada wananchi wetu.

Katika mchango wangu wa mwaka 2014 niliomba Polisi Ziواني utengenezwe uzio ambao ni mbovu, hufanya boma hilo likawa halina usalama wa kutosha. Wananchi wanaingia ndani bila kupitia mlango mkuu; sasa hili ni tatizo kubwa kwa sehemu yenye vifaa vya kipolisi kama bunduki na mambo

mengineyo. Naomba tena kwa mara ya pili uzio wa boma uongezwe katika bajeti hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nyumba za Askari ni mbovu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nyumba za Polisi Ziwani ni hatari kwa maisha ya binadamu yoyote, matatizo yanayozikabili nyumba hizi za Askari ni pamoja na kuvuja sana hasa wakati wa mvua, hazikaliki; zina nyufa nyingi wakati wowote zinaweza kusababisha maafa makubwa; miundombinu ya majitaka haifanyi kazi. Ni adha kubwa kwa Askari wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba malimbikizo yao ya posho wapatiwe haraka sana. Askari wanatekeleza amri wanayopewa bila ya kusita ingawa kufanya hivyo mara nyingi hulazimu kuingia katika madeni. Kwa muda mrefu sasa tumeambiwa kuwa madeni yanahakikiwa, ni lini sasa yatahakikiwa ili Askari wetu wapatiwe malipo yao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la posho ya chakula tumelipigia debe toka miaka iliyopita, tukionyesha ukweli kwamba Sh. 5,000/= hazitoshi. Mwaka uliopita yaani mwaka 2014 iliongezwa Sh. 100/= tu na kuwa ni Sh. 6,000/= posho hii ukiangalia kimazingira, haitoshi kabisa. Naomba waongezewe angalau zifike Sh. 10,000/=.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa mara nyingine tena, naunga mkono hoja.

MHE. HAJI KHATIB KAI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiofichika kwamba Jeshi la Polisi ndilo lenye dhamana ya ulinzi wa wananchi na mali zao. Vile vile ili Jeshi hili liweze kufanya kazi au kutekeleza wajibu wake huo ni lazima liwekewe mazingira mazuri ya kutekeleza wajibu wake kama vile makazi na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kitabu cha Hotuba ya Waziri, ametaja maboresho ya Jeshi la Polisi pamoja na kulifanya Jeshi hilo kuwa la kisasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani kulifanya Jeshi la Polisi kuwa la kisasa kwa upande mmoja ilhali kuna maeneo Jeshi hilo halina hata makazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nikichangia kwenye hotuba ya Wizara hii mwaka 2013/2014 nilisema Askari Polisi wa Kituo cha Polisi Wilaya ya Micheweni hadi sasa ni miaka 39 hawana nyumba na hadi sasa Serikali hii ya CCM haijafikiria kuwajengea nyumba Askari wa kituo hicho.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikiwa ni utaratibu wa kazi yao, usumbufu wanaoupata wa kwenda na kurudi kila siku, jambo ambalo linawafanya kutokuwa na hamu wala nguvu ya kutekeleza majukumu yao, kwani muda wote wanafikiria nitafika saa ngapi kazini, lakini pia wanafikiria nitafika nyumbani saa ngapi; kwa wale ambao wanaishi nje ya Micheweni; kutokana na hali hiyo, kamwe hatuwezi kulifanya Jeshi la Polisi kuwa la kileo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza sana OCD wa Kituo cha Polisi Wilaya ya Micheweni kwa juhudi ambayo ameionesha baada ya kuona Askari wake anaowaongoza katika kituo hicho jinsi wanavyosumbuka kwa kwenda na kurudi kila siku, kwa kutafuta wahisani, wafadhili, wafanyabiashara pamoja na sisi Wabunge wa Wilaya ya Micheweni, kukaa pamoja na kufikiria njia ya kuweza kuanzisha ujenzi wa nyumba za Askari wa kituo hicho na hadi sasa ujenzi huo umeshakamilika kwa hatua ya kuezekwa, ujenzi ambao utaweza kusaidia makazi ya zaidi ya Askari 30.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na juhudi ambayo ameionesha OCD wa Kituo cha Polisi Micheweni, nitamtaka Mheshimiwa Waziri wakati wa kufanya majumuisho aniambie Serikali kupitia Wizara yake itasaidia vipi juhudi za OCD huyu ili aweze kukamilisha ujenzi huu pamoja na kuongeza ujenzi wa jengo lingine ili kumaliza kabisa tatizo la makazi ya Polisi Micheweni?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nikichangia kwenye Wizara hii mwaka 2013/2014 nilisema Micheweni ni eneo lenye Madiko mengi, hivyo ni vyema Ofisi ya uhamiaji Wilaya ya Micheweni ipatiwe gari badala ya pikipiki, hasa ukizingatia wakati huu ambao dunia imekumbwa na changamoto kubwa ya ugaidi. Vile vile Micheweni ni eneo ambalo liko karibu sana na nchi jirani Kenya, nchi ambayo sote tunasikia yanayotokea (katika) nchi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo basi, kupatiwa usafiri wa gari Ofisi ya Uhamiaji Wilaya ya Micheweni kutawafanya Askari wa Uhamiaji kufanya doria kwa ufanisi zaidi na kuweza kuwabaini raia wa kigeni popote walipo, kwani Micheweni ni eneo lenye mchanganyiko wa raia wa Tanzania na raia wa Kenya na hata raia wa nchi nyingine wanaweza kuingia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni baada ya kufanya utafiti wangu mwenyewe, ndipo nimebaini kuna umuhimu mkubwa sana. Hivyo basi, namwomba Mheshimiwa Waziri anijibu: Je, atakuwa tayari kwa mapendekezo yangu ya kupatiwa gari Ofisi ya Uhamiaji Wilaya ya Micheweni ili kuiokoa Micheweni na Taifa zima kwa ujumla?

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nashukuru.

MHE. DKT. CYRIL A. CHAMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na wimbi la ujambazi katika Tarafa ya Kibosho Wilaya ya Moshi, wananchi wa Tarafa hiyo walijitolea kuchanga fedha ili kujenga Kituo cha Polisi katika kijiji cha Mkomilo, Kata ya Okani. Jitihada hizi ziliungwa mkono na viongozi mbalimbali wakiwemo Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Waziri Mkuu, IGP Mstaafu, Said Mwema. Kituo hiki kilifunguliwa na Mheshimiwa Rais, Juni 2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, hadi kituo kinakamilika, wananchi wa kibosho walikuwa wakidaiwa Shilingi milioni 97 na wameshindwa kuzipata kutokana na hali duni ya vipato vyao. Nililileta jambo hili Serikalini nikaiomba Serikali ioneshe kuwaunga mkono wananchi hawa kwa kumlipa mkandarasi kiasi kilichobakia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2012 aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Ndani Mheshimiwa Dkt. Emmanuel Nchimbi na aliyekuwa IGP, Ndugu Said Mwema kwa pamoja waliahidi kuwa Serikali ingeingilia kati na kulilipa deni hili. Hata hivyo pamoja na kuwakumbusha kila mwaka Serikali haijatumia ahadi yake hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikizingatiwa kuwa uamuzi wa wananchi kuchangia ili kukijenga Kituo cha Polisi cha kisasa ni wa busara na umeipunguzia Serikali mzigo wa kukijenga kituo hiki, ilitegemewa kuwa Serikali ingefanya wepesi kulipa kiasi hiki kidogo kilichobaki. Hivi sasa mkandarasi ameanza taratibu za kimahakama za kuweka zuio kwa Serikali kutumia kile kituo hadi hapo atakapolipwa fedha zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni matumaini yangu kuwa Serikali italipa jambo hili kipaumbele katika bajeti hii ya mwaka 2015/2016.

MWENYEKITI: Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, wachangiaji wetu wote wamekwisha. Sasa namwita Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi kwa dakika 15!

NAIBU WAZIRI WA WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru nami kwa kunipa fursa hii ya kuchangia kwenye hoja ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, kama ambavyo wenzangu wamefanya.

Naomba uniruhusu niishukuru familia yangu kwa kuendelea kunivumilia pale ambapo ninakuwa sipo karibu, lakini kubwa nawashukuru kwa kunipa *support* inayohitajika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia niwashukuru wapiga kura wangu wa Jimbo la Chumbuni, wapo wanaolalamika kwamba mara nyong'i sipo, lakini pia wapo wanaojua kwamba natafuta na kutafuta si lazima utafute nyumbani

kwako. Naendelea kuwaomba kwamba, tuendeleo kushikamana ili tuweze kufikia malengo na mwelekeo mkubwa upo mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nianze kutoa mchango wangu kwa kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote na kwa kuanzia nianze na Kamati ya Kudumu ya Ulinzi na Usalama. Wametoa ushauri mwingi, wametukosoa na mapendekezo mengi kwa Serikali; ni tamaa yetu kwamba, wataendelea kutuunga mkono kuhakikisha mapendekezo hayo ambayo yamepelekwa Serikalini na yale mashauri ambayo wametupa sisi, tunaahidi kuyatekeleza kikamilifu.

Nimshukuru pia Msemaji wa Kambi ya Upinzani, ingawa lazima nimwambie ukweli kwamba, hakutoa ushauri kwenye bajeti, isipokuwa alikuwa anaomba kura kwa wananchi na hasa kwa Askari Polisi na wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasikitisha kwamba hili limetokea na kubwa zaidi nafikiri nimitahadharishe tu asianze majigambo kwa sababu kuna usemi wa Kiswahili unasema; mkamia maji hayanywi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niende kwenye ufafanuzi wa baadhi ya hoja ambazo zimetokea. Nataka nianze na Fungu 14 - Zimamoto. Wabunge wengi wamezungumza kuhusu umaskini ilionao Zimamoto, umaskini wa watenda kazi, wa fedha, lakini kubwa zaidi umaskini wa vitendea kazi. Mimi nakubaliana nao na sijawahi kusema lugha nyingine tofauti na hiyo toka nimeingia Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tunafika mahala Waheshimiwa Wabunge tunaona jambo hili halipo, basi ni rahisi kuungana kwa pamoja tukahakikisha kwamba, tunazaa mbinu ili tuhakikishe Zimamoto inaimarika na kweli inakuwa jeshi la kulitegemea wakati dharura zinapotokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Jeshi la Zimamoto pia kulikuwa na hoja hasa Mheshimiwa Ahmed Salim alisema kwamba, kuna tabia ya kuchelewa, kwamba Zimamoto wanachelewa. Zimamoto wanaweza kuchelewa kwa mambo mawili makubwa ambayo yanaweza yakawachelewesha.

La kwanza, vitendea kazi ni kidogo ambavyo tunakubaliana, kwa hiyo, hata kama kunatokea matukio moja au mawili ambayo yako sambamba, ikitoka gari haiwezi kutoka nyingine mpaka pengeni ile irudi halafu ndiyo iweze kutoka. Lngine ni kwamba, tunajengaje humo ambamo tunategemea Zimamoto waje kutuzimia moto. *(Makofi)*

Inasikitisha hata kama itatokea ajali na taarifa zitakuja mapema, vifaa vipo, magari yapo, watendaji wapo, kuweza kufika ukazime moto Mbagala siyo

rahisi na maeneo mengine. Kwa hiyo, lazima tushirikiane kama kweli Jeshi la Zimamoto tunataka lifike kwa wakati, tutazame litapita wapi. Kama hatujajenga flyover makusudi ya Zimamoto, basi kwa kweli tuvunje baadhi ya nyumba tupanue miundombinu ili waweze kufika na kufanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na hoja nyingine kwamba, Jeshi la Zimamoto linahitaji kuimarishwa. Kama nilivyosema mwanzo, sisi kama Wizara tulivyoona Jeshi la Zimamoto lina matatizo makubwa ya kiutendaji, vifaa na vitendea kazi, tuliishawishi Serikali kwamba sasa tuipe Zimamoto *retention*. *Retention* tumeipata lakini mara nyingi kuna matatizo ya kupatikana fedha. Tunaomba hili tulisimamie kupitia kwenye kamati na watu wengine, Wabunge, ili tufike mahala hoja ya kuwa Zimamoto inahitaji kuimarishwa na ina uwezo wa kujimarisha yenyewe, tuikubali na tuifanyie kazi ili itusaidie.

Jambo lingine ni kwamba, Serikali tayari imechukua hatua, kama mwaka jana tumeajiri vijana 800, hawa wamegaiwa kwenye mikoa mbalimbali, lakini bado ni wachache mno. Hata kwa upande wa vitendea kazi, zimamoto inahitaji magari 280 na tuliyonayo labda ni 35 ambayo yanafanya kazi. Tuna safari ndefu kama kweli tunataka tujiokoe. Zimamoto ipo, lakini tuifanye basi ituokoe katika majanga ambayo yatatupata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fungu lingine ambalo nilitaka kulizungumzia ni Magereza. Magereza inafanya kazi nzuri, ina *potential* nzuri, lakini inakabiliwa na matatizo ya kibajeti kwa sasa. Magereza ina matatizo ya kuwa sasa hivi inalimbikiza madeni kila siku, kuanzia wazabuni wa aina tofauti, lakini hasa katika chakula cha wafungwa.

Fedha ambazo zinatolewa, shilingi 1500 haikidhi mahitaji ya chakula na ili wafungwa waishi ni lazima kupatikane mahala ambapo tunaweza tukapata fedha hata kwa kukopa. Kinachotokea ni kwamba, wajasiriamali wetu wa katikati hawa, tunawakopa na kila mwezi tunamkopa mwingine tunammaliza. Kwa hiyo, iko haja ya kutazama hasa Serikali tukaliweka sawa hili suala la fedha za chakula na kulipa malimbikizo ambayo yapo yakiwemo ya wafanyakazi, lakini na ya wazabuni, inaweza ikatusaidia tukawa na jeshi ambalo tunaweza tukaliita Jeshi la Serikali.

Suala la msongamano wa wafungwa na mahabusu; suala hili mara nyingi tunalizungumza, ni kweli kwamba kuna msongamano na bado hatujawa tayari, siyo tu upande wa Serikali kwa kusema tutatoa *Parole*, tutatoa *community services*, tutatoa vipi, lengo hasa la kuwapeleka watu kwenye magereza ni kutaka warekebishwe. Tukiwa tunashabikia tuondoe msongamano kwa kuwatoa tu hata kama hawajarekebishwa, nalo hilo pia ni tatizo.

Kwa hiyo, nafikiri tutazame na ni vizuri tu-*balance* vizuri kwamba, tuna haja ya kupunguza msongamano, lakini jambo kubwa la kufanya ni kupunguza uhalifu. Kila familia, kila chama cha siasa, kila kundi, tutazame tunaongeza nini kwenye magereza. Rahisi kusimama ukasema hatufanyi kitu kwenye kupunguza msongamano, lakini wewe jitazame unaongeza msongamano kiasi gani kwa maandamano ya kila siku yasiyokuwa na tija. (Makofi)

Suala la makazi ya askari limezungumzwa na watu wengi ambao wana huzuni, mpaka ndugu yangu Lema amelisema, ingawa ilikuwa ni kiminyio tu cha kutaka kuombea kura. (Makofi)

Wengine ni Mheshimiwa Esther Matiko, Mheshimiwa Mallac na wengine wamezungumza. Mheshimiwa Mallac amezungumza kuhusu Gereza la kule Mpanda, Kalila Nkulunkulu, matatizo yake na tumeyasikia, tutajitahidi kuhakikisha umeme, maji na ukarabati unafanywa katika Gereza lile ili wanaofika pale waweze kuishi maisha bora kuliko ambavyo wanaishi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba, kuna mipango mingi ya kuhakikisha makazi ya askari yanaboreshwa chini ya mpango wa maboresho na mipango mingine iliyokuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo pia amelizungumzia Mheshimiwa Chatanda, ni kuhusu kuhakikisha magereza inajitegemea kwa kilimo. Hili jambo tunalikubali na tunakiri kwamba kuna mwelekeo mzuri, tumeanza kufanya miundombinu ya umwagiliaji maji, lakini kilimo ni eneo ambalo tuna fursa kubwa na tukipewa nyenzo *we can show wonders*.

Mheshimiwa Arfi alizungumzia kuhusu Watanzania wapya ambao walipewa Utanzania kule Mishamo. Alikuwa anauliza je, wanayo haki ya kupiga kura? Ndiyo wale ni Watanzania kama tulivyo sisi, wanayo haki ya kupiga kura ya kumchagua, isipokuwa hawawezi wao kugombea Urais. Chini ya sheria zetu, mgombea Urais anatakiwa awe ni Mtanzania wa kuzaliwa, vinginevyo wana haki ya kumkataa na kumkubali mtu yeyote na wao wenyewe wanaweza kugombea hata Ubunge wa eneo lile wakamnyang'anya Mheshimiwa Arfi. (Kicheko/Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Buyogera alitupongeza kuhusu ujenzi wa *airstrip* kule Kasulu; ni kweli harakati zinaonekana zinarudi tena hasa za wakimbizi na kwa vyovyote tutataka njia ambayo itaweza kuwafikisha wahudumu pale haraka zaidi ili kuhakikisha wale wenzetu tunawapatia hifadhi iliyotukuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda, naomba nirudie kukushukuru kwa kunipa nafasi na kuwaomba Waheshimiwa Wabunge basi

tupitithe hii, tuiseme kwamba tusiipitithe kwa sababu ndogo. Tunaweza tukasema tunaweza tukafanya review na bado ikawa kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mtoa hoja, dakika 25.

Waheshimiwa Wabunge, Mawaziri wote wata-*wind up* pamoja. Baada ya Mheshimiwa Chikawe atakuja Mheshimiwa Dkt. Mwinyi na tutapitisha kwenye vifungu Wizara moja moja.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nihitimishe hoja ambayo niliwasilisha leo asubuhi ya Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwanza wewe, kwa kuendesha kikao hiki vizuri, lakini niwashukuru Waheshimiwa na wenzako; Spika, Naibu Spika na wengine wote waliokaa katika Kiti hicho, mmetuongoza vyema kwa kipindi hiki cha miaka hii na sisi tanawashukuru sana. Tumepata mafanikio, tumeweza kuyasema tuliyokusudia kuyasema kwa wananchi.

Napenda nichukue nafasi hii kuwashukuru Wabunge wote kwa ushirikiano wenu. Kila mwaka niliposimama hapa nikiwa Waziri wa Katiba na Sheria, nikiwa Waziri wa Utawala Bara na sasa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, mmenipa ushirikiano mkubwa sana na kila ninapoondoka huwa nawashukuru sana na nawaombea kwa Mungu. Nawashukuruni sana.

Naomba pia niwashukuru waliochangia katika hoja hii, leo nimepata michango 47; michango 29 ya maandishi na michango 18 ya watu waliozungumza ndani ya Bunge hili. Nataka niwashukuru wote, mmetoa michango mizuri sana na nitaizungumzia mmoja baada ya mwingine hapo mbele.

Nitoe pia shukrani nyingi sana kwa familia yangu, ambayo imenivumilia sana kwa kipindi hiki ambacho nimekuwa Bungeni na shughuli hizi za Bunge na hasa shughuli za Uwaziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, ni Wizara moja ngumu sana. Wizara ambayo ukipata nafasi ya kulala basi ukizidisha saa nne, tano, wewe una bahati. Kwa hiyo, nashukuru sana, wamenivumilia na mpaka sasa nafikiri wataendelea kuniombea ili huko mbele ya safari twende mnapopataka ninyi, labda pakubwa zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kuzungumzia Hotuba hii ya Kambi ya Upinzani. Safari hii kwa kweli nina neno moja tu, nimekuwa *disappointed*, kwa kawaida Kambi ya Upinzani huwa inanipa mawazo mengi ambayo baadaye

huwa nayatumia katika utekelezaji wa mambo yangu. Safari hii Kambi ya Upinzani Hotuba yake imejaa sana ndoto za ushindi, ndoto ambazo nina hakika hazitokuwa, maana ni ndoto. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme moja tu lililozungumzwa hapa kwamba, kunaweza kukawa na uchochezi wa kidini au kikabila. Niseme tu kwamba, jambo hili kama lipo na linafanywa na yeyote yule anayelifanya, nataka nimwambie halikubaliki, halikubaliki, halikubaliki. Hatutaruhusu uchochezi wa aina yoyote ambao utatuvurugia amani ya nchi yetu. (Makofi)

Mimi nilipopewa *instrument* hii ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, kazi niliyopewa ni kusimamia kuhakikisha kunakuwa na usalama ndani ya nchi hii. Kwa hiyo, kwangu mimi usalama kwanza, mambo mengine yoyote tutafuata nyuma baadaye. Ninataka nitoe onyo kwa hao wanaofanya uchochezi ama kupitia dini au kupitia makabila. Siyo sahihi, tutawachukulia hatua zinazopaswa kama tutawapata. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nizungumzie kwa ujumla hali ya usalama nchini. Tunayo makosa ambayo nchi yetu tumezowea kuwa nayo ya kawaida, wizi, watu kupigana kidogo, vibaka na kadhalika, hata mauaji, ni makosa ambayo tunaita kama *traditional*. Kwa miaka ya hivi karibuni yamezuka mengine mapya, usafirishaji haramu wa binadamu ama kwa ajili ya kazi, wanafanya *human trafficking for cheap labor* au *human trafficking* kwa ukahaba. Akina mama wanatolewa Nepal wandetwa huku Tanzania kwa shughuli hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa imezuka mpya kabisa katika hii *human trafficking; human trafficking of children for terrorism*. Hii ni hatari kwetu na ni jambo ambalo tumeliona na ni lazima tulichukulie hatua. Wanapofanya hii inayoitwa *radicalization* ya watoto wetu, watoto wadogo wanachukuliwa, wanafundishwa ugaidi. Siyo Tanzania tu, hii inatokea sehemu nyingi na tuseme ni *new crime* kwetu, haikuwepo, hatukuwa nayo. Kwa hiyo, na sisi kama Jeshi la Polisi na kama Serikali, tunajipanga kupambana na makosa haya ya jinai mapya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo mengine tena, haya ya *cybercrime*, makosa ya mtandao. Makosa haya ni hatari sana na ninashukuru juzi juzi tu hapa Bunge hili, kwa hekima zake lilipitisha Sheria ya *Cybercrime Law*, ni sheria nzuri sana. Kwa sababu kuna watu wanaolalamika wanasema mbaya, wanasema itawaziba midomo ya kusema. Sisi kwa kweli, utasema nini ambacho hatujakisikia! Hatuweki sheria hii kwa sababu ya maneno utakayosema, hapana, watu wanatumia hii mitandao, wanafanya benki zina-*collapse*, wanaiba kule, wanafanya benki *the whole financial system* ina-*collapse* kwa sababu ya wizi wa mitandao; hayo ndiyo sisi tunayaogopa.

System ya benki iki-collapse na uchumi wa nchi una-collapse unakwenda vibaya. Wanatumia mitandao katika makosa ya ugaidi, hayo ndiyo sisi tunayaogopa, lakini kusema mtatuzuia kusema, unataka kusema nini ambacho hatujakisikia! (Makofi)

Yanasema magazeti, yanasemwa kwenye radio, yanasemwa kwenye TV, hayo ya kusema sisi kwetu wala siyo *issue*, kwetu sisi ni usalama wa nchi yetu kwanza. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana makosa haya ya *cyber* sisi tutayachukua kwa nguvu sana na tutayafuatilia kwa karibu sana, kwa sababu yakiweza kufanikiwa, yanaweza yakayumbisha uchumi wa nchi yetu na nchi yetu kwa ujumla na usalama wa nchi yetu. Hapo sisi tuliopewa jukumu hili la kuangalia usalama wa nchi hii, tutakuwa tumeshindwa kufanya kazi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kosa lingine ambalo siyo la zamani sana lakini sasa limeanza kukua sana ni *road traffic accidents*. Hizi zimezidi mno kiasi kwamba, tunaona hii ni kama *phenomenon* mpya. Kweli tumekuwa tunapata matatizo barabarani, ajali zinatokea, lakini katika kipindi hiki cha hivi karibuni, ajali hizi zimekuwa nyingi mno na madhara yake yamekuwa mabaya sana, wananchi wengi sana wamekufa nawengi sana wameumia. Hata sijui kampuni za bima zina-survive vipi katika hali kama hii, kama hawa watu wote kweli wanalipiwa bima!

Kwa hiyo, nadhani haya ni mambo ambayo inabidi tuyawekee mikakati mpya hasa katika mwaka huu wa fedha unaokuja, tukae tuone ni jinsi gani tutafanya ili tuweze kupambana na makosa haya mapya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nimee kidogo mambo ambayo yamezungumzwa sana katika kikao hiki na jana asubuhi wakati Waziri Mkuu akijibu maswali na katika hotuba nyingine zilizopita ambayo pia yanatuhusu sisi kama Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

Moja, lilikuwa ni madai ya mahabusu wa kesi za ugaidi ambao wanadai kwamba hawapewi chakula na matibabu.

Sasa nataka niwathibitishie, madai haya hayana ukweli. Watu hawa kila wanapopata maradhi, wanatibiwa. Wapo ambao wameshawahi kulazwa Muhimbili; na wapo ambao mpaka sasa wana *clinic* zao Muhimbili. Kila ikifika siku ya *Clinic*, anapelekwa, anarudi.

Kwa hiyo, kusema kwamba hawatibiwi, siyo sahihi. Labda kama wangependa kwenda kutibiwa mahali pengine zaidi ya Muhimbili. Lakini

kutibiwa kwa kawaida kwa Mtanzania anapotibiwa, wanapata matibabu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu chakula, wanakula chakula ambacho mahabusu wengine wote wanakula. Kwa hawa, zaidi kuna kibali kimetolewa kwa *organizations* fulani za Kiislam kuwapelekea chakula; na wanapelekewa. Pia familia zao zimepewa kibali kuwapelekea chakula; na wanawapelekea.

Sasa kusema kwamba hawapati chakula, hii nchi haijafikia hatua hiyo. Hatua ya kusema mtu tutam-*starve* gerezani! Tutampa kile tulicho nacho, labda hiyo ndiyo tunaita ku-*starve*, lakini kwamba tunamnyima chakula, siyo sahihi.

Kwa hiyo, madai haya yaliyoletwa nafikiri siyo madai ya kweli. Lakini kama inabidi watu tufanye uchunguzi, tutaunda Tume itawa-*involve*, nami mwenyewe nitaiunda na Kamati ya Bunge muwemo, mwende mkatazame, mkazungumze nao mwasikie wanawaambia nini kuhusu chakula, matibabu na kuhusu *general treatment* yao wakiwa pale gerezani.

MBUNGE FULANI: Lini?

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mara moja! *Time is with me...*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, zungumza na Kiti!

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili lililozungumzwa sana ni kuhusu matumizi ya nguvu katika kadhia ya Profesa Lipumba pale Temeke, kwamba Polisi walitumia nguvu zaidi kuliko walivyostahili kutumia. Polisi hawakupiga risasi hata moja. Walipiga mabomu ya machozi. Sasa katika hali kama hiyo, nguvu zaidi maana yake ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hali ambayo watu wako Temeke karibu na Hospitali kwenye Ofisi za CUF, msitembee. Wanakuja kuzuliwa Mtoni Mtongani! Unajua ile *distance* ni muda gani pale? Ni *more than two kilometers*; walikuwa wanafanya nini huko? Ukiwaambia wanaandamana, wanasema hawakuandamana. Huko Mtongani walifikaje kutoka kule Ofisi ya CUF? Hayo ndiyo maandamano yasiyokuwa na kibali na walipopewa ilani, wakakataa Polisi wakachukua hatua ambazo walichukua. Sasa kama Tume ya Haki za Binadamu imesema kwamba zimetumika nguvu, siyo sahihi. Tume imetoa maoni yake, sisi tumeyasikia maoni yenu.

WABUNGE FULANI: Wamesema nini?

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Ni nini? Tume imetoa maoni yake; ni maoni ya Tume!

MWENYEKITI: Mheshimiwa! Waheshimiwa! Mheshimiwa Khatib!

Waheshimiwa Wabunge, mmejenga hoja, mmepewa muda wenu.

MBUNGE FULANI: Taarifa!

MWENYEKITI: Subiri Mheshimiwa! Wakati Serikali inajibu, huwezi ukasimama. Subirini, uko muda; kila jambo lina hatua yake. Litakuja swali la mshahara wa Waziri mtahoji. Mmehoji asubuhi, sasa anajibu. Wakati mnahoji, yeye alikaa, wala hakuwajibu. (*Makofi/Kicheko*)

No! no! no! no! Lazima tuwe na *fair playing field* humu ndani! Ninyi mmetoa hoja zenu, yeye anajibu. Akishajibu yeye, kuna muda na ninyi mtapata nafasi ya kuuliza, ndiyo mchezo wa ndani ulivyo huu, hamna lingine. Endelea Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Haki za Binadamu imetoa taarifa yake ambayo sisi tunasema ni maoni ya Tume na sisi tumeyapata. Tutayasoma, tutazingatia yale ambayo tunaona yanafaa kuzingatiwa. Tutafanya hivyo.

Jambo lingine lililozungumzwa sana na ukosefu wa nyumba za Askari Magereza, Askari Polisi, Askari wa *Immigration*, wote hawa wanayo matatizo makubwa sana ya nyumba. Kwa kulijua hili, Serikali inafanya mkakati wa kujenga nyumba takriban 4,100 kwa ajili ya Jeshi la Polisi, nyumba ambazo zitagharibu karibu Dola milioni 500. Tunaendelea na mazungumzo, tukikamilisha, basi nyumba hizi zitajengwa haraka na zitasambazwa sehemu zote za Tanzania.

Kwa sasa tuseme tu, pale *Oysterbay* zinajengwa nyumba kwa ajili ya Polisi na Kituo cha Polisi na kule Kunduchi zinajengwa nyumba pia kwa ajili ya Polisi katika kujaribu kuondoa tatizo hili la nyumba. Jeshi la *Immigration* nalo wamekuwa wanajenga nyumba sehemu mbalimbali; nyumba za kuishi maafisa na Ofisi zao kwa ajili ya matumizi ya Idara hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili la nyumba limezungumzwa na sisi tunalikubali, ni tatizo kubwa sana na tungependa kama tungekuwa na uwezo mkubwa tungelimaliza ili Polisi wote kwanza wakae *barracks* ili pale ikipigwa filimbi wote watoke, lakini sasa hivi Polisi wanakaa sehemu mbalimbali. Hili hatulipendi kama Jeshi la Polisi, lakini hatuna jinsi kwa sababu hali ndiyo iko hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapambana nalo kuhakikisha kwamba baada ya muda Polisi wote wanarudi *barracks* ili waweze kupatikana mara wanapotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine kubwa limezungumzwa ni la posho za Askari, hasa posho hii inaitwa *rational allowance*. Kama ninyi, nami vile vile napenda posho hii iwe kubwa.

Kamati ya Ulinzi na Usalama inafahamu, tumedai sana hili na tunaendelea kudai kila siku, lakini uwezo wa Serikali yetu pia tunaufahamu. Ila tunachokiomba kwa sasa, kuwe na *equalization* tu. Hata kama ni Sh. 1,000/= basi iwe ni kwa wote. Kwa sababu ile kutokuweka sawa kwa wote ndiko kunakoleta matatizo na malalamiko makubwa hasa kwa Jeshi la Polisi dhidi ya majeshi mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo ndiyo mengi yaliyozungumzwa kwa ujumla mengi na yamezungumzwa na wengi. Ila nachukua muda huu kwanza kukubaliana na Mheshimiwa Shibuda, ameomba faragha baina yake, mimi, Naibu Waziri na IGP, nasema sawa. Tupange, tukae hiyo faragha, tuzungumze. Kama katika mazungumzo hayo nia yetu ni kupambana na watu ambao wanafanya makosa dhidi ya *albino*, basi mimi niko tayari hata baada ya bajeti hii leo hii tukae tuzungumze. Ningependa tuzungumze tutafute muafaka.

Mheshimiwa Amina Makilagi amefanya mchango mzuri sana leo, mchango wake kwa kweli uliwafanya watu wengine wasivumilie, wakajaribu kum-*shut down* kwa sababu ulikuwa ni mchango mzuri sana. Ni mtu ambaye ana uzoefu na Jeshi la Polisi, amezaliwa kwenye *barracks* za Polisi, amekulia humo, anawajua, anaelewa matatizo yao na kwa kweli alichokisema ni kitu anachokijua. Nami nampongeza kwa mchango wake huo.

Mama Mshana katika mchango wake wa maandishi amezungumzia pale Misenyi kwenye Kituo cha Polisi cha Kyaka, kuna tatizo pale, hawana choo. Sasa basi nitamwagiza IGP ahakikishe katika Kituo hicho cha Polisi na vingine vyote, wafanye utaratibu vyoo vijengwe. Kwa kweli huwezi ukawa na Kituo cha Polisi halafu usiwe na choo. (Makofi)

Mheshimiwa Matiko Esther ameomba OCS wa Gibaso kule Tarime aondolewe. Sasa upangaji wa Watumishi wa Serikali katika vituo vyao unategemea sana uwezo wao na kadhalika. Lakini ombi lako wamelisikia, wataliangalia kama anastahiki, amekaa sana labda na nini, basi atahamia sehemu nyingine.

Mheshimiwa Selasini, IGP atafanya ukarabati wa hicho Kituo cha Mkuu kama ulivyoomba, kwa sababu ni kitu kidogo tu; mabati yanavuja au ile *slab* inavuja, basi ni kubadilisha *slab* au kuweka mabati juu yake na kufanya hiyo sehemu watu waweze kufanya kazi kwa ufanisi zaidi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia natoa pongezi kwa wananchi Rombo kwa kujenga hivyo Vituo vinne vya Polisi kwa kujitolea. Nafikiri hili ni jambo zuri sana na la kuigwa. *Of course* wako Waheshimiwa Wabunge wengine ambao wamejenga Vituo kama hivyo katika sehemu mbalimbali na vimefunguliwa na tunawa-*encourage* Waheshimiwa Wabunge wengine kama bado mnaweza katika kipindi hiki kilichobaki mfanye hivyo, mjenge vituo kusaidiana na Jeshi la Polisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Lema alizungumza kuhusu Vitambulisho vya Taifa na mamlaka ya Vitambulisho. Alisema kwamba Serikali lazima itoe ukomo wa muda ambao kila raia wa Tanzania atapatiwa Kitambulisho cha Taifa na gharama zitakazotumika katika kutengeneza vitambulisho hivyo; na je, wananchi wangapi wamepatiwa Vitambulisho vya Taifa; na fedha kiasi gani zimetumika hadi hivi sasa katika mchakato huu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ile *spirit* ya kuwa wazi, napenda kumtaarifu tu Mheshimiwa Lema kwamba Vitambulisho vya Taifa vinatolewa kwa raia mwenye umri wa miaka 18 na kuendelea; na kwa kuwa kila siku kuna baadhi ya wananchi wanatimiza umri huo, zoezi hili halina ukomo, litandelea, ndiyo maana tunakuwa na Ofisi; tunajenga Ofisi katika kila Wilaya kwa sababu kila siku kuna mtu atafikisha miaka 18 na ata-*qualify* kupata kitambulisho cha Taifa. Kila siku atapatikana mtu anayehitaji.

Kwa hiyo, tunakusudia kufungua Ofisi katika kila Wilaya katika mwaka wa fedha huu wa 2015/2016 na tutafanya utambuzi na usajili wa wananchi katika Wilaya zote hapa nchini. Ingawa zoezi hili halina ukomo, tunatarajiwa kukamilisha usajili wa Umma (*mass registration*) katika mikoa yote ya Tanzania kwa raia wenye umri wa miaka 18 na kuendelea katika mwaka wa fedha 2016/2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia mwezi wa Machi, 2015 wananchi 2,567,980 wamepatiwa Vitambulisho vya Taifa; na kati ya vitambulisho hivyo 2,056,560 vilitolewa katika Mkoa wa Dar es Salaam na 511,420 vilitolewa Zanzibar. Aidha, uzalishaji na ugawaji wa Vitambulisho vya Taifa unaendelea sasa katika Mkoa wa Pwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu kuanza kwa usajili, kiasi cha Shilingi bilioni 56,884 zimetumika katika zoezi. Gharama za mradi mpaka utakapokamilika, ni Shilingi bilioni 487. Gharama hizi zinahusisha ununuzi wa vifaa vya usajili, magari, ujenzi wa Ofisi katika kila Wilaya, malipo ya Mkandarasi na Mshauri Mwelekezi na gharama zote za uendeshaji wa mradi. Nafikiri majibu hayo ni *perfect* kwako, umepata *data*, umepata mpaka lini, zoezi hili linatakiwa kukamilika.

Mheshimiwa Yussuf Haji Khamis, Mbunge wa Jimbo la Nungwi, aliuliza kwamba licha ya vitambulisho kuanza kutolewa Zanzibar na Mkoa wa Dar es Salaam, wananchi wengi wanasumbuliwa kupata vitambulisho na wengi bado hawajapata. Katika kutoa Vitambulisho vya Taifa, Mamlaka imekuwa ikizingatia sheria, kanuni na taratibu zilizowekwa, hivyo hakuna usumbufu wowote ambao wamekuwa wakipata wananchi wakati wa utoaji wa vitambulisho hivyo. Aidha, hadi hivi sasa kwa upande wa Zanzibar wananchi waliopatiwa vitambulisho ni 511,420 sawa na asilimia 82 kati ya walioandikishwa 623,356. Kwa upande wa Mkoa wa Dar es Salaam, wananchi walipatiwa Vitambulisho vya Taifa, ni wale niliowataja 2,056,560 sawa na asilimia 84 kati ya wananchi 2,441,000 walioandikishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme kwamba hoja zote zilizotolewa tutazipatia majibu na tutaziweka kwenye kitabu ambacho tutawagawia Waheshimiwa Wabunge kabla Bunge hili halijaisha ili waweze kwenda navyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja.

MHE. SAMUEL J. SITTA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki

(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuhitimisha hoja yangu.

MWENYEKITI: Dakika ni 40.

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia kwa kuzungumza na kwa maandishi kwa michango yao mizuri ya kujenga. Waliochangia kwa maandishi idadi yao ni 12 na waliochangia kwa kuzungumza idadi yao ni tisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Wanajeshi wote, naomba nipokee pongezi zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge wote kwa kazi nzuri inayofanywa na Wanajeshi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa Wapigakura wa Jimbo langu la Uchaguzi la Kwahani kwa kuendelea kuniamini kuliongoza Jimbo letu kwa miaka kumi sasa. Napenda niwahakikishie kwamba nitaendelea kushirikiana nao katika kuliletea maendeleo Jimbo letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nichukue fursa hii vile vile niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa ushirikiano wao kwa kipindi chote nikiwa

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na vile vile nilipokuwa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii. Naomba niwaombe wabunge wote kila la kheri katika uchaguzi ulioko mbele yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, katika shukrani lakini siyo kwa umuhimu, naomba nimshukuru mke wangu na watoto wangu kwa kunivumilia; na vile vile kwa kunipa moyo wakati wote ninapokuwa natekeleza majukumu yangu ya Kitaifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya shukrani hizo, naomba sasa nijibu hoja za Waheshimiwa Wabunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze na hoja za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ulinzi na Usalama. Kwanza kuhusu masuala ya madeni ya mikataba; kama nilivyoieleza katika hotuba yangu chini ya kiambatisho namba moja, hoja namba mbili; madeni ya kimkataba yenye jumla ya Sh. 253,097,338,970/= yameshahakikiwa na Mkaguzi Mkuu wa Ndani. Takwimu za madeni hayo tayari zimewasilishwa Hazina kwa hatua stahiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu migawo ya fedha za Maendeleo, kama nilivyoieleza katika hotuba yangu Ibara ya 27 ukurasa wa 18, kwamba mapokezi ya fedha za maendeleo yamekuwa hayaridhishi, yaani ni asilimia 29.3 tu ambazo zimepatikana. Aidha, tumezungumza na wenzetu wa Hazina wazingatie mgao na kutoa kipaumbele kwa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kadiri bajeti zitakavyoidhinishwa. Tunaamini kuwa Hazina watatoa fedha zaidi ya hizi ambazo tumeshapata mpaka sasa kabla ya mwisho wa mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu pongezi kwa wapiganaji, tumezipokea na tunaishukuru Kamati kwa kufanya ziara huko DRC kwa kuwa imetia hamasa kwa wapiganaji wetu. JWTZ litafikisha pongezi hizo kwa vijana kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha wa 2014/2015 Wizara ilipata fedha Shilingi bilioni 11 kwa ajili ya kugharamia mafunzo ya vijana 10,000 kwa mujibu wa sheria. Katika mwaka wa fedha 2015/2016, bajeti iliyotengwa na Sh. 25,777,234,000/=, inayotosheleza vijana 20,000 kati ya vijana 34,100 wanaomaliza Kidato cha Sita mwezi Mei, 2015. Ushauri wa Kamati umepokelewa. Wizara itafanya mazungumzo na Hazina ili bajeti hii waangalie uwezekano wa kuiongeza ili vijana wote wanaomaliza Kidato cha Sita waweze kuchukuliwa na kupatiwa mafunzo kwa mujibu wa sheria kwa mkupuo mmoja ili kuwawezesha kuwahi mihula ya masomo ya juu inayoanza mwezi wa Septemba.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *Suma JKT Guard* kulinda maeneo ya Serikali, tumepokea maoni ya Kamati. Hata hivyo, *Suma JKT Guard* kwa sasa inatoa huduma ya ulinzi kwa taasisi za Serikali na taasisi binafsi kama ilivyoelezwa kwenye hotuba yangu ukurasa wa 36 Ibara ya 54 kuwa maeneo haya ni vituo vya kuzalisha umeme Kihansi na Mtera Mkoani Morogoro, Chuo Kikuu cha Dodoma, Wizara ya Fedha, Benki za CRDB na UBA, Mgodhi wa *Stamigold* Chuo cha Madini Nzega na Chunya, TEMESA Kivukoni na Busisi Kigongo Mwanza na TPDC. Mkazo wetu ni ulinzi madhubuti kuliko wingi wa malindo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa niingie katika kujibu hoja za Kambi za Upinzani kama ifuatavyo:-

Kwanza hatua iliyofikiwa kuhusu mchakato wa kuboresha sera na Sheria ya Ulinzi wa Taifa na Sheria ya JKT, Na. 16 ya Mwaka 1964. Kabla ya kufanya marekebisho ya sheria, tunakamilisha rasimu ya Sera ya Ulinzi inayojumuisha maoni na ushauri kutoka kwa wadau mbalimbali. Hata hivyo, kwa kuwa suala hili ni la Muungano, maoni ya upande wa pili wa Muungano yaani Serikali ya Mapinduzi Zanzibar bado yanasubiriwa. Mpaka sasa hatujaona upungufu wa kukwamisha utendaji wetu. Aidha, siyo kila upungufu unahitaji marekebisho ya sheria. Baadhi ya upungufu unaweza kubadilishwa kwa kanuni au maelekezo maalumu.

Pili, fursa za ajira kwa vijana wanaohitimu mafunzo ya Jeshi ya Kujenga Taifa; kama nilivyoeleza katika hotuba yangu ukurasa wa 28 hadi 29 ibara ya 41 na pia kiambatisho namba moja, hoja ya sita ukurasa wa 52, Wizara imekuwa ikitekeleza agizo la Rais kuhusu ajira katika vyombo vya ulinzi na usalama. Takwimu zinaonyesha kwamba kati ya vijana jumla 8,590, walijajiriwa mwaka 2014/2015 katika vyombo vya Ulinzi na Usalama kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, JWTZ 6,531, Polisi 906, Usalama wa Taifa 22, Magereza 1,107, Zimamoto vijana 100, TAKUKURU vijana 24, Taasisi na Makampuni mengine idadi yake ni 2,214.

Mheshimiwa Mwenyekiti, JKT linatekeleza utunzaji wa mazingira kwa kuotesha miche katika Makambi na kupanda miti kuzuka maeneo ya Makambi. Aidha, miche hiyo hugawiwa kwa wanakijiji wanaozunguka maeneo ya Kambi sambamba na kutoa elimu ya mazingira kwa wanavijiji wanaozunguka Makambi hayo. Kwa mfano, katika Siku ya Mazingira tarehe 1 Aprili, 2015, JKT katika Makambi mbalimbali walipanda jumla ya miche 246.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inashauriwa kwa Waheshimiwa Wabunge, waendeleo kuwahamisha wananchi katika maeneo yao ili waweze kutunza na kumiliki misitu kwa faida zao na vizazi vijavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa maghala ya kisasa katika maeneo ya Mahongole, Ugunja na Pemba yamefikia asilimia 90. Katika mwaka wa fedha 2015/2016 tumetenga Shilingi bilioni tano kwa ajili ya awamu ya pili ya ujenzi wa maghala utakaohusisha maeneo ya Shinyanga. Aidha, ukarabati wa maghala unaendelea katika vikosi vyetu kulingana na upatikanaji wa fedha kutoka Serikalini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu fedha zilizotengwa kwa ajili ya upanuzi na uboreshaji wa hospitali za Jeshi; fedha zilizotengwa ni Shilingi bilioni 4.9 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na siyo fedha za matumizi ya maendeleo. Katika bajeti ya mwaka wa fedha 2015/2016, fedha hizo Shilingi bilioni 4.9 ni kwa ajili ya kutoa huduma za tiba kwa Wanajeshi na wananchi wanaozunguka hospitali zetu katika vikosi mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ulipaji wa fidia kwa maeneo ya ardhi yaliyopimwa kwa ajili ya matumizi ya Jeshi; kwa fedha tulizopata katika bajeti ya mwaka wa fedha 2014/2015 tumetumia kulipia fidia katika maeneo ya Mahongole, Makambako na Kasanga, Rukwa.

Kama nilivyoieleza kwenye hotuba yangu ukurasa wa 40 na 41, Wizara haikuweza kulipa fidia kwa baadhi ya maeneo kama ilivyokusudiwa kwa mwaka wa fedha 2014/2015 kutokana na ufinyu wa bajeti. Maeneo haya ni pamoja na eneo la Ilemela, Mwanza. Kazi ya uthamini na kulipa fidia eneo la Mtaa wa Lukobe na Buduku yaliyopo Wilaya ya Ilemela itafanyika katika mwaka huu wa fedha 2015/2016. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ulipaji wa madeni ya Wazabuni na Wanajeshi; ni kweli Wizara ya Ulinzi na vyombo vyake ina madeni ya Wanajeshi na Wazabuni. Mpaka sasa Serikali imechukua hatua ya kuyahakiki madeni yote yanayoishia tarehe 30 Juni, 2013/2014. Madeni hayo yamekaguliwa na Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Serikali na takwimu zimewasilishwa Hazina kwa hatua stahiki. Jumla ya madeni yote yaliyohakikiwa kwa vyombo vyote vya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, yanafikia Sh. 100,330,047,448/= kwa mchanganuo ufuatao:-

Fungu 38 – Ngome, Sh. 50,618,301,656/=; Fungu 39 – JKT, Sh. 49,609,619,145/= na Fungu 57 – Wizara, Sh. 101,826,646,000/=.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pensheni kwa kada ya Majenerari Wastaafu, kuanzia cheo cha Meja Jenerari na kuendelea, limepatiwa ufumbuzi kwa kuboresha malipo hayo na wahusika wamefahamishwa hivyo. Kuhusu pensheni ya vyeo vingine, suala hili linashughulikiwa na wadau kwa kuwa ni mtambuka hususan Ulinzi, Hazina na Utumishi.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, familia za Wanajeshi waliofariki katika operesheni mbalimbali hulipwa mafao yafuatayo:-

Kwanza, familia ya Mwanajeshi aliyefariki, husafirishwa kwenda kwao; pili, fedha za rambirambi ambazo hutolewa na Mkuu wa Majeshi, ni posho inayolinga na misahahara ya miezi sita ya Mwanajeshi aliyefariki kulingana na cheo chake na haikatwi kodi; tatu, malipo ya pensheni ambayo hugawanyika katika makundi mawili; *Death Gratuity* na pili, *Survivors Benefit* kwa wenye utumishi wa miaka 20 na kuendelea, inayolipwa kwa miaka mitatu na baada ya hapo, inasitishwa. *Death pension* inalipwa kwa mjane kwa maisha yake yote, isipokuwa kama ataolewa tena. Kwa watoto, inalipwa hadi wanapofikisha umri wa miaka 21. Kwa wanajeshi waliofariki wakiwa katika operesheni za Umoja wa Mataifa, husafirishwa kutoka eneo la operesheni hadi nyumbani na kulipwa fidia na Umoja wa Mataifa kwa kiasi cha Dola za Kimarekani 70,000 kwa kila mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni kutotoa maelezo ya utekelezaji wa bajeti wa mwaka wa fedha 2014/2015. Maelezo ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka wa fedha 2014/2015 yametolewa kwenye hotuba yangu. Inashauriwa Mheshimiwa Mbunge apitie hotuba hiyo kuanzia ukurasa wa 16 ibara ya 24 hadi ya 62.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uanzishaji wa Idara ya Mafunzo ya Ufundi ndani ya JKT kwa ajili ya kuratibu mafunzo ya VETA. JKT linalo Kurugenzi ya Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) kwa ajili ya kuratibu mafunzo ya VETA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi sasa JKT kupitia Kurugenzi hiyo, inavyo vituo vya kutoa mafunzo ya Ufundi Stadi vitatu katika vikosi vya Mgulani, Makutopola na Male ambavyo vinaratibiwa na VETA na wahitimu kupewa vyeti vya VETA. Mahusiano kati ya VETA na JKT ni ya karibu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kujibu eneo hilo la hoja za Kambi ya Upinzani, sasa naomba niingie katika hoja za Waheshimiwa Wabunge ambao wamezitoa kwa kuzungumza na kwa maandishi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu tatizo la mpaka katika Kambi ya Mtabila na wanakijiji wa Kijiji cha Mgombe; hoja hii ni ya Mheshimiwa Agripina Zaituni Buyogera. Naomba nimjibu kwamba ushauri wake umepokelewa, zoezi la kuweka uzio wa mpaka kati ya Kambi ya Mtabila na Wanakijiji utatekelezwa kadiri ya upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu fidia ya Rusoti na Msati, wananchi hawajalipwa fidia na wameshasimamisha kufanya shughuli zao. Je, ni lini wananchi hao watalipwa fidia hii? Hii ni hoja ya Mheshimiwa Esther Matiko; na jibu lake ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilishaeleza kwenye hotuba yangu ukurasa wa 44, fidia ya eneo la Rusoti ilitipwa mwaka huu wa fedha kwa sababu mwaka uliopita pamoja na kutengwa fedha hizo hazikutolewa kama tulivyokusudia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kuhusu madeni ya Wazabuni kwamba yapewe kipaumbele katika malipo. Kama nilivyoieleza kwenye hotuba chini ya kiambatisho namba moja, hoja namba mbili, Mkaguzi Mkuu wa Ndani, alishakamilisha kazi za uhakiki wa madeni, ambapo madeni ya Wazabuni ni Sh. 100,330,047,448/= na ya kimkataba ni Sh. 253,097,338,970/=. Ni imani yetu kuwa Hazina watalipa madeni hayo kadiri ya upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu fidia kwa wananchi wa Korotambe; Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mara ndiyo inayohusika na ulipaji fidia, Jeshi la Kujenga Taifa liliombwa kukaa hapo kwa lengo la kuleta amani kati ya migogoro ya koo zilizokuwa katika eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Jeshi kutumika katika kutoa msaada kwa mamlaka za kiraia, hoja hii ilitolewa na Mheshimiwa Idd Azzan. Kwa mujibu wa Kanuni za Majeshi ya Ulinzi, Jeshi kutumika katika shughuli za usaidizi za mamlaka za kiraia kwa kuzingatia uratatibu maalum. Nafurahi kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba hata hivi sasa Jeshi liko kwenye maeneo mbalimbali likisaidiana na mamlaka za kiraia. Kwa mfano, Tegeta kwa sababu ya mafuriko, Mtoni Kijichi kutengeneza daraja na Kigoma na kwenye eneo ambalo sasa hivi kuna wakimbizi. Aidha, Jeshi pia huweza kutoa msaada kwa vyombo vya Ulinzi na Usalama endapo litaombwa kufanya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, usafirishaji wa wanajeshi kwenda Zanzibar kwa madhumuni ya kisiasa, hii ni hoja iliyotolewa na Mheshimiwa Khatib Said Haji. Jibu ni kwamba kwa kuzingatia Sheria ya Vyama vya Siasa na tangu kuanza kwa Mfumo wa Vyama Vingi vya Siasa mwaka 1992, JWTZ halijihusishi na mambo ya kisiasa. Aidha, JWTZ halijasomba vijana kutoka Tanga na Dar es Salaam, kwenda sehemu yoyote ya nchi yetu likiwemo Jimbo la Kitope kwa ajili ya kuandikisha wapigakura.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge atambue kwamba JWTZ lina chuo chake cha mafunzo eneo la Chukwani Zanzibar ambacho huchukua Wanajeshi kutoka Makambi yote kwa ajili ya mafunzo ya kijeshi. Hivyo, isiwachukulie kwamba ni mamluki. Vile vile napenda nimwambie Mheshimiwa Mbunge, kama anao ushahidi wa kutosha, basi atufikishie ili tuweze kuuona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuongeza idadi ya vijana wanaoajiriwa katika Jeshi kutoka Pemba, hii ni hoja ya Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar. Vijana

wanaochaguliwa kujiunga na JKT hutoka katika Mikoa yote ya uwiano sawa. Vijana hao baada ya kuhitimu mafunzo ya JKT huajiriwa katika taasisi mbalimbali ikiwemo JWTZ, kulingana na sifa zinazohitajika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu stahili za Wanajeshi kwamba ziongezwe kulingana na mazingira ya kazi, hoja hii ilitolewa na Mheshimiwa Moses Machali. Serikali imekuwa ikijitahidi kuboresha maslahi ya Wanajeshi wake mwaka hadi mwaka kadiri bajeti inavyoruhusu. Aidha, ushauri huo umepokelewa na utafanyiwa kazi kwa kushirikiana na Hazina ili kuona uwezekano wa kuongeza viwango hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kuwatenganisha Wanajeshi na familia zao, hoja hii ilitolewa na Mheshimiwa Said Arfi. Jibu ni kwamba siyo lengo la Jeshi kutenganisha Wanajeshi na familia zao, ila kuna mazingira tofauti yanayoweza kusababisha hilo. Kwa mfano, haya yafuatayo:-

Kwanza, operesheni mbalimbali za kijeshi zikiwemo za kusaidia mamlaka za kiraia; pili, mafunzo ndani na nje ya nchi ya wanafunzi na mkufunzi; tatu, majukumu ya ulinzi wa amani nje ya nchi; na nne, majukumu ya ulinzi ya mipaka ya nchi yetu (*detachment*). Majukumu hayo hutekelezwa kulingana na hitajio la muda wa kukamilisha jukumu lenyewe. Sehemu hizo hazihitaji kuambatana na familia zao. Wanapokamilisha majukumu, hurejea na kuungana na familia zao.

Aidha, upo utaratibu wa kiseru na kisheria wa kuendesha mafunzo ya kijeshi kwa kuwatumia Wanajeshi wenyewe kwenda maeneo ya mafunzo na wakishakamilisha majukumu hayo hurejea kwenye vikosi vyao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu fidia katika maeneo ya Mitaa ya Lukobe na Nyanguku, Wilayani Ilemela, hii ni hoja ya Mheshimiwa Mkiwa Kimwanga. Kazi ya upimaji na kuweka mpaka ilishakamilika. Aidha, timu ya wataalam wetu walikwenda Mitaa ya Lukobe na Nyanguku Wilaya ya Ilemela kufanya ukaguzi kama tulivyowaahidi kwa kushirikiana na Halmashauri husika. Inawezekana wakati timu hiyo iko huko, Mheshimiwa Mbunge hakuwa na taarifa. Hivyo hatua inayofuata ni ya kufanya uthamini chini ya Halmashauri na Wizara ya Ardhi ndipo tuweze kulipa fidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu madai ya fidia, wananchi wa eneo la JWTZ, Ramsoti Tarime; hii ni hoja ya Mheshimiwa Nyambari Nyangwine pamoja na Mheshimiwa Esther Matiko. Kama nilivyosema kwenye hotuba yangu, ulipaji fidia wa eneo la Ramsoti, utafanyika mwaka wa fedha 2015/2016, zoezi la kupima na kulipia fidia litaendelea maeneo mengine kama Ilemela, Lukobe na Kigongo Ferry, Mwanza; Kimbiji, Temeke; Rasinondwa, Kigoma; Tanganyika Parkers, Arusha; na Kaboya, Muleba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Makambi ya JKT kwamba yatumike kuzalisha mazao ya chakula kwa wingi na hata biashara ili kuondoa tatizo la njaa hapa nchini, ni hoja ya Mheshimiwa Nyambari Nyangwine. Ni kweli kwamba JKT lina mashamba makubwa yanayofaa kwa shughuli za kilimo na mifugo. Tatizo kubwa ni upatikanaji wa mtaji wa kuendeleza mashamba hayo. Hivyo, JKT inaendeleza mashamba hayo kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha kwa mwaka wa fedha 2014/2015, ekari 5,800 za mazao ya chakula na biashara zimelimwa. JKT itaendelea kuongeza ukubwa wa maeneo ya kilimo kadiri hali ya fedha itakavyoruhusu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kuanzishwa Kambi ya JKT Wilaya ya Manyoni, Kijiji cha Sanjaranga, hii ni hoja ya Mheshimiwa Paul Lwanji. JKT haijapewa eneo rasmi la kuweza kuanzisha Kambi kwa sasa. Kimeanzishwa Kiteule cha Mokiwa katika Wilaya ya Manyoni. Tukipatiwa eneo, Jeshi la Kujenga Taifa litakuwa tayari kuanzisha Kambi hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu wa kurejeshwa kwa Kambi ya JKT Mpwapwa, kwamba ni lini Kambi hiyo itarejeshwa? Ni hoja ya Mheshimiwa Gregory Teu. JKT ilipata ushirikiano mkubwa katika Uongozi wa Wilaya ya Mkoa wa Dodoma kurudisha eneo hilo JKT. Kutokana kuwepo Kituo cha Mifugo, bado ya Wilaya ya Ulinzi na Kujenga Taifa pamoja na Wizara ya Mifugo zinakamilisha mazungumzo ili JKT liweze kutumia eneo hili kufundisha stadi za kazi hususan kilimo na mifugo. Hata hivyo, JKT lina mpango wa kujenga Chuo cha VETA cha kisasa eneo la Kongwa. Ujenzi huo umechelewa kutokana na uhaba wa fedha. Juhudi za kupata wabia pia zitazingatiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu hatimiliki kwa maeneo ya Jeshi, hoja iliyotolewa na Mheshimiwa Rita Kabati; kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi iliyopo, hakuna fursa ya maeneo ya Jeshi kupewa hatimiliki. Hata hivyo, mazungumzo yanaendelea kati ya mamlaka husika ili hatimaye maeneo ya Jeshi yapewe hati miliki baada ya kufanya marekesho ya Sheria za Ardhi zilizopo.

Kuhusu mwenendo wa matumizi ya mishahara, kwamba, kwanini kuna zaidi ya asilimia mia kufika Machi kwa Fungu la Ngome? Hii ni hoja ya Mheshimiwa Diana Chilolo. Makadirio yaliyofanyika yalikuwa bila ongezeko la mishahara. Aidha, idadi ya Askari wapya walioajiriwa ni kubwa kuliko waliostaafu. Hazina wanalifahamu suala hili na hakutokuwa na upungufu wowote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hoja ya hitaji la matrekta katika Halmashauri ya Wilaya ya Kilindi, hoja iliyotolewa na Mheshimiwa Beatrice Shellukindo. Kama ilivyo kwenye hotuba yangu, SUMA JKT iliagiza matrekta katika awamu mbili. Awamu ya kwanza yaliletwa matrekta 1,846 na awamu ya

pili, matrekta 268. Matrekta yote yaliuzwa kwa utaratibu mbalimbali kwenye Halmashauri.

Hivi sasa SUMA JKT inafanya juhudi za kukusanya madeni ili kuwezesha kuagiza upya na yatakapofika, Waheshimiwa Wabunge watapewa taarifa rasmi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la Mafunzo ya Mgambo kufanyika kwa lazima, ni hoja ambayo pia ilitolewa na Mheshimiwa Beatrice Shellukindo. Jibu ni kwamba jukumu la kuwapata Wanamgambo ni la Wilaya na Mkoa. Kazi ya Jeshi ni kutoa Wakufunzi na vitendea kazi. Hivyo, kama kuna hali ya kushurutishwa kujiunga na Mafunzo ya Mgambo, Kamati za Ulinzi za Wilaya na Mkoa zifanyie kazi kero hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ujenzi wa daraja la Mwakigimbe Tanga, hoja ya Mheshimiwa Dunstan Kitandula; ombi la Mkoa wa Tanga kujengewa daraja limepokelewa. Jeshi lilishatuma timu ya kufanya tathmini ya ujenzi huo, matokeo yanaonyesha kazi hiyo inaweza kufanywa. Hivyo, tutawapelekea gharama zinazohitajika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na hoja ya Mheshimiwa Yusuf Salim, kwamba tuwe na Sera ya Ulinzi yenye kutilia mkazo vita vya kisasa ikiwemo Teknolojia ya Habari na Mawasiliano. Jambo hili tunakubaliana nalo, ni kweli kwamba vita sasa imebadilika sana na kwa maana hiyo katika eneo hili, ni lazima mkazo uwekwe na Jeshi letu liko tayari kufanya hivyo.

Pia alitaka *Special Forces* ijengwe vema na wapatiwe zana za kisasa. Jambo hilo linaendelea kufanyika, *Special Forces* zetu zinajengwa imara ili kuweza kutoa huduma kwa kadri zinavyohitajika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile alitaka kujua kama kuna Bima kwa Askari wanaokwenda kulinda amani. Utaratibu huu kwa sasa haupo, lakini kama nilivyosema katika maelezo yangu, ni kwamba lolote likimkuta Askari anayekwenda kwenye ulinzi wa amani, nimeishaeleza utaratibu wa kuwafidia kwa maana ya wale wanaoumia, wanaofariki dunia na kadhalika.

Aidha, alikuja na hoja kwamba Jeshi linachukua vijana kutoka Ofisi za CCM na kwenda kuwaandikisha ili wapige kura. Hili suala nilishalisemea na ninarudia kusema kwamba suala hili hatuna taarifa nalo na hatudhani kama hii ni sahihi. Kama ushahidi upo kama mnavyosema, tutakuwa tayari kuupokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Njwayo alitoa pongezi kwa kuanzisha Chuo cha Tiba Lugalo. Alitaka wataalam wa kutosha wasambazwe

kwenye Kambi zote. Tunakubaliana na Mheshimiwa Njwayo. Chuo hiki ni cha muda mrefu isipokuwa sasa kinajiandaa kuwa Chuo Kishiriki cha Tiba Muhimbili.

Mheshimiwa Juma Sururu Juma alitaka Hospitali ya Bubu iimarishwe ili itoe huduma bora zaidi. Sasa hivi tuko katika utaratibu wa kuziboresha hospitali zote za Jeshi la Wananchi wa Tanzania katika maeneo yote. Kazi kubwa imeishafanyika na kila tutakapopata uwezo, hospitali hizi zitaongezewa uwezo ili ziweze kutoa huduma siyo kwa Wanajeshi na familia zao tu, bali kwa wananchi kwa ujumla.

Aidha, alitaka uzio uwekwe kati ya nyumba za watu na Kambi ya Mwanyani. Hili ni jambo ambalo nina taarifa nalo na ninaweza kusema kwamba, kadri uwezo utakavyoruhusu tutakuwa tunatenganisha Makambi haya na nyumba za wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Shibuda, yeye alitoa pongezi tu kwa JKT. Kwa niaba yao, tunazipokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rajab Mbarouk, alihoji kwamba Serikali inachukua hatua gani kuhakikisha milipuko kama ya Mbagala na Gongo la Mboto haitokei tena? Jibu ni kwamba kama tulivyosema kwenye hotuba yetu, fedha za bajeti iliyopita zimetumika katika kuimarisha maghala ya milipuko. Mwaka huu tumeweka fedha nyingine kwa ajili ya kuendelea kuimarisha maghala hayo, lakini kazi hii inafanyika kwa ufanisi kama nilivyosema, asilimia 90. Kazi hii imekaribia kukamilika na kwa maana hiyo sasa maghala haya yana uimara unaotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, alitaka uangaliwe uwezekano wa kuziondoa Kambi za Jeshi ndani ya miji mikubwa kama Dar es Salaam. Katika hili nataka tu nimweleze Mheshimiwa Mbunge kwamba miji mikubwa nayo inahitaji ulinzi. Kwa hiyo, ukiondoa Kambi, maana yake watakosa ulinzi. Cha msingi hapa ni kwamba tuboreshe mazingira ya Kambi hizo, tuboreshe maghala ya milipuko na tuhakikishe kwamba usalama unapatikana katika maeneo hayo, lakini siyo kuziondoa Kambi hizo.

Pia ikumbukwe kwamba siyo Kambi zote zina milipuko, bali baadhi ya Kambi ni kwa ajili ya *logistics* tu, zina maghala ya vyakula na vitu kama hivyo. Kwa hiyo, ni muhimu ziwepo ili ziweze kutoa huduma kwa Wanajeshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani kwa kiwango kikubwa nitakuwa nimegusia maeneo yote ambayo Waheshimiwa Wabunge wametoa kwa maandishi na kwa kuzungumza. Pia nitakuwa tayari kutoa maelezo zaidi nitakapotakiwa kufanya hivyo wakati wa kupitisha vifungu.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

MWENYEKITI: Ahsante. Hoja imeungwa mkono. Katibu!

KAMATI YA MATUMIZI

MATUMIZI YA KAWAIDA

Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi

Fungu 14 – Jeshi la Zimamoto na Uokoaji

Kif. 3001 - Fire and Rescue ServicesSh. 20,737,320,000/=

Kif. 3002 - Fire & Rescue Serv. Training Inst...Sh. 1,736,276,000/=

Kif. 3003 - Fire Safety... ..Sh. 673,820,000/=

Kif. 3004 - OperationsSh. 1,585,055,000/=

Kif. 3005 - D' Salaam Regional OfficeSh. 456,915,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi pamoja na Marekebisho yake)

Kif. 3006 - Arusha Regional Office... ..Sh. 486,054,000/=

Kif. 3007 - Dodoma Regional OfficeSh. 323,324,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

Kif. 3008 - Mwanza Regional OfficeSh. 619,796,000/=

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi pamoja na Marekebisho yake)

Kif. 3009 - Mbeya Regional OfficeSh. 430,598,000/=

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

Kif. 3010 - Kinondoni Regional OfficeSh. 415,155,000/=

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi pamoja na Marekebisho yake)

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Kif. 3011 - Mara Regional OfficeSh. 264,521,000/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya
Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

Kif. 3012 - Kigoma Regional OfficeSh. 237,755,000/=

MWENYEKITI: Mheshimiwa Machali!

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. *Item 230400 - routine maintenance and repair of vehicles and transportation equipment.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumwuliza Waziri wa Mambo ya Ndani, tunaona wanatenga fedha kwa ajili ya ku-repair magari, lakini baadhi ya maeneo kwa Mkoa wa Kigoma hatuna huduma za Zimamoto na wananchi wamekuwa wakichangishwa fedha wakati mwingine wakitegemea kupata huduma hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kupata kauli ya Serikali, ni lini Wilaya kama Kasulu, Kibondo pamoja na maeneo mengine nao wanaweza kuyaona magari katika maeneo hayo? Siyo wana-repair tu halafu yamekaa maeneo fulani fulani, majanga ya moto yanatokea watu wanapata hasara. Naomba kauli ya Serikali kuhusiana na suala hili.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri!

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tulivyosema kwenye majumuisho, ni kwamba Jeshi la Zimamoto lina matatizo ya magari na mengi kati ya yaliyopo yanahitaji kutengenezwa. Tukishatengeneza tutatazama wapi penye shida kubwa na risk ili tupeleke.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya
Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 3013 - Pwani Regional OfficeSh. 403,980,000/=

Kif. 3014 - Manyara Regional Office... ..Sh. 254,575,000/=

Kif. 3015 - Geita Regional OfficeSh. 220,442,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya
Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 3016 - Temeke Regional OfficeSh. 493,937,000/=

Nakala ya Mtandao (Online Document)

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi pamoja na Marekebisho yake)

Kif. 3017 - Singida Regional Office Sh. 235,749,000/=

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

Kif. 3018 - Tabora Regional Office Sh. 331,865,000/=

MWENYEKITI: Mheshimiwa Rage!

MHE. ISMAIL A. RAGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *Item 220300 fuel, oil and lubricant*, mwaka jana Mkoa wa Tabora walipata Sh. 27,750,000/=, mwaka huu zimepungua, nami nimekuwa shahidi katika Mkoa wa Tabora, nafikiri ndiyo tunaongoza kwa mauaji katika nchi hii. Kwa hiyo, Askari wanapata taabu sana kwenda kufanya kazi zao vizuri.

Je, Waziri anaweza akarekebisha au akaeleza ni kwanini amepunguza fedha ya mafuta?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri!

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba bajeti yote imepungua kwa asilimia 19. Hata hivyo, pale ambapo kutakuwa na matatizo ya mafuta kwisha katika mkoa wowote ule, Makao Makuu itasaidia.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

Kif. 3019 - Iringa Regional Office Sh. 310,115,000/=

Kif. 3020 - Rukwa Regional Office Sh. 233,573,000/=

Kif. 3021 - Ruvuma Regional Office Sh. 276,066,000/=

Kif. 3022 - Kagera Regional Office Sh. 284,995,000/=

Kif. 3023 - Mtwara Regional Office Sh. 311,637,000/=

Kif. 3024 - Lindi Regional Office Sh. 260,835,000/=

Kif. 3025 - Njombe Regional Office Sh. 238,949,000/=

Kif. 3026 - Shinyanga Regional Office Sh. 329,915,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Kif. 3027 - Ilala Regional OfficeSh. 510,360,000/=

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi pamoja na Marekebisho yake)

Kif. 3028 - Kilimanjaro Regional OfficeSh. 414,531,000/=

Kif. 3029 - Morogoro Regional OfficeSh. 368,444,000/=

Kif. 3030 - Katavi Regional Office... ..Sh. 261,875,000/=

Kif. 3031 - Tanga Regional OfficeSh. 442,609,000/=

Kif. 3032 - Simiyu Regional OfficeSh. 231,257,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

Fungu 28 – Jeshi la Polisi

Kif. 1002 - Finance and AccountingSh. 1,938,675,000/=

MWENYEKITI: Mheshimiwa Rajab!

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Katika subvote hiyo 1002, item 210100 - basic salaries – pensionable posts, nataka maelezo kutoka kwa Mheshimiwa Waziri ni kwanini mishahara imepungua kwa kiwango kikubwa kutoka Shilingi milioni 847 hadi kufikia Shilingi milioni 572?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri!

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kilichotokea hapa ni baadhi ya Wafanyakazi kufariki na kustaafu. (Kicheko)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Matiko! Mheshimiwa Machali! Mshahara wa Waziri bado. (Kicheko)

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 2001 - Police Main ForceSh. 176,414,185,000/=

MWENYEKITI: Mheshimiwa Machali.

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Niko kwenye item 210100 - basic salaries – pensionable posts.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali hili litafanana na swali ambalo limeulizwa na Mheshimiwa Rajab. Labda tu niongezee maelezo, kama Mheshimiwa Waziri atatoa maelezo kwamba watu wamefariki na wengine wamestaafu, sasa pengine ni-pause swali kwa sababu na hapa pia fedha zimepungua kwa takribani Shilingi bilioni moja. Serikali ina maana haina mpango wa kuajiri wafanyakazi wengine ili kuziba hilo gap ambalo lipo sasa? Kama watu wamefariki, tunategemea kwamba, kuna watu wengine *professionals* ambao wanatakiwa. Ni nini kauli ya Serikali? Mheshimiwa Waziri atoa maelezo kuhusiana na lile swali la mwanzoni, nilitaka niulize hilo kwa sababu lilikuwa limeishaulizwa, hakuna namna.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu ya upungufu katika kifungu hiki wala siyo watu kufariki, hapana! Fedha zimepungua kwa sababu kifungu hiki kilitumika kulipa mishahara ya Askari wapya; na hivyo kwa sasa mishahara hiyo imehamishiwa kwenye Kamandi zao walikokwenda. Kwa hiyo, ndiyo maana kuna upungufu, hakufa mtu pale. (Kicheko)

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya
Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2002 - *Police Marine* Sh. 1,651,218,000/=

MWENYEKITI: Mheshimiwa Masoud.

MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Niko katika *Subvote 2002, item 220300 - fuel, oils and lubricants*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka wa fedha 2014/2015 kulikuwa na Sh. 335,500,000/= na mwaka huu kuna Sh. 279,418,000/=. Haya ni mafuta ya kuendeshea boti, mafuta kwa ajili ya vilainisho na mitambo. Hii ni *Police Marine* na inaonekana wazi kwamba Serikali haitilii mkazo hata kama bei ya mafuta itapungua kidogo, maana najua hamtashindwa cha kusema, kusema bei ya mafuta imepungua; la kusema mtakuwa nalo wenyewe. Lakini imebainika kwamba wakati mwingi kunapotokea ajali baharini na kwenye maziwa, unaambiwa boti hazina mafuta. Watu wamekuwa wakipoteza maisha siku hadi siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba maelezo ya Serikali, ni kwanini kuna upungufu huu wakati ajali za boti kwenye bahari na maziwa zinaendelea kuongezeka siku hadi siku? Naomba ufafanuzi.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu!

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, utaona katika sehemu hii siyo *marine* tu, hata Police Zanzibar, *Air wing*, TAZARA, FFU, *Traffic*, *Airport* na wengine zimepungua kwa sababu zitalipwa na Mkuu wa Jeshi la Polisi mwenyewe.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

Kif. 2003 - *Railway Police Division*... ..Sh. 1,410,552,000/=

MWENYEKITI: Mheshimiwa Machali!

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Nitajielekeza pale kwenye *item 210300 - personal allowances (non-discretionary)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaona kwamba katika mwaka wa fedha ambao utaishia tarehe 30 Juni, walitenga Sh. 35,500,000/= na *this year* kwa maana ya mwaka ujao wa fedha wa 2015/2016 wametenga Sh. 15, 500,000/=.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu nimeeleza kwamba ukiwasikiliza Askari wanaofanya kazi na Shirika la Reli, wanalalamikia kutolipwa stahili zao mbalimbali ikiwemo muda wa ziada na fedha nyingine ambazo walistahili walipwe. Nimeona kwenye kifungu hiki, ni posho ambazo ni za lazima.

Sasa naiuliza Serikali, mnapopunguza fedha wakati huko kuna malalamiko makubwa, Serikali inatuambia nini Wabunge pamoja na Wafanyakazi hawa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, eatalipwa namna gani stahili zao ambazo wamekuwa wakilalamika kwa muda mrefu ili kusudi waweze kufanya kazi kwa tija na pengine wasiweze ku-sabotage, maana yake wakati mwingine tunawashawishi sasa wanaweza kufikia hata ku-sabotage miundombinu ya Shirika la Reli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pesa zinapungua, lakini malalamiko huku ni makubwa. Nili- *declare interest* nikasema kwamba mimi ni Waziri Kivuli wa Uchukuzi, kwa hiyo, naelewa ninachokizungumza. Ni kitu gani ambacho kinaendelea huko? Naomba kauli ya Serikali, watu hawa watalipwaje wakati mnapunguza pesa hizi?

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Kama nilivyotangulia kusema mwanzo, ni kwamba watu hawa watalipwa na Mfuko wa Mkuu wa Jeshi mwenyewe.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

Kif. 2004 - Police Signals Branch Sh. 1,429,768,000/=

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

Kif. 2005 - Police Zanzibar... .. Sh. 7,734,830,000/=

MWENYEKITI: Mheshimiwa Masoud!

MHE. MASOUD ABDLAH SALIM: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Bado niko katika subvote 2005 kwenye item 220300 ile ile ya fuel and rubricants. Kwa upande wa Zanzibar mwaka 2014/2015; Sh. 244,100,000/= halikadhalika mwaka huu wa fedha 2015/2016 kuna Sh. 244,100,000/= vilevile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri anayosema kwamba fedha hizi zinahamishwa kwenda kwa Mkuu wa Polisi, lakini kiwango cha hapa bado kiko vilevile na inaelekea suala zima la mambo haya ya ununuzi wa mafuta, kwa majibu kama haya, bado hayakidhi haja. Kwasababu tatizo ambalo linaonekana la ajali kwa upande wa Zanzibar, kwenye bahari kuu na kwenye maziwa limekuwa likiongezeka. Sasa kwa kuweka takwimu hii bado kwetu haitufungi na fedha hii kwenda kwa Mkuu wa Polisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba maelezo ya kina, tuambieni; hayo majibu ya Mkuu wa Polisi bado hayatoshi. Naomba ufafanuzi.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Zanzibar hakuna kilichopungua, lakini Bajeti ya Jeshi la Polisi imepunga kwa asilimia 20 na hasa walipokata sana ni kwenye mafuta. Kwa hiyo, kubakia hivi hivi, tunashukuru.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

Kif. 2006 - Police Airwing Sh. 2,460,124,000/=

Kif. 2007 - Police Tazara Sh. 1,635,425,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

Kif. 2008 - *Field Force Unit*... .. Sh.1,108,023,600/=

MWENYEKITI: Mheshimiwa Machali!

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nina swali dogo kwa Serikali. Mwaka wa fedha uliopita naona kwenye *item 210100 - basic salaries - pensionable posts*, walikuwa wana takribani Sh. 355,596,800/=. Mwaka huu pia naona hapa kuna upungufu. Swali langu ni moja. Je, Serikali hamjawaongezea fedha Askari hawa wa Kitengo cha *Field Force*? Au kuna nini kimetokea ambacho kimepelekea mpaka tunaona kiwango cha mishahara kama vile kimepungua?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, wafanyakazi kwenye *Force* kama *Field Force* siyo *stationary*, wanabadilika, wanaongozwa wapi; kwa hiyo, mishahara katika eneo hili hauwezi ukalinganishwa kwamba umepungua au umeongezeka.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 2009 - *Traffic Police*... .. Sh. 878,532,000/=

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

Kif. 2010 - *Police Airport* Sh. 1,835,605,000/=

MWENYEKITI: Mheshimiwa Rajab!

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Katika *subvote* hiyo ya 2010 niko katika *item 2010100 - Basic salary*. Katika swali langu la kwanza kule nyuma, niliambiwa watu walifariki na wengine watapata fedha kutoka katika Mfuko wa Polisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nauliza, hapa katika *Airport* ni kwa nini mishahara imezidi kwa kiwango kikubwa, kutoka Shilingi milioni 500 hadi Shilingi milioni 900, lakini halikadhalika hata posho zimetoka Shilingi milioni 400 kwenda Shilingi milioni 700. Je, hapa wamezaliwa wanya kama kule walikufa?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri!

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kufa na kuzaliwa siku zote, hatuwezi tukapinga. *(Kicheko)*

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilichotokea hapa ni kwamba yale malimbikizo mnayolalamikia kwamba Polisi hawapewi vyeo, hawapewi fedha zao kulingana na vyeo, ndiyo utekelezaji wake huo, msiojope. *(Kicheko/Makofi)*

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

Kif. 2011 - *Police Dogs and Horses* Sh. 978,671,000/=

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

Kif. 2012 - *DSM Special Zone* Sh. 8,378,612,000/=

MWENYEKITI: Mheshimiwa Masoud!

MHE. MASOUD ABDALLA SALIM: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. *Subvote 2012 Dar es Salaam Special Zone* iko katika *item 220200 - utility supplies and services*. Mwaka jana 2014/2015 kulikuwa kuna Shilingi milioni 180, mwaka huu kuna Shilingi 48; ukitilia maanani ni kwamba hii Dar es Salaam kama ni *special zone* na matakwa yake na mahitaji yake kwenye shughuli hii inakuwa ni kubwa sana. Naomba maelezo ya kina, ni kwa nini kuna upungufu mkubwa wa kiasi hiki katika *Dar es Salaam Special Zone*?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mwenyekiti, majibu!

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hiki ambacho kinalipia umeme, tumeongeza *efficiency* kwa kufunga Luku. Kwa hiyo, matumizi ya ovyo ovyo yatakuwa hayapo sasa.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

Kif. 2013 - *Police Ilala* Sh. 9,472,449,000/=

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

Kif. 2014 - *Police Kinondoni*... .. Sh. 9,471,199,000/=

MHE. IDD M. AZZAN: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye *subvote 2014, item 220300 - Fuel Oil and Lubricant*. Tunafahamu Kinondoni jinsi ilivyo, ukubwa wake, wingi wa watu, wingi wa uhalifu na mambo mbalimbali. Mwaka huu wa Fedha unaoisha, tulipewa kwenye kifungu hiki Shilingi milioni 196, lakini hivi sasa kwenye

Nakala ya Mtandao (Online Document)

mwaka wa fedha unaokuja, mmepunguza na kutoa Shilingi milioni 112, tofauti ya karibu Shilingi milioni 80.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba maelezo ya kina, ni kwa nini kifungu hiki tumekipunguza? Kwasababu hicho kifungu cha mwaka huu unaoishia, hiyo Shilingi milioni 196 mafuta yalikuwa yanakwenda mpaka nusu mwezi tu, yamekwisha, hela hakuna. Leo badala ya kutuongezea, mmepunguza sana. Ni kwasababu gani mmepunguza kwa kiasi hiki? Ama mnataka watu wa Kinondoni tuendelee kuwa na uhalifu huu bila ya Polisi kufanya kazi yoyote?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba majibu tena ya uhakika.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu!

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema awali ni kwamba Bajeti imepungua. Ni lazima kimahesabu tutafute *proportion* ya kupunguza hata kama mahali pana umuhimu. Kwa hiyo, Kinondoni ndiyo wamepata nyingi ukilinganisha na Mikoa mingine na bado kama kutakuwa na tatizo, basi *headquarters* itasaidia kama kawaida.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

Kif. 2015 - Police Temeke... .. Sh. 7,243,588,000/=
Kif. 2016 - Police Arusha... .. Sh. 10,722,187,400/=
Kif. 2017 - Police Iringa... .. Sh. 5,889,254,000/=
Kif. 2018 - Police Kilimanjaro Sh. 10,520,137,700/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

Kif. 2019 - Police Kigoma... ..Sh. 7,849,868,000/=

MWENYEKITI: Mheshimiwa Machali!

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Najielekeza pale kwenye *item* namba 210300 - *Personnel allowances (Non Discretionary)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakumbuka mwaka wa fedha uliopita nilihoji, iwapo hiyo Shilingi milioni 30 iliyokuwa imetengwa ni kwa ajili ya kuwalipa posho ambazo ni stahili za Askari wa Jeshi la Polisi Mkoa wa Kigoma wakiwemo Askari ambao wanapatikana kwenye Jimbo langu? Kwasababu wamekuwa na

Nakala ya Mtandao (Online Document)

malalamiko mbalimbali juu ya posho zile ambazo ni lazima; kwa mfano, uhamisho, masaa ya ziada na posho mbalimbali ambazo ni za lazima.

Sasa mwaka huu naona wametenga Shilingi milioni 40, naomba kuiuliza Serikali, mnadhani kiwango hiki ambacho kinapungua, bado hakijafikia hata kiwango cha mwaka 2013 ambacho kilikuwa ni Shilingi milioni 82 ambazo zilitengwa, kitaweza kukidhi madai ya Askari Polisi ili hatimaye waweze kuwa na moyo wa kuendelea kufanya kazi yao? Kwa sababu hii Shilingi milioni 30 mwaka 2014 mlisema itatosha, lakini hakuna chochote mpaka leo hii. Nini kauli ya Serikali?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu asiyeshukuru kidogo, hawezi kushukuru kikubwa, ukweli ni kwamba hapa kwa bajeti ya mwaka jana imeongezeka kwa Shilingi milioni 10 na hiyo ni asilimia 20. Kwa hali tuliyonayo kwa kweli, pia inategemea wale watu ambao wanastahiki wako wangapi.

Kwa hiyo, kwa sasa Kigoma mwaka 2014 walitengewa Shilingi 30 na mwaka huu tumewapa Shilingi milioni 40 ili kumaliza matatizo yaliyokuwepo.

(Kifungu kilivyotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

Kif. 2020 - Police Kagera Sh. 11,806,407,000/=
Kif. 2012 - Police Lindi Sh. 5,480,744,000/=
Kif. 2022 - Police Mwanza Sh. 11,519,859,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

Kif. 2023 - Police Mara... .. Sh. 7,239,492,000/=

MWENYEKITI: Mheshimiwa Matiko!

MHE. ESTER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, subvote 2023 - Police Mara, ukienda kwenye kifungu kidogo cha 220300 - Fuel Oil and Lubricants utaona kwa mwaka wa fedha uliopita walitengea Police Mara Shilingi milioni 221,100 lakini mwaka huu wa fedha wametutengea Sh. 55,500,000/= tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukizingatia jiografia ya Mara na hizi fedha walizotenga, sidhani kama wana dhamira ya dhati ya ulinzi na usalama kuwepo kwenye Mkoa wetu. Kwa hiyo, nataka kujua ni kwa nini wameshusha kwa takribani Sh. 165,600,000/= wameziona?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri!

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, hii hapa ni ukomo wa bajeti, lakini bado Mara hawatakuwa hawafanyi kazi kwasababu ya mafuta. *(Makofi)*

(Kifungu kilivyotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

Kif. 2024 - Police Tarime – Rorya Sh. 5,128,200,000/=

MWENYEKITI: Mheshimiwa Matiko!

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, Subvote 2024 Mkoa wa Kipolisi wa Tarime Rorya, Kifungu ni hicho hicho 220300 - *Fuel Oil and Lubricants*, naomba Mheshimiwa Waziri asitoe majibu mepesi sana; tukiwa Bungeni tunakuwa *serious* zaidi. Tunahitaji kujua na atuambie kabisa mbadala wa hizi fedha kama hazipo sasa hivi, tutazipata wapi na kwa mujibu upi. Asiseme tu kwamba hawatashindwa kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka 2014 walitenga Sh. 173,700,000/=, mwaka huu Mkoa wa Kipolisi wa Tarime Rorya, mmetenga Sh. 103,800,000/= tu; na mara nyingi unakuta raia wakipata matatizo, wakipiga simu Polisi wanaambiwa gari hazina mafuta na kwamba raia ndiyo aweke mafuta. Kwa hiyo, tunavyo hoji hapa tunatoa hoja za msingi, mtueleze mbadala wa mafuta kwa hawa Maaskari, kwa magari ya Polisi.

MWENYEKIT: Mheshimiwa majibu mbadala!

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, tutatumia hizi hizi tulizonazo, mbadala hakuna.

(Kifungu kilivyotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

Kif. 2025 – Police Mbeya Sh. 10,549,976,000/=

MHE. GODBLESS J. LEMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekaa kimya muda mrefu kama Waziri wa Mambo ya Ndani Mtarajiwa, sasa naona kuna mizaha na nisingependa kwa sababu naumia roho. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani kabisa kwenye Mkoa wa Mbeya Subvote 2025 Kifungu cha 220300 - *Fuel, Oils and Lubricants* mwaka 2013/2014 walikuwa wana bajeti ya Shilingi milioni 400; na mwaka 2014/2015 bajeti ya Shilingi milioni 179; mwaka 2015/2016, bajeti ya Shilingi milioni 81.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni hatari kama tutaliacha Jeshi la Polisi lianze kupita madukani kutafuta mafuta kwa ajili ya kazi za raia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwelewa sana Mheshimiwa Waziri, anajibu kwa *sympathy* kwamba hela ni hizi hizi. Lakini hata pale nilipotaka kunyayuka, nilitaka kuongelea suala la Arusha, mmekata mafuta Mkoa wa Arusha takribani kwa asilimia 50; Mbeya sasa mmekata kwa takribani asilimia 50. Polisi inawezaje kufanya kazi za usalama kama hawana mafuta ya kutembea? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri!

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kwamba Tanzania ni Mikoa. Kwenye Kasma ya mafuta tukishapewa, tunaigawa kwa Mikoa na hatubakizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila Mkoa ambao tutakwenda na wale ambao hatujawafikia, watakuja na hoja hii hii, kwasababu *universally* hiki ndicho tulichokifanya kwamba Kasma ya mafuta imepungua na sisi tukapunguza *accordingly, proportionally*.

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge ni lazima tukubaliane na hili kwamba ndiyo *reality*. Sasa hivi Mbeya, halafu watasimama wengine, lakini siyo mzaha. Hatuko kwenye mzaha kabisa! Lakini hii ndiyo *reality* katika bajeti ambayo tumetengewa.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, hoja hizi za Bunge ni *very serious* na ninajua *constrains* na matatizo ambayo Wizara mnayo. Lakini Kamati ya Ulinzi na Usalama imeshawasilisha maombi maalumu kwenye Kamati ya Bajeti ili suala hili la mafuta liwe *revealed* na angalu waongezewe fedha ili waweze kufanya kazi vizuri. *(Makofi)*

Kwa hiyo sasa, naomba tukifika kwenye kifungu kama hiki cha mafuta, mjue Kamati ya Bajeti inashughulikia na tunategemea pesa hizi ziongezwe.

(Kifungu kilivyotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

Kif. 2026 - Police MtwaraSh. 7,431,525,000/=

Kif. 2027 - Police MorogoroSh. 12,245,395,000/=

Kif. 2028 - Police ManyaraSh. 6,827,511,000/=

Kif. 2029 - Police SingidaSh. 7,214,819,000/=

Kif. 2030 - Polisi PwaniSh. 9,174,033,000/=

Kif. 2031 - Police RuvumaSh. 6,116,078,000/=

Kif. 2032 - Police RukwaSh. 5,102,381,000/=

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Kif. 2033 - Police ShinyangaSh. 6,999,198,000/=
Kif. 2034 - Police Tabora... ..Sh.6,496,994,000/=
Kif. 2035 - Police TangaSh. 8,920,034,000/=
Kif. 2036 - Police Mjini Magharibi... ..Sh. 11,135,196,000/=
Kif. 2037 - Police Kusini UngujaSh. 4,563,055,000/=
Kif. 2038 - Polisi Kaskazini Unguja... .. Sh. 3,665,210,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya
Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

Kif. 2039 - Police Kaskazini Unguja Sh. 3,451,432,000/=

MHE. ENG. MOHAMMED HABIB JUMA MNYAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, niko kwenye hiyo *subvote* 2039, kifungu 2010100 - Police Kusini Pemba. Kuna ongezeko la fedha katika 2010100 kiasi cha Sh. 266,201,000/= ambazo sababu kubwa ni marekebisho ya mishahara ya askari, baada ya kupandishwa vyeo na ongezeko la idadi la Askari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jambo zuri sana, tunapenda askari wetu kuongezwa mishahara na kupandishwa vyeo. Nina tatizo moja ambalo naomba Mheshimiwa Waziri anipatie ufafanuzi, kwamba katika bajeti nyingi sana tunaongeza mishahara, tunapandisha vyeo, lakini zile gharama ama fedha ambazo Askari anastahiki kuipata baada ya kupandishwa cheo, anakaa hata miaka miwili hajaipata. Limekuwa ni kero kubwa sana kwa Askari, tunapitisha bajeti, inazungumzwa namna nyingine kama hivi, unakuwa *pleased*, unafurahi na Askari wanafurahi, lakini badala yake hawalioni hilo ongezeko miaka nenda rudi, wakati mwingine inafika hata miaka mitatu.

Nataka Mheshimiwa Waziri atufafanulie, ongezeko hili la Shilingi milioni 266 kwa sababu ya ongezeko la mishahara na Askari waliopandishwa vyeo, wata-*realize* lini Askari na wajue kweli kwamba bajeti hii na ongezeko hili limewasaidia Askari? Naomba ufafanuzi huo. Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, ufafanuzi!

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka huu bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani tumepata asilimia 61 mpaka sasa. Kwa hiyo, itakapotokea kwamba tutazipata zote, nina uhakika kabisa watazipata. Tukipata chini ya hapo; tukipata kama tulivyopata mwaka huu, *61 percent of the total budget*, watapata kiasi hicho tu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Rukia! Mheshimiwa Mnyaa, umeshajibiwa. Ndiyo utaratibu, umeshajibiwa!

MHE. RUKIA KASSIM AHMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nipo katika *subvote* hiyo hiyo 2039, lakini katika *item 220300 - Fuel and Lubricant*. Mkoa wa Kusini Pemba ndipo kuna Mji Mkuu wa Pemba, kuna *Airport* na bandari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kuwatengea mafuta, Shilingi milioni 81 ni kuwaonea sana na kwa kweli hawataweza kufanya kazi. Sasa basi, nadhani wasilinganishwe Mkoa wa Kaskazini na Kusini Pemba. Hii fedha ni ndogo sana, naomba ufafanuzi wako Mheshimiwa Waziri. Watashindwa kufanya kazi.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri! Waheshimiwa Wabunge, lakini nilishasema vilevile kuwa eneo la *fuel*, Kamati ya Ulinzi na Usalama imepeleka maombi maaalum kwenye Kamati ya Bajeti ku-*review* hizi pesa zilizotolewa, kwa sababu ni ndogo na Jeshi la Polisi bila mafuta inakuwa ni kama *almost* limekaa halina kazi ya kufanya. *(Makofi)*

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

Kif. 2040 - Polisi Kaskazini Pemba Sh. 3,417,595,000/=

MWENYEKITI: Mheshimiwa Rajabu!

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nipo katika *subvote* hiyo ya 2040 - Polisi Kaskazini Pemba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika *item 230400 - Routine Maintenance and Repair of Vehicle*. Mkoa wa Kaskazini Pemba katika kufanya marekebisho na ku-*repair* magari yake, mwaka juzi haikupatiwa fedha, mwaka jana haikupatiwa fedha, mwaka huu mmeiwekea Sh. 1,200,000/=. Hivi Mheshimiwa Waziri, hata tairi za magari tuliyonayo Mkoa wa Kaskazini Pemba huwezi kununua? Mwaka 2013 hamkuwawekea fedha, mwaka 2014 hamkuwawekea fedha, mwaka huu mmewawekea fedha Sh. 1,200,000/=. Mmekusudia *RPC* akaibe ili atengeneze magari? Naomba maelezo! *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu!

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rajabu tusikasirike! Kuna kitu kinaitwa kikomo cha bajeti. Lakini niseme tu kwamba kama mwaka 2013 ni sifuri, mwaka 2014 ni sifuri, mwaka huu tunaenda kuzuri! *(Kicheko)*

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya Mabadiliko yoyote)

MHE. ALLY K. MOHAMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, hamna barabara huko!

Kif. 2041 - *Police Dodoma Sh. 7,800,513,000/=*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Lema!

MHE. GODBLESS J. LEMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, *subvote 2041, item 230900 - Routine Maintenance and Repair of Naval Operations Including Sea*, wametengewa sifuri. Lakini mwaka wa fedha 2013/2014 mahali ambapo kulikuwa hakuna bahari Dodoma, walikuwa wametengenewa Shilingi milioni 39.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba niondolewe hii *confusion!*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu!

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazungumzia Dodoma. Mwaka 2014 hakukuwa na kitu na mwaka huu hakuna kitu. Hakuna bahari wala ziwa.

MWENYEKITI: Kifungu hiki kinaafikiwa!

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

Kif. 2042 - *Police Geita Sh. 5,774,893,000/=*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Bukwimba!

MHE. LOLESIA J. M. BUKWIMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Nipo katika *sub vote 2042 - Polisi Geita, item 410500* inazungumzia habari ya *Acquisition of Household and Institutional Equipments*.

Mwaka 2014 tulitengewa Shilingi milioni 50, lakini mwaka huu tulitengewa Shilingi milioni nne tu, ni kiwango kidogo sana tukizingatia kwamba huu ni Mkoa mpya, tunahitaji vifaa vya kutendea kazi katika Idara ya Polisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kupata maelezo kwamba tutapata wapi hivyo vifaa sasa kama tumetengewa kiasi hiki kidogo cha fedha kwa mwaka huu?

MWENYEKITI: Waheshimiwa tunaingia kwenye *Guillotine* saa 1.20. Mheshimiwa Waziri!

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, vifaa hivi vinafununuliwa, hawazekani kila mwaka unanunua hivyo hivyo. Vilishanunuliwa mwaka 2014, mwaka huu vinanunuliwa pungufu.

(Kifungu Kilichotajwa hapo juu Kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

Kif. 2043 - Police KataviSh. 3,635,391,000/=
Kif. 2044 - Police Njombe... ..Sh. 4,412,645,000/=
Kif. 2045 - Police SimiyuSh. 4,160,534,000/=
Kif. 3001 - Police College MoshiSh. 10,411,701,000/=
Kif. 3002 - Police College..Sh. 2,104,237,000/=
Kif. 4001 - Police Vehicles Maint. Unit Sh. 4,427,194,000/=
Kif. 5001 - Police Medical UnitSh. 2,067,217,000/=
Kif. 6001 - Police Building BrigadeSh. 3,624,143,000/=
Kif. 7001 - Criminal Investigation Div.Sh.10,762,391,000/=
Kif. 7002 - Stock Theft Prevention Unit... ..Sh. 427,481,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya Mabadiliko yoyote)

Fungu 29 - Jeshi la Magereza

Kif. 1001 - Prisons HeadquartersSh. 17,848,992,000/=

MWENYEKITI: Mheshimiwa Aliko!

MHE. ALIKO N. KIBONA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Miaka miwili iliyopita nyuma, Jeshi la Polisi lili-engage baadhi ya staff kuendelea katika mkataba wa miaka miwili. Baada ya kumaliza mkataba wao, walio wengi tulionao huko Majimboni...

MWENYEKITI: Hii ni Magereza lakini!

MHE. ALIKO N. KIBONA: Magereza, sawa! Tulionao huko Majimboni hawajalipwa *gratuity* yao. Ningependa kupata maelezo na kwa vyovyote sasa hivi wanasikiliza, ni lini watapata *gratuity* yao? Je, pesa hii inaweza kutosha kwa shughuli hiyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu!

Nakala ya Mtandao (Online Document)

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi la Magereza kama yalivyo Majeshi mengine, kuna malimbikizo ya namna hiyo. Maombi yameshakwenda Hazina, kuna fedha nyingi zimeshahakikiwa. Sasa heri na hawa wako mle wanaweza kupata mafao yao.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

Kif. 1002 - Finance and AccountsSh. 234,700,000/=
Kif. 2001 - Parole DepartmentSh. 908,141,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

Kif. 2002 - Prisons Welfare & Rehabil ...Sh. 129,232,246,000/=

MWENYEKITI: Mheshimiwa Matiko!

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Subvote 2002 - Prisons Welfare and Rehabilitation, lakini naenda kwenye kifungu 210200 - Basic Salaries - Non Pensionable.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2014/2015 ilikuwa ni sifuri, mwaka huu ni Shilingi bilioni 10,774. Nilikuwa nataka tu nijue ni kwanini ime-shoot kihivyo kutoka sifuri mpaka Shilingi bilioni 10,774? Ni kwa ajili ya malipo gani?

MWENYEKITI: Majibu Mheshimiwa Waziri!

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, huu ni mshahara wa wale ambao ni wafanyakazi wasiokuwa na masharti ya kudumu. Mwaka 2014 kwa makosa Hazina iliweka sifuri, lakini ikatoa barua ya kusahihisha hiyo *addendum letter*, kwa hiyo, mwaka huu inatakiwa iwe hivyo.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

Kif. 2003 - Resettlement of OffendersSh. 2,456,371,000/=
Kif. 2004 - Prisons Arusha... ..Sh.192,286,000/=
Kif. 2005 - Prisons Dar es Salaam... ..Sh. 455,277,000/=
Kif. 2006 - Prisons Dodoma. Sh. 303,518,000/=
Kif. 2007 - Prisons KigomaSh. 197,286,000/=
Kif. 2008 - Prisons Tanga..... ..Sh. 227,638,000/=
Kif. 2009 - Prisons KageraSh. 182,110,000/=

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Kif. 2010 - Prisons Mwanza	Sh. 257,990,000/=
Kif. 2011 - Prisons Tabora	Sh. 197,286,000/=
Kif. 2012 - Prisons Mbeya	Sh. 242,814,000/=
Kif. 2013 - Prisons Singida	Sh. 166,928,000/=
Kif. 2014 - Prisons Coast...	Sh. 182,075,000/=
Kif. 2015 - Prisons Lindi...	Sh.197,286,000/=
Kif. 2016 - Prisons Manyara...	Sh. 154,002,000/=
Kif. 2017 - Prisons Mtwara	Sh. 152,759,000/=
Kif. 2018 - Prisons Ruvuma...	Sh. 182,116,000/=
Kif. 2019 - Prisons Rukwa...	Sh. 182,172,000/=
Kif. 2020 - Prisons Mara...	Sh. 182,110,000/=
Kif. 2021 - Prisons Iringa...	Sh.182,110,000/=
Kif. 2022 - Prisons Kilimanjaro	Sh. 198,315,000/=
Kif. 2023 - Prisons Morogoro.....	Sh. 242,835,000/=
Kif. 2024 - Prisons Geita	Sh. 83,640,000/=
Kif. 2025 - Prisons Katavi...	Sh. 81,890,000/=
Kif. 2026 - Prisons Njombe	Sh. 84,370,000/=
Kif. 2027 - Prisons Simiyu...	Sh. 86,340,000/=
Kif. 2028 - Prisons Shinyanga	Sh. 187,285,000/=
Kif. 3001 - Prisons Staff College	Sh. 2,976,615,000/=
Kif. 3002 - Prisons Driving School	Sh. 450,144,000/=
Kif. 3003 - Prisons Trade School	Sh. 850,710,000/=
Kif. 3004 - Prisons College Kiwira...	Sh. 1,749,783,000/=
Kif. 4001 - Prison Building Brigade	Sh. 1,674,822,000/=
Kif. 4002 - Prison Industries...	Sh. 763,541,000/=
Kif. 4003 - Prison Farms..	Sh. 1,467,582,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya
Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

Fungu 51- Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na NIDA

Kif. 1001 - Administration and HR MgntSh. 2,404,038,722/=

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, kutokana na muda, tumebakia na dakika 25 tu. Kwa utaratibu wa kanuni, huwa tunapewa majina na vyama. Kwa hiyo, wale ambao majina yao hayapo hapa, kwa mujibu wa kanuni sitaweza kuwaita. Nitaita tu; tena sitaweza kuita watu wote ambao wameandikishwa na Vyama kutokana na muda uliokuwepo.

Kwa hiyo, tunaanza na Mheshimiwa Lema Waziri Kivuli wa Mambo ya Ndani.

MHE. GODBLESS J. LEMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nilikuwa nataka ufafanuzi kwa Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani; ni kwanini *traffic* wamekuwa wasumbufu sana barabarani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Jimbo la Arusha peke, yale *traffic* wamewa-*position* katika mitaa yote ambayo ni *strategic* na wanakamata sana watu. Kule Arusha *traffic* anapewa alama ama *marks*; anayekamata makosa mengi anapata alama 'A'; anayofuatia anapata 'B', imekuwa ni kero na siyo Arusha peke yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kumwuliza Mheshimiwa Waziri, ni kwanini Jeshi la Polisi au Wizara yake imeamua kukifanya Kitengo cha *traffic* kuwa sehemu ya kitengo cha TRA kwa ajili ya ukusanyaji wa mapato badala ya kuzuia uhalifu barabarani?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, leo asubuhi Mheshimiwa Lema alikuwa anasema atapewa nchi kwa sababu *traffic* hawafanyi kazi. Sasa hivi analalamika. (*Makofi*)

In fact, Serikali haina nia yoyote ya kuwasumbua wananchi wala madereva. Lengo la kuongeza *traffic* ni kuongeza *visibility* ili madereva ambao wanaendesha wanavyotaka waone kuna Askari na hilo tuna uzoefu nalo.

Suala la *traffic* kupewa madaraja, hili nafikiri ni maneno ya barabarani, sisi hatuyafahamu. Sijui nani anatoa hizo *grade*. Kama yupo na anafahamika, tupewe ili tuelezane na Mawaziri wajue *grade* ipi ni ipi! (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Masoud!

MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM: Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kupata ufafanuzi juu ya Askari Polisi wastaafu ambao nilisema kwa muda mrefu na imeonekana kwamba wale ambao wameajiriwa miaka ya nyuma iliyopita ni kwamba pensheni zao za miaka ya 1960 mpaka 1990 ni ndogo sana, lakini miaka hii imekuwa pensheni zao ni kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya msingi ni kwamba kwanini basi tusichukue mishahara ya wastaafu na wanaostaafu sasa ili pensheni ya wale walijajiriwa zamani ilingane na wastaafu wa sasa kutokana na ukali wa maisha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo hili ni la muda mrefu na viongozi wetu, wale Mawaziri wamekuwa wakituahidi kwamba watarekebisha mfumo mzima wa namna ya pensheni katika Jeshi letu hili la Polisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri atupe ufafanuzi wa kina.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri!

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la *formula* ya kukotokoa mafao *ina-cut across* kwenye sekta nyingi, siyo Polisi peke yake. Kwa sababu kuna *factor* ya mshahara na mshahara wa zamani ulikuwa Sh. 300/= . Kwa kweli hilo ni tatizo. Isipokuwa Serikali mara nyingi, hata kama ni *formula* hiyo, lakini inatazama ni njia gani ya kuwasaidia wastaafu. Wamekuwa wanabadilishiwa malipo yao kutokana na Serikali inavyoamua pale ambapo bajeti inaruhusu.

Kwa hiyo, Serikali itaendelea kulitazama hili, lakini nafikiri siyo sawa kuchukua pesa ya leo tukaipiga hesabu na wakati ule ambao wamestaafu.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Machali!

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Inafahamika kwamba *best practice* katika kuendesha Serikali ni kwamba siyo vizuri sana kwa Serikali iliyo makini kukuta kwamba kuna chombo kimoja kinaonekana kukibeba chombo kingine katika utaratibu mzima wa utendaji na utoaji haki. Kama kuna utaratibu huo, hiyo inakuwa ni sera ambayo ni mbovu na mbaya inayopaswa kufutuliwa mbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumejitokeza *contradiction* hapa wakati Waziri wa Mambo ya Ndani ana-*wind up* akasema kwamba matokeo ya uchunguzi ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora kuhusiana na sakata la CUF hayo ni maoni ya Tume, *just opinion*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafahamu kwa mujibu wa *principles of natural justice* na tukirejea kitabu ambacho naamini Waziri wa Mambo ya Ndani ni msomi mzuri tu, ni Mwanasheria mzuri, kitabu cha Profesa Chris Peter Maina cha *Human Rights in Tanzania* katika *principles of natural justice* anasema kwamba, "*no person shall be a judge of his own cause or his own case.*"

Mheshimiwa Mwenyekiti, inaeleweka bayana kwamba Waziri wa Mambo ya Ndani ni *interested part* ambaye ni Kiongozi wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Sasa suala hili ambalo lilikuwa linahusisha baadhi ya Askari ambao wameonekana kutumia nguvu na Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ni chombo cha Serikali ambacho katika suala hili tulitegemea kuwa kama ni Hakimu, ni *referee* wa kuangalia Jeshi la Polisi lilitenda haki kwa Viongozi hawa wa Chama cha Wananchi CUF na wafuasi wote waliotandikwa na kupatwa na madhara yaliyowakuta. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa swali langu ni moja na kama Serikali haitaweza kutoa majibu ya kuridhisha nakusudia kuondoa shilingi ili suala hili lijadiliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri Mheshimiwa Mathias Chikawe anapata wapi ujasiri wa kuweza kubeza matokeo ya chombo makini? Anapata wapi haki hiyo? Chombo hiki cha Serikali, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora. Naomba kauli ya Serikali, Waziri atueleze ni kwanini anabeza matokeo hayo na kwamba ni suala tu, ni *opinion* hiyo. Unakuwaje Hakimu kwenye kesi ambayo inakuhusu wewe?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Machali muda wako umekwisha, lakini Mheshimiwa Waziri alimalizia kwa kusema, mapendekezo hayo yatafanyiwa kazi na hatua zitachukuliwa. Wewe na Mheshimiwa Rajab mkapiga makofi, nami niliwaona.

MHE. MOSES J. MACHALI: Hapana! Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba ajibu.

MWENYEKITI: *No, no, no!* Ngoja, hebu kaa chini kwanza. Mheshimiwa Waziri alimalizia kwa kusema kwamba mapendekezo ya Tume yatafanyiwa kazi na hatua zitachukuliwa kufuatana na maagaizo. Ndicho alichozungumza na *Hansard* zipo. Humu ndani kuna *Camera*, tukirudi muda ule utakutwa wewe na Mheshimiwa Rajab mlikuwa mnapiga makofi.

Subiri, sijakwambia kama hatajibu, lakini ninakuambia vilevile kilichotokea humu ndani name nilikuwa naangalia. Ndiyo kazi yangu! Mimi ni *referee* humu! Mimi sina timu humu, nikikaa hapa.

Mheshimiwa Waziri!

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri ndugu yangu niliposema ni maoni, kwake ikamaanisha kama nimebeza. Siwezi kubeza chombo kama kile. Nilishiriki katika kuanzisha Tume ya Haki za Binadamu, mimi mwenyewe. Naiheshimu sana na ninawaheshimu wote wanaofanya kazi pale. Hata siku moja siwezi kubeza maoni yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema, ni maoni yao. Siwezi kusema siyo yao, ni ya nani sasa? Hapana! Ni ya Tume na sisi kama Wizara tunayapokea; tunasema hili kwa kweli wamesema sawa na ni lazima tufanye hivi. Ndiyo tutakachokifanya. Sasa sioni ugomvi unakuja wapi!

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni ya Tume tutayachukua, tutaisoma taarifa, tutakaa, tutasema hili ni sawa, hili siyo sawa. Pale ambapo siyo sawa,

tutawaambia Tume, hapa mmekosea. Sasa mwisho wa yote, kama hatuelewani kabisa na Tume, tutakwenda Mahakamani, ndiyo sheria inavyosema. (Makofi)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Machali!

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, narejea tena kwa kusema tu kwamba mtuhumiwa hawezi kuwa Hakimu wa kesi inayomhusu.

Sasa yeye anasema kwamba ameiangalia; Tume hii ilipewa jukumu la kulichunguza Jeshi la Polisi; Waziri wa Mambo ya Ndani ni sehemu ya Jeshi la Polisi, ni *Custodian* huyu ambaye analiongoza Jeshi la Polisi. Leo kusema tena Tume imetoa taarifa halafu yeye ndio anaanza kuchunguza matokeo ya Tume, hii siyo *best practice globally*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa shilingi suala hili lijadiliwe. Waheshimiwa Wabunge, naomba mniunge mkono kwa sababu haiwezekani kwamba wewe Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ndiye ambaye unahusika; na siku ile wakati suala hili limeibuka pia ulikuwa unajaribu kuwa-*defend* kwa kiasi kikubwa. Tunaomba utuambie, unapata wapi ujasiri wa kuweza kubeza matokeo ya chombo kikubwa hiki cha Kiserikali ambacho ni muhimu? Halafu unataka kuwa Hakimu kwa sababu hili suala linakuhusu!

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa hoja naomba suala hili lijadiliwe.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Masoud!

MHE. MASOUD ABDALLA SALIM: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naungana na mtoa hoja kwa sababu tu, Mheshimiwa Waziri wakati akitoa maelezo yake alisema kwamba Profesa Ibrahim Haruna Lipumba alifanya maandamano akitokea Temeke kufika Mtoni Mtongani ndipo Askari walipomvamia. Alikuwa kwenye gari. Askari waliomdhalilisha Profesa Lipumba, Mwenyekiti wetu wa Taifa wa CUF, alisema ni amri kutoka juu. Sasa amri kutoka juu ni kutoka kwa nani? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, walitumia nguvu kupita kiasi, alikuwa kwenye gari lake anaelekea zake kule Mbagala kwenda kuondoa watu. Sasa ulikuwa ni ujanja tu ambao walikusudia kumdhalilisha na Vyombo vya Habari vilikuwa vinaonesha, picha zote, magazeti na kila kitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasema hapa, bado Mheshimiwa Waziri akubali tu kwamba amri kutoka juu ndiyo iliyotumika na isitoshe Tume ile ya Haki za Binadamu imetoa maelezo yake, Serikali ikiri makosa kwamba Askari

waliofanya vile wachukuliwe hatua za kisheria ionekane basi kwamba kuna haki sawa kwa wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha hoja yangu hiyo. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa kibona!

MHE. ALIKO N. KIBONA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Suala analolizungumzia Mheshimiwa Machali ni suala ambalo bado *lina-ring* kwenye vichwa vya watu, ni jambo ambalo liligusa hisia za watu wengi, wale ambao wanahuruma kwa binadamu wenzao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sote tunakubali kwamba Tume iliundwa. Tume ipo, nami ninachokiona hapa na ambacho ni lazima wote tukubaliane ni ule mfumo uliopo kwamba muda huu inabidi tuanze kuangalia upya kwamba Tume za namna hii zinapoundwa, matokeo yake yasijadiliwe na wahusika wenyewe, lakini kwa utaratibu uliopo lazima Tume ipeleke matokeo Serikalini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumbe sasa, nadhani siyo haki kusema kwamba Wizara ya Mambo ya Ndani isichunguze, isipokee mapendekezo ya Tume kwa sababu huo ndiyo utaratibu uliopo kwa sasa. Lakini baadaye kuna haja ya kuangalia upya, matokeo ya namna hii yakitokea mhusika asiwe tena Wizara ya Mambo ya Ndani. Ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante, muda wako umekwisha. Mheshimiwa Lusinde!

MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kujadili hoja ya Mheshimiwa Machali, lakini nianze kwa kumpa pole rafiki yangu kwa kumiminwa kwenye uchaguzi, naona sasa hata kungea anashindwa; yuko *ng'a, ng'a ng'aaah!* *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza Waziri siyo sehemu la Jeshi la Polisi, kama Mzungumzaji alivyojaribu kujenga hoja. Waziri anaongoza Wizara, lakini yeye siyo sehemu ya Jeshi la Polisi. Jambo la pili, Mheshimiwa Waziri amejibu vizuri kwamba wanapokea, wanatazama, wanasema hili sawa litachukuliwa hatua, hili linaweza kwenda Mahakamani kama hatukukubaliana. Kumbe wapeleke wapi na chombo kinachotoa haki ni Mahakama? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa ni lazima tukubaliane kwamba tunaishi kwa mfumo wa kufauata sheria. Hata ingekuwa Polisi amevunja sheria za wazi za nchi, huna namna yoyote ya kumuua yule Polisi isipokuwa umshitaki. Kwa hiyo, siungi mkono hoja hii.

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Lusinde. Mheshimiwa Waziri wa Nchi!

NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi (Uratibu), kwanza napenda nipongeze tu hoja ya Mheshimiwa Machali, lakini pia niseme tu kwamba alichokijibu Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani yuko sawa. Ukienda kwa undani wa jambo hili, Tume yenyewe imevunja Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kujadili na kulichunguza jambo ambalo tayari lilikuwa Mahakamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiisoma Katiba, inaeleza wazi kwamba mambo yaliyopo Mahakamani kwenye Ibara ya 131 kwa wale ambao wana Katiba, Ibara ndogo ya (2) inaeleza wazi na nitaomba niisome kama ifuatavyo:-

“Tume haitachunguza mambo yafuatayo, kwa madhumuni ya kutekeleza majukumu yake: (a) Jambo lolote ambalo lipo mbele ya Mahakama au chombo kinginecho cha Kimahakama.” (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili liko Mahakamani, tunazungumzia Tume ya Haki za Binadamu. Jambo hili lipo Mahakamani na Tume imechunguza jambo lililoko Mahakamani ambayo matokeo yake yanaweza kuathiri shughuli za Mahakama. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Mbunge arudishe Shilingi ya Mheshimiwa Waziri na jambo hili aliache Serikali ifanyie kazi katiak upungufu ambao umezungumzwa kwenye ripoti hiyo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi!

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimsihi Mheshimiwa Machali apunguze ukali wake na arudishe hii shilingi kwa sababu tu nimesema tutaisoma hiyo ripoti, tutaifanyia kazi; yale yanayohusu kufanyiwa kazi, tutayafanyia kazi mara moja. Zaidi tufanyeje? Tusemeje? Mheshimiwa Machali, tusemeje?

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Waziri. Mheshimiwa Machali, funga hoja yako!

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya ku-consult na wenzangu lakini pia naomba niweke *record* sahihi ya alichokizungumza Kaimu Waziri wa Nchi. Mamlaka ya Tume, kwanza siyo Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ambayo inazungumziwa hapa kwenye Ibara ya 131 fasili ya (1) ambayo umeizungumzia. Hii Tume ipo ni *permanent* na jana tu tumepitisha bajeti yake. Kwa hiyo, tunapofanya nukuu ya vifungu wakati mwingine *citation* kwa misingi ya usahihi na siyo vinginevyo. (Makofi)

Mheshimiwa Waziri naomba nikubaliane, isipokuwa ningependa labda nipate *statement* moja ya mwisho; hili jambo la kwenda mkafanye kazi ya

kupitia matokeo ya Tume, mtaifanya kwa muda gani ili kusudi mji-commit, mtaifanya kwa muda gani na pengine tuone sasa haki inatendeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, msiwe *defensive* sana kwa baadhi ya vitu, kwa sababu naamini siyo Askari wote ambao wanahusika katika kufanya vitendo hivyo.

Wapo baadhi ya Askari ambao ni waadilifu, lakini kuna baadhi ya Askari ambao vilevile sio waadilifu na ndiyo wachache ambao wameweza kufanya hayo waliyoyafanya. Kwa hiyo, msiwa-*protect* wale Askari wachache ambao wanaonekana wana-*lack integrity*. Timiza wajibu wako ili kusudi kuhakikisha kwamba tunajenga Jeshi lenye weledi, lenye kuweza kufanya kazi kwa misingi ambayo inakubalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme tu kwamba narudisha shilingi hiyo. Ahsante nashukuru.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Beatrice Shellukindo!

MHE. BEATRICE M. SHELUKINDO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba nimwulize Mheshimiwa Waziri, utaniwia radhi sauti yangu kidogo inakatakata. Wilaya ya Kilindi tangu ianze takribani miaka 12 haijawa na Kituo cha Polisi. Kwa muda wote huu tumekuwa tukitumia *Police Post*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka kadhaa tumekuwa tukiahidiwa kwamba tutatengewa bajeti ya kujengewa kituo.

Sasa namwomba Mheshimiwa Waziri, kama haiwezekani kujenga kwa wakati mmoja: Je, mnaweza hata kutenga kwenye bajeti basi, mwaka wa kwanza mkaanza *stage* moja, mwaka unaofuatia mkaendelea? Tumejitahidi baadhi ya Kata kujenga Vituo vya Polisi. Sasa namwomba Mheshimiwa Waziri, katika hili la Kituo cha Wilaya ambapo tumetenga eneo kubwa, anaweza akatuambiaje wananchi wa Kilindi? Ahsante. (*Makofi*)

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa hoja aliyowasilisha ndugu yangu Mheshimiwa Beatrice. Nataka nimhakikishie kwamba Jeshi la Polisi linakusudia kujenga vituo imara kabisa vya Polisi katika kila sehemu ambapo hakuna. Ila niseme, kama wamejenga vya Kata, labda hivyo wamejitolea. Hatutawaomba wajitolee, hiki ni kikubwa zaidi cha Wilaya.

Kwa hiyo, nataka nichukue *undertaking* kulitaka Jeshi la Polisi kuhakikisha kwamba katika bajeti inayokuja, maana katika bajeti hii hakuna; katika bajeti inayokuja wa-*undertake* kujenga kituo kamili, siyo kwa kuanza kidogo kidogo,

kujenga mara moja. Kwa hiyo, watu wa Kilindi wakae wasubiri kituo hicho katika bajeti ijayo. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Ole-Medeye!

MHE. GOODLUCK J. OLE-MEDEYE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya ya Arusha kwa jiografia yake inazunguka Jiji la Arusha ama Wilaya ya Arusha na wamekuwa wakipata matatizo sana kwamba wanapotuhumiwa na Polisi au na mtu akiripoti Polisi kwamba huyu ni mtuhumiwa, anachukuliwa kutoka kona moja ya Wilaya; kwa mfano, mpaka wa Monduli au mpaka wa Longido, mpaka wa Simanjiro, anapelekwa mpaka Makao Makuu ya Wilaya yaliyopo USA, matokeo yake, hata uwezo wa ndugu kama familia iko katika hali ambayo siyo nzuri kiuchumi, hata uwezo wa ndugu kwenda kuwadhamini inakuwa ni shida sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa na maombi yafuatayo kwa Mheshimiwa Waziri, kwamba ili kuwapunguzia wananchi wa Halmashauri ya Wilaya ya Arusha adha wanayoipata hivi sasa, Serikali ikubali kwamba badala ya Makao Makuu ya Polisi Wilaya ya Arumeru kuwashughulikia wananchi wa Halmashauri ya Wilaya ya Arusha, kituo kikuu cha Polisi kilichopo Arusha Mjini, kiwe *designated*, ndiyo Kituo cha Polisi kwa Halmashauri ya Wilaya ya Arusha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vinginevyo, Serikali ikubali kupanua na kupandisha hadhi Kituo cha Polisi Ngaramtoni ili kitumike kwa ajili ya kutoa huduma kwa wananchi wa Halmashauri ya Wilaya ya Arusha badala ya hatua ya hivi sasa, wanapelekwa USA na ukweli wanaenda kunyanyasika sana kule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia Mahakama ya Wilaya, ipo katika Halmashauri ya Wilaya ya Arusha ambayo inahudumia Wilaya mbili, Arumeru na Arusha. Gereza Kuu la Arusha lipo Arusha. Nashukuru sana.

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Waziri majibu!

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Namshukuru Mheshimiwa Ole-Medeye kwa hoja yake, lakini hii nashindwa kuitolea fatuwa moja kwa moja, hii ni lazima niseme kwamba tuwaachie Jeshi la Polisi wa *study* hizo *logistics* za Ngaramtoni, Arusha, Arumeru halafu tutoe uamuzi ambao utawasaidia wananchi ambao Mheshimiwa Ole-Medeye anawakilisha. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mbunge!

MHE. SYLVESTER MASSELE MABUMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Ni Sera ya Serikali yetu kuhakikisha kwamba wafanyakazi wake wote wanahudumiwa sawasawa ipasavyo. Lakini kwa muda mrefu sasa Jeshi la Polisi hasa Polisi yenyewe wamekuwa wakiidai Serikali malimbikizo ya likizo lakini pia posho mbalimbali na imefika wakati Polisi anapokwenda kozi anatakiwa ajigharamie nauli na mambo mengine. Nataka kumwuliza Mheshimiwa Waziri: Je, sera hii ya kuagiza Polisi wanapokwenda kozi wajilipie wenyewe ilianza lini? Ni lini Serikali italipa mafao haya ambayo Polisi wanadai ili waweze kutumika vizuri hasa wakati huu tunapoelekea Uchaguzi Mkuu? Ahsante sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu!

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba baadhi ya wakati Jeshi linakuwa halina fedha mkononi ambazo zingewezesha kusafirisha Askari ambao wanatakiwa waende kwenye masomo. Wakati huo siyo masomo tu, hata wakati mwingine kutekeleza kazi zao, hushauriwa kwamba wapate fedha ambazo wanaweza kufanya shughuli hiyo na baadaye kurejeshewa. Hakuna Askari ambaye ataambiwa hivyo halafu asirejeshewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba kuna malimbikizo, lakini kama tulivyosema katika wakati tofauti ni kwamba fedha hizi ambazo zinadaiwa zimeshahakikiwa na tunasubiri tupewe fedha ili ziwafikie walengwa.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Matiko!

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nataka nipate tu ufafanuzi nijue ni hatua gani zimechukuliwa, kwa sababu tumekuwa tukiendelea kushuhudia kwa nchi yetu ya Tanzania baadhi ya Askari Polisi wakitenda kinyume na wajibu wa Askari Polisi. Wanatumia nguvu nyingi kuliko hali halisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshuhudia Watanzania wakinyanyaswa, wakilemazwa na wengine wakiuawa. Tulishuhudia juzi, mwaka huu kule Momba, mwanamama mjamzito wa miezi nane au tisa, alikuwa karibu ajifungue alipigwa na Askari Polisi. Kilichotokea, mtoto wake akafia tumboni, yule mwanamama akatolewa mtoto amefariki na kizazi kikaondolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tumeendelea kushuhudia, juzi Mheshimiwa Tundu Lissu alisema kuna kijana ameuawa huko Njombe na kwingineko kote.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi Jeshi la Polisi hata tunavyoingia hapa, sisi akinamama kama mashine zimelia, tunakaguliwa na Askari Polisi, lakini tumeshuhudia Askari wakiume wakiwapiga wanawake!

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nijue ni hatua gani zimechukuliwa kwa Askari wa kiume wanaowapiga wanawake na kuwadhalilisha?

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa ufafanuzi kama ifutavyo, kwamba ni utaratibu wa Jeshi la Polisi kuwadhibiti Polisi wake. Wako Polisi tumewafukuza kazi, ni wengi; wako Polisi wameshitakiwa Mahakamani; wako wale tuliowashitaki kwenye Mahakama ya Kijeshi mbali; lakini walioshitakiwa Mahakamani kwa kufanya vitendo ambavyo ni kinyume na taratibu za Polisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, wako wengi. Naweza nikakutafutia *statistics* baadaye nikakupa. Ninazo kwenye makaratasi haya mengi hapa, lakini tunachukua hatua hizo za kuwafukuza, kuwashitaki Mahakamani na kuwashitaki kwenye Mahakama za Kijeshi ambapo wanapewa adhabu wanazostahili.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tunaingia kwenye *Guilotine* sasa!

Kif. 1001 - *Administration and HR Mgnt* ... Sh. 2,404,038,722/=
Kif. 1002 - *Finance and Accounts*... .. Sh. 509,728,600/=
Kif. 1003 - *Policy and Planning* Sh. 18,585,501,200/=
Kif. 1004 - *Probation & Comm. Serv. Div.*....Sh. 2,229,443,783/=
Kif. 1005 - *Govnt Communication Unit* Sh. 234,527,295/=
Kif. 1006 - *Mgnt Inform. System Unit* Sh. 190,099,000/=
Kif. 1007 - *Internal Audit Unit* Sh. 186,633,400/=
Kif. 1008 - *Procurement Mgnt Unit*... .. Sh. 242,771,400/=
Kif. 1009 - *Complaints Division* Sh. 207,211,000/=
Kif. 1010 - *Legal Services Division* Sh. 447,653,000/=
Kif. 4001 - *Refugees Unit*.. .. Sh. 608,022,600/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

Fungu 93 - Idara ya Uhamiaji

Kif. 2001 - Immigration Zanzibar Sh. 5,983,458,000/=
Kif. 2002 - Immigration Mainland Sh. 48,587,765,000/=
Kif. 2003 - Regional Immig. Offices... .. Sh. 15,440,881,000/=
Kif. 2004 - TZ Reg. Immigr. Training Acad ... Sh. 1,533,102,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

MIPANGO YA MAENDELEO

Fungu 14 - Jeshi la Zimamoto

Kif. 3001 – Fire and Rescue Services Sh. 1,500,000,000/=

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

Fungu 28 - Jeshi la Polisi

Kif. 2001 - Polisi Mainforce... .. Sh. 6,118,468,000/=
Kif. 2005 - Polisi Zanzibar Sh. 300,000,000/=
Kif. 2020 - Polisi Kagera Sh. 450,000,000/=
Kif. 2022 - Polisi Mwanza Sh. 565,000,000/=
Kif. 2023 - Polisi Mara Sh. 535,000,000/=
Kif. 2026 - Polisi Mtwara Sh. 12,500,000/=
Kif. 2044 - Polisi Njombe Sh. 530,000,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

Fungu 29 - Jeshi la Magezeza

Kif. 2002 - Prisons Welfare and Rehab... .. Sh. 21,716,000/=
Kif. 4001 - Prison Building Brigade... .. Sh. 1,547,500,000/=
Kif. 4003 - Prison Farms Sh. 52,500,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

Fungu 51 - Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi

Kif. 1003 - Policy and Planning Sh. 76,214,722,000/=

Kif. 4001 - Refugees Unit Sh. 750,000,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

Fungu 93 - Idara ya Uhamiaji

Kif. 2002 - Immigration Mainland Sh. 5,800,000,000/=

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

(Bunge lilirudia)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, mkiona wakati mwingine nachelewa, mjue vifungu hivi vina taabu hivi! Kwa hiyo, tuvumiliane tu. Mheshimiwa Mtoa Hoja?

T A A R I F A

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa Taarifa kwamba Kamati imepitia Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na kuipitisha, pamoja na mabadiliko yaliyofanywa kabla na kuipitisha bila ya marekebisho yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja!

WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

(Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ya Mwaka 2015/2016 yalipitishwa na Bunge)

MWENYEKITI: Walioafiki wameshinda na Bajeti imepita. Tunawapongeza Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri, wewe na timu yako.

Tunajua Wizara yako inafanya kazi kwenye mazingira magumu sana, lakini vilevile nampongeza IGP na timu yake yote ya Polisi, wanafanyakazi katika

mazingira magumu sana. Lakini nategemea Kamati ya Bajeti itafanya kazi nzuri ya kutizama tena upya na kutizama pale itakapopaweza, basi iweze kuongezea. Katibu!

KAMATI YA MATUMIZI

MATUMIZI YA KAWAIDA

Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa

Fungu 38 - Ngome

Kif. 1001 - *Defence Forces Headq...* ... Sh.1,128,593,740,000/=

Kif. 1007 - *Land Forces Command* Sh. 12,338,249,000/=

Kif. 1008 - *Air Defence Command* Sh. 9,336,856,000/=

Kif. 1009 - *Navy Command...* Sh. 6,723,568,000/=

Kif. 1010 - *Military Hospitals...* Sh. 6,041,428,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi pamoja na Marekebisho yake)

Fungu 39 - Jeshi la Kujenga Taifa

Kif. 1001 - *The National Service Force...* Sh. 292,296,992,000/=

Fungu 57 - Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa

Kif. 1001 – *Administration and HR Mgnt* ...Sh. 18,794,164,000/=

MHE. MASOUD ABDALLA SALIM: Mheshimiwa Mwenyekiti, sina nia kubwa ya kuchukua mshahara wa Mheshimiwa Waziri, jirani yangu, lakini wakati akitoa majibu hapa Mheshimiwa Waziri wetu wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, alieleza kwamba wastaafu walio katika cheo cha *Major General* na kuendelea, basi *pension* zao tayari zimepatiwa ufumbuzi, kwa maana kwamba sera yao, taratibu zao na sheria zao zimekamilika na kuna asilimia kubwa ambayo wanapata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hoja yangu ya msingi, nikiwa Waziri Kivuli, niliposoma asubuhi nilimwambia tatizo kubwa linakuja kuanzia cheo cha *Private* hadi *Brigadier General*, *pension* zao ni ndogo, hali zao za maisha ni mbaya. Wamefanya kazi kwenye miaka ya 1960 na wengine miaka ya 1990, lakini bado hakuna sera yoyote, wala taratibu zozote za kupatiwa fedha zao.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri nakumbuka kwa wakati tofauti alitueleza kwenye Kamati yetu kwamba mchakato na utaratibu mzuri umeandaliwa wa hawa wa *Private* hadi *Brigadier General*. Lakini mpaka sasa bado ni kilio. Hatuoni mchakato wake unakwenda vipi na hali zao za maisha zinaendelea kuwa mbaya zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utueleze, ni lini sasa Cheo cha Kuanzia *Private* hadi *Brigadier General* na wao sera yao itakamilika kupata *pension* kubwa? Kwa sababu naelewa hali ya maisha ilivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ufafanuzi wa kina.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri! Mheshimiwa Waziri, nakuomba ungesogea kidogo ili nikuone na mimi

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumjibu Mheshimiwa Masoud kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba, kama walivyosema wenzangu wa Wizara ya Mambo ya Ndani kwamba kutokana na ukokotoaji wa *Pension* hutegemea mishahara, wale waliostaafu zamani *pension* zao ni ndogo sana. Hilo linatambulika na tulishalizungumza mara kadhaa, lakini suala hili siyo kwa Jeshi peke yake, suala hili ni kwa Serikali nzima, kwa maana ya Watumishi wa Umma na Vyombo vingine vya Ulinzi na Usalama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, litakapotekelzwa, lazima lihusishe watu wote hawa. Huwezi kubagua sehemu moja ukaacha nyingine. Tuko katika mazungumzo na Hazina; wanaona umuhimu wa kurekebisha *pension* hizo kwa sababu kwa kweli, zimepitwa na wakati na ni kidogo mno! Lakini wanatuambia kwamba watafikia sehemu watupe jibu la kuongeza *pension* hizo kwa kadiri hali ya uchumi itakavyoruhusu.

Kwa hiyo, nakuomba Mheshimiwa Mbunge, uvute subira wakati Serikali inashughulikia jambo hili, ila linahusu watu wengi mno. Kwa hiyo, chochote kitakachoongezwa maana yake, *budget implication* yake itakuwa kubwa sana. Ndiyo maana limechukua muda kidogo, lakini mategemeo yapo kwamba fedha hizo zitaanza kurekebisha kadiri uchumi utakavyokuwa unaendelea kukua. (Makofi)

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya
Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

Kif. 1002 - Finance and Accounts... .. Sh. 326,261,100/=

Kif. 1003 - Policy and Planning Sh. 549,283,000/=

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Kif. 1004 - Internal Audit Unit Sh. 223,542,000/=

Kif. 1005 - Procurement Mgmt Unit Sh. 155,344,000/=

Kif. 1006 - Legal Services Unit... .. Sh. 122,570,000/=

Kif. 1007 - Govnt Communic Unit Sh. 87,969,000/=

Kif. 1009 - Independent Telecom. Network...Sh. 121,338,900/=

Kif. 2001 - Industries, Construction & Agric ...Sh. 455,755,000/=

Kif. 2002 - Military Research and Dev.... ..Sh. 309,261,000/=

Kif. 2003 - Building Consulting Unit Sh. 266,671,000/=

Kif. 2004 - Estate Mgt and Dev. Unit Sh. 370,412,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

MIPANGO YA MAENDELEO

Fungu 38 - Ngome

Kif. 1001- Def. Forces HQ Command... .. Sh.12,000,000,000/=

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

Fungu 39 - Jeshi la Kujenga Taifa

Kif. 1001 - The National Service ForceSh. 7,000,000,000/=

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

Fungu 57 - Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa

Kif. 1001 - Administration and HR Mgmt Sh. 137,958,000/=

Kif. 1003 - Policy and Planning Sh. 250,000,000/=

Kif. 1009 - Indep. Telecom. Network... .. Sh. 7,556,800,000/=

Kif. 2001 - Industries, Constr. and Agric' ... Sh. 39,870,000,000/=

Kif. 2002 - Military Research and Dev.... Sh. 164,000,000,000/=

Kif. 2003 - Building Consulting Unit... .. Sh. 933,200,000/=

Kif. 2004 - Estate MGT and Dev. Unit Sh. 7,390,000,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

(Bunge lilirudia)

MWENYEKITI: Mheshimiwa mtoa hoja!

T A A R I F A

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa Taarifa kwamba, Kamati imepitia Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Fungu 38 – Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania, Fungu 39 – Jeshi la Kujenga Taifa na Fungu 57 – Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016 kifungu kwa kifungu pamoja na marekebisho yaliyofanywa awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

(Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ya Mwaka 2015/2016 yalipitishwa na Bunge)

MWENYEKITI: Ahsante. Hoja imeungwa mkono! Walioafiki wameshinda na Bajeti imepita. *(Makofi)*

Nakupongeza Mheshimiwa Waziri na Timu yako, mnafanya kazi nzuri sana. Nampongeza CDF na Chief of Staff na watu wote wa JKT kwa kazi nzuri mnayoifanya! *Keep it up you are doing a good job. (Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa 3.00 asubuhi.

(Saa 1.38 usiku Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumamosi, Tarehe 23 Mei, 2015, Saa Tatu Asubuhi)